

## **Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**Kikao cha Sita – Tarehe 28 Aprili, 2009**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Jenista J. Mhagama) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge habari za asubuhi, tunaendelea na shughuli zetu za leo, kabla sijamwita Katibu nichukue nafasi hii kuwapongeza Wafanyakazi wote kusheherekea siku yao ya kimataifa ya Usalama mahali pa kazi, baada ya kusema hayo namwomba Katibu atupe utaratibu wa kazi za leo.

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA:**

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Majukumu na Hesabu zilizokaguliwa za Tume ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2005.

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Majukumu na Hesabu zilizokaguliwa za Tume ya Utumishi wa Umma ulioishia tarehe 30 Juni, 2006.

Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Majukumu na Hesabu zilizokaguliwa za Tume ya Utumishi wa Umma kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2007.

**MHE. JOHN M. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:**

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2008/2009.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO (K.n.y. MHE. DR. WILLIBROD P. SLAA -  
MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka 2008/2009.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 68

**Uanzishwaji wa Vijiji Vipya Kishapu**

**MHE. FRED M. TUNGU** aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali ilishaahidi kutoa kipaumbele kwa Wilaya ya Kishapu katika ugawaji wa vijiji vikubwa kwa mwaka 2008/2009 na kwamba Halmashauri imeshawasilisha maombi ya kugawa na kuanzisha vijiji vipya 24.

Je, Serikali imetoa idhini ya kuanzisha vijiji vipya vingapi kwa Wilaya ya Kishapu, kutokana na maombi yaliyowasilishwa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA  
NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fred Mpendazoe Tungu, Mbunge wa Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya kugawa vijiji vikubwa na kuanzisha vijiji vipya kwenye Halmashauri zote zilizowasilisha maombi yao katika Ofisi yangu, ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, yamekwisha chambuliwa; ili kutambua maombi yaliyokidhi vigezo na yale ambayo hayakukidhi vigezo ya kuwezesha kuanzisha au kugawa Vijiji vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumbukumbu zilizopo katika Ofisi yangu zinaonyesha kuwa maombi yaliyopokelewa na tayari yamekwisha chambuliwa kutoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu ni 23 na siyo 24 kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Idadi ya vijiji vipya vilivyokubalika itatolewa kwa pamoja katika tangazo la Serikali la Vijiji, Mitaa na vitongoji vitakavyofanya uchaguzi wa mamlaka ya Serikali za Mitaa mwezi Oktoba mwaka 2009. Tangazo hili litatolewa na Serikali miezi sita kabla ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Naomba kuliarifufu Bunge lako tukufu kwamba mchakato wote umekamilika ikiwa ni pamoja na hatua ya mwisho ya tangazo la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wanaopenda kufahamu idadi ya maeneo mapya yaliyokubalika wavute subira hadi hapo tangazo la Serikali itakapotoka, kwani kazi ya kuhakiki orodha ya vijiji,

vitongoji na Mitaa inakamilishwa ili iweze kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kwa mujibu wa sheria za nchi yetu.

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza, kwanza naomba nishukuru kwa majibu yaliyotolewa na Serikali yanatoa matumaini kidogo ingawaje yamekuwa ya jumla sana.

Kwa kuwa, leo ni tarehe 28 zimebaki siku mbili mwezi huu kwisha na kwa kuwa Serikali imesema itamaliza mchakato na kukamilisha zoezi hili siku mwezi Aprili mwaka huu, mimi naomba nikubaliane kuvuta subira kwa kuwa zimebaki siku mbili.

Kwa kuwa vijiji vikipitishwa vitaleta mabadiliko katika maeneo ya utawala wa Kata na kwa kuwa maeneo ya Kata yatabadilika na kuleta tofauti katika utawala wa tarafa.

Je, katika tangazo la Serikali tutegemee vile vile kwamba kutakuwa na mabadiliko katika maeneo ya utawala katika Kata.

Kwa kuwa Wilaya yetu ya Kishapu ni kubwa sana ikiwa na vijiji kama 103 naamini vijiji hivi 23 vinaweza kupitishwa ikawa ni Wilaya yenye Vijiji 126, hauoni kwamba upo umuhimu mkubwa sana kuligawa Jimbo la Kishapu kabla ya uchaguzi wa mwaka 2010?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu ni uchaguzi wa Serikali za Mitaa na tukisema Serikali za Mitaa tunaanzia ngazi ya vijiji, vitongoji pamoja na Mitaa, kwa hiyo tangazo la Serikali litatoa majina ya vijiji, vitongoji pamoja na mitaa, suala la Kata litatolewa miezi sita kabla ya uchaguzi Mkuu. Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira tuende kisheria na kanuni ambazo tumejiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti kuhusu suala la pili la uanzishwaji wa maeneo mapya kuhusu kuligawa Jimbo la Kishapu, suala hili lipo mikononi mwa Tume ya Uchaguzi na naomba Mheshimiwa Mbunge angelielekeza hilo upande wa Tume ya Uchaguzi ya Taifa ili waone kwamba kuna uwezekano wa kuyagawa hayo maeneo au hakuna uwezekano. Mimi Ofisi yangu inashughulika na Vijiji, Vitongoji pamoja na Mitaa.

**MHE. DR. GUINDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, kuna baadhi ya vijiji ambavyo vimekwisha kamilisha hatua zote ambazo ni pamoja na kuteua Wenyeviti wa Vijiji. Vilevile na wale watendaji wa Vijiji lakini vijiji hivyo vimekuwa vikiendelea bila ya kupata namba ya Vijiji;

Je, Waziri anaweza kueleza kwamba hiyo hatua itakamilika lini kwani kwangu pia kuna vijiji vya namna hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wenyeviti wa vijiji, vitongoji na Kata hawateuliwi bali wanachaguliwa na wananchi.

Naomba nimpe sahihisho ili aone kwamba kama wameteuliwa, wameteuliwa isivyo halali, na kwa vile vijiji ambavyo tunaviita vijiji bubu ambavyo haviko kwenye GN kwa mwaka huu vyote tumevihalalisha ili viwe vijiji kamili ili wananchi waweze kuwachagua Wenyeviti wao pamoja na Kamati zinazohusika.

Na. 69

### **Biashara ya Hewa Mkaa**

**MHE. COSTOR R. LIGALLAMA** aliuliza:-

Kwa kuwa, chini ya mkataba wa Kyoto palianzishwa mpango wa *Clean Development Mechanism (CDM)* ikihusisha biashara ya Hewa Mkaa:-

(a) Je, biashara hii ya Hewa Mkaa inaratibiwa vipi na Ofisi ya Makamu wa Rais kitengo cha Mazingira ya Maliasili na Utalii?

(b) Je, ni hatua zipi zinatakiwa kutekelezwa na vijiji vya Wilaya ya Kilombero na vingine katika nchi hii katika mpango wa kulipwa fedha kutokana na kuhifadhi misitu na hivyo kufidia hewa mkaa inayozaliswa na nchi zenye viwanda vingi na vikubwa duniani chini ya Mkataba wa Kyoto?

(c) Je, wananchi wa Tanzania wana ufahamu wowote wa kutosha juu ya biashara hiyo ambayo inaweza ikawa motisha au kichocheo kwa suala zima la uhifadhi wa mazingira?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Castor Ligallama, Mbunge wa Kilombero, lenye sehemu (a), (b), (c) kama ifuatavyo:-

(a) Biashara ya hewa mkaa ni sehemu ya juhudi za nchi zilizoridhia Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi. Na ule wa Kyoto kupunguza gesijoto zinazosababisha mabadiliko ya Tabianchi.

Chini ya Mkataba wa Kyoto, nchi zilizoendelea zinatakiwa kupunguza viwango vyao vya uzalishaji gesijoto kwa angalau asilimia tano kulingana na viwango vyao vya mwaka 1990.

Hivyo basi kwa mujibu wa sheria ya usimamizi wa Mazingira sura 191 Ibara ya 75, Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira ndiyo Mratibu wa shughuli zote za mabadiliko ya tabianchi kitaifa. Katika kuratibu biashara ya hewa mkaa, Ofisi ya

Makamu ya Rais inaandaa taratibu na miongozo yenye vigezo na masharti ya kushiriki katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa. Miongozo hii imesambazwa kwa wadau mbalimbali nchini.

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais imeunda Kamati ya Kitaifa inayohusisha sekta zote ili kupitia na kushauri kabla ya kupitisha miradi ya kupunguza ama kunyonya gesijoto. Uratibu huo pia hutekelezwa kupitia maafisa mazingira walioteuliwa katika kila sekta.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kijiji kiweze kufaidika na mpango wa kulipwa fedha kutokana na kuhifadhi misitu ni muhimu kuandaa mradi unaolenga kuhifadhi misitu hiyo ndani ya eneo lake. Aidha, vijiji vinaweza kushirikiana na AZAKI pamoja na vyama vya kiraia kuandaa miradi ya aina hii, katika kuandaa mradi hatua zifuatazo zinatakiwa:-

(i) Kijiji kiwe na eneo lisilopungua hekta 500 hadi 1500. msitu katika eneo kama hilo huweza kunyonya kati ya tani 8000 na 16,000 za hewa mkaa kwa mwaka. Na hii inaweza kukiingizia kijiji ama Halmashauri kati ya dola za Marekani 80,000 hadi 200,000 kwa mwaka (kama tani moja ya *carbon credits* itanunuliwa kwa dola kumi.

(ii) Kuhakikisha kuwa eneo la msitu linakamilikiwa kisheria;

(iii) Kupata watalaam wa kupima kiasi cha hewa mkaa kinachoweza kupatikana katika eneo hilo; na

(iv) Kutafuta soko la *carbon credits*.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi walio wengi hawajawa na ufahamu wa kutosha kuhusu biashara ya hewa mkaa. Hii ni kwa sababu suala zima la mabadiliko ya tabianchi ni geni sana na halijaeleweka vema kwa wananchi

Juhudi mbalimbali za kuelimisha umma zimekuwa zinafanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na wadau wengine kwa lengo la kukuza weledi wa wananchi katika ngazi zote kuhusiana na suala la mabadiliko ya tabianchi pamoja na fursa za biashara ya hewa mkaa inafahamika.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Waziri ambayo ametoa elimu kubwa kwa Watanzania wengi juu ya biashara hii nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa, nchi yetu ni maskini na watu wake ni maskini kwa nini zinapotokea fursa hizi za kimataifa tunakuwa wa mwisho kuchangamkia. Je, Waziri hajui kwamba ujanja ni kuwahi na kupata, kwani nchi jirani kama Kenya wamefanya hivi na wamepata, biashara ya *AGOA* wamefanya hivi na wamepata. (*Kicheko*)

(b)Kwa kuwa, katika Wilaya yangu ya Kilombero, kuna Kampuni kutoka nchi jirani ya *Green Resources* ambayo wamepewa hekta nyingi za ardhi na wanalima miti na wao kwa uhakika wanapata fedha kutokana na biashara hii ya hewa mkaa, Je, wanakijiji ambao wameiga na wameshiriki katika kilimo hiki cha miti watalipwa fedha hizo kutokana na kutokujua. Je, wanaweza kulipwa hata fidia?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MAZINGIRA:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana kwa swali hili ambalo kwa kweli linatupa fursa ya kuelezea umma wa Watanzania maana na jinsi ya kuchukua fursa hii ya kuingia katika biashara hii ya gesi mkaa.

Lakini pia mwaka huu ni mwaka ambao Umoja wa Mataifa umetangaza kwamba ni mwaka wa mabadiliko ya tabianchi na katika siku ya Mazingira mwaka huu tutazungumzia masuala haya haya ya mabadiliko ya mabadiliko ya tabianchi na katika moja ya hatua ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi ni kushiriki katika biashara hii ya gesi mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania hatujachelewa kwa kweli katika nchi za Afrika zilizofanya vizuri ni pamoja na Tanzania na sisi ndiyo wa kwanza katika miradi na sasa tuna miradi kumi na mbili ambayo itashiriki chini ya mpango wa *Clean Development Mechanism* na mradi wa kwanza ni ule mradi wa kutengeneza gesi unaotokana na taka wa Mtoni katika Wilaya ya Ilala lakini tuna miradi kumi na mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana ya mradi ule wa *green resources* swali la pili si kweli kwamba wameshaanza kulipwa, katika utaratibu wa kuuza gesi mkaa kupitia utaratibu wa misitu ni nchi ya Brazil peke yake ambayo imekwishaanza kupata manufaa hayo, na sisi Tanzania tumesaini Mkataba wa makubaliano na nchi ya Norway na tuna fedha takribani dola milioni mia moja ambazo tunaingia mkataba na kushirikisha taasisi za kijamii, kushirikisha Halmashauri na sekta zetu za umma kuweza kuwa na miradi ya kijamii na kweza kuibua fursa za kutumia misitu yetu ili kuweza kushiriki katika biashara hii ya mkaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo Tanzania tunafanya vizuri msiwe na wasi wasi na tutaendelea kufanya vizuri zaidi.

Na. 70

### **Bunge Kueleza juu ya Gawio la Fedha kwa SMZ**

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika miaka ya nyuma Bunge limekuwa likielezwa juu ya uimara wa ushirikiano wa kiuchumi kwa pande zote za Muungano kwa mfano juu ya idadi ya fedha za gawio la asilimia 4.5 kwa SMZ ambapo kwa mwaka 2007/2009 ilikuwa shilingi 27,338,623,000/=.

- (a) Je, kwa nini mwaka huu haikuelekezwa idadi ya fedha hizo kama inavyofanyika kila mwaka?
- (b) Je, Serikali itakubaliana nami kwamba kutamkwa kwa kima cha fedha hizo ndani ya Bunge na ndani ya Baraza La Wawakilishi (BLW), Zanzibar, kunatoa elimu muafaka ya maana na umuhimu wa Muungano?
- (c) Je, kutotamkwa kwa idadi ya fedha hizo sasa litakuwa ni jambo la kudumu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO**  
alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Viti Maalum, lenye vipengele (a),( b), na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli kwamba katika hotuba yangu ya Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2008/2009 kiasi cha fedha za gawio kwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hakikutajwa wazi. Hata hivyo katika ukurasa wa 99 wa kitabu cha hotuba hiyo, ziliombwa jumla ya shilingi 55,205,678,400/= kwa fungu 31 ambapo kati ya fedha hizo shilingi 23,040,964,000/= zilitengwa na kuidhinishwa na Bunge kama gawio la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kutoka kwa wafadhili kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

(b) Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba kutamkwa kwa kima cha fedha za gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndani ya Bunge na ndani ya BLW si tu kwamba kunatokea elimu mwafaka kwa maana ya umuhimu wa Muungano bali pia kunadhihirisha umuhimu wa Muungano huu katika masuala ya kukuza na kuendeleza uchumi wa Taifa letu.

(c) Suala la kulijulisha Bunge kiasi cha fedha za gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni la kudumu na litakuwa likifanyika kila mwaka wakati wa Bunge la Bajeti.

**MHE. MOHAMMED RAJAB SOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri; kuweka sawa masuala ya Muungano haoni vema ushiriki wa viongozi wakuu wa Nchi hii kuahidi kutekeleza masuala ambayo ni ya kijamii yatauweka vizuri Muungano wetu?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Soud mia juu ya mia.(kicheko/Makofi)

Na. 71

**Upungufu wa Watumishi wa Afya Nchini**

**MHE. PASCHAL C. DEGERA** aliuliza:-

Kwa kuwa, hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa watumishi wa afya nchini na kwamba hali hiyo inasababisha utoaji wa huduma za afya kukwama.

Je, Serikali inachukua hatua gani za uhakika kuondoa tatizo hili?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paschal Costantine Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama Ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa kuna upungufu mkubwa wa watumishi wa afya nchini. Hali hii inasababisha upatikanaji wa huduma za afya kuwa katika kiwango cha chini.

Kwa kuliona hilo Serikali ya awamu ya nne kupitia Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ilianzisha mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM). Madhumuni ya mpango huu ni kuboresha utoaji na upatikanaji wa huduma za afya nchini kwa kuwa na zahanati katika kila kijiji kituo cha afya kila kata na kuziimarisha hospitali za Wilaya na Mikoa. Baadhi ya mikakati ya utekelezaji wa mpango wa MMAM ni pamoja na:-

(i) Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya afya nchini kwa kuongeza idadi ya vyuo na udahili wa wanafunzi. Tangu kuanza kwa utekelezaji wa mpango huu, idadi ya udahili wa wanafunzi imeongezeka kutoka 1,013 mwaka 2006 hadi kufikia 3,831 mwaka 2008. Matarajio ni kwamba idadi ya wadhiliwa itaongezeka mwaka hadi mwaka.

(ii) Kupunguza muda wa mafunzo bila kuathiri ubora wa mafunzo husika ili kuzalisha watalamu wengi na kwa muda mfupi. Mfano muda wa mafunzo ya uuguzi ngazi ya cheti umepunguzwa kutoka miaka mitatu hadi miaka miwili. Aidha, muda wa mafunzo ya uuguzi ya Stashahada umepunguzwa kutoka miaka minne hadi miaka mitatu.

(iii) Kuongeza mafunzo ya kada mpya za Tabibu Wasaidizi *Clinical Assistants* ambao baada ya kuhitimu watafanyakazi kwenye zahanati.

(iv) Serikali imelenga masharti ya ajira kwa watumishi wa afya ambapo sasa wanaajiriwa bila kufanyiwa usaili. Kwa kuzingatia utaratibu huo, Wizara inawapangia vituo vya kazi wahitimu wote wa kada mbali mbali za afya ili kwenda kufanya kazi kwenye Sekretariati za Mikoa, Halmashauri za Manispaa, Miji na Wilaya. Katika kipindi cha 2006/2008 jumla ya watumishi 11,748 wamepangiwa vituo vya kazi.



(v) Serikali inashirikiana na taasisi isiyo ya kiserikali ya Benjamin William Mkapa *HIV/AIDS Foundation* kuajiri watumishi wa afya kwa ajili ya kwenda kufanya kazi kwenye vituo visivyofikika au kukalika kwa urahisi.

Mpaka sasa jumla ya watumishi 275 wameajiri kupitia taasisi hiyo na wamepangwa kufanya kazi kwenye Halmashauri za Wilaya mbalimbali nchini

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niongeze swali la nyongeza,

(1)Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jibu la Naibu Waziri la msingi amesema katika kipindi cha mwaka 2006/2008 watumishi wa afya 11, 748 nataka kufahamu Wilaya ya Kondoa walipangwa wangapi?

(2)Kupitia mpango wa MMAM Wizara inategemea kumaliza lini tatizo la upungufu wa watumishi wa afya nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nimesema kwamba Watumishi 11,748 wamepangiwa vituo kati ya 2006/2008, si rahisi kusema Kondoa wamepangiwa watumishi wangapi kwa sababu itakuwa ni vigumu mimi kukariri Halmashauri zote kujua kwamba kila Halmashauri imepangiwa Watumishi wangapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakachokisema ni kwamba kama anataka kujua kuanzia mwaka 2006/2008 basi mimi nitamfanyia *print out* ambayo nitampatia aweze kuona ni watumishi wangapi wamepangwa Kondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti swali la pili kama nilivyosema katika jibu la msingi, Serikali inajitahidi kuweza kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanaweza kupatikana na wanaweza kutumwa katika maeneo tofauti.

Hivyo bado nasisitiza kwamba kutumia mikakati hii tunajitahidi ili wanafunzi waweze kudahiliwa na tupate watalaamu wa kutosha ili waweze kukidhi haja na mahitaji katika Tanzania nzima.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kuniruhusu kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Naibu Waziri amekiri kuwa Wizara ya Afya kuna upungufu mkubwa wa Watumishi na kwa kuwa Serikali sasa hivi ina mchakato mkubwa sana wa kuanzisha zahanati katika kila kijiji.

Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba utakapoanza mchakato huu utasababisha huduma duni zaidi kuliko sasa hivi?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) ni mpango wa miaka kumi na sikubaliani na wewe kwamba kuongeza zahanati kila Kijiji, na vituo vya afya kila Kata na kuboresha hospitali zetu za Mikoa na Wilaya kwamba tutazorotesha ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati niliyoizungumzia ni kuhakikisha kwamba tunaongeza watalaamu wa kutosha na kwa sababu ni mpango wa miaka kumi mimi nina imani kwa sababu tumefanyia utafiti hakutakuwa na kuzorota kwa kazi bali tutakuwa tunaboresha kazi na kutoa huduma za afya kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge Merce na Waheshimiwa Wabunge wote msiwe na wasiwasi, Wizara ya Afya iko madhubiti na Serikali yetu ina mpango muhimu ili kuhakikisha kwamba huduma zinaboreka.

Na. 72

### **Serikali Kutoa Chakula kwa Wananchi wa Mpwapwa**

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE** aliuliza:-

Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla wanakabiliwa na tatizo kubwa la upungufu wa chakula kutokana na ukame uliosababishwa na kukosekana kwa mvua za kutosha; na kwa kuwa baadhi ya wananchi hao hawana chakula kabisa hivi sasa:-

Je, ni lini Serikali itatoa huduma ya chakula kwa wananchi hao hasa ikizingatiwa kuwa hivi karibuni Serikali ilitoa tamko kuwa, kuna akiba ya kutosha ya chakula na kwamba hakuna mwananchi atakayekufa kwa njaa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo:-

Wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika imekuwa ikifuatiliwa kwa karibu na kutathimini hali ya uzalishaji wa chakula nchini kwa kipindi chote cha msimu wa 2008/2009.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa George Malima Lubeleje, kuwa katika kipindi cha msimu huu wa uzalishaji wa mazao wa 2008/2009, maeneo mengi ya Mkoa wa Dodoma yamekabiliwa na upungufu wa mvua kwa vipindi mbalimbali hali inayoashiria kupungua kwa matarajio ya mavuno hivyo, upatikanaji usioridhisha wa chakula katika mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, mvua zilianza kunyesha katika maeneo mengi ya Mkoa wa Dodoma kati ya wiki ya tatu na ya nne ya mwezi Desemba, 2008. Hata hivyo, mvua

zimenyesha kwa mtawanyiko usioridhisha na kusababisha mazao ya chakula katika baadhi ya maeneo ya mkoa huo kama vile ya Wilaya ya Mpwapwa kunyauka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kufuatia mazao yaliyopandwa awali kunyauka, Serikali kupitia mfuko wa maafa ilitoa jumla ya shilingi milioni 595 kwa Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya ununuzi wa usambazaji wa jumla ya tani 350 za mbegu za mtama kwa wakulima katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Dodoma ikiwemo Wilaya ya Mpwapwa kwa ajili ya kurudia kupanda.

Hata hivyo, pamoja na hatua hiyo mwenendo wa mvua katika baadhi ya maeneo ya mkoa wa Dodoma bado haujawa mzuri japokuwa mvua inatazamiwa kuendelea kunyesha hadi mwishoni mwa mwezi Aprili, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, mwanzoni mwa mwezi Aprili, 2009, Wizara baada ya kushauriana na Ofisi ya Waziri ilipeleka wataalam katika mkoa huo ambao kwa kushirikiana na wataalam wa Wilaya ya Mpwapwa walifanya tathmini ya haraka ya hali ya chakula.

Tathmini hiyo ilionyesha kuwa jumla ya watu 10,987 au asilimia 6 ya watu katika maeneo yaliyofanyiwa tathmini wanakabiliwa na upungufu wa chakula na watahitaji kupatiwa tani 395.5 za chakula cha msaada kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia mwezi Mei, hadi Julai 2009. Kati ya watu hao jumla ya watu 2,237 watahitaji kupatiwa tani 80.5 za chakula cha bure na wengine 8,750 waliobaki watahitaji kupatiwa tani 315 za chakula cha bei nafuu ya shilingi 50 kwa kilo.

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei, 2009 Wizara itafanya tathmini ya awali ya hali ya chakula nchini Mpwapwa itakayotoa mwelekeo wa uzalishaji wa mazao ya chakula msimu wa 2008/2009. Aidha, tathmini hiyo itaainisha maeneo yanayotazamiwa kuwa na upungufu wa chakula katika mwaka 2009/2010.

Kutokana na tathmini hiyo, endapo itathibitika kuwa hali ya chakula katika Wilaya haitakuwa nzuri katika kipindi cha baada ya mwezi Julai, 2009 Serikali itachukua hatua muafaka kukabiliana na hali hiyo.

Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa George Malima Lubeleje kwa kufuatilia kwa umakini mkubwa maendeleo ya watu wa jimbo lake la Mpwapwa na Serikali iko tayari kushirikiana naye hasa kuhakikisha kwamba hakuna mwananchi atakayekufa kwa njaa. (*Makofi*)

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tunaishukuru Serikali, Wilaya ya Mpwapwa ilitewa mbegu tani 120 za mtama na eneo lililopandwa ni hekta 133 na kwa kuwa zaidi ya asilimia 75 ya eneo ambalo lilipandwa mtama, mimea ilinyauka na kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri anasema kwa Wilaya ya Mpwapwa ambayo ina karibu watu laki tatu ni watu 10,000 tu wana tatizo la chakula.

(a) Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba hiyo tathimini iliyofanyika haikuwa sahihi kwa sababu watu 10 ni sawa sawa na vijiji viwili tu vya Wilaya ya Mpwapwa?

(b) Kwa kuwa eneo la Mjini, Mji wa Mpwapwa kuna taasisi mbalimbali na kuna wakazi wa Mji wa Mpwapwa wapatao zaidi ya 60,000 na wanategemea kupata chakula kwenye soko la Mpwapwa na kuna upungufu wa chakula katika Vijiji. Je, Serikali itakapotuletea chakula cha msaada na cha bei nafuu, je, wananchi wa Mpwapwa Mjini nao watafikiriwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyosema kwamba mwezi ujao yaani keshokutwa tunaanza tathimini nyingine ambayo itakuwa inaonyesha hali halisi ya chakula.

Kwa hiyo, iwapo hali itagundulika tofauti na ilivyo hivi sasa na tathimini tulizonazo hivi sasa basi Serikali itachukua hatua kama inavyofanya maeneo ambayo yana njaa mengine. Lakini kama nilivyosema kwamba tumeshawatengea chakula kwa hiyo, ni jukumu lake Mheshimiwa Mbunge kufuatilia kuanzia keshokutwa mwezi wa tano kiweze kufika kwa wananchi wa Mpwapwa.

Suala la pili, kuhusu taasisi ambazo ziko Mjini Mpwapwa suala la ugawaji wa chakula na tathimini inatokana na Halmashauri ilivyoona ni maeneo gani yana njaa katika Halmashauri hiyo. Kwa hiyo, yeye kwa kuwa ni Mjumbe wa Kamati ya Madiwani katika Halmashauri ya Mpwapwa nadhani atatoa usharikiano mzuri kuonyesha maeneo hayo ambayo yatakuwa yanahitaji chakula kwa hiki ambacho kitakuja sasa hivi. (*Makofi*)

**MHE. JOHN S. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri ningependa nimwulize swali.

Kwa kuwa hali ya Mpwapwa ndiyo hali iliyoko katika Mkoa mzima wa Dodoma narudia ndiyo hali iliyopo katika Mkoa mzima wa Dodoma. Je, badala ya kufanya tathimini ya Mpwapwa tu na kuweka chakula cha haraka kwa ajili ya Mpwapwa tu, Waziri haoni umuhimu wa kuanza kugawa chakula hicho kilichopo cha haraka kwa Wilaya zote za Mkoa wa Dodoma na kufanya tathimini kwa Mkoa mzima badala ya Wilaya ya Mpwapwa peke yake?

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tathimini ambayo imeelezwa na Naibu Waziri, tena ufasaha mkubwa haikufanywa katika Wilaya ya Mpwapwa peke yake. Imefanywa katika Wilaya zote za Mkoa wa Dodoma na vile vile imefanywa katika Wilaya za Mikoa 12 nchini na tathimini hiyo imeonyesha ya kwamba kuna watu 780,000 katika maeneo mengi nchini ambao wanahitaji msaada wa chakula.

Serikali imetenga tani 28,000 katika muda wa miezi mitatu kwa ajili ya kusaidia wananchi katika maeneo yaliyokabiliwa na ukame. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa John S. Malecela kutupa muda ili tuweze kumpa takwimu za Wilaya zingine na chakula

kilichopo ili kuhakikisha ya kwamba wananchi wa Tanzania wanapata msaada wa chakula na kwamba hakuna Mtanzania atakayekufa kwa sababu Serikali inachukua hatua na iko makini kufanya hivyo. (*Makofi*)

**MHE. JOB Y. NDUGAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mwaka huu msimu huu wa kilimo pamekuwa na mvua kidogo sana katika Mkoa wa Dodoma na Mikoa mingine kiasi kwamba hata mtama ambao umegawanywa kama mbegu kwa wananchi na wenyewe umekauka hali ni mbaya sana. Mwaka huu ni mwaka wa baa la njaa. Tumejibu kutoka kwa Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba timu ya tathimini ilitumwa kwa mfano Mpwapwa ambako wameona kama watu 10,000 hivi ndiyo wenye shida ya njaa. Watu 10,000 ni kama kijiji kimoja. Je, haoni kwamba timu hizi za tathimini zinahitaji kuimarishwa ili walete tathimini halisi Serikali badala ya huu mchezo ambao unaendelea kwa jambo ambalo ni kubwa ambalo ni baa la taifa? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tathimini ziko nyingine na majibu yanatofautiana kati ya tathimini na tathimini na wakati wote Serikali itakuwa inahakikisha kwamba tathimini zinazotoka zina-reflect hali halisi ya maeneo hayo. (*Makofi*)

Na. 73

### **Upatikanaji wa Mbegu Bora za Mifugo**

**MHE. WILSON M. MASILINGI K.n.y. MHE. GOSBERT G. BLANDES** aliuliza:-

Kwa kuwa, wafugaji wa jimbo la Karagwe wanahangaika bila mafaniko kupata mbegu bora za kisasa za Ng'ombe, mbuzi, kondoo, kuku na samaki kwa lengo la kuwa na mifugo yenye tija ili kujiongezea kipato:-

Je, Serikali imejiandaa vipi kutatua tatizo hili haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mbunge wa Karagwe, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikitekeleza mikakati mbalimbali ya kuhakikisha kwamba mbegu bora zinapatikana kwa kuhimiza matumizi ya mbegu bora kwa njia ya uhimilishaji.

Kituo cha uhimilishaji cha Taifa (*NAIC*) kilichopo mkoani Arusha kimeongezewa idadi ya madume bora ya mbegu kutoka madume 23 mwaka 2007/2008 hadi kufikia 34 mwaka huu, mtambo mpya wa kutengeneza hewa baridi ya Nitrojeni wenye uwezo wa kuzalisha lita kumi za hewa hiyo kwa saa umenunuliwa.

Aidha, uwezo wa maabara umepanuliwa kwa kununua vifaa vya kisasa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa mbegu bora hadi kufikia dozi 100,000 kwa mwaka ikilinganishwa na uzalishaji wa awali wa dozi 65,000.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha usambazaji wa mbegu bora za ng'ombe wa maziwa na nyama, Serikali imeanzisha vituo vya kanda vya uhimilishaji katika kanda ya Ziwa (Mwanza) na Nyanda za Juu Kusini (Mbeya) Sanjari na kuimarisha kituo cha uhimilishaji cha Taifa/cha Kanda ya Kaskazini kilichoko Arusha. Katika mwaka 2008/2009 Wizara imepanga kuanzisha vituo vya uhimilishaji katika kanda ya Mashariki (Kibaha) na ya kati (Dodoma).

Mheshimiwa Spika, katika kanda ya Ziwa tayari mtambo wa kuzalisha hewa baridi ya Nitrojeni wenye uwezo wa kuzalisha lita tano kwa saa, mitungi ya kuhifadhi mbegu bora na vifaa vingine mbalimbali vya uhimilishaji vimewekwa katika kituo cha kuchunguza maradhi ya mifugo Mwanza kwa ajili ya kutoa huduma katika Wilaya za Kanda ya Ziwa ikiwemo Karagwe. Wizara inatoa wito kwa Halmashauri zote nchini ikiwemo Halmashauri ya Karagwe kuweka mipango ya uhimilishaji katika mipango yao ya maendeleo ya mifugo.

Mheshimiwa Spika, mbali na utafiti wa mbegu bora katika Kituo cha Mpwapwa Wizara inaendelea kusimamia Shamba la Kitulo lililopo wilayani Makete (Iringa), linalozalisha mitamba ya maziwa aina ya *Friesian*, Ngerengere (Morogoro), Mabuki (Mwanza), *Sao Hill* (Iringa) na Nangaramo Wilayani Nanyumbu (Mtwara) yanayozalisha Mitamba Chotara ya maziwa nguruwe na mbuzi bora wa nyama.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mbegu bora za kuku, Serikali imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuanzisha vituo vya kutotolea vifaranga wa mayai na nyama kwa ajili ya kusambaza mbegu bora za kuku kwa wafugaji.

Hivi sasa vipo vituo kumi na viwili vya kutotoa na kusambaza vifaranga hapa nchini vya *Interchick Ltd (Dar es Salaam)*, *Euro Poultry (Dar es Salaam)*, *Kibaha Education Centre (Kibaha)*, *Ruvu JKT (Kibaha)*, *Mkuza Chicks (Kibaha)*, *Ideal Chicks (Dar es Salaam)*, *Arusha Poultry Farm (Arusha)*, *Kibo Poultry Farm (Kilimanjaro)*, *Matembwe Poultry (Ruvuma)*, *Mwanza Hatchery (Mwanza)* *Iringa Hatchery (Iringa)* na *Kiluvya Poultry (Dar es Salaam)*. Hivyo namshauri Mheshimiwa Mbunge kuwajulisha wafugaji wa Karagwe wanaohitaji mbegu bora za mifugo kutoka mashamba ya Serikali kuwasilisha na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi na wale wanaohitaji mbegu za kuku bora kuwasiliana na vituo vya kutotolea vifaranga kupitia Halmashauri zao za Wilaya.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Serikali inafanyakazi nzuri sana kama ilivyodhihirishwa na jibu kwa swali la msingi kwamba utafiti mkubwa umefanyika katika maeneo kadhaa, Iringa, Arusha, Mwanza na Karagwe ni mbali sana huko ni karibu na Uganda na Jimbo la Muleba Kusini linapatikana na Karagwe. (*Makofi*)

Je, Serikali itapokea ushauri wangu kwamba swali la Mheshimiwa Mbunge Gosbert G. Blandes imchukuliwe ndiyo mawaliano kati ya wananchi wa Karagwe na Serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi ili kusiwepo tena kuwajibika kwa Mbunge kurudi tena kuwasiliana na Halmashauri na wafugaji ili waweze kuwasiliana na Wizara ili mashirikiano mazuri yaliyopo kati ya Mheshimiwa Naibu Waziri na Mheshimiwa Blandes yaweze kuimarika zaidi?

**MWENYEKITI:** Majibu hasa suala zima la kuweka mahusiano yawe karibu zaidi na Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema katika swali la msingi ni kwamba Wizara yetu iko tayari kuweka mahusiano na Wilaya zote za Tanzania ili kuhakikisha kwamba mbegu hizi zinapatikana.

Tunachokifanya sasa hivi katika Kituo cha *NAIC* tunakaribisha wataalam kutoka Wilaya ambao watakwenda kule Arusha na kujifunza na baada ya kujifunza sasa wanaweza kuwa na mitungi yao kule Wilayani ambao wanaweza kwenda nao wakapata mbegu bora kule kama ni Mwanza kwa walio kanda ya ziwa na kule Mbeya ambao wako katika kanda za nyanda za juu Kusini na hivi karibuni tutaweka mitambo tena Kibaha. Kwa hiyo, watu walioko sehemu za Pwani wanaweza kuipata. Dodoma napo tunatarajia kuweka na kule Arusha mbegu zinapatikana kwa hiyo mahusiano Wizara yangu inaweka mahusiana mazuri tu na kila Wilaya hapa nchini, zikiwemo hizo za Karagwe Muleba.

**MHE. MOHAMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa suala hili la kuhangaika kwa wananchi wa Karagwe ni sawa na wananchi wa Jimbo langu la Mkanyageni na Pemba yote kwa ujumla. Na kwa kuwa tumeziona juhudi za Serikali katika mifugo hasa ng'ombe, kuku lakini hatujaona juhudi za Serikali katika samaki. Na kwa kuwa Wizara hii imeunganishwa mifugo na uvuvi ili kunyanyua hawa wavuvi wa visiwa vyote pamoja na ukanda wote wa Pwani.

Na kwa kuwa hivi sasa kuna mipango mingi sana ya ufugaji wa samaki baharini pamoja na Lulu. Je, Wizara yako imefanya nini ili kuhakikisha kunyanyua maisha ya wananchi katika suala la ufugaji wa samaki baharini pamoja na Lulu? Je, kama imeanza ina mipango hiyo itafanya kwa Visiwani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri jibu swali moja tu, kwa maswali ya nyongeza hayaruhusiwi mawili. Kwa hiyo, utajibu moja katika ya hayo. Kuhusiano na kitoweo cha samaki.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba samaki wanaendelea kupungua tukichukulia kama ziwa Victoria Sangara wamepungua kutoka tani 750,000 kwa miaka mitatu na sasa hivi kuna tani 27000. bila kuchukua hatua za hatari wananchi watakuwa hawana samaki. Kwa hiyo, Wizara yangu imeanzisha kurugenzi ku-*culture* ambayo kazi yake ni ufugaji wa samaki na hii itahimiza kwa wananchi kufuga samaki na viranga tutakuwa tunavitoea

kwa mfano hapo Kingulwila tunavyo vifaranga. Kwa hiyo, tunalitambua hilo na kama itahitajika kufanya kazi hiyo Pemba na Zanzibar sisi tutashirikiana na Wizara ya Kilimo na Mifugo ili tuweze kufanya kama tunavyoshirikiana katika kazi *deep sea fishing authority*. Kwa hiyo, hatuna matatizo ni kazi tu ya kuwa na mawasiliano na kuanza ushirikiano.

Na. 74

### **NJIWA KUTAGA MAYAI MAWILI**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. HAROUB SAID MASOUD)**  
aliuliza:-

Kwa kuwa wafugaji wengi wa ndege aina ya Njiwa wamegundua kuwa mara nyingi ndege hao hutaga mayai mawili tu:-

- (a) Je, ni njiwa wote hutaga mayao mawili?
- (b) Kama jawabu ni ndiyo, je, nini kinachosababisha watage mayai mawili tu?
- (c) Kama sio njiwa wote hutaga hivyo, je, wafugaji hao wafanye nini ili njiwa hao nao watage zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Harobu Said Masoud, Mbunge wa Koani, lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa njiwa wote hutaga mayai mawili tu katika mzunguko mmoja wa utagaji. Hii inatokana na mfumo wao wa uzazi kama Mwenyezi Mungu alivyowaumba. (*Makofi/Kicheko*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mngetulia inawezekana Mheshimiwa Diana Chilolo ameachia swali la nyongeza na mwenye swali. (*Kicheko*)

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili iweze kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri lina ujumla sana; na kwa kuwa hata binadamu wapo akinamama ambao huwa wanakosa uzazi, lakini anafanyiwa utafiti wa kitaalam na madaktari hatimaye anazaa. Je, Serikali haiwezi kufanya utafiti wa kitaalam kuhusu njiwa ili kuona uwezekano wa kutaga mayai zaidi ya mawili? (*Makofi/Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kujibu swali hili kiutaalam sasa. Tumeona kwamba



njiwa mara nyingi huzaliwa wa kike na wa kiume. Sasa kinachotokea pale kitaalam kuna *theory* mbili. La kwanza, ni kwamba mtu anapokuwa ni wa kiume huwa lazima apokee *chromosome* ya X na Y, na hivyo inayoonekana katika *theory* hii ni kwamba yule njiwa wa kiume huwa anatoa *sperm* za aina mbili ambazo ni X na Y ambazo ni mbili tu zinapoenda kufanya *fertilization* moja ina *pare* ya kike ambayo ni X, X, anatoa njiwa wa kike. Halafu na ile ya Y ina *bear* na X, Y na kutoa ya kiume. Kwa hiyo, inaonekana *theory* ndivyo zilivyo. Lakini vilevile hata yule wa kike naye inawezekana *ovary* zinatoa mayai mawili tu yenye X X.

Kwa hiyo, anapokuja kukutana na huyu wa kiume ndiyo lazima wazae wa kiume na kike. Lakini kama utafanya *artificial insemination* huchukua mayai ya njiwa nyingine, ukaenda ukaongeza mawili katika uzazi ule yanaweza yaka-*fertilize* ukapata hata kumi, lakini hii *artificial insemination* lakini walivyoubwa hawa ni kwamba njiwa huzaliwa wawili na hivyo ni kwamba X and Y ndiyo zinatoka kwa kiume na kupelekwa ku-*fertilize* XX za kike. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba tuelewane swali la nyongeza mhusika anayetaka atasimama wakati wa mwanzo na si baada ya kukolezwa na majibu. (*Kicheko*)

Na. 75

### **Ahadi ya Kujenga Vyuo vya VETA kila Mkoa**

**MHE. FATMA A. MIKIDADI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilishatoa ahadi Bungeni ya kujenga Chuo cha *VETA* Mkoani Lindi; na kwa kuwa ni sera ya Taifa kuwa na vyuo vya *VETA* katika kila Mkoa na hatimaye Wilayani.

(a) Je, ahadi hiyo itatekelezwa lini?

(b) Je, ni Mikoa mingapi bado haijajengewa vyuo vya *VETA* na kwa nini?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi kutoka Jamhuri ya Korea alikabidhiwa rasmi maeneo yote ya ujenzi mwezi Agosti na Septemba, 2008 na alitakiwa kuanza kazi mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshafanya mawasiliano na Ubalizi wa Korea kuhusiana na kuchelewa kwa kuanza kazi ya ujenzi wa Vyuo vya VETA. Mkandarasi ameahidi kwa maandishi kuwa ujenzi utanza mara moja tarehe mwezi Mei, 2009.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ambayo ilikuwa haijajengwa vyuo vya VETA ni mitatu ambayo ni Pwani, Manyara na Lindi. Hii ilitokana na ukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya watu wa Korea fedha imepatikana kwa ajili ya ujenzi wa vyuo hivyo vya VETA. *(Makofi)*

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Naibu Waziri. Kutokana na majibu haya inaelezwa kwamba kulikosekana na fedha za ujenzi na ndiyo maana Mkoa wa Lindi haukupata VETA.

Lakini kwa taarifa nilizokuwa nazo ni kwamba kuna baadhi tayari walikwishaanza kujengwa vyuo vya VETA kabla ya Mkoani. Je, ilikuwaje wao wakaanza Wilayani kujengwa kabla ya Mikoani? Naomba nifahamishwe.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kama kigezo ilikuwa ni Mikoa kwanza, ilikuwaje Wilaya kabla ya Mkoa wa Lindi.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENTIA M. KABAKA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Fatma Mikidadi kwa ufuatiliaji wake wa karibu wa ujenzi wa Chuo hiki cha VETA cha Mkoa wa Lindi.

Lakini pia naomba nimwarifu kwamba hizi zilikuwa programu mbili *source* ya fedha ni tofauti. Kwa hiyo, hakuna uhusiano kati ya Vyuo vya VETA vya Wilaya ambavyo vitaanza ambavyo tutakuwa tumevijenga ifikapo mwaka 2010 kama ilivyo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi na ujenzi wa Vyuo hivi vya Mkoa. Itosheke tu kuridhika kwamba Chuo chake katika Mkoa wake kitaanza kujengwa mwezi Mei na Mkoa wa Lindi sherehe ya kuanza ujenzi itafanyika katika Mkoa ule. *(Makofi)*

**MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona, kwa kuwa mchakato wa ujenzi wa chuo hiki ulianza tokea mwaka 2003 na ukakamilika 2004, hapo katikati hatujui kitu gani kilikuwa kinatokea mpaka jengo hili limechelewa ujenzi wake.

Je, Serikali imejiandaa kama mkandarasi huyu mwezi Mei, akiamua kuchelewa tena bila kutoa sababu kuchukua namna nyingine ya kuweza chuo hiki kujengwa ili na sisi watu Lindi tukakomboka?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. GAUDENSIA M. KABAKA):** Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mudhihir kwamba

sasa hivi ndugu zetu wa Korea pamoja na mkandaras kutoka Korea wamefanya kwa kiingereza tunaita *commitment* ya kuanza ujenzi wa chuo hiki naomba tusahau yaliyotokea huko nyuma wote tunajua kwamba kabla ya ujenzi kuna maandalizi makubwa ikiwemo kutafuta pesa. Lakini sasa vyuo hivi vitatu vinaanza kujengwa na naomba uamini kwa sababu tayari tuna *commitment* ya wananchi wa Korea na *contractor*.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante kwa kunipa ili niulize swali dogo la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ili suala la kuanzisha vyuo vya *VETA* kila wilaya limetamkwa ndani ya ilani ya Chama cha Mapinduzi, na kwa kuwa zipo wilaya ambapo tayari wadau wameshajitokeza na wameanzisha vyuo vya *VETA* bila kupitia Serikali mfano mzuri kile chuo cha Songela kilichopo kata ya Ulemo Jimbo la Iramba Magharibi.

Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje wapo tayari kushirikiana na huyu mdau aliyeanzisha hicho chuo cha Songela pale Ulemo katika kukiendeleza?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI – MHE. GAUDENSIA M. KABAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunawapongeza sana watu binafsi wanaoisaidia Serikali kujenga mashule, kujenga vyuo vya *VETA* na taasisi nyingine za kielimu pamoja na taasisi zingine za kuleta maendeleo. Vyuo vya *VETA* binafsi vinavyojengwa na wananchi vyote vinasajiliwa chini ya Wizara ya Elimu na mafunzo ya ufundi kwa kupitia *VETA*, kwa hiyo wanapokuwa wamemaliza ikihitajika msaa kwa mfano wa vifaa sisi tuko tayari kusaidiana nao na wakati ambapo tulipokuwa tunafanya survey kujua ni wilaya zipi hazina vyuo vya *VETA* tuliondoa vile ambavyo tayari vinavyuo vya watu binafsi kwa sababu tayari Serikali inaweza kusaidia na wale binafsi kuendesha vile vyuo.

**MHE. FAIDA M. BAKAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante sana Mwenyekiti, kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza, kwa kuwa elimu itolewa na vyuo hivi vya *VETA* ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii na kwa kuwa inaonekana kwamba vijana wa kiume ndio zaidi ambao wanajiunga na vyuo hivi. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati muafaka wa kuhamasisha vijana wa kike nao kujiunga na vyuo vya *VETA* ili kujiletea maendeleo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba nimpongeze Mheshimiwa Faida Bakar, kwa mawazo yake ya kuona kwamba kuna umuhimu wa kuwahimiza vijana wa kike kujiunga na vyuo vya *VETA*. Na ndio hivyo tunavyofanya na tuko tayari kufanya hivyo.

Na. 76

### Uwiano wa Shule za Sekondari Wilayani Mufindi

**MHE. BENITO W. MALANGALILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Mufindi ina shule za sekondari zaidi ya arobaini na kati ya hizo ni shule tatu tu ndizo zina kidato cha tano na sita:-

(a) Je, Uwiano huo ni sawa?

(b) Kwa kuwa na Mbunge wa Jimbo hilo aliwahi kupendekeza kuwa shule kama za Mgololo, Igowole, Itengule, Sadani na Mdahulo zipewe kibali cha kuwa na vidato vya tano na sita. Je, Serikali inasemaje juu ya pendekezo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA ) alijibu:-**

Kwa niaba ya Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa William Benito Malangalila, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya elimu na mafunzo ya ufundi ya mwaka 1995 haitoi mwongozo wa kuanzisha shule za kidato cha tano na sita kwa kuangalia uwiano wa shule za kidato cha tano na sita na idadi ya shule za kidato cha 1 hadi 4 zilizopo katika Wilaya.

Hata hivyo ni azma ya Serikali kuona kwamba kila tarafa inaanzisha shule moja ya kidato cha tano na sita ili kutoa fursa kwa wanafunzi wengi wenye sifa za kujiunga na kidato cha tano na sita baada ya kufaulu mitihani ya kidato cha nne.

(b)Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la kuzifanya shule za sekondari za Mgololo, Igowole, Itengule, Sadani na Mdabulo kuwa na vidato vya tano na sita, lilifanyiwa kazi na Wizara yangu na shule ya Igowole ilipewa kibali cha kuanzisha kidato cha tano mwezi Mei, 2008. Shule zilizobakia hazikukidhi vigezo vya msingi vinavyotakiwa ili ziweze kuanza kidato cha Tano.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nifanye sahihisho dogo kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Mimi naitwa Benito William Malangalila.

**MWENYEKITI:** Masahihisho yamezingatiwa, endelea.

**MHE. BENITO W. MALANGALILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niishukuru sana Serikali kwamba imesema hizi shule nilizozitaja hazikupewa usajili kwasababu hazikukidhi vigezo. Sasa naomba atuelekeze ni vigezo gani ambavyo hazikukidhi ili mara tu zitakapokidhi vigezo hivyo ziweze kusajiliwa kuwa shule za kidato cha tano na sita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Shule ya Igowole ni kweli ilianzisha kidato cha tano lakini ilikuwa ni kwa wasichana tu. sasa ili shule iwe na kidato cha tano nadhani iwe na wasichana na wavulana kama sisi wenyeji wa Mufindi tulivyojenga

kidato cha kwanza hadi cha nne kwa wasichana na wavulana. Sasa shule hii ya Igowole itachukua wanafunzi wa kidato cha tano wanaume na wasichana?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa elimu na Mafunzo ya Ufundi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Benito Malangalila, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo ili shule iweze kupewa hadhi ya kuwa kidato cha tano ni kama ifuatavyo: Wizara imeweka vigezo muhimu vya kuzingatia. Kwanza ni vyumba vya madarasa vya kutosha wanafunzi wote, jengo la utawala, jengo la maabara au majengo vyumba vitatu vya maabara kwa shule zenye mchepuo wa Sayansi. Maktaba yenye samani na matumizi ya wanafunzi 40 kwa wakati mmoja. Mabweni ya kutosheleza wanafunzi wote, vitanda, mashubaka, kabati, maliwato na mafulio. Ukumbi wa chakula, jiko na vifaa muhimu vya kupikia.

Mheshimiwa mwenyekiti, vigezo vingine ni nyumba za walimu, nyumba ya mlezi, viwanja vya michezo na uwepo wa huduma muhimu kama vile maji, umeme na zahanati. Vigezo hivi vikifikiwa Halmashauri inaweza kuomba kibali cha kufungua kidato cha tano na cha Sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili anasema kwamba shule yao walitaka iwe ya wavulana na wasichana. Naomba tu kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba ukaguzi ulipofanyika, miundo mbinu iliyokutwa haikukidhi kuweza kupeleka wanafunzi wa jinsi hizo mbili. Kwa hiyo, naomba tu nimsihi pengine waongeze juhudi zaidi kwa kushirikiana na Serikali katika mwaka huu wa fedha ili tuweze kuwaongezea jinsi hiyo. Hata hivyo niseme tu si vibaya mukawapa wasichana fursa zaidi.

**MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Masharti yaliyoelezwa na Naibu Waziri ni Magumu sana na kama tutachukulia uanzishwaji wa kidato cha tano na sita kwa utaratibu tulioutumia katika shule za Kata sidhani kama tunaweza tukapata matokeo mazuri. Sisi wilaya ya Mpwapwa tulikusudia kuanzisha shule za kidato cha tano na sita katika shule ya sekondari ya Wota, Rudi, Kibakwe na Ihavu, lakini masharti haya ni magumu. Sijui serikali haioni haja ya kuja na mpango mahususi utakaohusiana na suala zima la uanzishaji wa kidato cha tano na sita maana mahitaji yake ni mengi. Sio tu kwa haya aliyoyataja lakini pia hata upatikanaji wa walimu hao?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa elimu na Mafunzo ya Ufundi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Simbachawene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi hazina masharti magumu bali ningependa tu kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kwamba shule hizi za kidato cha tano na sita madhumuni yake makubwa ni kukuza na kujenga utaifa na uzalendo.

Wanafunzi wanaopangwa kwenda kwenye shule zile hawatoki kwenye maeneo ya karibu; kwa lugha ya kigeni *catchment areas*. Shule hizi hupokea wanafunzi kutoka mikoa yote ya Tanzania kutegemea na ulinganishi wa masomo yao. Ndio maana tunapenda kuwepo na mabweni ya kutosha, nyumba za walimu, miundombinu inayoridhisha na na inayovutia na mambo mengine muhimu kama vile maji, umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi zina masharti magumu kwasababu pale ndio ngazi ya awali ya kutengeneza wataalamu waliobobea. Kwasababu wanaanza kutengeneza fani maalumu, ndio madhumuni ya ulinganishi wa masomo. Sasa kuwachukua tu kama tulivyowachukua kwenye Kata, maji, vitanda wakalale majumbani kwao, haitawezekana. Naomba tu tushirikiane kwa pamoja ili tuweze kuziboresha shule hizi tufikie malengo tusije tukaachwa nyuma kwa kutaka kwenda haraka.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, swali linalofuata lilikuwa liulizwe na Mheshimiwa Jenista Joachim Mhagama, Mbunge wa Peramiho. Na kwa kuwa, niko hapa Mezani na nina maslahi na swali hilo nisingejitendea haki mwenyewe wala atakayenijibu swali hilo kama litaulizwa leo. Ninaomba lipangwe kwenye *order paper* ya kesho ili niweze kujitendea haki na kumtendea haki atayelijibu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, wenye masali ya nyongeza kwenye swali hili, tutakutana nalo kesho. Hivyo sasa naomba nimuite Mbunge, anayefuata Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, aweze kuendelea na swali linalofuata.

Na. 77

**Hatua za Kisheria Kwa Waliosababisha Hasara Katika Zoezi la Uuzwaji wa Nyumba za Serikali**

*(Swali lililotajwa hapo juu liliondolewa na Mwuliza Swali)*

Na. 78

**Ujenzi wa daraja la Mto Lukwamba Wilayani Nanyumbu**

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA** aliuliza:-

Kwa Kuwa, Serikali ilishaahidi Bungeni kwamba, kuanzia mwaka wa fedha 2007/2008 itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja la mto Lukwamba linalounganisha vijiji vya Mburusha na Mpombe katika Kata ya Napacho Wilayani Nanyumbu:-

(a)Je, ni kiasi gani cha fedha kilichotengwa kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo kwa mwaka wa fedha 2007/2008 na mwaka wa fedha 2008/2009.

(b)Je, ni lini sasa ujenzi wa daraja hili muhimu kwa wananchi wa Nanyumbu utakamilika.

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dustan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo;-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge ya kwamba wakati ninajibu swali Na. 171 katika Mkutano wa saba wa Bunge lako tukufu hapo mwezi Aprili 2007, niliahidi kuwa kuanzia mwaka wa fedha wa 2007/2008 Serikali ingeanza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja la mto Lukwamba lililopo katika barabara ya Michinga – Mpombe kadiri hali ya Bajeti itakavyoruhusu. Pamoja na hivyo, Wizara yangu katika mwaka wa fedha 2006/2007 ilikwishafanya usanifu wa barabara ya Madimba – Kitaya – Mnongodi – Mbuyuni – Mapili – Mitemaupinde, kipande chenye urefu wa kilometa 100 pamoja na daraja la Lukwamba kwa gharama ya shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa Bajeti, Wizara yangu haikuweza kutenga fedha za ujenzi wa daraja hilo katika mwaka wa fedha 2007/2008 na 2008/2009. Katika kutimiza azma ya ujenzi wa daraja hilo, Serikali imepanga kutenga fedha katika mwaka wa fedha 2009/2010 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa daraja la Lukwamba.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya Serikali ya mwaka 2007 yalinitia matatani sana. Kwani nilipokuwa nafanya mkutano katika vijiji vya Mburusa, Mpombe, Lichela na Mitonga, ambao wanaathirika sana na daraja hili walikuwa wameniambia kwamba Mheshimiwa Mbunge, umeshindwa kututulia kero zetu. Sasa hii naona kwamba imenitia matatani sana. Je, serikali haioni kwamba haikunitendea haki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, majibu haya yalifanyiwa utafiti na ahadi hii sasa inatolewa tena. Naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, Daraja hili litakwisha lini kutengenezwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, napenda nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dustan Mkapa, kwa pamoja kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda tu nimhakikishie Mbunge pamoja na wananchi wa wote wa eneo hili ambako daraja hilo lipo kwamba Serikali inatoa kauli thabiti na makini na kwa kauli hii tuliyoitoa kwamba mwaka huu wa fedha tunatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hilo, aichukulie kwamba ni ahadi thabiti na kwahiyo juu ya lini daraja hilo litakamilika, maana sasa hivi ndio tunaanza. Kwa hiyo, kuweza kujua kwamba ni lini litakamilika nadhani tusebiri tu tutakapokuwa tumeanza tutatoa taarifa kwasababu maandalizi mengine ya awali yalikuwa yameshafanyika.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya kutia matumaini ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini ujenzi wa madaraja haya yaliyoko Kata ya Napacho, Mburusa na Mpombe, hayatakuwa na maana sana kama hakutakuwa na ukamilikaji wa ujenzi wa daraja la Nangoo lililopata mafuriko mwaka 1990. Ningependa kusikia kutoka Serikalini, mpango gani wa haraka unafanywa kuimarisha daraja lile la Nangoo ili uendane sambamba na madaraja yanayotajwa?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Miundombinu, ningependa kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Njwayo, Mbunge wa Tandahimba, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kwamba ujenzi wa daraja hili ambalo Mheshimiwa mkapa ameliuliziahautakuwa na maana kama haya mjadaraja mengine ya Nangoo pamoja na Nanganga kama yatakuwa hayajakamilika. Napenda tu nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge, pamoja na Wabunge wote na wananchi wa eneo hili ya kwamba sasahivi Serikali ina mpango kwanza wa kulijenga hili daraja la Nanganga mwaka huu wa fedha 2008/2009 kwa shilingi milioni 900, fedha hizi zimetengwa na kwa kuanzia tunadhania kwamba kuanzia mwezi Mei daraja la Nanganga litaanza kujengwa.

Lakini vilevile Wizara imetenga fedha kiasi cha shilingi milioni 1000 katika mwaka wa fedha wa 2009/2010 kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Nangoo na kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza katika mwaka ujao wa fedha wa 2009/2010. Na kusema kweli tukishakamilisha madaraja haya tutakuwa tumeshakamilisha kazi ya kurejesha madaraja yote yaliyokuwa yameathirika katika mafuriko ya mwaka 1990.

Na. 79

### **Kujenga Kituo cha Polisi Nangurukuru**

**MHE. HASNAIN G. DEWJI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Mji wa Nangurukuru katika Wilaya ya Kilwa ni sehemu muhimu na ni makutano ya barabara ya Liwale, Lindi, Kilwa Masoko na Dar-es-Salaam:-

Je, serikali ina mpango gani wa kujenga kituo cha polisi pale Nangurukuru ili kuimarisha ulinzi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hasnain Gulamabas Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ingependa vituo vya Polisi katika maeneo mbalimbali yenye makazi ya watu, shughuli za kiuchumi, kijamii na kilimo ikiwemo Mji wa Nangurukuru katika wilaya ya Kilwa ili kusogeza huduma za Polisi za kulinda



Usalama wa Raia na mali zao. Hata hivyo, nia hiyo nzuri ya serikali haitekelezeki kutokana na ufinyu wa Bajeti inayotengwa kwa madhumuni ya ujenzi wa vituo vya polisi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha ulinzi katika mji wa Nangurukuru, Jeshi la Polisi Mkoani Lindi kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola imeweka kiambata, *Check Point*, chenye askari wa kutosha katika mji huo. Aidha eneo hilo litaendelea kupata huduma ya polisi kutoka kituo cha polisi Kilwa Kivinje na Kilwa Masoko.

**MHE. HASNAIN G. DEWJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza ni hivi kituo cha Polisi, kinagharimu kiasi gani cha pesa?

Kwa kuwa, *Check Point* sio suluhu ya kituo cha Polisi pale Nangurukuru, Serikali iko tayari kutusaidia kutupa vifaa vya ujenzi ili tuweze kutafuta nguvu za wananchi tukajenga kituo hicho badala ya kusubiri Bajeti kila mwaka hadi mwaka miaka inakwenda na usalama ni muhimu pale Nangurukuru? (*Makofi*).

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dewji, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, anataka kujua hivi kujenga kituo kimoja cha polisi kinagharimu kiasi gani? Kabla sijakujibu Mheshimiwa Mbunge; ziko Wilaya 24 katika Tanzania leo, ambazo hazina vituo vya Polisi. Na unapozungumzia gharama yake bila kukuambia ni pesa kiasi gani kwasababu inategemea umbali wapi kituo kitakapokuwa na vifaa vya ujenzi vitavyokwenda, lakini mahitaji ya pale kituo kinahitaji ukishajenga ni lazima chenyewe kiweze kujitosheleza kiwe ni kituo ambacho kitakuwa na mahabusu, kiwe ambacho kitakuwa na nyumba angalau tatu za mapolisi na kadhalika, hii tunazungumza gharama ya kutosha.

Kwa hiyo, ningekuomba tu Mheshimiwa uelewe kwamba nia ya serikali ni kuhakikisha kwamba usalama wa raia wake katika Tanzania unakuwa salama, nia hiyo ipo na shabaha hiyo ipo. Lakini tatizo linakuja katika uwezo na kutokana na uwezo ndio maana tunasema tunakwenda hatua kwa hatua; suala lako tumelizingatia na tutaendelea kulizingatia. Lakini Mheshimiwa Mbunge nitakuwa nakwambia uwongo nikikwambia hapa kwamba kweli hiyo azma tutaweza kuitekeleza kwasababu hali ya fedha haituruhusu kufanya hivyo na ndio maana tukasema tuanzia kwa kuweka *check point*.

Na. 80

### **Kufungua Vituo Vya Polisi Na Vituo Vidogo**

**MHE. BALOZI ABDI MSHANGAMA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga kituo kipya cha Polisi Lushoto na Kufungua *Police Post* zilizojengwa na wananchi wa Mlola na Kwai?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, Mbunge wa Lushoto, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya kituo cha Polisi Lushoto tunaiielewa vizuri kwani hivi karibuni Mheshimiwa Lawrance Kego Masha, Mbunge na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, alitembelea kituo hicho. Kituo hicho ni cha kwanza kujengwa hapa nchini, hivyo ni kituo kikongwe. Serikali itakikarabati ili kuhifadhi na kudumisha kumbukumbu ya kituo hicho wakati inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga Makao Makuu ya Polisi Wilaya ya Lushoto kadiri Bajeti itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vidogo vya Polisi vilivyojengwa na wananchi wa Mlola na Kwai vitafunguliwa mara baada ya ujenzi wake kukamilika.

**MHE. BALOZI ABDI MSHANGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake. Mwaka 2006 niliwahi kupewa majibu kama hayo kwamba Kituo kipya cha Lushoto kingejengwa 2007 na kwamba vile vituo vidogo vingefunguliwa. Sasa swali langu la nyongeza ni hivi; hivi ni lini hasa kituo kipya cha Polisi Lushoto kitajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili la nyongeza. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri au Wizara ya Mambo ya Ndani, wako tayari kumtuma Mheshimiwa Kamanda wa Mkoa Siro akakague vituo vile vidogo na kutushauri mambo ya kukamilisha ili vifunguliwe Julai mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Balozi Abdi Mshangama, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mheshimiwa Balozi alipata jibu hilo mwaka 2006 na halikuweza kutekelezeka ni kwasababu zilezile nilizozitaja kwamba upo uhaba mkubwa wa Bajeti na sio kwamba nia haipo. Lakini yapo matatizo ya kifedha lakini nia wala Serikali haijasema kwamba haitafanya, itafanya na hilo kwa kweli tunalizingatia. La pili ni kwamba juzi tu *RPC* amekwenda katika vituo hivi ameona mapungufu yaliyopo ili kuweza kukamilisha hizi sehemu mbili. Kwanza kumekuwa na matatizo ya kupiga sakafu, kumekuwa na matatizo ya kuweka milango na madirisha na kumekuwa na matatizo ya kupiga plasta. Kwa hiyo, hayo yakishakamilika nataka nikuhakikishieni na ninatamka kwamba hizi na ni mbili zitaweza kufunguliwa.

Na. 81

## **Kujenga Mahakama Wilayani temeke**

**MHE. RIZIKI O. JUMA** aliuliza:-

Kwa Kuwa, majengo yanayotumika kama Mahakama katika wilaya ya Temeke ni mabovu mno na hayatoshi:-

Je, ni lini serikali itawajengea Mahakama wananchi wa wilaya ya Temeke ili Mahakimu wa Temeke waondokane na mtiririko wa kusikiliza kesi chini ya mti?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kuna haja ya kujenga majengo ya Mahakama Wilaya ya Temeke kutokana na ubovu na kutotosheleza kwa majengo ya Mahakama yaliyopo kwa sasa. Serikali haipendezwi na hali ya mbaya ya miundombinu ya Mahakama hiyo pamoja na nyingine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza wakati nikijibu swali Na. 57, serikali inaendelea na juhudi za kuboresha miundombinu ya Mahakama kwa awamu. Hata hivyo, kwa kuzingatia kwamba kuna miradi ya ujenzi wa majengo ya mahakama inaendelea sehemu zingine za nchi na kutokana na ufinyu wa Bajeti ya Mahakama, serikali kipindi hiki haitaweza kujenga majengo ya Mahakama Wilaya ya Temeke ila itafanya hivyo pindi fedha za kufanya hivyo zikipatikana.

**MHE. RIZIKI O. JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, haki inayocheleweshwa ni haki inayovunjwa. Na kwa kuwa, hali hii iliyopo wilaya ya Temeke inachangia kucheleweshwa kwa kesi nyingi kusikilizwa kutokana na hali halisi ya upungufu wa majengo na ubovu. Na kwa kuwa, Mahakimu wetu wanashindwa kufanya kazi zao ipasavyo kutokana na hali halisi ilivyo:-

Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba kuna haja ya kuchukua hatua za dharura ili kukabiliana na hali hiyo ili wananchi wetu wakaweza kupata haki zao kwa wakati muafaka? (*Makofi*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Mheshimiwa Waziri haoni kwamba kutokuwa na Mahakama ambazo ni za uhakika zilizokamilika kiutendaji kunazidisha mrundikano wa mahabusu katika magereza yetu, hali inayopelekea kufanya magereza hayo kuzidi kiwango cha kimataifa.

Je, Serikali inasemaje kuhusiana na hilo?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua hilo ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Mbunge na Mwaka ujao wa fedha tutafanya ukarabati kwenye jengo lile la Mahakama ya Temeke. Ikumbukwe kwamba Mahakama ile ya temeke sio jengo la Mahakama, ila ni Ofisi ya Halmashauri ya Manispaa ya Temeke.

Kwa hiyo, tukipata fedha za kutosha tutatafuta sehemu na kujenga Mahakama ya Wilaya ya Temeke. Na pia katika mwaka ujao wa fedha tumepanga kujenga Mahakama sehemu za Kigamboni ambayo pia ni sehemu ya Temeke. Kwa hiyo, itapunguza mlundikano wa makesi yaliyoko pale kwenye Mahakama ya Temeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kutokuwa na Mahakama nzuri katika sehemu ya temeke haizidishi mahabusu magerezani kwasababu Mahakimu waliopangwa kwenye Mahakama ya Temeke bado wanafanya kazi zao kwenye maeneo yaleyale ambayo wamepangwa. Sehemu za Mahakama bado zipo lakini ni ile tu hali ya majengo ndio ambayo hairidhishi.

Lakini ukweli ni kwamba sehemu ya kufanyia zile kazi za Mahakama bado ziko palepale. Kwa hiyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hali iliyoko Temeke itabadilika baada ya muda, *Legal Sector Reform Program* pia inatupa fedha kwa ajili ya kukarabati majengo yetu. Kwa hiyo, nina uhakika kwamba muda hautaenda mrefu hali ya Temeke itabadilika. (*Makofi*)

Na. 82

### **Vikao Vya Mahakama ya Rufaa**

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS** aliuliza:-

Kwa kuwa, mara baada ya kuvunjika kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1979, Tanzania ilianzisha Mahakama ya Rufaa ili kukidhi mahitaji ya muundo wa Mahakama; na kwa kuwa Mahakama ya Rufaa huendesha vikao vyake kwa kipindi cha muda maalum kisichopungua mwaka mzima:-

(a)Je, kwanini vikao vya Mahakama ya Rufaa visifanyike kwa kipindi cha kila miezi sita hususan katika mashauri ya Jinai ambayo yanahitaji kusikilizwa kwa haraka?

(b)Kama ni gharama kufanya vikao hivyo kwa muda huo, kwa nini serikali isibuni utaratibu mwingine wa jaji mmoja mmoja kuzunguka Kanda kila baada ya miezi mitatu?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Vuai Abdallah Hamisi, Mbunge wa Magogoni, kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kawaida Mahakama ya Rufaa inaendesha vikao vyake kwa mwaka katika vituo vyake vya Zanzibar, Dodoma, Tanga, Tabora, Mbeya, Arusha, Mwanza, Dar-es-Salaam, Mtwara na Iringa. Hata hivyo hukaa mra moja kwa kila kituo isipokuwa Dar-es-Salaam ambapo vikao hukaa zaidi ya mara moja kwa mwaka kwa sababu hapo ndipo Makao Makuu ya Mahakama ya Rufaa na kuna mashauri mengi kuliko vituo vingine nchini. Kutofanyika kwa vikao vingi zaidi katika vituo vingine kunatokana na ufinyu wa Bajeti ya kuendesha vikao, upungufu wa Majaji wa Mahakama ya Rufaa, na wingi wa rufaa katika vituo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mazingira ambayo hupelekea kuwa na kikao zaidi ya kimoja cha Mahakama ya Rufaa katika baadhi ya vituo. Mazingira hayo ni pamoja na wingi wa rufani pamoja hali ya Bajeti ambayo inakuwepo kwa wakati huo. Vilevile kama kuna uharaka wa kusikiliza rufaa yoyote, rufaa hiyo hupangwa kusikilizwa Makao Makuu na wahusika huarifiwa kuhudhuria huko.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na sheria na kanuni zinazohusu uendesaji wa mashauri katika mahakama ya rufaani, (*The Appellate Jurisdiction Act* na *The Tanzania Court of Appeal Rules*), rufaa yoyote inapeleka mahakama ya rufaa husikilizwa na majaji wasiopungua watatu na sio jaji mmoja. Ni baadhi ya maombi tu ndiyo husikilizwa na jaji mmoja kwa hali hiyo ni vigumu kwa jaji kuzunguka katika vituo kusikiliza rufaa peke yake kwani itakuwa kinyume cha sheria.

Hata hivyo Serikali imeendelea kuboresha Bajeti na kuongeza idadi ya majaji ya Mahakama ya Rufaa na pindi hali itakapokuwa nzuri zaidi ni imani yetu kuwa vikao vya Mahakama ya Rufaa vitaongezeka.

**MHE. VUAI ABDALLA KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Mwanasheria lakini hoja yangu ni ya msingi. Kwa hiyo, haioni Mheshimiwa Mwanasheria hoja hii kuitilia maanani pale Bajeti itakapokuwa imeongezeka?

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Bajeti itakapoongezeka basi tutaboresha utendaji wa kazi wa Mahakamani ya Rufaa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge muda wa maswali umekwisha, maswali yote yaliyopangwa katika siku hii ya leo nayo vilevile tumeweza kuyamaliza kwa wakati unaotakiwa kabisa.

Waheshimiwa Wabunge ninayo matangazo kabla hatujaendelea na ajenda nyingine, nimeletewa taarifa kidogo nitoe ufafanuzi na Waheshimiwa Wabunge kadhaa

waliosaini katika taarifa hii. Wameniomba tu nikumbushie kuhusu utaratibu tunapokwenda kufanya *consultation* na Mheshimiwa Waziri Mkuu kufanya majadiliano yoyote na Mheshimiwa Waziri Mkuu basi wametuomba tukumbuke ule utaratibu wetu wa kupita kupitia upande wake wa mkono wa kulia na si kwa mkono wa kushoto ambapo mara zote mtu anayefanya hivyo amekuwa ikimwitaji Waziri Mkuu kujisogeza ndipo mtu aweze kupita.

Kwa hiyo, naomba tu nikumbushe huo utaratibu ili uweze kuzingatiwa.

Waheshimiwa Wabunge wageni tulionao pale kwenye *Speaker's Gallery*, nimepewa orodha ya wageni wafuatao, ninaomba nitambue uwepo wa Balozi wa Uingereza bibi Daniel Kona, na mwambata wa mambo ya siasa Bwana John Bland Shoo, na mshauri wa mambo ya siasa Pascal Mayalla. Karibuni sana *we are very much happy for your presence in our house we wish you good stay here in Dodoma and safe journey back to Dar es Salaam*, karibuni sana siku nyingine. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge sijui naona kuna wageni wengine pale lakini naona sijapata maelekezo nasubiri niendeleo kupata maelekezo, lakini nimeambiwa pia wako wageni wa chama cha Wabunge wanawake wa Tanzania yaani *TWPG Tanzania Women Parliamentarian Group*, ambao ni maafisa sita wa *Hansen Foundation* ya Ujerumani na vilevile wawakilishi kutoka *Civil Society Foundation* ya Dar es Salaam, naomba tafadhali wasimame wageni hao kama wako hapa ndani. Waheshimiwa Wabunge wageni wanaofuata ni wajumbe themanini wa mkutano mkuu wa umoja wa vyama vya waandishi wa habari Tanzania ambao wanaendelea na mkutano wao mkuu hapa Dodoma. Tafadhali waandishi hao ningeomba wasimame mahali walipo karibuni sana sana katika shughuli zetu za Bunge tunafurahi kuwaona.

Waheshimiwa Wabunge baada ya kuwatambua hao ninao wageni wa Mheshimiwa Dr. Batlida Burian Waziri Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, nao ni wafuata, bibi Ruth Molle, Katibu Mkuu wa Ofisi ya Makamu wa Rais, karibu sana Bwana Erick Murugusi Mkurugenzi wa Mazingira ofisi ya Makamu wa Rais Prof. Cleofancy Migiro Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uzalishaji Endelevu, tunafurahi sana kukuona Bwana Froom Jagwancy, *Senior Rule Development Economist* kutoka benki ya dunia, Christian Peter *Senior Natural Resources Specialist* na David Lack - *Senior Agricultural* karibuni sana. Waheshimiwa Wabunge wageni wa Mheshimiwa Paul Lwanji, Mbunge, ambao ni Bwana Michael Peter wa Katibu wa Jimbo. Ndugu Ibrahim Nangali Mwenyekiti wa CCM wa Kata ya Mgadu na Mussa Bakar mtendaji wa kijiji wa Kata.

Wageni wa Mheshimiwa Dr. Aisha Omar Kigoda, Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, ambao ni wajukuu zake Aisha Bona na Ibrahim Nuru. Waheshimiwa Wabunge naomba niwatambulishie Wabunge wa Mtwara wana mgeni naye ni Mwenyekiti wa CCM, Wilaya ya Tandahimba, Mama Sofia Siri Makonyola. (Makofi)

Halafu kuna wageni 22 wa Mheshimiwa Celina Kombani, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hao ni wanafunzi kutoka Chuo

cha Serikali za Mitaa, Hombolo wakiongozwa na Ndugu Sprian Mbungando. Wageni wa Mheshimiwa Jacob Shibiliti ambao ni maafisa wa Taasisi ya Maendeleo *ADET Action Tanzania* ni Festus Peter - *Translator and Communication Officer*, Ndugu Swetbert Msiba, *Director* na Khalifan Shaban - *Program Officer*. Aidha Maafisa saba kutoka Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wanaendelea na ziara ya mafunzo katika Bunge letu. Naomba maafisa hao wasimame, karibuni sana. Wageni 15 wa Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, ambao ni Makatibu na wenyeviti wa UWT kutoka Mkoa wa Lindi wakioongozwa na Ndugu Akinai Mshuhuo Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Lindi. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kuna mgeni wa Mheshimiwa Kapten John Komba, ambaye ni Bwana Victor Kombani Zambia, Mwenyekiti wa walemavu Mbinga Magharibi, karibu sana. Waheshimiwa Wabunge ninaomba pia nimtambulishe mume wa Mheshimiwa Hawa Ghasia, ninaomba pale alipo asimame. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge sasa ninazo taarifa za vikao. Taarifa ya kwanza ninaomba Waheshimiwa Wabunge Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii, anaomba kuwatangazia wajumbe wote wa Kamati hiyo kwamba kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo saa saba mchana katika ukumbi na 231. Ninaomba sana wajumbe wa Kamati wasikose kuja tuweze kupitia ripoti ya Kamati yetu.

Waheshimiwa Wabunge, Ndugu John Joel. kwa niaba ya Katibu wa Bunge. Huyu siyo Mheshimiwa, anaomba niwatangazie wenyeviti wote wa Kamati za Kudumu za Bunge kuwa watakuwa na mkutano maalum unaohusu dhana ya matumizi ya uzalishaji endelevu. Mkutano huo utafanyika leo saa tano asubuhi, katika Ukumbi wa Pius Msekwa badala ya Ukumbi wa Mheshimiwa Spika kama tulivyozoa.

Mheshimiwa George Simbachawene, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo, anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo ya sheria Ndogo kwamba leo tarehe 28 Aprili, 2009 kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo saa tano asubuhi, katika ukumbi wa Pius Msekwa. Sasa vikao hivi viwili vinagongana nadhani makatibu mtatusaidia kuona nani akae wapi na nani akae wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Switi, Mbunge wa Viti Maalum na Katibu wa *TWPG* anaomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge wanawake wote ambao ni wanachama wa *TWPG* niwaharifu kuwa leo siku ya Jumanne tarehe 28 saa saba mchana kutakuwa na kikao cha kuonana na wafadhili kutoka shirika la *Hansen Foundation* kikao hicho kitafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa saa saba. Kwa hiyo vikao hivyo vyote vya Pius Msekwa tutaomba tu Makatibu mtusaidie kuviratibu.

Halafu nimeomba na Mheshimiwa Job Ndugai Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumku ya Ardhi Maliasili na Mazingira niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake na wao leo tarehe 28 Aprili, 2009 saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati katika ukumbi namba 227 gorofa ya pili Waheshimiwa Wabunge mnaombwa kuhudhiria wajumbe wa Kamati hiyo bila kukosa.

Mheshimiwa Omar Kwaangw' Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, na yeye anaomba niwatangazie wajumbe wa Kamati hiyo leo tarehe 28 kutakuwa na kikao cha Kamati saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa, sasa vikao hivi vikao huko Pius Msekwa leo kutakuwa na shughuli kweli. Lakini kuna kumbi nyingi makatibu mtatusaidia tu kututengenezea utaratibu katika eneo hilo la Pius Msekwa.

Halafu nimeombwa na Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, kwamba niwatangazie wajumbe wa Kamati ya Maandalizi ya Mkutano wa 55 wa CPA kuwa kutakuwa na mkutano leo hii saa tano asubuhi katika ukumbi namba 133. Sasa tangazo hili Mheshimiwa Dkt. Raphaeli mara zote huwa tunatangaza matangazo ya Kamati kwa muda wa saa tano, sasa hili mtaangalia mtazingatia utaratibu unaona unafaa.

Waheshimiwa Wabunge ninatangazo kutoka kwenye ofisi ya Katibu wa Bunge, Katibu wa Bunge anaomba kukumbusha niwatangazie Wabunge kuwa leo ndio mwisho wa kurejesha fomu kwa wale wanaotaka kugombea nafasi za uwakilishi katika maeneo mbalimbali, Bunge la Afrika, APRM, Chuo kikuu cha Sayansi za Afya ya Jamii Muhimbili kwa hiyo tafadhali sana wale waliokwisha kuchukua fomu na wale ambao hawajachukua lakini walikuwa na nia walisahau, basi leo ndiyo siku ya mwisho ya uchukuaji na urejeshaji.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge tunaombwa sana kukumbuka hilo ili tuweze kukamilisha taratibu za chaguzi zetu.

Waheshimiwa Wabunge pamoja na Mheshimiwa Balozi wa Uingereza kwenye *Speakers Gallery* kuna pia Balozi wa Sweden ndugu yetu Staphan Helston asante sana. *Thank you very much for your presence.* Waheshimiwa Wabunge nafikiri hayo ndiyo ambayo yalikuwa kwenye meza yangu kwa siku hii ya leo ninaomba niseme kwamba baada ya matangazo haya basi sasa tunaweza kuendelea na ratiba inayofuata, na ninaomba Katibu atuongoze.

## **MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

### **Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasimali za Maji wa Mwaka 2009 (*The Water Resources Management Bill, 2009*)**

### **Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2009 (*The Water Supply and Sanitation Bill, 2009*)**

*(Kusomwa Mara ya Pili )*

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. ZABEIN MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa nafasi ambayo umenipa ili nami niweze kuchangia hoja ambayo iko mbele yetu ambayo ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu na kama tunavyofahamu maji ni uhai.



Aidha, naomba nichukue nafasi hii nimpongeze kwa dhati jirani yangu Profesa Mark Mwandosya, Waziri, Mheshimiwa Injiniya Chiza Naibu Waziri, Ndugu Wilson Mkama Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri waliyofanya ya kututayarishia Miswada hii miwili ambayo wameitayarisha kwa kisayansi kabisa Miswada hii ambayo inatekelezeka.

Aidha, kabla sijaendelea kwa niaba ya wananchi wa Kondoa Mjini naomba nichukue nafasi hii nimshukuru kwa dhati Mheshimiwa Waziri kwa jinsi alivyoshughulikia suala la upatikanaji wa pampu za maji kupeleka katika eneo la Kilimani kutoka kwa mkandarasi. Mheshimiwa Waziri kazi yako ni nzuri ilikuwa haionekani kabisa kwa mkandarasi kuleta pampu hizo.

Lakini wananchi wanakushukuru sana na wanakukaribisha sana na wanakukaribisha tena Kondoa ili safari hii usiishie Kondoa Mjini uende vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitachangia hoja ya Muswada wa usimamizi wa rasilimali za maji. Katika kifungu cha 7 pamoja na kuwa na kuwa ni muhimu kwa wananchi kulinda vyanzo vya maji, lakini vile vile ni muhimu zaidi kwa wananchi hao ambao wanapaswa kulinda vyanzo hivyo vya maji nao pia waweze kupata maji kwa ajili ya matumizi yao wapewe kipaumbele ili nao wapate maji. Labda nitoe mfano katika Jimbo la Kondoa Kaskazini kuna chanzo cha maji cha Mtaro wa Ntomoko. Chanzo hiki wananchi wanaoishi katika eneo hili kwa miaka yote wamekuwa wakilinda na kutunza chanzo hiki cha maji.

Lakini wananchi hawa wanaofanyakazi nzuri hawapati maji kwa matumizi yao. Naomba nichukue nafasi hii niwapongeze kwa dhati wananchi hao kwa kazi nzuri wanayofanya pamoja na kuwa wao wenyewe hawapati maji kwa matumizi yao.

Hivyo basi ni muhimu kwa kifungu hiki kwenda sambamba na upatikanaji wa maji kwa wananchi wanaoishi karibu na vyanzo hivi ili waone umuhimu na wajibu wa kutunza na kulinda vyanzo vya maji kwa faida ya sasa na faida ya baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mtaro wa Ntomoko ulijengwa mwaka 1972 kwa malengo ya kuhudumia wananchi 23,000 kwa sasa idadi ya watu imeongezeka sana hadi kufikia 80,000.

Kwa ongezeko hili kubwa la watu ni dhahiri kuwa miundombinu iliyojengwa mwaka 1972 haiwezi kukidhi mahitaji ya ongezeko kubwa la watu hao ikizingatiwa pia na uchakavu wa miundombinu hiyo ili kufikia malengo ya kifungu cha 4 vifungu (a) (b) (c) na (d) ni dhahiri kuwa Serikali iwe na mipango madhubuti kwa kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji. Miundombinu ambayo tayari imekwishachakaa ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati wa mtaro wa Ntomoko ambao kwa kusema kweli kwa hivi haufanyi kazi, maji hayawafikii wananchi ambao wamelengwa. Hivi ukifanyiwa ukarabati ili wananchi mfano wa vijiji vya Kilele cha ng'ombe na Makrinya nao waweze kupata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitembelea kijiji cha Makrinya, kuna mwananchi aliniletea maji katika chupa maji ambayo wanatumia kwa kweli nilifadhahika kwa sababu maji yale yalikuwa si maji ya kutumia kwa matumizi ya binadamu. Kwa hivyo Mheshimiwa Waziri nadhani litazingatiwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha nne, kifungu kidogo cha b pamoja na mambo mengine kimesisitiza kuwa maji salama ya kunywa ni haki ya msingi ya kila binadamu, sasa hili kutimiza malengo haya yaliyoainishwa katika kifungu hicho ni muhimu basi Serikali kuwa na mipango endelevu ya upatikanaji wa maji safi na salama ya kunywa na ya kutosha.

Vinginevyo malengo haya yatakuwa ni ndogo na hayatakamilika nasema hivi kwa sababu nitoe mfano wa Kondoa, katika Wilaya ya Kondoa ni asilimia chini ya 30 ya wananchi wanaopata maji na maji haya ni lazima yachemshwe kabla ya kunywa.

Hivyo basi ongezeko la upatikanaji wa maji uende sambamba na maji hayo kuwa safi na salama. Sote tunafahamu kuwa maji ni uhai, na haki ya msingi kwa kila mwananchi kwa msingi huu ni muhimu Serikali kutoa kipaumbele kwa sekta ya maji kwa kuongeza na kutenga Bajeti ambayo inaweza kutosha kwa sekta hii. Kwa sababu kama bajeti haitaongezwa kwa kweli Miswada hii hata ikipitishwa na kuwa na ni sheria haitaweza kutekelezeka na itakuwa ni kama ni bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Miswada kupitishwa kuwa sheria na ishaallah mimi naamini kabisa itapitishwa na itakuwa sheria ili basi sheria iweze kukidhi malengo ambayo yamekusudiwa na Serikali ni muhimu kwa Serikali kuhakikisha kuwa Halmashauri zina wataalam wenye sifa na uwezo wa kazi.

Nasisitiza hili kwa sababu Halmashauri zetu nyingi hazina waalam wa maji na naomba nitoe tu mfano wa wilaya yetu ya Kondoa, wilaya ya Kondoa haina *engineer* wa maji mpaka sasa, Wizara ilileta *engineer* wa maji lakini *engineer* huiyu aliondoka baada ya muda mfupi tena bila hata ya kuaga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa Halmashauri ya Kondoa imekuwa ikileta maombi kwenye Wizara ili tupatiwe *engineer* wa maji kujaza pengo lilioachwa wazi mpaka sasa hatujapata *engineer* wa maji.

Mheshimiwa Waziri kama ulivyotusaidia kwa mkandarasi kutuletea zile *pump* mbili ambazo mwanzo zilionekana hazitaletwa naomba basi na hili nalo utusaidie ili tuweze kupata *engineer* wa maji katika Wilaya ya Kondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yetu kuwa sheria hizi zikitekelezwa ipasavyo na Bajeti ya sekta ya maji ikiongezwa ni dhahiri kuwa upatikanaji wa maji utaboreshwa sana. Kwa heshima na taadhima naomba niunge mkono hoja Miswada hii miwili kwa asilimia mia moja ahsante sana. (*Makofi*)

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie juu ya Miswada hii muhimu sana kwa watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote na mimi niungane na wananchi wa Jimbo langu kutoa rambirambi kwa msiba wa Mheshimiwa Rwilomba aliyekuwa Mbunge wa Busanda na Mheshimiwa F. Kabuye wa Biharamulo Magharibi na wengine wote ambao misiba imetukuta hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono Miswada hii. Ni Miswada muhimu sana hasa huu wa sheria ya usimamizi, wa rasilimali za maji na sheria mpya ya huduma za maji na usafi wa mazingira. Kwa kweli nadhani imekuja katika muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji si dogo. Tunapozungumza tatizo la maji nadhani tunajaribu kusawazisha na matatizo mengine. Linataka kuonekana kama ni la kawaida. Kwa kweli tatizo la maji ni tatizo zito ni tatizo sugu linalowakumba wananchi wetu.

Mimi jimboni kwangu sasa hivi mwezi huu unapoisha mwezi wa 4 unakwenda mwezi wa tano watu wanaanza kufikiria adha ya kulala nje.

Jana nilipokuwa namsikia Mheshimiwa Vullu anazungumza habari za akina mama nilimwelewa kabisa kwa sababu akina mama wa Rungwa, akina mama wa Kitanula, akina mama wa vijiji vingi Kata ya Mgandu, Kata ya Idodiandole hata Kata ya Itigi na Kata ya Ipande wengi wana adha hiyo ya kulala nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka 48 toka tupate uhuru. Ni asilimia 30 tu ya watu wenye uhakika wa kupata maji. Lakini leo hii, asilimia hii bado haina uhakika wa kupata maji. Sasa Serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi sana sijui ni kiasi gani sasa toka tumepata uhuru, fedha ambazo zimetolewa kwenye sekta ya maji? Ni triloni ngapi kwa mwaka huu au mwaka zilitolewa kwa ajili ya maji na ni fedha kwa ajili ya maji lakini tatizo hili limeendelea kuwepo. Wananchi wetu kwa kweli wanashindwa kuelewa kama miradi hii inayotolewa ni endelevu au ni ya kulipua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana Mamlaka hizi zitakazoundwa kutokana na sheria hii ijaribu kuangalia utendaji. Nilimsikia Mheshimiwa Ndugai alivyokuwa analalamika kuhusu miundombinu ya maji tunayoletewa ilivyo mibovu.

Lakini mimi ninaona pia kwamba kuna suala la mgongano wa maslahi. Mimi nadhani naliweka hivyo mgongano wa maslahi kati ya wanaopima visima hivyo na wachimbaji. Ni kwa nini watalaam waende kupima fedha zimetolewa unakuta kisima kimoja shilingi milioni 30, milioni 40 *advance part* inakwenda na huyu mpimaji ni mtumishi wa Serikali, ni mtaalam anaondoka anakwenda kupima, akisha kupima anasema hapa kuna maji na anaweka alama.

Sasa mchakato ule unaendelea wa kumtafuta mkandarasi wa kuja kuchimba. Anapokatikana mkandarasi wa kuja kuchimba, mkandarasi anakuja kuchimba hakuna

maji. Ni kitu kinachoshangaza wananchi wengi sana. Maana inakuwa ni kazi ya kubahatisha.

Mimi ninaomba mamlaka hizi zitazame sana tatizo hili sasa. Maana ya hivyo ni kwamba fedha hizo za kupima, za kupima na kupima nadhani ni shilingi milioni mbili, milioni tatu, za kuchimba zote zinakwenda na majiau zinapotea bure.

Nina mifano mingi jimboni kwangu, ambapo watu wameshindwa kupata maji, pamoja na kwamba Serikali imetoa pesa. Sasa hili tatizo ninaomba liangaliwe ni nani anayekomoa mwenzake kati ya mpimaji na mchimbaji? Huyu ni wa Serikali na huyu mkandarasi ni mtu anayeteuliwa, lakini unakuta wanakosa maji; ni nani anayekomolewa hapa? *Definitely*, usemi kwamba mafahali wawili wanapogombana ziumiazo ni nyasi; hapa mwananchi ndiye anayeumia. Mimi ninaomba sana hili suala liangaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mabwawa siwezi kusisitiza umuhimu wake, kila mmoja anaujua lakini tatizo kwenye sehemu ya mabwawa limekuwa ni kwamba, wanapokwenda kuchimba na kujenga mabwawa hayo, tatizo linabaki pia kwenye ujenzi usiokidhi viwango. Mfano mzuri ni Bwawa la Rungwa, lililojengwa miaka kama kumi iliyopita, lakini miaka mitatu iliyopita lilibomoka. Ukifika katika lile Bwawa ukaliangalia, hakika utasikitika; watu wamejenga kingo, kuta na kadhalika, lakini hakuna nondo za kutosha, hakuna zege la kutosha sasa unatarajia nini? Mabango mengi tunatengeneza lakini yanaharibika.

Kwa hiyo, ningeliomba sana, maana hakuna *privileges* za hapa na pale; hizi nondo, *cement* na kadhalika, jinsi wanavyokwenda kujenga porini mabwawa haya, utakuta vifaa vinavyopaswa kujengewa ili mabwawa haya yawe imara havifiki kwenye *site* na hata wakati wingine vyote havitumiki ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana kwa sababu tatizo la maji hasa kwa maeneo yetu ya wafugaji, pamoja na wananchi, nadhani suala la uhakika katika kutoa *solution* ya maji ni mabwawa. Tumeona visima hivi vimekuja, wameweka *wind mills* miaka nenda rudi, wameweka pampu za kusukuma kwa *diesel* zinaharibika, hatuna uhakika wa maji.

Sasa nilidhani kwamba, Serikali na Wizara kwa ujumla, ijaribu kuona maeneo haya, si kwamba watu walale katika maeneo ya kutafuta maji usiku, lakini wawe na uhakika wa kufuga mifugo. Sasa hivi kwangu watu wanafikiria kuhama na mifugo yao kwenda kutafuta maeneo yenye maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hizi Mamlaka zinazokuja, ziharibu kuangalia uwezekano wa kukamilisha haya mambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mifuko tunayoiunda ya maji kwa ajili ya *maintenance* ya visima na mashine hizo, nayo imekuwa tatizo na imekuwa ni mizigo kwa vijiji. Sasa mimi nilidhani kwamba, ingekuwa nafuu basi Serikali ingefirikia kama inataka kuwasaidia hawa wananchi, basi waingie mkataba wa aina yake, wapewe hela na

Serikali kwamba bwana sisi tunaona katika kutanzua matatizo yenu, maana kila siku tunapokuwa tunazi-*service* hizi *machine* utakuta mara kwa mara zinaharibika. Wataalamuu wanakuja kila siku kutengeneza, lakini wiki moja na ya pili mashine imeharibika. Sasa muda mwingi ni kutuma wataalamuu kwenda kujaribu ku-*service* na wanaolipia hizo ni wananchi, wanauza mifugo yao wanasumbuliwa. Sasa mimi naona ingekasimu shughuli zote, wanavijiji hawashirikishwi kikamilifu hata katika mchakato wa kutafuta maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninashauri wananchi katika kutafuta maji na katika mchakato mzima wahusike moja kwa moja. Nilikuwa nafikiri kama inawezekana, hata kama ni shilingi milioni 30 kuchimba kisima katika kijiji fulani, basi wao wenyewe washirikishwe katika kutafuta huyu mtaalamu wa kupima maji na hao watu wa kwenda kuchimba maji; vinginevyo, tutaendelea kuwa na matatizo haya na hatutatoa *solution* yoyote kwa ufumbuzi wa haya matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani hasa wa kulaumiwa? Ndiyo maana nasema hizi Mamlaka ziangalie, ajulikane hasa ni nani wa kulaumiwa, kwa sababu kama Serikali inatoa pesa ambazo zinatakiwa kwenda kuchimba visima au kutengeneza mabwawa, lakini hakuna kitu kinachofanyika cha kuweza ku-*solve* haya matatizo miaka nenda rudi sasa ni nani wa kulaumiwa? *Definitely*, nadhani wataalamuu wetu ni watu wa kulaumiwa na sielewi tuwafanye nini, kwa sababu tumejaribu sana kuwaomba, wapo waaminifu lakini wapo wengi pia ambao siyo waaminifu. Sasa makundi haya mawili ndiyo ambayo yanatupa shida na umeona toka jana wanazungumza kwamba; sisi kwetu tunahitaji mhandisi huyu aondoke na huyu aje, huyu afanye hivi na kadhalika; lakini ukweli ni kwamba, tuna tatizo hilo na nadhani Wizara hii ijaribu kuchuja kwa kina juu ya wataalamuu ambao tunao katika hii Sekta ya Maji.

Mimi nilidhani pia kwamba, hii *suggestion* ninayoitoa ya kuwashirikisha wananchi moja kwa moja, basi ijaribu kuangaliwa ili ijulikane kama kijiji kitashindwa kujipatia maji katika ushirikishi huo, basi isiilaumu Serikali, wabaki pale na tatizo lao kwa muda mrefu mpaka hapo watakapokuwa wamejirekebisha. Lawama ibaki kwao wenyewe badala ya kuitwisha Serikali kila siku na Serikali *of course* ni hao hao wataalamuu na wataalamuu nao tuwatwishe lawama. Mimi nilikuwa nafikiri tuliangalie suala hili kwa kina; vinginevyo, tutaendelea kuwa na matatizo hayo miaka nenda rudi na hatutakuwa na *solution* yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Job Ndugai hakuwa na peke yake katika kilio chake cha miundombinu; hizi pampu na mashine za maji zinaletwa kwa mamilioni ya pesa kama milioni 40, 50 au 60, inakuja kijijini watu wanafanya sherehe baada ya sherehe siku mbili au tatu inanza kuhakikiwa, mara inanza hapa ina tatizo, pale ina tatizo. Sasa wataalamuu ndiyo wanapiga hodi, inakuwa ni kazi ya kufanya *service* ya ile mashine na mwisho inakufa.

Mfano mzuri, mimi nina Kijiji cha Doroto pale watu wanahangaika sana, lakini walipewa pampu nzuri ilikuwa ni ya matumaini kabisa, ukiiona kwa macho utadhani

kwamba matatizo yote yamekwisha lakini ilipofika pale ikawa kilio ni mzigo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapomalizia katika hoja hii, ninakubali mara nyingine huwa si rahisi sana kuunga mkono hoja hii, lakini nimeisoma nimeona Mamlaka hizi zinaweza zikatusaidia katika hii sheria mpya. Kwa hiyo, niwapongeze walioufikisha Muswada huu na ninawatakia kila la kheri.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Lwanji, kwa mchango wako.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. MARGARETH A. MKANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuandaa vizuri Muswada huu.

Nitaanza mchango wangu kwenye sehemu II, ukurasa 11(b), ambapo kipengele hicho kimefafanua wazi kuwa lengo ni kuwezesha usawa katika matumizi ya maji safi na salama kwa kila mtu kwa vile maji ni haki ya msingi kwa binadamu. Kwa msingi huo, naamini Serikali itaendelea kutoa huduma za maji kwa wananchi wake, licha ya kwamba itasaidiwa na wadau wengine mbalimbali, lakini Serikali itakuwa ndiye Msimamizi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka ya hivi karibuni, Serikali imefanya juhudi za kuhamasisha wananchi kuvuna maji ya mvua ili yaweze kutumika katika shughuli za nyumbani na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefarijika sana kwa vile uhamasishaji huo sasa unahimizwa zaidi katika Muswada sehemu ya III kipengele (12)(1), ukurasa wa 14 wa Muswada; na kwamba uvunaji huo hautamlazimisha mhusika kupata kibali cha matumizi ya maji (*Water Use Permit*), kama inavyotakiwa na Muswada. Ningependa uamuzi huu kwa sababu wananchi wamepunguza urasimu katika utekelezaji wa suala hili, lakini naomba ufafanuzi endapo mtu alikwishajenga kisima bila kukidhi ujazo unaotakiwa itakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ninalofarijika nalo ni uwezo wa Waziri mwenye dhamana ya maji kutetea maslahi ya nchi katika sehemu ambazo rasilimali maji inapotumika na nchi zaidi ya moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 57, kipengele cha 103, kwa kuwa maji ni haki ya msingi kwa binadamu wote, nimefurahishwa na kiwango cha adhabu kwa mtu yeyote atakayechafua chanzo chochote cha maji na kuathiri afya za binadamu mifugo, samaki, mazao na kadhalika. Kipengele hiki cha Muswada, nadhani kitakomesha uchafuzi wa maji unaofanywa na wachimbaji wadogo wadogo wa madini, ambao

hutiririsha zebaki katika mito na kadhalika, kwa vile sumu itokanayo na zebaki ina madhara makubwa kwa binadamu na wanyama.

Rai yangu ni kwamba; ni muhimu mamlaka ziwe makini katika suala hili ili kuwaokoa wananchi na madhara mbalimbali.

Baada ya kuchangia haya, naunga mkono hoja.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara wakati wa kukamilisha mchakato wa utafiti wa mabwawa ambayo yamejaa tope na thamani yake ifikiriwe Bwawa la Igombe – Tabora Mjini; Bwawa la Kazima – Tabora Mjini; na Bwawa la Loya - Tabora Mjini ili wakazi wake wapate maji safi na salama.

Kwa kuwa Manispaa ina maeneo makubwa ambayo yana vijiji pia, naomba wachimbiwe visima vifupi kama vile Ndevelwa, Misha na Itonjanda.

- Kisima cha Kitete Mjini kifanyiwe ukarabati kwani kina maji safi na hakikauki hata wakati wa kiangazi.
- Mabomba ni chakavu sana tangu Mkoloni.
- Uvunaji wa maji ya mvua kwa mito inayotapakaa kama vile Mto Wala ambao hupokea maji mengi toka sehemu mbalimbali.

Natoa shukrani kwa Wizara kutimiza ahadi ya Rais alipokuwa Nzega, sasa Bukene maji yanatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono.

**MHE. KHADIJA SALUM AL-QASSMY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuniwezesha na mimi kutoa maoni yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuipongeza Serikali, kwa kuleta Muswada huu wa Sheria Mpya ili uongeze ufanisi katika sekta hii muhimu, hasa ukizingatia kuwa maji ni muhimu kwa uhai wa binadamu, pamoja na viumbe vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu wa sheria ukipita, itungwe kanuni haraka ili iweze kutoa nafasi nzuri zaidi za utendaji kwani hivi sasa katika nchi yetu, bado upatikanaji wa maji ni mgumu hadi kufikia wananchi kunywa maji ya tope au kunywa maji pamoja na wanyama, ambayo si salama kwa afya zao na kuwahatarishia maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ipange bei za maji kwa kuzingatia hali ya maisha ya watu, sio kuwapangia bei ambazo haziwezi kulipwa na wananchi. Vile vile naomba wahakikishe kwamba, bili wanazolipa ziwe sawa na matumizi sio; kuwakisia watu na kuwabambikizia madeni ambayo hayalingani na matumizi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu ametujaalia nchi hii ina vyanzo vingi vya maji na kwa kweli ni aibu kwa nchi hii kukosa maji safi na salama kwa asilimia kubwa, kwani wenzetu nchi za nje wengine hawana maji baridi, lakini wanageuza maji chumvi kuwa maji baridi na wananchi wanafaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iipe Wizara hii kipaumbele katika bajeti kwani maji ni uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali iangalie sana katika Kiwanda, hasa kwa kuzingatia siku za karibuni tumeona kwenye vyombo vya habari vikionesha jinsi ya maji taka na yenye sumu, yakitiririshwa katika makazi ya watu na kuwasababishia madhara makubwa na vile vile kuharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. JACOB D. SHIBILITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa kutoa nafasi hii ili nitoe mchango wangu. Nianzie kwa kutoa pongezi kwa Waziri wa Maji, Mheshimiwa Profesa Mwandosya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Chiza na Katibu Mkuu, Ndugu Wilson Mkama, kwa kazi nzuri ya maandalizi ya Muswada huu. Pia nawashukuru Wakurugenzi na Watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu umechambuliwa vizuri sana, hivyo nauunga mkono asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kupitisha Miswada mbalimbali, pamekuwepo na uzembe wa utekelezaji wa shughuli mbalimbali ambazo sheria nzuri zinazotungwa na Bunge hazifuatwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Maji na Katibu Mkuu, hivi karibuni walitembelea Wilaya ya Misungwi kukagua miradi ya maji. Moja wa maeneo waliyokagua ni Bwawa la Nyashitanda, waliagiza likamilike; kazi imefanyika lakini maji yanayobaki katika bwawa hilo ni kidogo mno, kitu ambacho huenda yakaisha kabla ya msimu wa mvua unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza hayo nikimaanisha kuwa, huenda wataalamu wetu hawaandai michoro mizuri ili kumaliza tatizo la maji. Niombe sana pamoja na kupitisha sheria hii, neno rasilimali ni pamoja na bwawa; ni kitu ambacho kimetumia rasilimali za watu hivyo kama bwawa halitasaidia itakuwa kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri aliahidi kurudi tena naomba katika ziara zake afike ajionee kama kutahitajika marekebisho basi yafanyike mapema ili chanzo hiki cha maji kwa wananchi wa Mwamboku kitumike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Misungwi inafahamika kuwa ina matatizo makubwa, hadi sasa Wananchi wa Misungwi asilimia 35 ndio wanaopata maji safi na salama; hii imeongezeka hivi karibuni baada ya *Quick Win* kukarabati visima katika Wilaya yetu, kabla ya hapo ilikuwa ni asilimia 28 tu.



Hivyo, natoa pongezi tena kwa Mheshimiwa Waziri na wenzake wote Wizarani, kwa juhudi ya kuwapunguzia matatizo Wananchi wa Misungwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sihoji juu ya Mradi wa Maji Misungwi; ule wa kutoka Ziwa Victoria eneo la Nyahiti; kwa sababu hatua zinaendelea vizuri pamoja na Sheria ya Manunuzi ya Umma kuchelewesha baadhi ya mambo; hata hivyo, si vyema kutotambua juhudi za Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sheria hii ni vyema wahusika wenye Mamlaka walazimishwe kuwahi kutatua matatizo ya maji pindi yatokeapo, maana huwa hawana mbadala kutokana na mazoea. Mfano, Mradi wa Maji toka Ihelele kwenda Shinyanga kuna vijiji ambavyo vinapata maji toka chanzo hicho. Pindi bomba au tanki likipata hitilafu ni vyema watendaji/wataalamu wawahi vinginevyo wananchi watatumia maji yasiyo salama na hivyo afya zao kuwa hatarini.

Mwisho, nirudie kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeza Wizara ya Maji kwa kuleta Miswada hii miwili, ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya Wananchi wa Tanzania katika Sekta ya Maji. Pongezi za pekee kwa Waziri wa Maji na Naibu wake, kwa kuiendesha vyema na kwa busara Wizara hii na juhudi zao kuonekana kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie mambo mawili yafuatayo; utwaaji wa maeneo ya wananchi kwa ajili ya miradi ya maji; na umwagaji maji machafu baharini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nia njema Serikali hutwaa ardhi kwa ajili ya miradi ya maji, jambo ambalo ni utaratibu na la kawaida. Hivi sasa kwenye Jimbo langu limezuka balaa la utwaaji na eneo kubwa huko Kisarawe II, Wilaya ya Temeke, kinyume na makubaliano ya awali ya utwaaji wa eneo la mradi.

Mambo yafuatayo yamejitokeza:-

Kwanza, kutumika kwa michoro mitatu tofauti kwa mradi mmoja, hivyo kuwafanya wananchi kutowaamini wataalamu haidolojia ifuate ramani/mchoro upi.

Pili, Mradi kutwaa eneo linalohusisha Majenzi ya Nafuu (Nyumba) wakati kuna eneo kubwa linaloweza kukidhi eneo la mradi bila wananchi kuashiria kubomolewa nyumba zao.

Tatu, ukubwa wa eneo la mradi kiutamulimu ni kubwa sana; hivyo imewafadhaisha wananchi hawa wakilinganisha na Mradi wa Ruvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeyasema hayo kwa madhumuni ya kuiomba Wizara kwa makini katika maeneo hayo.

Utaratibu wa kumwaga majitaka mijini katika bahari au vyanzo vya maji ni utaratibu tuliouzoea lakini kutokana na maradhi ya kisasa yaliyopo (HIV), inasemwa eneo la kumwaga majitaka kutoka Hospitali ya Aga Khan, Ocean Road ni hatari kwa jamii na kusababisha harufu kali na uzito wa maji. Hii inawezekana ni kutokana na njia fupi iliyojengwa kutoka Hospitali hadi kwenye kimwagio. Ujenzi wake ungestahili uwe kama ulivyojengwa na Hospitali ya Ocean Road ambao hauna usumbufu.

Huu ni mfano tu; hivyo Wizara izingatie namna ya kutoa maelekezo ya ujenzi wa maji taka mijini.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai lakini yapo katika hatari ya kutoweka kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya matumizi yake. Maji yanateketea kutokana na *over-deforestation* (ukataji miti); *over-grazing* (mifugo); *over-cultivation* (kilimo); na *over-population*.

Napendekeza Wizara isimamie vyanzo vya maji kwa kushirikiana na Wilaya hadi ngazi za vijiji na kuweka alama za mpaka za kudumu. Vilevile ninashauri yafuatayo:-

- Ng'ombe wazuiwe kua vyanzo vya mito hasa katika Mabonde ya Rukwa, Luiche, Malagarasi, Usangu, Ruaha, Pangani, Dakawa, Ruvu, Kilombero, Ruvuma, Rufiji na kadhalika.
- Mikakati ifanywe kutunza vyanzo vya mito yote iliyoko Mikoa ya Kusini na Kusini Nyanda za Juu ili kuzuia maji katika mito mikuu yasikauke.
- Serikali ichague mabonde mazuri na makubwa kama Mtera, Tokanya, Hombolo na kadhalika na kujenga mabwawa makubwa ya maji ili kuongeza maji nchini
- Serikali itoe mwongozo kuhusu madhara ya miti ya kigeni (*exotic trees*) ili miti hiyo isipandwe ovyo nchini.
- Ng'ombe watunzwe na kufugwa katika Mikoa ya Kati, Tabora, Singida, Dodoma, Arusha na kujenga mabwawa kwa matumizi ya mifugo. Taifa liwe na programu ya kujenga mabwawa
- Kila kijiji nchini iwe na mikakati ya kutunza vyanzo vya maji na kuvuna maji.
- Bodi za maji zipewe madaraka makubwa ya kutunza vyanzo vya maji
- Mito na vyanzo vyote vya maji nchini viorodheshwe na viwe vinakaguliwa na kuandikiwa ripoti ya utunzaji kila mwaka.

- Vyanzo vya maji viwekewe mipaka kama mashamba ya Hifadhi ya Taifa (*National Parks*).

*It is now or never.*

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Miswada hii Bungeni, ambayo tumeisubiri kwa hamu sana. Aidha, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara yake, kwa kazi nzuri na ngumu inayofanyika. Nipende kuanza ku-*declare interest* kwa kukumbusha kuwa mimi ni Mjumbe wa Bodi ya Mto Pangani, lakini kama Mbunge wa Kilindi ni moja wa wadau wakubwa kutokana na tatizo kubwa la maji ndani ya Wilaya ya Kilindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, *Director of Water Resource* atakuwa ndiye mwenye jukumu la kumshauri Waziri kuhusu masuala yote ya maji. *Page 15 (item 15(2))* na *page 18 (item 20 (2 na 3))* kuwa pia kutakuwa na *National Water Board* ambayo ina *advisory role, duplication of roles*, nashauri ili ku-*coordinate* ushauri huu kwa Waziri, *Director of Water Resource* awe kwenye Bodi ya Maji ya Taifa.

Pili, *page (item 21(a))* inazungumzia kuwa watajadili, yaani *National Water Board* masuala yoyote yanayohusu Sekta ya Maji ambayo yatapeleka kwao na Waziri au Wizara nyingine zozote, (*Sector Ministry*) na watapendekeza utekelezaji kwa Waziri au *Sector Ministry*. Napendekeza kwamba, kulingana na utawala bora na vilevile ili kwenda kwa utaratibu ni vyema yote yakapitia kwa Waziri wa Maji tu, yawe yanatoka kwenye *Sector Ministries* au kwingineko yote yatokee kwa Waziri au ofisi yake. Ku-*deal directly* na *Sector Ministry* kunaweza kuleta mchanganyiko. Napendekeza kipengele hiki cha *Sector Ministry* kiondoke.

Tatu, natambua wazi kuwa mgawanyiko wa mabonde si lazima uzingatie *Administrative Borders*. Lakini ni *reality*, ni ngumu sana ku-*manage* usimamizi wa maji katika Wilaya moja kwa kupitia mamlaka za mabonde zaidi ya moja. Kwa mfano, Wilaya ya Kilindi, sehemu moja iko chini ya Bonde la Mto Pangani na sehemu nyingine iko chini ya Bonde la Mto Wami. Napendekeza kuwa ingekuwa ni utekelezaji mzuri na wenye tija, kwa sababu sehemu kubwa ipo chini ya Bonde la Mto Pangani, Kilindi ikabaki katika mamlaka moja tu. Hili liko chini ya mamlaka ya Waziri.

Nne, kuhusu *Membership of National Water Board, first schedule* inasomeka; *at least of one third of members should be women*. Nadhani kwa dunia ya leo, wanawake hawawi *limited* hivyo. *At least* isomeke; *gender balance should be considered* kwani wanawake wanaweza kuzidi wanaume vilevile. *Just imagine*, Waziri akiwa mwanamke anaweza kuteua wanawake zaidi, je, wakati huo tuandike *at least one third should be men. It doesn't really sound healthy*.

Tano, *page 19 (item 23)*, kwa vile wataalamuu wa maji wanapatikana katika mabonde yetu kwa mfano, *groundwater experts hydrologists*; na kwa kuwa kwa siku za karibuni tumeona wakandarasi wanavyovurunda katika utekelezaji wa miradi, ambapo

baadhi fedha zimetumika na miradi kutokamilika. Napendekeza katika kazi (*functions*) za Wataalamu wa Bonde, watumike pia kwenye utafiti wa maji katika mabonde husika na Wizara ikubaliane na wafadhili kama *World Bank* ili watambue hawa ndiyo wataalamu na ndiyo ambao wanaelewa maeneo hayo vizuri. Aidha, fedha watakalolipwa zitakuwa chache kuliko hawa wakandarasi. Ikibidi iwe ni lazima wataalamu hawa wawe ndiyo wanafanya utafiti, na ndipo wakandarasi wachukue tenda za utekelezaji wa miradi.

Sita, Bodi ya Mto Pangani tuliomba turuhusiwe tupandishe viwango vya *water user fees*, lakini tulijibiwa kuwa tusingi kidogo kwani litakuwa ni zoezi la nchi nzima. Sasa kwa vile Bonde letu watumiaji maji wameelewa umuhimu wa huduma hii na wao ndiyo wamekuwa wakiomba tuangalie viwango hivyo, ili Bonde liweze kutoa huduma nzuri zaidi; hivyo, nilikuwa naomba kama itawezekana kupitia kifungu cha 25 na 26 (uk.26), viangaliwe ili mabonde yapange viwango vyake kulingana na matumizi na uelewa wa watu wanaowahudumia; hii itaongeza bajeti na hivyo ufanisi wa kazi ya usimamizi na udhibiti.

Saba, kifungu cha 23 (*page 20*), kuna kipengele kinachohusu *Basin Board to advise Director on technical aspects of trans-boundary water issue*. Kipengele hiki nadhani kinahitaji kuongezewa nguvu kwani kwa mabonde ambapo kuna *trans-boundary water* mfano, Jipe, taarifa zimekuwa zikitolewa kuhusu magugu maji, nadhani kutoa taarifa pekee haitoshi, kuna haja ya ku-*empower* mabonde ili yaweze kushughulikia masuala haya kwa kushirikiana na nchi zinazopakana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ni muhimu sana Miswada hii kupita kesho. Ahsante.

**MHE. MKIWA A. KIMWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba kuchangia Muswada wa Maji uliopo mbele yetu.

Kwanza, napenda kumshukuru Waziri wa Maji na Umwagiliaji, pamoja na Naibu wake. Pili, napenda kuwafahamisha kuwa katika Jiji la Mwanza, angalau sasa kuna sehemu ambazo zilikuwa hazipati maji na hivi leo zimeanza kupata maji. Pia nafurahi kwa Muswada huu kuletwa kwa wakati muafaka. Mimi binafsi napenda sheria hii iwabane wale wote ambao wanaharibu vyanzo na pia kuvichafua. Katika Ziwa Victoria kuna uchafuzi mkubwa wa Ziwa hilo, hata kufikia baadhi ya hoteli kubwa au viwanda vikubwa kuelekeza mabomba ya maji taka ndani ya ziwa hilo.

Tunaitaka Bodi ambayo itateuliwa, ifuatilie hilo na pindi watakapobaini kuna uchafuzi kwa mtu yeyote achukuliwe hatua kali, tusiishie kutunga sheria na bila kuzitekeleza. Mfano, Sheria ya Maji ambayo inatamka kwamba, kama mtu yupo chini ya mita 400 anahitajika kupatiwa maji bila matatizo. Sheria hii inawasaidiaje watu waishio kando ya Ziwa Victoria kama Kata za Sangabuye, Bungogwa, Kirumba, Mkolani na nyinginezo, ambao hajawahi kupata maji safi na salama, japo wanaishi kando ya Ziwa; pamoja na sheria hii inayojadiliwa Serikali inasema nini pia kuhusiana na hili? Hamwoni kama ukosefu wa maji safi kwa watu hawa unaweza kuwa ni chanzo cha

uchafuzi wa maji, kwa kufua na kuoga, kuosha vyombo na hata nguo za wagonjwa wa magonjwa ya mlipuko kama kuhara ambazo zinafuliwa moja kwa moja ziwani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali pia itoe elimu ya kutosha kwa watu juu ya utunzaji wa maji ili waweze kujua nini ambacho kinafanyika na wao wajibu wao ni nini? Pia tuomba huduma za maji kwa kulaza mabomba hayo katika barabara kuu, Serikali ijue kwamba watu ambao wanaishi barabara za ndani ya mitaa wengi wao hawana uwezo wa kununua mipira ya maji zaidi ya miwili kwa sababu ya ukosefu wa fedha; hawaoni kama watu hawa wanakosa haki yao ya msingi, pia maji safi na salama?

Gharama ni kubwa sana katika uunganishaji, naishauri Serikali kupitia Wizara yako na sheria za maji, impunguzie mzigo Mtanzania hasa Mama wa Kitanzania, ambaye ndiyo anapata tabu ya maji. Akina mama wengi ndiyio ambao wanapata shida ya maji na wengi huyafuata mwendo mrefu sana. Ahsante.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Miswada hii ya Maji ni muhimu na imekuja wakati muafaka, ukizingatia maji ni muhimu katika maisha ya kila siku ya mwananchi bila maji hakuna uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na sheria hii kutoihusisha Jiji la Dar es Salaam kwa sababu wana sheria ya DAWASCO, lakini bado matatizo ni mengi katika Jiji la Dar es Salaam. Nashauri kwamba, ili sheria hii mpya iweze kufanya kazi katika hii Mikoa mingine, lazima Serikali kupitia Halmashauri, watoe elimu ya kutosha jinsi ya kutunza vyanzo vya maji. Kwa mfano, pale Moshi katika Mto Njoro kuna (chemchemi), chanzo cha maji lakini wakazi wa pale wanaitumia sehemu ile vibaya; wanaosha magari katika eneo lile na maji yale watu wanayatumia kwa matumizi ya kunywa na kupikia. Hii inaonesha ni jinsi gani watu hawajapata elimu ya kutosha jinsi ya kutunza vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili sheria hii iweze kufanya kazi lazima Wizara ya Maji na Miundombinu washirikiane kwanza kwa kuanza kujenga (*Central Sewerage System*), *especially* katika Mji wa Mwanza. Kwa wale watu wanaoishi Milimani, je, majitaka ya nyumba zile huwa yanaelekezwa wapi? Mvua zikiinyesha maji machafu huchanganyika na maji safi na hii hupelekea magonjwa ya mlipuko. Hivyo basi, kuna kila sababu sheria hii ifanye kazi na mifumo hii isijengwe karibu na mifumo ya maji safi kama ilivyo katika Jiji la Dar es Salaam, maji safi wakati wa mvua huchanganyika na maji taka.

Mwisho kabisa, kwa kuwa maji ni muhimu katika kukuza uchumi na hata kilimo kunategemea maji, nashauri Wizara ya Maji wapewe bajeti ya kutosha ili waweze kuchimba visima kwenye vijiji kwa bei nafuu, kwa sababu bei za sasa ni za juu sana, ambapo mwananchi wa kawaida ambaye hata mlo mmoja kwa siku ni shida, hawezi kuchimba kisima.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kuunga mkono hoja iliyoko mbele yetu. Muswada huu ni muhimu pale tu

utakapotekenezwa ipasavyo. Swali langu ni kwamba; je, Wizara hii itawezaje kutekeleza azma za Muswada huu kwani bajeti yake kila mwaka huwa haikidhi mahitaji?

La pili, Muswada huu pia unazungumzia kuhifadhi vyanzo vya maji, lakini kuna wafugaji ambao wengi wao hutumia maeneo ya vyanzo vya maji kwa kunyweshea mifugo yao kwa kuwa Serikali haijawatoshelezea mahitaji ya mifugo yao kwa kuwajengea malambo. Hivyo, kwa ushauri wangu, Wizara ihakikishe inatengewa bajeti ya kutosha ili iweze kujenga malambo ya kunyeshwea ng'ombe na hapo itaweza kufanikisha zoezi la kulinda na kutunza vyanzo vya maji.

La tatu, kuna maeneo mengine ni makame sana, kiasi kwamba hata namna ya wananchi wa maeneo husika hupata tabu sana ya kupata maji. Je, Muswada huu unawapa nafasi gani watu wa maeneo kame?

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi sina ila naunga mkono hoja na Mungu awatangulie katika kutekeleza hoja kwa manufaa ya Watanzania wote. Ahsante.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, napenda kumpongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote, kwa kuleta Muswada huu. Muswada huu umefika muda muafaka, kwani sheria zilizokuwepo za mwaka 1949 na ya 1974 ni za zamani; zimepitwa na wakati. Sheria hizi ni nzuri zaidi ukilinganisha na sheria zilizopita, Muswada huu unatoa nafasi pana kwa watu wa kawaida, sekta binafsi au jamii kushirikishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kuna watu siku hizi wanalima kwenye mabonde hadi kwenye kingo za mito, maji yanapungua na mto kukauka kabisa. Katika Muswada huu nimeona vitendo hivi vinakatazwa, lakini sikuona ni adhabu gani atapewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, *water user permit* ilikuwa ikitolewa, basi inakuwa ya kudumu. Muswada huu unatoa nafasi kwa Bodi za Maji za Mabonde kupanga *duration* ya *water user permit*. Nashauri ili kuleta usawa katika mabonde yote, Wizara ingepanga muda wa umiliki ili kila bonde lizingatie, badala ya kila moja kuwa na utaratibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne, kipengele cha 44(2), kinatoa adhabu kwa mtu anayevuta maji zaidi ya kiasi alichoruhusiwa. Kipengele cha 55(1) na (2) kinatoa adhabu kwa yule anayepanua visima na kutumia maji zaidi bila ya *water permit*. Kipengele cha 51(3), 101 na 103, vyote vinatoa adhabu au faini. Naona kima cha shilingi 300,000 hadi 500,000 au 1,000,000 ni kidogo. Kiwango kwenye sehemu zote nilizozitaja, adhabu iwe kati ya shilingi 5,000,000 hadi 10,000,000.

Tano, kipengele cha saba, *Director of Water Resources* ataandaa rejesta ya *water permits*. Napendekeza vile vile kuwe na mikakati ya kutafiti na kuandaa rejesta ya *water resources* za Taifa hili, kila Bonde liwe na listi ya vyanzo vyote. Hii itasaidia katika kupanga mipango ya utoaji maji kwa wananchi wetu sasa na baadae.

Sita, Muswada huu unazipatia Bodi za Mabonde na Mabonde majukumu makubwa. Hii ni hatua nzuri, kwani inapeleka madaraka karibu na watu. Tatizo ni kuwa katika mabonde na hasa Bonde la Ziwa Victoria, kuna upungufu mkubwa wa watendaji na wataalamu; nafasi nyingi zipo wazi. Majukumu ya bonde yanahitaji *hydrologists*, *limnologists* na *environmental engineers* wanaojua sayansi ya ziwa na kadhalika. Sheria hii ikishakuwa tayari ili iweze kusimamiwa vizuri, inabidi mabonde yote yawe na watumishi na wataalamu wa kutosha.

Saba, kadiri Watanzania wanavyozidi kuongezeka, migogoro ya maji inazidi. Ofisi ya Bonde la Ziwa Victoria haina Mwanasheria, migogoro yote inabidi ipelekwe Wizarani. Hali hii inachelewesha ufumbuzi, tunaomba Ofisi ya Bonde la Ziwa Victoria ipewe Mwanasheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, Watendaji wengi wa Bonde akiwemo na Afisa wa Bonde, wanapata mishahara midogo. Kazi wanazotakiwa kufanya ni kubwa na nyingine ni za hatari; ili kuwaongezea ari ya kufanya kazi, naomba kuwepo *incentive package* na mishahara iongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, naipongeza Wizara ya Maji kwa kuleta Maafisa Maendeleo ya Jamii. Maafisa hawa sasa wanafanya kazi nzuri ya kuhamasisha juu ya matumizi mazuri na endelevu ya maji na umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji. Watu wengi wamezoea kuwa maji ni ya bure, walipewa na Mwenyezi Mungu, basi Maafisa hawa watasaidia kuwaelewesha na kuhamasisha ulipaji (*water user fees*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya mabonde ni makubwa, bodi zinaandaa mipango mizuri, lakini hazipatiwi fedha za kutosha. Ninaomba bajeti za ofisi za mabonde ziongezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa maji katika uhai wa viumbe vyote na Taifa kwa ujumla, udharura wake ni muhimu kwa wananchi, wakaelezwa vizuri wakati Waziri atakapokuwa anatoa majumuisho. Naunga mkono hoja hii ya Waziri na kumpongeza sana Waziri kwa jinsi alivyoiendesha vizuri Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, atoe maelezo ya kina kwa nini maeneo ambayo yana maji ya bomba (hasa mjini), huchimba visima sehemu hizo bila kibali rasmi kitakachozingatia usalama wa maji kwenye visima vyenyewe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bonde la Rukwa lina Bodi ambayo wajumbe wake wote wanatoka sehemu mbalimbali; lakini hakuna hata mjumbe anayetoka Mkoa wa Rukwa ambao una eneo kubwa la Bonde lenyewe. Nashauri Mheshimiwa Waziri, aone uwezekano kumpa nafasi mjumbe kutoka Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niishukuru sana Wizara, kwa jinsi wanavyotusaidia kufanikisha Mradi Mkuu wa Maji unaofadhiliwa na Benki ya Dunia. Ombi kwa Wizara hii ni kufuatilia utekelezaji wa Mradi huu kwa karibu, kutokana na matatizo ya umbali na Dar es Salaam. Umbali huu, unasababisha kushindwa kupata wazabuni wengi na wenye uwezo unaostahili. Umbali huu unatuwia vigumu kuwapata wataalamu wa kutosha kuendesha shughuli za usimamizi kitaaluma, kutokana na kukosa vivutio vya kuishi Mikoa ya pembezoni, Waziri alipe kipaumbele suala hili Sumbawanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Mheshimiwa Waziri atoe mapendekezo kwa Mamlaka za Miji kuona njia ya kuwapunguzia gharama wakazi wa miji wakati wa kuunganisha maji taka kwenye mfumo mzima. Mamlaka nyingine zinatoza shilingi 5,000, lakini nyingine hazitozi hata senti moja. Je, isingekuwa vizuri tukaandaa mwongozo unaofanana kwa miji yote ya kati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia kwa maeneo ambayo yanachukuliwa kwa ajili ya hifadhi ya vyanzo vya maji na kadhalika ni budi yapatiwe ufafanuzi na hasa kwa kuwa sheria ya fidia ambayo iko wazi na ukiifuatilia utaona kuwa, vigezo vinavyotumika siyo vibaya na vikitumika ipasavyo na ieleweke na kila mmoja; malalamiko yanaweza kupunguza hisia ya kudhani Serikali inawaonea. Mheshimiwa Waziri au Mheshimiwa Naibu Waziri, ingefaa wakalifafanua hili (taratibu za fidia).

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kumilikisha maeneo ambayo mabomba ya maji yanakopita kuwa chini ya mamlaka za maji. Nashauri kuwa katika maeneo ya Miji, kazi hii ni budi ifanywe kwa uangalifu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Serikali lazima iendelee na sera yake ya kutoa huduma ya maji kwa bei nafuu kwa maeneo yenye kipato kidogo. Suala la ruzuku kwa maeneo kama hayo ni budi yakapewa mwongozo kitaifa ili kuwe na mtiririko unaofanana katika miji yetu mbalimbali. Elimu kwa watendaji wote na wadau (wananchi) wote, ndiyo nguzo kuu ya kupunguza matatizo mbalimbali yahasuyo maji kama rasilimali muhimu kwa Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hizi.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niupongeze Muswada huu wenye madhumuni ya kutoa huduma za maji na usafi wa mazingira. Malengo ya Muswada huu kwa mujibu wa Muswada ni mazuri, yanayozingatia ushirikishwaji wa wananchi, kinachohitajika ni utekelezaji tu.

Aidha, bado yapo maeneo ambayo yana changamoto za miundombinu ya maji; naomba kushauri wakati umefika wa kutafakari pale inapobidi huduma hizi za miundombinu za kutoa huduma ya maji ifanyike na sekta binafsi, lakini kwa uangalizi wa Serikali na Wizara.



Mheshimiwa Mwenyekiti, sio sawa kwa mfano eneo kama Dar es Salaam kuna Bahari ya Hindi, bado maeneo mengine yanapata maji kwa mgao; mfano, Jumatatu, Jumanne na Ijumaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mvua hatuna miundombinu fasaha ya kutunza maji ya mvua. Kwa mfano, Mkoa wa Iringa, Mto Ruaha unapita maeneo mengi sana, lakini tumeshindwa kujenga hata bwawa kwa ajili ya umwagiliaji, uvuvi, kupendezesha mazingira na kadhalika.

Kifungu cha 4(f), *promotion of public/private sector partnership*; nashauri utaratibu huu uongezwe kasi, ari na nguvu.

Ukurasa 11, kifungu cha 5(6), wajibu wa Waziri wa Serikali za Mitaa; atawajibika kuhakikisha kuwa Serikali za Mitaa zinatekeleza matakwa ya sheria ya maji.

Katika Muswada huu, *section 31* imetajwa sana; ni vyema kuonesha kama ni *section 31 of this Act or other; example, 13(1)(b) section 31; 8(1)(b) section 31; 8(1)(c) section 31*.

Kifungu cha 17, *Chief Executive Officer* awe *appointed for a term of 5 years*, lakini hii haimzuii endapo akikosea kuwa *fired*; kwani ilani inatekelezwa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la maji linapokuwepo hasa katika kaya, kimsingi wanawake ndio wanateseka sana; wao hutumia muda mrefu kutafuta maji hasa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara itafakari kuweka huduma za maji katika shule za msingi na sekondari na yawe maji safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naogopa kutafakari mazingira ya vijijini, ambako watoto hutembea muda mrefu kwenda shule na wakifika hadi saa nane mchana anasoma na baada ya hapo anahitaji nusu saa kufika nyumbani tena bila maji na akifika nyumbani anatumwa akachote maji.

Naomba miundombinu ya maji iwepo lakini ni vyema kufikia pia miundombinu itoe maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 18, *section 21* inaeleza majukumu ya *supply and sanitation authorities* na kwa mujibu wa Muswada huu, kutakuwa na *public private partnership*. Ningependa kujua endapo *water supply provider* wanafanya kazi kinyume na kanuni, taratibu na sera; je, watawajibika vipi? Sheria haisemi *beneficiary* wa *water services* atalindwaje?

*The Water Resources Management Act, 2009*; tukianza na tafsiri ya *water* kuna maneno *or (7) "works" or (8)*.

*Section 4(c)* baada ya neno *of water* badili *in the public* nashauri iwe *for public interest*.

*Section 5.7 duty to protect water resources; imetambua individuals tu vipi kuhusu company na mashirika?*

Masuala ya *pollution, section 39* haijieleza endapo *company* au *individual* aki-*pollute* maji atawajibika vipi, lazima iwe ni kosa (*offence*) na kuwepo na *penalty*?

Ukurasa wa 64, first schedule, section (4); *the Minister may dissolve the National Water Board*, hakuna sababu.

Section 13(13), *offence*; sehemu ya 56 *offence* zote zimezingatia *any person* na sio *company* ikanyang'anya leseni, stop order, *penalty* na kadhalika.

Ukurasa wa nne wa Muswada umezingatia sana mtu badala ya shirika au *company*; mfano kifungu cha 43(1), *a person who direct...*

*Section (7); every person residing in mainland* hasa *company* za vinywaji baridi au moto, bia, soda na kadhalika. Kampuni za madini na kama ni *company* hata faini yake inabidi iwe tofauti. *Section (44); any person ... section (87) no person ... 87(3)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji yetu ni safi lakini sio salama. *Section 4(1)(b)*, wametuambia ni haki ya msingi ya mwanadamu (*basic human right*). Sehemu ya (x) imeelezea kuhusu mabwawa kuwa ni maeneo ya uwekezaji; Iringa Ruaha Ipogolo Dam, Wilaya ya Ludewa kuna vyanzo vingi; Makete Dam.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, pamoja na Naibu wake, kwa Muswada huu wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kitu cha lazima sana katika maisha au uhai wa binadamu na kila Mtanzania ana haki ya kupata maji safi na salama na Serikali inatarajia kuunda bodi/vyombo katika ngazi mbalimbali, kwa nia ya kusimamia rasilimali maji. Tatizo langu ni hili; kutokana na Serikali kuunda vyombo vingi vya kusimamia rasilimali maji, ada na tozo mbalimbali zitakazotowza zitafanya maji kuwa ghali na Mtanzania wa kawaida kutomudu gharama za maji. Bodi zitakazoundwa zitahitaji posho itakayotokana na ada au tozo na tumeona katika maeneo mengi, Kamati za Maji zimeshindwa kazi kutokana na kukosekana kwa mapato. Ushauri wangu ni kwamba, vyombo vitakavyosimamia rasilimali maji vipunguzwe au viwe na vyanzo vingine vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukosefu wa watumishi ni tatizo kubwa katika ngazi ya vijiji na kata; na hasa katika usimamizi wa miundombinu; je, sheria itawasaidiaje wananchi katika hili?

Wataalamu wa rasilimali maji wanapogundua eneo lenye chanzo cha maji, taarifa itolewe mapema kwa wananchi ili wasiendeleo kuendeleza eneo husika; kama maendeleo

yalikwishafanyika, wananchi wa eneo husika walipwe kwa wakati ili wakafanye shughuli za maendeleo maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna utaratibu mbovu wa Idara ya Maji kutoa bili za maji kwa watumiaji au wananchi, hata kama maji hayakupatikana kwa kipindi kirefu; huu ni uonevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kuwa *water table* kwa Mkoa wa Dodoma iko juu; hivyo gharama ya kuweka miundombinu ya maji kwa wananchi siyo ghali. Je, ni lini Wananchi wa Mkoa huu na hasa Wilaya za Bahi, Chamwino, Kongwa na Dodoma Mjini, watalipwa huduma ya maji safi na salama na hasa maeneo ya vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitafurahi kusikia kuwa sheria hii itakapotekelezwa itawabana wachimbaji wa madini wanaoharibu mazingira kujali athari zake; mfano mzuri wa wachimbaji hao ni machimbo ya dhahabu ya Mkoani Maza, Buhemba Gold Mine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utunzaji wa mazingira, maeneo ya ujenzi wa makazi ya watu uzingatiwe ujenzi wa nyumba usiozingatia utunzaji mazingira mkoani Mwanza hasa katika milima ya mkoa huo. Najiuliza maji machafu, uchafu unaotoka katika nyumba zilizojengwa bila mpangilio; Serikali inasemaje katika hili? Wananchi washauriwe mapema kabla ya kuendeleza eneo husika kwa nia ya kutunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROFESA IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Waziri wa Maji, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu, pamoja na Watumishi wote wa Wizara. Hongera nyingi sana; kwanza, kwa kutupatia ujenzi wa mradi wa maji katika Mji wa Utete, Ikwiriri na Kibiti. Hata hivyo, bado naiomba Wizara initimizie upatikanaji wa maji katika Vijiji vya Kiwanga, Ngorongo, Nyikanza na Kipo mpaka Kipugira.

Pongezi nyingi sana kwa kuleta Miswada hii ya miwili; Miswada ni mizuri na haina utata. Hakuna ubishi kwamba, imeletwa kwa wakati, naomba Wizara ifikirie mambo yafuatayo:-

(a) Mto Rufiji unamwaga maji yake Indian Ocean; tutafanya mipango ya kutumia maji ya Mto Rufiji kwa matumizi ya majumbani, umwagiliaji, *hydropower* na kwa uvuvi.

(b) Kwa vile 80% ya magonjwa hasa ya kuhara (kwa mfano, *WHO* 2000, watu bilioni nne waliugua kuhara dunia nzima na kulikuwa na vifo 2.2 milioni). Kwa hiyo, huduma za maji ni muhimu; tuhakikishe tunawapatia maji watu wengi.

(c) Mafunzo iwe na Programu Maalumu ya Kufundisha Wahandisi na Hydrogeologists kwa wingi. Chukua mfano wa Baba wa Taifa, katika kutekeleza Programu ya Maji Tanzania 1970s, aliamrisha mafunzo kwa wahandisi zaidi ya 200 kwa

kuwapeleka India wataalamu wengi wa Wizara hiyo, takriban wengi wanang'atuka kwa umri (Kata Mti Panda Miti).

(d) Tunaomba *National Hydrographic Survey* ifanywe nchi nzima ili kubaini kiasi cha maji chini ya ardhi (*ground water*), yako kiasi gani kwa kila mkoa Tanzania. Tutengeneze ramani ya maji chini ya ardhi iwekwe katika mtandao ili iwe rahisi kurejea taarifa za maji chini ya ardhi nchi mzima. Kuna matatizo ya *aquifer depletion*; nchi zifuatazo tayari zimepata matatizo ya *over pumping* nazo ni Beijing, Manila na Bangkok. Naiomba Wizara ifanye utafiti juu ya *underground water potential* kwa Mji wa Dodoma, tusije tukapata *acquife depletion*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Muswada wa Raslimali ya Maji naomba yafuatayo yafanyike:-

(a) *Section 18, page 17*, naomba iongezwe *subsection* ya 8 ya kumlinda huyu *authorized officer* katika kutimiza majukumu yake anaweza akaumiza au akaumizwa, lazima apewe kinga ya kisheria; anaweza akaingia mahali na akashambuliwa; je, ni sheria au section gani itakayomlinda?

(b) *Section 79, page 44*, naomba tuongeze *National Water Register* ya pili, itakayoshughulikia *water inventories*; yaani mito yetu maziwa, mabwawa, *underground water potential* yetu, visima vingapi nchi nzima na tufahamu kila kisima kinatoa maji kiasi gani. Taarifa hizi zitolewe kila mwaka na ikiwezekana ziwekwe katika mtandao wa *internet for easy reference*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie Muswada huu. Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake, kwa kuandaa Muswaada huu muhimu sana katika ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia. Naunga mkono hoja hii.

Kwanza, niseme kwamba, katika nchi yetu tumejaaliwa kuwa na maji mengi sana, ambayo yapo ardhini na katika vyanzo mbalimbali tumeshindwa kwa muda mrefu sana kuweza kuyatumia ipasavyo; hivyo, naiomba Serikali kwanza itoe taaluma ya kutosha kuanzia ngazi ya vijiji, juu ya utunzaji wa rasilimali hii muhimu, kwani matumizi ya maji ni mabaya mno katika maeneo yote.

Serikali ijikite zaidi kuhakikisha kuwa, wananchi wetu wanafikiwa na huduma hii huko vijijini ili tuweze kuitumia sheria hii ipasavyo na tuwahakikishie upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na upungufu mkubwa wa maji kadiri siku zinavyosogea, hii inatokana na mahitaji zaidi ya huduma hii; je, Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na hali hii hasa kwenye maeneo ya miji ambako kuna ongezeko kubwa la wakazi, viwanda na hivyo kupelekea maji kuhitajika zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusisitiza juu ya uchavuzi wa maji, kwani kumekuwa na uharibifu wa maji kwa sababu hakuna tofauti baina ya matumizi ya maji kwa mifugo na matumizi ya nyumbani; je, kuna mikakati gani iliyoandaliwa ya kuwaelimisha Watanzania juu ya matumizi mazuri ya maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijitahidi kuweka mikakati madhubuti kuhusu uvunaji wa maji ya mvua, mbona kuna maeneo watu wanavuna maji ya mvua na kutumika katika kipindi cha mwaka mzima. Elimu ya utunzaji wa maji itiliwe mkazo na miundombinu ya maji iboreshwe kwani maji ni uhai.

**MHE. MWANTUMU B. MAHIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa wakati. Maombi yangu ni yafuatayo:-

Vijiji ambavyo vyanzo vya maji vinapita au kuanza viheshimiwe na ufanywe utaratibu ili nao wapate maji. Inatia huruma pale ambapo maji yapo kwao, lakini wakazi hawapatiwi mbinu za kutumia maji hayo mfano ni Hale, Korogwe na Muheza. Aidha, umiliki wa vyanzo vya maji uzingatie haki za binadamu; vipi chanzo kiwe Muheza hati miliki iwe ya Tanga?

Naomba Wananchi wa Muheza wapatiwe maji ili wawe hamasa ya kutunza chanzo hicho cha Mto Zigi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya maji ishirikishe zaidi wadau hasa uanzishwaji wa mifuko ya maji; elimu kubwa inahitajika, kwani wananchi walio wengi wanadhani si jukumu lao. Naamini elimu pekee itasaidia kuwezesha vyanzo vya maji kutunzwa na kuendelea huduma hiyo kwa jamii. Naomba semina, warsha na mikutano juu ya utunzaji wa maji, vitolewe haraka ili kunusuru uharibifu wa maji na vyanzo vyake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapata tabu kuona ni wapi katika Miswada ambapo suala la *demand management* limewekwa wazi. Hii ina maana kuwa upotevu wa maji utazidi kuendelea kwa vile sheria haipo wazi, inayompa DWR kuweka kiwango cha juu cha upotevu wa maji unaofanywa na watumiaji wa maji kama vile Mamlaka ya Maji Mijini na kadhalika. Sheria ni vyema ikataja hili badala ya kuja kutungiwa kanuni pekee. Kanuni zitaainisha kiwango kinachoruhusiwa kupotea na adhabu zake.

Hakuna adhabu zinazooneshwa kwa wavunjaji sheria chini ya *Wetland Ramsay Protocol* ili kutunza maeneo haya ambayo ni vyanzo vya maji. Pia sheria ingeeleza wazi; maingiliano yake na uvunaji wa misitu unaolenga kuharibu vyanzo vya maji. Sheria ya Maji inatakiwa iwe *supra* kwa kudhibiti uharibifu wa vyanzo vya maji kama vile *wetlands*, misitu na ukulima unaoharibu *river/lake banks* na *siltation* ya vyanzo vya maji. Sheria ya Maji (WRA) chini ya DWR ni vizuri ikawa *supra* kwa sheria za misitu, kilimo na *energy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii, kumpongeza Waziri wa Maji na Umwagiliaji, pamoja na Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu, ambao wamechangia Miswada hii kuhusu Rasilimali muhimu ya Maji, pamoja na Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hizi zimekuja kwa wakati muafaka, naziunga mkono hoja zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ningependa kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibali cha matumizi ya Maji (*Water Use Permit*) ni kizuri kumpa haki na kumlinda aliye nacho na kuhakikisha kutokuwepo matumizi mabaya kwa sehemu inayohusika. Ipo haja ya utekelezaji wa sheria hii chini ya kanuni au vipengele fulani, kutoa fursa kwa wananchi kutumia kiasi fulani cha maji; kwa mfano ingawa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya Tanga imepewa *water rights* ya Mto Zigi; hakuna mantiki kwa wananchi wanaokaa kando kando ya Mto huo chini ya Bwawa la maji Mabayani kutoruhusiwa kutumia maji yanayomiminika kutoka kwenye bwawa hilo kwenda Bahari ya Hindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na udhibiti, nadhani ipo haja ya kuwaruhusu wananchi wanaoishi kando kando ya Mto Zigi chini ya Bwawa la Mabayani kuwa na utaratibu mzuri wa kuruhusiwa kutumia maji hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa taasisi zinazohusika na uendeshaji na udhibiti wa rasilimali za maji na huduma za maji na usafi wa mazingira ni mpana mno na unaweza ukawa na gharama kubwa zaidi ya tija na ufanisi unaotarajiwa na pia kwenda kinyume cha dhana ya madaraka kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ngazi ya Kitaifa, Wizara na *EWURA* zingetosha kwa kazi ya kusimamia Sera ya Udhibiti; sioni umuhimu wa kuwepo Mamlaka ya Kusimamia Mfuko wa Taifa wa Utekelezaji wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuamini kwamba, madaraka ya Mheshimiwa Waziri kuteua Wajumbe wa Bodi za Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira zitahusisha Mabaraza ya Serikali za Mitaa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama vile sheria hii inavyotoa haki na ulinzi kwa mamlaka za maji, naamini sheria pia itazipa wajibu mamlaka hizi kuwahudumia na kuwatendea haki wateja wao ipasavyo na mamlaka hizi kuwajibika kisheria pale ambapo zinatoa huduma hafifu na kuwatoza wateja wao isivyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja kwa Serikali kwa ujumla, kuiwekea Sekta ya Mtaji kipaumbele maalumu ili kukidhi kilimo, viwanda na shughuli nyingine

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote mbili.

**MHE. JUMA SAID OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujalia uzima na afya na hivyo kuweza kushiriki kikao cha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maji ni Uhai kwani viumbe vyote vinategemea maji kwa uhai wao; kwa mfano, binadamu na wanyama wanategemea mimea kwa ajili ya kupata chakula, bila ya kuwepo kwa maji mimea haiwezi kutengeneza chakula na hivyo kutoweza kuishi. Mimea ikitoweka, hapana shaka binadamu na wanyama nao watatoweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatumia maji kwa mahitaji mbalimbali kama vile kupikia chakula, kunywa, kumwagilia katika kilimo cha umwagiliaji na kadhalika; hivyo maji ni muhimu na lazima kwa viumbe vyote vilivyo hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina mito mikubwa, maziwa makubwa, pamoja na bahari, ambamo ndani yake viumbe mbalimbali wakiwemo samaki wanaishi. Samaki na baadhi ya viumbe wengine wanaoishi majini, wanatumika kama chakula na pia biashara ambayo husaidia kuwapatia kipato wananchi pamoja na kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maji ni muhimu sana kwa uhai na maendeleo ya binadamu, kuwepo kwa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ni jambo muhimu sana. Hivyo, kuletwa kwa Miswada hii miwili ya sheria hapa Bungeni ni muhimu na jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna migogoro kati ya wakulima na wafugaji kuhusiana na suala zima la maji; ni vyema sheria zikaweka wazi kuhusu utumiaji wa maji si kwa wakulima na wafugaji tu, bali kwa watu binafsi, taasisi mbalimbali na mashirika mbalimbali ambayo yanatumia maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna uharibifu wa vyanzo vya maji unaofanywa na watu binafsi, pamoja na taasisi mbalimbali; ni vyema elimu ikatolewa kuhusu umuhimu wa kulinda na kutumia rasilimali za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna ukosefu wa mvua unaosababisha ukame takriban kila mwaka; ni vyema elimu ya kuvuna maji ya mvua ikatolewa ili yaweze kusaidia wakati wa upungufu wa mvua, badala ya kuyaachia yaishie baharini tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hizi.

**MHE. DKT. GUIDO G. SIGONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya kero kubwa katika huduma za maji na usafi wa mazingira ni uchafu wa maji taka

yanayobadilika kuwa madimbwi. Kwa mfano, maeneo mengi, miaka ya nyuma hasa mijini, yalikuwa na miundombinu ya mifereji ya kutoa maji taka. Hivi sasa mifereji mingi kwenye maeneo hayo imeziba, kiasi cha kusababisha kuwepo kwa madimbwi ya maji taka.

- (a) Je, Sheria imetoa ushauri wa suluhisho gani katika kurekebisha hali hiyo?
- (b) Maeneo karibu yote mifereji imeziba sababu ni kutokana na kujenga majengo juu yake; je, sheria inatoa suluhisho gani juu ya miundombinu ya maji taka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya Ziwa Rukwa pamoja na yale ya Mlima Kwimba yameathirika vibaya sana kutokana na uharibifu unaofanywa na binadamu wenyewe; matokeo yake Ziwa linaendelea kukauka, wakati Mlima Kwimba, Jimbo la Songwe, miti inakatwa, kiasi cha kusababisha ukaukaji wa chemchemi na vyanzo vingine vya maji. Je, Sheria inatoa suluhisho gani juu ya hali hiyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbona asilimia 60 ya *pump* zilizofungwa kwenye visima Wilayani Chunya hasa kwenye Jimbo la Songwe zimeharibika kabla hata ya kumaliza mwaka mmoja tangu *pump* hizo zifungwe?

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Naibu Waziri, pamoja na Watendaji wote wa Wizara, kwa kuuleta Muswada huu ambao ni mzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ripoti ya Tatu ya Maji ya Dunia ya Umoja wa Mataifa (3<sup>rd</sup> UN WWDR), ambayo chimbuko lake ni *Rio Earth Summit* ya 1992 na Tamko la Umoja wa Mataifa la 2000, ambapo katika taarifa hii, Jumua ya Kimataifa imeweka malengo kupunguza kwa asilimia 50 tatizo la maji ifikapo 2015, kwa watu ambao kwa sasa hawapati au hawana uwezo wa kupata maji safi na salama.

Ripoti hii inasisitiza kwamba, malengo haya yatafikiwa kwa kuweka mikakati ya kusimamia rasilimali ya maji (*developing water management strategies*), kwa hiyo, Muswada huu ni muhimu sana ili kuweza kufikia malengo haya ya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu malengo ya maendeleo ya dunia, Tamko la Malengo ya Milenia, linasisitiza kwamba, utekelezaji wa malengo yaliyo mengi yanategemea sana upatikanaji wa maji safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *goal* namba moja; *Eradicate Extreme Poverty*; Taarifa ya *World Water Development* inaonesha kwamba, kiwango kikubwa cha umaskini kina uhusiano mkubwa sana na sehemu ambazo wananchi wanapata shida ya maji. Kwa hiyo, usambazaji wa maji vijijini, utasaidia sana kupunguza umaskini na hivyo kufikia Malengo ya Milenia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wengi hasa wa kike, wanashindwa kumaliza shule za msingi kutokana na kutumia muda mwingi kutafuta maji sehemu ambazo maji



hayajafika. Hili ni moja ya Malengo ya Milenia kuona kwamba, watoto wote wanapata elimu ya msingi. Kwa hiyo, kusimamia rasilimali ya maji ni muhimu sana katika kufikia Malengo ya Milenia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Waziri atoe taarifa kuhusu Miradi ya *Quick Win* imefikia wapi? Sasa hivi Wilaya ya Makete ina vijiji 10 vilivyopendekezwa kwenye mpango huu, wananchi wangependa kujua utekelezaji wake upo katika kiwango gani? Miradi hii itasaidia sana kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ianzishe miradi ya uvunaji wa maji ya mvua katika Mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SAMSON F. MPANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Muswada ulioletwa mbele yetu, ambao kwa maoni yangu naona umechelewa kidogo, napenda ushauri ufuatao uzingatiwe katika Muswada huu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hydrogeological map ya Tanzania ni ya zamani sana, ingetakiwa iboreshwe ili kuondoa mtafaruku kati ya wakazi na upatikanaji wa maji chini ya ardhi, ili kuondoa adha kwa wakazi waishio kwenye sehemu zenye maji chini ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *outcrop aquifer* naomba iundwe sawia na chanzo cha maji, kwa kuwa mabonde sita kati ya tisa yaliyogawiwa hapa nchini ambayo yana ushirikiano na nchi nyingine, kuwepo ushirikiano na usimamizi wa tunzo na tozo stahiki ili kuepusha migongano kati ya nchi na nchi. Napendekeza kuwepo na bodi inayosimamia maji hayo. Aidha, *trans-boundary aquifers* zitafitiwe na zilindwe ipasavyo.

Kwa kuwa Sera za Maji (2002), mikakati, na hadi leo sheria, imechukua muda mrefu sana; napendekeza zitungwe kanuni haraka ili kuonesha umaana wa kuanzisha Sera ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, japo matatizo mengi yapo kwenye miradi mikubwa kama vile *Quick Win* iendane na mpango wa awali ulivyoandaliwa, mfano Wilaya ya Kilwa tumepata Mradi wa *Quick Win* visima kumi, lakini hakuna kisima hata kimoja kilichochimbwa au maandalizi ya miundombinu yake kama vile umeme na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Muswada huu uzingatie pia walemavu katika utumishi angalau asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kuunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naanza kwa kuunga mkono hoja zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuunga mkono hoja, bado ningependa nirudie kilio changu cha kukumbushia ahadi ya Serikali ya kurudisha miundombinu katika vyanzo vya maji vya Mkululu, Chiwambo na Lupaso.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili sasa linataka kuwa hadithi tu, badala ya kuonekana kweli tunajali watu. Sasa ni mwaka wa tatu tangu suala hili lizungumzwe, lakini mpaka sasa Serikali imekuwa na kigugumizi katika kutimiza ahadi zake. Kwa jicho la huruma, naomba Serikali itimize ahadi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria hii inakuja wakati muafaka, tunaomba watendaji wa mamlaka haya wawe ni watu ambao wana uchungu mkubwa kwa wananchi ambao wana matatizo makubwa. Wawe na tabia ya kwenda vijijini ili wakashuhudie wenyewe jinsi wananchi wanavyohangaika kutafuta maji kwa maisha yao. Wawe wakali kwa watu ambao wataonekana wanakiuka taratibu na sheria za utunzaji wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusirudie makosa ya kuwaacha watu wa mijini kuhodhi maji kwa kujiwekea *motor* wao wenyewe bila kupata kibali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. WILLIBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja ya *Water Resources Management* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji, kwa kuuleta Muswada huu muhimu, ambao nimeuomba tangu 1998 na Wizara kutuma Wataalamu wake Wilayani Karatu na hususan kufanya ukaguzi wa *Water Rights* kwenye mito yote, kwenye mashamba ya mikataba (*kahawa*), katika maeneo ya Oldeani.

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, naupongeza sana Muswada huu ambao katika vipengele kadhaa unaondoa sasa ule utaratibu wa kutoa haki kwa mmiliki mmoja wa mto mzima, kama ilivyotokea kwenye maeneo ya Oldeani, ambako wananchi wengi kwenye vijiji vilivyoko *down stream*, yaani chini ya mto, kunyimwa kabisa maji kwa kuwa mto mzima unaelekezwa kwenye kumwagilia kahawa na mamia ya wananchi wanaotegemea mto huo kukosa kabisa maji kwa matumizi ya nyumbani (kunywa, kupikia na matumizi ya kawaida ya binadamu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi, ni imani yangu kuwa, baada ya sheria hii kupita, Wataalamu wa Wizara/Bonde, watapita upya kufanya tathmini ya mito hiyo ili maji hayo yagawanywe kwa uwiano kati ya mashamba ya mikataba na wananchi hasa wa Vijiji vya Endasharpwet, Changarawe na Mangola Juu na hasa Vitongoji vya Midabini ambavyo vimenyimwa kabisa maji.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu, kabla ya kifungu cha 45 (kabla ya *Schedule*) kufanya kazi, kigezo kikubwa kiwe ni kuangalia mahitaji ya wananchi kabla ya mahitaji ya kibiashara hasa inapohusu kutoa kibali (*water right*). Wafanyabiashara wanao uwezo wa kuchimba *bore holes* au visima virefu, ambavyo wananchi wa kawaida peke yao hawawezi. Mathalan, Wilaya ya Karatu ambapo visima hivyo vinaenda umbali wa kati ya mita 150 – 200 chini ya ardhi, yaani mara mbili ya urefu wa uwanja wa mpira ni lazima sheria ilinde kwanza wananchi wake, kwani maji ni uhai kabla ya biashara, japo biashara nayo ni muhimu.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri haraka sana, sheria hii ikipita Waziri atengeneze Kanuni anazotakiwa kutengeneza kwa mujibu wa kifungu cha 45(5); vinginevyo, suala hili likiachiwa holela wananchi wataumia sana. Hivi sasa kuna maeneo ndoo ya maji ya lita 20 inauzwa kati ya shilingi 300 na 500, wakati Sera ya Taifa ni shilingi 20 tu; ni muhimu sana kuwalinda wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri, anipe ufafanuzi wa kina kuhusu kifungu cha 49(2)(a) na 50(1 - 3), kama *principle ya beneficial use of whole permit... no permit shall be cancelled or reduced except in propotion with all other permits granted...*” Mheshimiwa Waziri, anajua kuwa wananchi wetu katika maeneo mengi hawana hati miliki; je, katika hali kama hiyo hasa kwa Vijiji vya Endashangwet na Mangola Juu Wilayani Karatu, ambapo mashamba ya kahawa yalichukua Hati Miliki ya mito mizima. Naomba nihakikishwe Wananchi hao watanufaika vipi na sheria hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri ya neno *beneficial use of water* hainipi uhakika wa kipaumbele katika maeneo yaliyotajwa kati ya *social, economic and environmental*. Katika vijiji visima vinakosa maji; kipaumbele kinakuwa wapi?

Sheria ya 1973 angalau ilitoa kipaumbele kwa binadamu kwanza kuliko haya mengine. Naona tukiachia hivi hivi, tafsiri hii inaweza kuleta mgongano mkubwa. Nilitegemea tafsiri hii itapewa pia kipaumbele katika vipengele vya sheria ili kumlinda binadamu kwanza kabla ya mengine yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani za dhiti. Nitaunga mkono Miswada hii nikipata tu majibu ya kuridhisha katika maeneo haya muhimu sana, katika kumlinda mwanadamu hasa kwa mifano ya Wilaya ya Karatu, ambayo hakuna *surface water* na kidogo iliyoko imemilikiwa na wakulima wakubwa wachache (*up stream*), bila kuacha hata tone la maji kwa vijiji (*down streams*).

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami nishiriki kuchangia Muswada ulioko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nami natoa rambirambi kwa Waheshimiwa Wabunge, waliopata misiba mbalimbali kama ilivyotolewa na Mheshimiwa Mwenyekiti; kwa ujumla poleni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa aina ya pekee naomba kuwapa pole ndugu au rafiki zangu, watoto wa Mzee wetu Adam Sapi Mkwawa, Spika Mstaafu, kwa msiba uliowapata wa mama yao mzazi. Poleni sana, nasema Roho za Marehemu zipate Rehema kwa Mungu zipumzike kwa amani. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye hoja iliyopo mbele yetu. Sisi sote tunajua kwamba, maji ni uhai. Ili maji haya yasilete madhara kwa binadamu, napenda kuwapongeza Waziri na Naibu Waziri, kwa kuleta Muswada huu sasa, ukiwa shirikishi kwa wadau wote.

Muswada huu unashirikisha wadau wote; hivyo, wote watajua kwamba ni mradi wao wataungalia kwa makini. Itakuwa tofauti sana na ile miradi ya zamani, ambayo ililetwa na Serikali ambayo ilikuwa ikiharibika watu hawajali. Wizi wa vyuma chakavu ulikuwepo kwani watu hawana uchungu navyo. Kwa Muswada huu, wadau wanashirikishwa hadi ulinzi na usalama, hivyo watalinda bila tatizo. Kwa kuwa wanajua tatizo la maji lilivyo nchi nzima, mimi naamini watalinda bila tabu na bila manung'uniko kwani ni chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka kuchangia kidogo, kwani ni mmoja wa Wanakamati ambao tumeipitia kwa undani zaidi. Njia za mabomba yanapopita hakuna alama yoyote hivyo watu wanajenga juu bila kujua; hivyo kama Wizara hii ikishirikiana na mipango miji ili miundombinu mingine kama hii ya maji ijulikane au ipangwe ipasavyo ili bomba lijulikane linapita wapi. Ziwekwe alama kama vile kwenye *TAZAMA Pipe Line* kote ili bomba/mabomba yaangaliwe hivyo kuzuwia watu wasijenge juu yake au wasilime na pengine kulibomoa. Anayetokea kuharibu bomba hili au njia yote ya bomba, basi apewe adhabu kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, pale panapopita bomba la maji taka, usafi wa mazingira basi isiwe hiari bali wote wajiunge katika mfumo huu na washiriki kikamilifu ili kulinda na hapo utaona wale wanaoachia vyoo vyao au maji machafu, watajulikana na hivyo watakatwa. Muswada huu shirikishi ni mzuri mno; kila mtu (*community* nzima), itaona mali yao na wapewe elimu kwamba, maji ni uhai wasipoyatunza yatawadhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiria kutoa huduma kwa watu binafsi na kuyauza itakuwa tatizo, hasa kwa wananchi wetu kule kijijini ambao wamezowea kuteka maji bure. Nafurahi kukuarifu kwamba, wanapenda na wapo tayari kuchangia na kuuangalia mradi ili wapate maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kueleza kwamba, maji mengi sana yamepatikana Bukene ila bado hayajafika Mjini Bukene. Mkinisukumia yaweze kufika kwenye matanki ili yapatikane majumbani ni safi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Miradi ya *Quick Wins* sisi bado hatujaipata, lakini watu wapo tayari kushirikishwa kuwa na miradi mingi ya maji ili wapate maji. Lengo ni kupata maji na wapo tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuipongeza Serikali kupitia Waziri Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, pamoja na Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Injania Chiza, kwa kuleta Miswada hii miwili, ambayo ni muhimu sana kwa maslahi ya Watanzania wakiwemo Wananchi wa Mkoa wa Singida, hususan wanawake ambao ni watumiaji wakuu wa maji. Pongezi hizi ni pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara na Wataalamu wote walioshiriki kuandaa Miswada hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, kabla sijaanza kutoa maoni au ushauri wangu, napenda kuunga mkono Miswada hii na ninawatakia utekelezaji mwema wenye tija kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukiri kuwa Miswada hii ni muhimu sana kwani maji ni muhimu sana kwa maisha ya binadamu, wanyama, mimea na matumizi ya nyumbani. Hivyo basi; ni vyema kupitia Miswada hii kutunza vyanzo vya maji, pamoja na kuvuna miti ya mikaratusi, ambayo ina tabia ya kunyonya maji mengi sana. Miti hii ipo sana Manispaa ya Singida na kasi ya kuivuna ni ndogo sana. Athari ya miti hii ni kubwa sana, kama kweli tunapitisha Miswada hii ni vyema kauli itolewe ya kuivuna haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kuwa, yapo mabonde ambayo yanatunza vyanzo vya maji, bali watu wamevamia maeneo hayo na kujenga nyumba za kuishi na kusababisha kuua vyanzo hivi vya maji. Matumamini yangu ni kuwa, Miswada hii miwili ikipitishwa, itasaidia mabonde yenye kuvamiwa wataondolewa watu ili vyanzo hivyo viendeleo kuhifadhi maji kwa maslahi ya uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua wazi kuwa, Serikali ilipitisha utaratibu wa kuvuna maji ya mvua kwa kilimo na matumizi ya nyumbani, bali mkakati endelevu ni mdogo sana. Kupitia Miswada hii miwili, Mradi huu upewe kipaumbele ili kuondokana na tabia ya kupoteza maji ya mvua ovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mradi wa Kilimo cha Umwagiliaji, ambao Singida upo maeneo mengine hususan Wilaya ya Manyoni ili mradi huu wa Singida uzae matunda. Ninaiomba serikali iende Singida kuangalia mashine zote zilizofungwa kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, zenye piston moja zilifungwa upya ili ziwe na nguvu ya kusukuma maji. Kupitia Miswada huu, ninaiomba iwe changamoto kwa Waziri na Naibu Waziri, kuja Singida kuona mashine hizi zenye piston moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la maji mijini; mfano, kwenye Manispaa ya Mji wa Singida, kwani vituo vya maji (*Vioski*), bado ni vichache. Hivyo basi, kwa malengo ya Miswada hii ni vyema kipaumbele kitolewe kuongeza vituo vya maji, Manispaa ya Singida, pamoja na maeneo yenye kufanana matatizo nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru Serikali kupeleka maji vijijini, lakini bado kuna tatizo la utunzaji wa maji hayo na utaratibu wa kuuza maji hayo ili mashine inapoharibika kuwe na fedha za kutengenezea. Utaratibu huu bado sio mzuri, fedha zinaliwa tu na Kamati za Maji. Miswada iweke utaratibu mzuri, pamoja na kusambaza bomba hadi kwenye makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa kujitahidi kutoa huduma ya maji kwa wananchi. Napenda kushauri kuwa, kuwe na utaratibu endelevu kuweka dawa ya kuua vijidudu kwenye matenki ya maji ili wananchi wanaotumia kuepukana na maradhi yanayotokana na maji, kwani wananchi wengi huwa hawachemshi maji ya kunywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kurudia tena kuunga mkono Miswada hii na nikiwa na matumaini kuwa, utekelezaji wake baada ya kupitishwa utazaa matunda makubwa.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naungana na waliotangulia, kutoa pole kwa familia za Mheshimiwa Phares Kashemeza Kabuye na Mama Asha Mkwawa, aliyekuwa mke wa Spika wa Kwanza wa Bunge letu, Hayati Chifu Adam Sapi Mkwawa. Mungu awape subira ndugu wote wa Marehemu, ambao wametangulia mbele ya haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu suala zima la maji. Kama inavyosemekana, maji ni uhai, tuyatunze nayo yatutunze. Napenda kumuuliza Mheshimiwa Waziri, vyanzo vyetu vya maji vinatunzwa vipi kwa vile kuna watu kwa makusudi wanafanya juhudi ya kuhakikisha wanavihujumu vyanzo vyetu vya maji? Tanzania ina rasilimali ya maji mengi kutokana na mito yetu na maziwa mbalimbali tuliyonayo. Ni sababu zipi zinazopelekea Serikali kushindwa kusambaza maji sehemu kadhaa zilizokosa maji? Mpaka leo Watanzania katika baadhi ya sehemu wanaendelea kutumia maji ambayo siyo safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chakusikitisha zaidi, bado binadamu wanashirikiana maji na wanyama na ushahidi upo; katika Barabara Kuu ya Dodoma - Dar-es-Salaam, wapo wananchi wanaoshirikiana kutumia maji ya mabwawa, pamoja na wanyama kwa kuoga, kufulia, kupikia na wanyama kunywa vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu wakazi wa Jiji la Dar-es-Salaam. Hali inayojitokeza inahatarisha maisha ya wananchi. Wapo baadhi ya wananchi wanaokata mabomba ya wenzao na kujiunganishia wao. Katika kitendo hicho cha ukataji bomba na kuunganisha kwingine, huwa kuna uchafu unaoingia; utakuta si wananchi wote wanaochemsha maji ya kunywa. Kwa utaratibu huu, inaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko. Waziri anatuambia nini kuhusu vitendo hivi viovu vinavyofanywa na wananchi wasiwatakiwa mema Watanzania wenzao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uharibifu mkubwa unaofanywa na baadhi ya wafanyakazi wa maji. Wanatumia nafasi yao kama mafundi waunganishaji wa maji, matokeo yake wanaharibu mabomba na mbaya zaidi maji yanatiririka na kupotea ovyo ardhini na wakati mwingine kuharibu mazingira kwa kuwepo na hali ya maji maji, ambayo baadaye huleta rangi ya kijani katika maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia pia kuhusu maji taka. Katika Serikali zetu za Mitaa, kuna baadhi ya mitaa ina utaratibu mzuri wa maji taka, ambayo yanaunganishwa moja kwa moja kwa mashimo makubwa (*Central Sewerage System*). Tunaiomba Serikali ihamasishe wananchi kutumia huduma hii ya maji taka kwa vile itasaidia kuepuka magonjwa ya mlipuko na pia gonjwa sugu la malaria linaweza kupungua kutokana na kupungua kwa mashimo yaliyopo katika nyumba za walala hoi, ambao wanachimba vyoo ambavyo ndivyo nyumba za kuzalia mbu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji taka yanapomwagwa kuna usalama gani kwa wananchi? Katika Jiji la Dar-es-Salaam, Wilaya ya Ilala, Kata ya Vingunguti, ndiko yanapomwagwa maji taka. Je, Serikali inatueleza nini kuhusu usalama wa wananchi wanaoishi jirani na mabwawa hayo ya maji taka?

Pia kuna yale magari ambayo yanabeba maji taka ambayo wakati yakielekea sehemu husika, huwa yanapita barabarani na wakati mwingine maji humwagika na hupeperushwa na upepo na kuwafikia wapita njia au kumwagika katika viwiliwili vyao. Je, Mheshimiwa Waziri, haoni hii ni hatari kwa jamii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, isitoshe Serikali haiwezi kutafuta njia mbadala ya usafirishaji huo wa maji taka. Badala yake mabomba ya kunyonya maji taka huwekwa kiholela tu juu ya magari; nashauri yahifadhiwe vizuri. Je, wafanyakazi wa majitaka wana usalama gani kutokana na kazi hii nzito wanayofanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kuzungumzia kuhusu matumizi ya maji ya bahari. Kuna baadhi ya nchi, hutumia maji ya bahari kwa shughuli mbalimbali isipokuwa kunywa tu, baada ya utaratibu wa kuyasafisha kufanyika. Mara nyingi wenye hoteli ambao wako ufukweni ndio wanatumia njia hiyo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha wawekezaji wa hoteli zilizopo kwenye fukwe za bahari kutumia maji haya ya bahari kwa shughuli zao ili kupunguza matumizi ya maji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niipongeze Wizara kwa kuleta Muswada huu, wakati huu ambapo rasilimali nyingi za maji zimeharibiwa kiasi kikubwa. Naamini, baada ya sheria hii kupita, rasilimali za maji zitaendelea kulindwa na kuboreshwa. Naunga mkono Miswada hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuboresha Miswada hii, naishauri Wizara iharakishe uundaji wa kanuni ili sheria itakaposainiwa na Rais, ianze kutumika haraka. Aidha, naishauri Wizara kupitia Sheria hii, kulinda rasilimali za maji. Hivi sasa vyanzo

vya maji kama Milima ya Livingstone, Mto Ruaha na Kilimanjaro, vimeharibiwa sana. Naiomba Wizara katika utekelezaji wa Sheria hii ni vyema ikashirikiana kirasilimali na Wizara ya Maliasili, Idara ya Misitu na Nyuki ili kuongeza nguvu za kifedha na kisheria kulinda misitu ambayo ni vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara pia iratibu matumizi ya maji, hasa kwa matumizi ya kilimo na ufugaji. Wafugaji wachimbiwe mabwawa ili wasitangetange hadi maeneo ya hifadhi kwa kutafuta maji. Naiomba Wizara isaidie kuimarisha vikundi vya matumizi ya maji (*Water User Associations*), ili viweze kujiendesha, badala ya wajumbe wake kufanya kazi kwa kujitolea na hivyo kukosa motisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naipongeze Wizara kwa kujenga visima Bukoba. Kwa kweli wamejitahidi lakini kwa upande wa vijijini bado. Muswada huu ni muhimu sana kwetu sote, lakini ili ukae vizuri ni muhimu Wizara ya Maji ikae na Wizara ya Ardhi wanaosababisha uharibifu wa vyanzo vya maji kwa kutoa ardhi iliyoko kwenye vyanzo hivyo na kuwapa wananchi wanaojenga na kulima. Mtu anapatumia kwa shughuli zake analazimika kujenga kwa gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji inanza kuwahamisha hao watu kuhusu vyanzo vya maji; je, hii sio gharama kubwa kwa Serikali na inaitoa Serikali lawama? Je, ni kwa nini Serikali imewazuia kwa kuweka mabango sehemu zote za mijini pamoja na vijijini watu wakapewa elimu?

Uchafuzi wa mazingira hasa kwa maeneo kama ya Dar-es-Salaam; watu wanakata mabomba makubwa wanachota maji na wenye mabomba wanaletewa bili; unaripoti hawafuatilii, ukizunguka mtaani unakuta maji yanamwagika. Mvua ikinyesha maji safi na maji machafu ya viwandani na kwenye masoko wanayafungulia yanachanganyika yanaingia kwenye mabomba yanayokatwa halafu watu wanakunywa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindupindu tayari kwa wakazi na kuna vijiji ambavyo viko mbali na mito hasa kwa sehemu ambazo walichimba visima maji yana rangi kama yamewekewa maziwa. Wangesaidiwa kujengewa visima, hasa Vijiji vya Bukoba Vijijini, Karagwe na Mkenge. Muswada huu ukipita nao wasaidiwe kujengewa visima wafaidike na mradi wa maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, Wizara ya Ardhi wadhibitiwe kugawa vyanzo vya maji, pamoja na ukataji wa mabomba udhibitiwe. Tukishadhibiti tutafaidika na maji tuliyonayo hasa sisi, maji ya kunywa tunatumia ya Uganda na sisi tutafaidika nayo. Kwa hiyo, mchango wangu ndio huo; maji ni uhai kwa kila kiumbe chenye uhai au mwanadamu. Ahsanteni.

**MHE. MWAJUMA HASSAN KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuweza kuchangia mada iliyoko mbele yetu.



Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake wote katika Wizara hii. Maji ni muhimu sana na mabadiliko ya sheria yamekuja wakati muafaka, kwani yatarekebisha mambo mengi ambayo yana utata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vileile naipongeza Serikali kwa kutaka kuanzisha Mfuko wa Maji ili wananchi waweze kukopa, lakini natoa angalizo; huduma hii itolewe kwa usawa, isije kuwa na upendeleo na iwafikie walengwa. Serikali ihakikishe inasomesha wataalamu wengi, kwani katika Wizara hii kuna upungufu mkubwa wa wataalamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali inapotoa ankara za maji wahakikishe kuwa ni za uhakika, kuliko kuwakisia wananchi na kuwapa ankara ambazo si za matumizi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na ninaomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji na Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza. Nichukue fursa hii, pia kumpongeza Katibu Mkuu wa Wizara na Watendaji wa Wizara hii, hasa kwa kuleta Muswada huu muhimu ndani ya Bunge hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wahenga walivyonena kuwa; maji ni uhai na bila maji uhai wa binadamu, viumbe na mimea, hautakuwepo; maneno haya ni sahihi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuletwa kwa sheria hizi mbili kutasaidia kwa namna moja ama nyingine, kuiboresha sekta hii na hata kujenga mazingira kwa wenye nacho na wasio nacho kuwa na haki sawa katika matumizi ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na zawadi hii ya maji toka kwa Mungu, lakini siku hadi siku matatizo ya maji yanaendelea kuathiri jamii, hasa jamii iliyo na hali duni kutokana na taratibu ambazo hazikuwagusa.

Upungufu au ukame unaoathiri nchi yetu unatokana na hali ya uharibifu wa mazingira au uharibifu wa vyanzo vya maji.

Wananchi wa kada ya chini waelimishwe juu ya kuifahamu sheria katika masuala muhimu hasa ya kutunza vyanzo vya maji. Elimu itasaidia kuiboresha sekta hii na kuondoa migongano ya hapa na pale. Mamlaka za Halmashauri za Wilaya, Miji na Manispaa, ndizo ziwe wasimamizi wa sekta hii kwa ngazi zote za vijiji na mijini.

Kamati za Maji za Watumiaji kwa maeneo mbalimbali ziwe na majukumu ya kuisimamia sekta hii kwa eneo lake na zifanye mawasiliano na mamlaka zilizopo juu yake, yaani Halmashauri kwa masuala mbalimbali.

Eneo la kumi la Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali ya Maji, sehemu inayohusu mabwawa (*Dam safety and flood management*), sheria kwa nini haikutamka namna ya kuyaendeleza mabwawa ya asili au maziwa yale ambayo yanaathiriwa na hali ya mazingira na hata kutishia kutoweka? Mfano mzuri ni Ziwa Kitangiri lililopo Iramba Magharibi, kina chake kinapungua mwaka hadi mwaka. Hivyo ni muhimu sheria ione namna ya kunusuru hali ya namna hiyo ili kulinda ziwa hilo.

Mabwawa yaliyochimbwa kwa shughuli za uvunaji wa maji, sheria iwadhhibiti wale wanaoziba maeneo ya vyanzo ambavyo ndivyo vinavyokusanya maji na kujaza mabwawa hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji holela wa madimbwi unaofanywa na makampuni ya ujenzi, madimbwi hayo yaimarishwe ili yasaidie wananchi katika kukusanya maji kwa matumizi ya binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa sekta hii ya maji, upo umuhimu wa kutumia kwa uangalifu rasilimali inayotolewa na Serikali/Wahisani kwa ajili ya sekta hii ya maji. Wale wanaofuja fedha za sekta hii, lazima sheria iwabane ili kuiimarisha sekta hii.

Fedha za wahisani kama vile World Bank, Water Aid na kadhalika, zielekezwe kwenye Mikoa inayoongoza kwa ukame ili kuwa na miradi mingi, badala ya utaratibu wa sasa wa kugawa fedha kwa kila Wilaya kwa miradi kumi kumi, jambo ambalo tija yake inakuza nguvu kwa maana maeneo mengine yana maji ya kutosha. Pia Waziri alieleze Bunge hili Tukufu ni lini miradi ya awamu ya pili ya fedha za ufadhili wa Benki ya Dunia itaanza hasa Jimbo la Iramba Magharibi. Sheria itaje mamlaka ya watu binafsi, taasisi za dini na mashirika mbalimbali, ambayo yanamiliki maji; namna ipi inayowadhhibiti wamiliki hawa katika kuruhusu wananchi wengine kutumia maji bila vikwazo.

Kufanya hivyo, kutaondoa utata kwa baadhi ya wamiliki kutumia vibaya umiliki wao; mfano mzuri kampuni ya CHICO, wajenzi wa kampuni iliyokuwa inajenga Barabara ya Shelui – Singida eneo la Ulemo (Iramba Magharibi), walikuwa na Kisima lakini walikitumia peke yao na hata walipomaliza kazi ya ujenzi walikiharibu kwa kukijaza kokoto!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. RAPHAEL B. MWALYOSI:** *First, clause 6(2)(b), substitute the word “reserve” with the word “conservation”.*

*Clause 8; Strategic Environmental Assessment should apply to programmes. Therefore the beginning of the clause should say “where a major water programme” is planned ... not water project.”*

*Clause 12(2) should include a statement that such water harvesting works should be subjected to E/A.*

*Clause 22, Basin Water Boards: The Rufiji Basin has another Authority – RUBADA which operates under a special and Legal Act (Rufiji Basin Development Authority Act). This proposed Act ignores the existence of the RUBADA Act and has decided to propose these new Basin Water Boards as if RUBADA does not exist; hence major operational conflict between RUBADA and the Rufiji Water Board. Need for clarification in clause 31.*

*The idea of coming up with integrated Management Plans that include a water balance or water budget is planable but too ambitious especially.*

*(a) When one tries to forecast basin water demands which are not static but ever changing over time.*

*(b) Where one has to determine the supply side which is ever changing/actually shrinking due to climate change and other causes.*

*(c) Considering the costs of determining the supply of water, i.e. obtaining the necessary data information.*

*Clause 34: The idea of possibilities to prohibit human activities beyond 60 metres from ... or a water source is problematic if it is applied without other similar laws addressing prohibition of activities around water sources eg. Environmental Management Act, Agriculture ect. The major problem here is the designation and definition of source.*

*Clause 35(2): Cancellation or reduction of permits should not only consider proportionalities but also priorities that is the relative importance of the water permit e.g. compare the need or permit for domestic water supply with a permit for irrigation farming.*

*Clauses 37 and 38 provide excellent ideas about establishment of protected zones and ground water controlled areas. These initiatives are particularly relevant in dry lands and semi-arid areas.*

*Clause 54: It should be made clear in this clause that ground water permits should be given only as a last resort because frankly this is stored water for use only when we have exhausted surface water sources.*

*Clause 63: Is it not necessary to state the minimum level or amount of discharge that requires a permit to deal with small and insignificant discharge levels which cumulatively may have significant impacts?*

*Clause 98, 99 and 100: I am glad these clauses are in this Act, which gives this Ministry powers over projects such as the Magadi Extraction Project in Lake Natron, which is a trans-boundary water body. It is important the Minister explains the relevance of this Act to the Magadi Project.*

Miswada hii yote haioneshi *impact assessment results* kama zimefanywa hasa kwa vile maji ni rasilimali yenye athari ya moja kwa moja ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwa kazi nzuri mnazofanya, pamoja na mazingira magumu ya ufinyu wa bajeti.

Pili, napenda kuwapongeza kwa kuleta Miswada hii yote miwili kwa pamoja, ambayo ikipitishwa na Bunge letu Tukufu, itasaidia sana kuboresha usimamizi wa huduma za maji katika maeneo ya miji na vijijini na utunzaji wa vyanzo vya maji ambavyo vinaharibiwa sana, ufyekaji, uchomaji na moto kilimo kisichozingatia utalaamu.

Tatu, naunga mkono Miswada hii yote miwili kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono hoja hii, naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwanza, napenda kuishukuru Serikali kwa niaba ya Wananchi wa Mpwapwa, kwa kutupatia mradi mkubwa wa kuboresha huduma ya maji Mji wa Mpwapwa kwa gharama ya shilingi bilioni 2.7. Kwa kuwa huduma za maji ni muhimu sana kwa maendeleo na uchumi wa nchi na kwa kuwa maji ni uhai:-

- Je, Serikali ina mikakati gani ya kufufua miradi yote ya maji ambayo haifanyi kazi vijijini vikiwemo baadhi ya Vijiji vya Wilaya ya Mpwapwa na Mkoa wa Dodoma kwa ujumla?

- Kwa kuwa Mirdi ya Maji ya Awamu ya Tatu inayofadhiliwa na Benki ya Dunia inachelewa sana kutekelezwa kwa Wilaya ya Mpwapwa, Vijiji vya Mima, Kimagai, Mzase, Iyoma na Chunya; je, utekelezaji wa miradi hii utanza lini ili kuondoa tatizo la maji katika vijiji nilivyovitaja?

- Kwa kuwa maeneo kame uwezekano wa kuchimba visima virefu ni mdogo; je, kwa nini Serikali isichimbe mabwawa katika maeneo hayo ili kupunguza tatizo la maji kwenye Mkoa kame ukiwemo Mkoa wa Dodoma na Wilaya ya Mpwapwa?

- Je, Serikali itakubaliana na mimi kwamba, Sekta ya Maji ipewe kipaumbele kwa kutengewa fedha za kutosha kuanzia bajeti ya 2009/2010?

- Katika miradi mikubwa ya maji ipo haja ya kujenga mitambo ya kusafirishia maji (*Water Treatment Plant*) kama vile *sedimentation tank*, *storage tank*, *filtration tank* na *chlorination tank* ili maji yawe safi na salama; hii itasaidia sana kuzuia

magonjwa kama vile *typhoid fever*, kipindupindu, magonjwa ya kuhamisha (*dysenteries*) na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani kwa Waziri, pamoja na Wataalamu wote wa Wizara hii, kwa kuandaa Muswada huu na kuuleta hapa Bungeni.

Kulingana na umuhimu wa rasilimali hii ya maji kwa viumbe vyote, kiukweli haukutakiwa kuletwa kwa Hati ya Dharura ili kutoa fursa ya kusoma na kuchangia vizuri. Tanzania tuna changamoto kubwa sana inayotukabili, kuhusiana na upatikanaji wa maji. Pamoja na nchi yetu kuzungukwa na maziwa, bahari na mabonde ya maji, bado asilimia kubwa ya wananchi wa vijijini hawapati maji safi na salama.

Muswada huu unaeleza kwamba, maji yatakuwa bidhaa kama bidhaa nyingine na hivyo kuweza kupata bidhaa hiyo ni nguvu ya anayehitaji. Ningependa kujua Muswada huu umeangalia vipi uwezo wa Watanzania walio wengi? Uchumi wa familia za Watanzania wengi umezingatiwa kwa kiwango gani? Je, ikiwa upatikanaji wa maji utategemea nguvu ya mwananchi anayehitaji; ni lini Watanzania walio maskini (80%) watapata maji safi ambayo ni haki yao ya msingi?

Kutokana na baadhi ya taasisi zisizo za Serikali kukosa uaminifu na uzalendo, wamekuwa wakitumia ujanja ujanja kutumia rasilimali hii ya maji. Vipi viwanda ambavyo vimekuwa vinatumia maji kwa miaka mingi bila kulipa na wengine wameunganisha maji kwenda kwenye hoteli zao na nyumba zao kinyume na taratibu?

Kifungu cha 44(b); faini kwa anatakayetumia maji bila kibali cha Serikali. Faini ya shilingi 300,000 hadi 500,000 au kufungwa miezi sita. Faini hii ni ndogo sana na haiwezi kutoa fundisho kwa atakayepatikana na kosa kama hili. Mwaka jana White Sand Hotel walipatikana na tuhuma za kuunganisha maji kinyume; vyombo vya habari vilizungumza sana lakini hakuna adhabu ya uhakika ya kutia funzo iliyotolewa. Adhabu kwa kosa hili iongezwe angalau ifike shilingi 3,000,000 au kifungo cha mwaka na kuendelea.

Suala lingine ambalo ni muhimu sana kuzingatiwa; ni jinsi gani watumiaji wakubwa wa maji kama viwanda vikubwa wanashiriki kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji? Hawa wanaweka *pump* za maji mtoni na wanatumia maji mengi sana. Serikali iweke utaratibu wa kuwashirikisha wadau hawa kwenye uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu kali sana zichukuliwe kwa wale wote wanaochafua maji, hasa viwanda vinavyomwaga maji machafu kutoka kiwandani kwenda mtoni. Kwanza, wanaua viumbe ndani ya maji na pili, maji haya yanatumiwa na wananchi. Serikali ianzie Kiwanda cha Sukari Mtibwa kilichopo Turiani – Morogoro. Wamechimba mabwawa ya kukusanya maji machafu, lakini yakijaa usiku

wanayafungulia kwenye mto. Hili ni tatizo kubwa na wananchi wa maeneo hayo wamelalamika sana, lakini hakuna hatua zinazochukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu naomba sana uanze utekelezaji wake Mkoa wa Tabora, ambao Mkoa mzima hauna maji safi na salama. Pale mjini maji wanayotumia wananchi ni kama chai ya rangi. Jambo la ajabu; wakija Viongozi wa Kiserikali, Wataalamu wa Maji wanaweka dawa ya kusafisha maji na hayo maji kuonekana meupe; wakishaondoka maji yanabaki na rangi yake. Hapo ni mjini.

Tabora yenye misitu mingi na mabonde mengi ya maji na vyanzo vikubwa vya maji, bado wananchi hawana maji. Huko Wilayani ndiyo usiseme hali ni mbaya; Wilaya ya Urambo maji yana rangi ya maziwa; vijijini huko wananchi wanachota maji kwenye visima vifupi walivyochimba wenyewe kwa mikono. Maji ya visimo hayo ni hatari kwa afya zao lakini hawana la kufanya.

Suala lingine ni gharama za uchimbaji wa visima virefu ni kubwa sana. Kisima kimoja kina gharama zaidi ya shilingi 15,000,000. Kwa gharama hizi ni ndoto kwa wananchi kuweza kumudu bila kupata ufadhili na wafadhili hawapo. Serikali iangalie jinsi ya kutumia wataalamu wake zaidi na kupunguza gharama hii ili wananchi hata kwa kuchangishana, waweze kumudu.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu wake, Mheshimiwa Eng. Chiza, pamoja na Watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi, hivi karibuni kumekuwa na taarifa mbalimbali, pamoja na wawekezaji wanaotoka nje katika lengo la kuwekeza katika mazao ya kukamua mafuta kama vile jatropha. Mengi kati ya makampuni hayo, yameamua kuwekeza katika eneo la Pwani ya Bahari ya Hindi. Kijiografia, nafahamu kuwa mvua hutengenezwa kwa mzunguko, vivyo hivyo mito na bahari.

Je, Wizara inalizungumzia vipi suala hili? Kuna wataalamu wetu wa ndani wa kutosha kutoa ushauri juu ya hilo na kuona kama hakuna athari ya kuweza kuleta ukame?

Ugawaji wa ardhi unashirikisha Wizara yako ili kulinda vyanzo vya maji?

Muswada huu una athari na mipango ya umeme wa maji i.e. *Stigler's Gorge*?

Hali yetu kuhusiana na *global warming* ikoje (*rate ya problem*)?

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa juhudi alizozionesha kwa kuwasilisha Muswada hii miwili muhimu kwa wakati unaofaa. Naunga mkono hoja hizi mbili kwa asilimia mia moja.

Aidha, napenda kuwapongeza wasaidizi wake; Mheshimiwa Eng. Chiza, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Bwana Wilson Mukama na Watendaji wengine wote Wizarani na kwenye taasisi chini ya Wizara hiyo, kwa kumsaidia Waziri kwa juhudi na uadilifu ambao umemuwezesha kuwasilisha Miswada hii kwa ufanisi mkubwa. Hata hivyo, kwa sababu hali ya Wilaya ya Lushoto ni ya milima, ninaomba mhandisi wa maji mwenye uzoefu. Hivi sasa yupo *technician*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hizi kwa dhati.

**MHE. MGANI I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha maji yanapatikana kwa matumizi ya binadamu na pia kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tupate maji ya kutosha, jambo la kwanza ni lazima tutunze na kusimamia vyanzo vya maji kwa faida ya sasa na vizazi vijavyo. Usimamizi wa vyanzo vya maji, unahitaji ushirikiano mkubwa kati ya Wananchi, Halmashauri za Wilaya na Serikali Kuu. Utatu huu pekee ndio utafanikisha jambo hilo. Sasa ni kazi ya Serikali Kuu kuwashirikisha wadau husika. Mabadiliko ya hali ya hewa yanapelekea tatizo la maji kuwa kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Miswada yote miwili, zinatakiwa ziundwe Bodi zenye uwezo na Watendaji wenye uwezo kwa ngazi zote. Hii itasaidia sana kuilinga na kuitumia vizuri rasilimali maji bila upendeleo na mizengwe. Mpaka sasa usambazaji wa maji umekuwa na urasimu mkubwa, ambao wananchi wengi hawajapata bahati ya kupata kwa uwiano mzuri; inawezekana kabisa ni mipango mibovu inayotekelezwa na Halmashauri nyingi za Wilaya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na wananchi tunaishi Vijiji vya Matongo, Isene, Senene, Munung'una, na Mazazigili, tunaomba tupatiwe maji. Muda wote ambao nimekaa Bungeni, vijiji nilivyovitaja hapo juu ambapo mimi ndiko ninakotoka, hatujapewa maji safi na salama. Nimekuwa naomba kwako, kwa wasaidizi wako na Halmashauri ya Wilaya, mpaka sasa sijafanikiwa. Nadhani kwa kuletwa na kupitishwa kwa Miswada hii mipya; mimi na wananchi wa maeneo niliyoyataja, tutapata huduma muhimu ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Iramba Mashariki kuna skimu mbili za umwagiliaji; Skimu ya Mwangeza na Msingi. Skimu hizi zilijengwa kwa kiwango cha chini, mafuriko yalipokuja mwaka juzi zikabomoka. Serikali iliahidi humu Bungeni kuzitengeneza skimu hizi za umwagiliaji, lakini mpaka leo bado fedha hazijatengwa. Naomba sana, mwaka huu fedha zitengwe kupitia kanda za umwagiliaji, ambapo Mkoa wa Singida uko chini yake, ziweze kujengwa ili kukuza kilimo cha umwagiliaji kwa faida ya Wananchi wa Iramba Mashariki na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii mia kwa mia na naendelea kuwaomba waendeleo kuchapa kazi kwa nguvu mpya, baada ya Sheria hii kupitishwa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri na Wataalamu wote wa Wizara, kwa kuleta Miswada hii. Pamoja na kwamba, Miswada imeletwa kwa Hati ya Dharura, bado ni mizuri kwa sababu nia ni kuweka taratibu nzuri za Sekta ya Maji kwa ujumla. Hata hivyo, naleta masahihisho na maoni yafuatayo:-

(i) Interpretation, clause 3; kwenye tafsiri neno ‘*mean*’ baada ya *customary water rights* lisomeke ‘*means*’.

(ii) Kifungu cha 13(1); nashauri maneno ‘*nation policy*’ yasomeke ‘*Nation Water Policy*’. Kifungu cha 13 (c) maneno *Basin Water Boards* yasomeke *Basin Water Board*. Herufi za kwanza ziwe kubwa.

(iii) Kifungu cha 16(g); maneno *basin water boards* yasomeke *Basin Water Board*. Herufi za kwanza ziwe kubwa.

(iv) Kifungu cha 23(v); maneno *appointment of* yasomeke *appoint the*.

(v) Kifungu cha 34; neno *section* lianze na herufi kubwa *Section* na mahali pengine lilipoandikwa hivyo lisahihishwe kwa mfano kifungu cha 43(1) neno la nne.

(vi) Kifungu cha 36; kinahitaji masahihisho na kisomeke hivi; *where, in the opinion of the Basin Water Board, in the event of the drought and natural disaster...*”

(vii) Kifungu cha 52(1)(d); maneno mawili ya mwanzo, yaani *may be* yaondolewe.

(viii) Kifungu cha 86; nashauri maneno yote yaliyotolewa maana (*definition*), yaende kwenye *interpretation clause 3*, kwa maana hiyo kifungu hicho kifutwe.

(ix) Jedwali la kwanza, kifungu cha 5, kuhusu Waziri kuvunja Bodi ya Taifa ya Maji (Uk. 65) na kifungu cha 4 (Uk. 66); Waziri kuvunja Bodi hiyo hiyo. Nashauri zitolewe sababu zitakazomfanya Waziri avunje Bodi hiyo. Wasiwasi wangu ni kwamba, inawezekana Waziri aliyeteua Bodi hiyo kaondolewa kwenye Wizara husika kaja Waziri mwingine na akataka kuweka jamaa zake. Hivyo, Sheria itaje sababu zitakazomfanya Waziri avunje Bodi za Maji za Mabonde na ile ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema moja kwa moja kwamba, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, ikiwa ni pamoja na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalamu wote wa Wizara, kwa maandalizi yao pamoja na juhudi wanazozifanya kuhusu kuboresha huduma ya maji kwa wananchi.



Pamoja na yote hayo, napenda kuipongeza Serikali kwa juhudi kubwa zinazoelekezwa Wilayani Kibondo na hususan Mkoa wa Kigoma, kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya maji bila matatizo. Wilaya ya Kibondo na hasa Makao Makuu ya Wilaya, kwa Miaka yote tangu tumepata uhuru, bado tatizo la maji ni kubwa na hata tulipokuwa na wimbi la wakimbizi ambao wameondoka na kuacha wananchi wakiwa na hali mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba, Serikali imejitahidi kuondoa tatizo la maji Kibondo Mjini, kwa kutoa fedha kiasi cha shilingi milioni mia moja, bado fedha hizo ni kidogo mno kuweza kutoa huduma ya maji Kibondo Mjini kwa wakazi wapatao 23,000. Kwa masikitiko makubwa, napenda kusema kuwa, suala la maji ni muhimu kwa wananchi; hivyo ni vyema Wizara itambue hilo. Sasa hivi Wananchi wa Kibondo Mjini wanapata maji mara moja kwa wiki, wakati Wizara ingeweza kuweka utaratibu mzuri wa kuondoa kabisa tatizo la maji kwa kuvuta maji kutoka chanzo cha mahi hadi kwa wananchi, mahali ambapo ni kilomita 25 (kwenye Kambi ya Wakimbizi ya Nduta).

Aidha, niipongeze Serikali kwa juhudi za kutenga fedha kwa vijiji (*Quick Wins*). Fedha hizo, pamoja na juhudi za Serikali, lakini bado ni kiasi kidogo mno; ni vyema fedha hizo ziwe zinazotolewa kufuatana na idadi ya vijiji na idadi pia ya wakazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongelea miradi ya umwagiliaji katika Mkoa wa Kigoma, bado haijakidhi mahitaji kwa sababu upembuzi umechukua muda mwingi zaidi ya utekelezaji, kiasi ambacho Wananchi wa Mkoa wa Kigoma wameshachoka. Kwa mfano, miradi ya umwagiliaji katika Mabonde ya Luiche, Mukuti, Kumngondogondo, Kumsenga na Luguzye, uchunguzi wake umechukua muda mrefu kiasi kwamba, wananchi wameshachoka na hadithi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna Wilaya ambayo haina huduma ya maji katika Tanzania nzima, isipokuwa Wilaya ya Kibondo. Naomba Serikali ilionee aibu hili ili kurudisha imani kwa wananchi.

**MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri wa Maji na Umwagiliaji, kwa kuwasilisha Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji ya Mwaka 2009 na Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira wa Mwaka 2009 kwa ufasaha mkubwa.

Miswada yote miwili imekuja kwa muda muafaka na naunga mkono hoja zote mbili. Nianze na Muswada wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji. Nimefarijika sana kuona kuwa Muswada huu hauongelei matumizi ya maji tu bali vilevile ulinzi wa rasilimali za maji hasa vyanzo vya maji dhidi ya vitendo haribifu kama vile uchafuzi wa mazingira na vitendo au shughuli za binadamu zinazosababisha mmomonyoko wa ardhi. Madaraka anayopewa Waziri chini ya Muswada huu ili kulinda rasilimali za maji yanaridhisha.

Ibara ya 103 ya Muswada huu, inapendekeza adhabu ya faini isiyopungua shilingi milioni moja na si zaidi ya shilingi milioni 10 au jela si chini ya miezi sita na si zaidi ya

miaka 2 au yote mawili. Jela na faini kwa mtu yeyote anayekutwa na hatia ya uchafuzi wa mito au vijito. Adhabu hii haina tatizo kwa mtu binafsi, lakini ni ndogo mno kwa kampuni au kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nauona udhaifu au ulaini huo wa adhabu hata chini ya ibara ya 64, ambapo ingekuwa vyema adhabu kwa uchafuzi unaofanywa na viwanda, migodi au makampuni; iwe kubwa zaidi. Vyombo hivyo vina uwezo mkubwa wa kifedha na kitaalamu, kulinda mazingira zaidi ya mtu binafsi. Aidha, Muswada uko kimya kuhusu fidia kwa mtu au jamii inayoathirika kwa uchafuzi wa maji. Nimalizie kwa kujadili kwa kifupi sana; Muswada wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara kwa akili ya ubunifu kuanzisha Mfuko wa Maji. Kunzia miaka ya 90; michango ya mashirika ya fedha duniani kusaidia Sekta ya Maji katika nchi zetu imepungua sana. Aidha, bajeti zetu za kila mwaka ni ndogo mno, kuweza kujibu vilio vya maji nchi nzima. Hivyo, mfuko huo utasaidia kuziba pengo hilo linalolizidi kuwa kubwa. *National Water Investment Fund* inatujengea uwezo wa ndani kutawala mazingira yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia kuunga mkono hoja.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kuleta hoja hii Bungeni. Maji ni uhai.

Mchango wangu ni maji yanayotiririka kutoka Mto Ruhuhu na kuingia Ziwa Nyasa. Ziwa Nyasa lina Mito miwili mikubwa inayoingiza maji kutoka milimani. Mito hiyo ni Songwe - Mbeya na Ruhuhu – Ruvuma. Sina hakika kuhusu hali ya Mto Songwe kwa sasa, lakini kuna uharibifu mkubwa sana wa chanzo cha maji kwenye Mto Ruhuhu. Mto huu haukauki tangu enzi za Adamu na Eva, lakini kwa sasa kuna hofu kubwa sana kwa mto huu kukauka. Hii inatokana na wachimbaji wadogo wadogo, ambao huchimba madini kwenye mashimo karibu na chanzo cha mto huo kisha kuchekecha udongo kwenye chanzo cha maji cha Mto huo. Matokeo yake, chanzo kile hufukiwa na udongo huo unaochekechwa na kusababisha kina cha maji kupungua. Naomba Bunge lipitishie Muswada huu ili kudhibiti hali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Miswada hii ni muhimu sana na hasa kwa kipindi hiki ambapo dunia inapitia hatua mbalimbali za mpito na changamoto nyingi katika Sekta ya Maji. Sambamba na kuunga mkono Miswada hii, naomba kukumbusha na kutoa angalizo kuwa kitu gani kifanyike na hasa baadhi ya maeneo ambayo hayajapata fursa ya kutumia vizuri rasilimali za maji ziweze kulindwa na vyanzo vya maji viweze kupimwa na kuboreshwa.

Maeneo ya Kanda ya Ziwa sehemu ya Speke Bay hadi Mji Mdogo wa Lamadi uko kandokando mwa Ziwa Victoria. Naiomba Wizara hii kupitia Miswada hii, itoe

kipaumbele kwa ajili ya upatikanaji wa maji kwa Mji Mdogo wa Lamadi, pamoja na kuboresha mazingira yaliyo kando kando ya Ziwa.

Kuna kila sababu, kupitia Miswada hii; suala la maji kwa matumizi ya binadamu na mifugo liwe historia kwani kama vyanzo vya maji vitalindwa, vitapimwa na kutumika vizuri, kutatoa fursa kwa wananchi kupata huduma hii muhimu.

Naunga mkono hoja hizi sambamba na ombi la kuwapatia maji Wananchi wa Mji Mdogo wa Lamadi. Ahsante.

**MHE. WILSON M. MASILINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapa pole Mheshimiwa Waziri na Timu yake kwa kazi nyingi sana. Je, Mradi wetu wa Bwawa, Kijiji cha Bunyagongo, maandalizi ya kuanza kujenga yataanza lini? Nawatakiwa kila la kheri katika kuwasilisha Miswada.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Napenda kufahamu kama Muswada wa Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira uta-*apply* nchi nzima, maana nakumbuka kama Waziri alisema ita-*apply* kote kasoro Dar es Salaam kwa kuwa Dar es Salaam ina Sheria yake; *is it* au nilisikia vibaya?

**MHE. JOEL N. BENDERA (NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi, kwanza, kumpongza Waziri, Mheshimiwa Profesa Mark J. Mwandosya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, Katibu Mkuu, Ndugu Wilson Mukama, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi nzuri wanayofanya kwa kuleta Muswada huu kwa wakati muafaka na hasa jinsi wanavyopambana na tatizo la maji katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Mark J. Mwandosya, kwa kutembelea Korogwe, kwa ajili ya kujionea mwenyewe matatizo ya maji Wilayani Korogwe na Mkoa wa Tanga kwa ujumla. Ziara ile ilikuwa ya manufaa sana kwetu sisi Wananchi wa Korogwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitaelekeza katika maeneo yafuatayo:-

Ninaunga mkono Miswada yote miwili kwani itasaidia sana kuboresha hali ya upatikanaji wa maji kwa wananchi wetu nchini Tanzania.

Ninashauri suala la *Water Right* litazamwe upya, kwa miradi ambayo inashabihiana kati ya Wilaya na Wilaya au Mkoa kwa Mkoa. Ninaona sio busara kwa maji yanayotoka Korogwe na kwenda Handeni (Mradi wa HTM), Handeni wawe na *Water Right* na Korogwe ambao ndio wenye maji na mto unapita katikati ya mji wasiwe na *Water Right*.

Jambo hili ni zito sana na Wananchi wa Korogwe hawataelewa kwa kutokutumia maji ya mradi wa HTM eti kwa sababu tu Korogwe hawana *Water Right*!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Wizara ione hili haraka ili na Korogwe nao wafaidike na Mradi wa HTM.

Korogwe ni Mji ambao una shida sana ya maji. Nimekuwa nikiomba toka nimeingia ndani ya Bunge hili mwaka 1995 kwamba, Wizara ifanye kila linalowezekana, kuboresha chanzo cha maji ya Tabora HTM kilichoko Korogwe kisaidie au kiwe chanzo cha maji cha kudumu kwa Mji wa Korogwe na Handeni.

Kutoka chanzo kilipo na Korogwe ni kilomita 15 tu. Tayari pale Tabora kuna miundombinu, kwa hiyo, ingekuwa busara sana kama Tabora pangeandaliwa hasa ikizingatiwa kwamba, maji ni mengi yangetosha Korogwe Mjini na baadhi ya vijiji vyake kupata maji ya kutosha na Handeni nao wakapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa nikiahidiwa tu kwamba, mradi huo utanza na hata gharama nikaambiwa kwamba ni milioni moja. Cha kusikitisha ni kwamba, nimekuwa nikiahidiwa tu na kupewa tamaa ya mradi. Ninaomba sana Wizara sasa wanipatie jibu la uhakika ni lini mradi huu utanza rasmi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni wa kitaifa, ambao naamini ukiboreshwa vizuri utaokoa matatizo ya maji ya vijiji vingi vilivyopo katika Wilaya tatu za Mkoa wa Tanga ambazo ni Korogwe, Handeni na Muheza. Napenda sana kueleza Wizara kwamba, Korogwe ni mji unaokua sana. Mahitaji ya maji ni makubwa sana. Kwa mantiki hiyo, Mamlaka ya Bodi ya Maji Korogwe inaweza kupata fedha nyingi za kuendesha maendeleo ya maji. Suala hili ni la kiuchumi, ninaomba sana tulipe uzito unaostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kero ya maji Korogwe sasa ni janga, ninaomba sana Wizara ichukue hatua za haraka.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono Muswada wa Usimamizi wa Rasilimali za Maji na Udhhibiti wa Matumizi ya Maji. Hata hivyo, kuna dosari kadhaa katika Sekta ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mgongano katika mchakato wa kuwapatia wananchi maji hususan wa vijijini. Mgongano huu hutokea baina ya wapimaji wa maji kubaini maeneo ya kuchimba na wataalamu wachimbaji. Kwa kawaida wataalamu wa kupima huwa ni wa Serikali, lakini wachimbaji maji huwa ni wakandarasi. Visima vingi vinavyopimwa hubainika kukosa maji vinapochimbwa, hasara ya rasilimali fedha hutokea kwa njia hiyo na kuchimbwa kwa visima hewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabwawa mengi yanayojengwa, hayajengwi kitalaamu; ni *sub-standard (poor workmanship)*. Kazi ya ujenzi wa mabwawa ni ya kulipua lipua na matokeo yake ni mabwawa haya kupasuka/kubomoka yanapojaa maji, kwa sababu kinga zake hazikujengwa kwa uimara. Fedha nyingi sana zimezama kwa njia hii na kusababisha hasara kubwa na lawama nyingi kwa Serikali ingawa Serikali hiyo

hiyo ndiyo iliyotoa mafungu hayo ya fedha. Ninatarajia basi kuwa mamlaka husika zitazingatia usalama wa mabwawa na udhibiti wa mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashine na pampu za maji zinazoletwa au kununuliwa na kuletwa na Wizara ni mbovu, huletwa na kufungwa, lakini baada ya kufanya kazi kwa muda mfupi na kuwaacha wananchi wakifadhaika baada ya kurejeshwa kwenye matatizo ya awali ya ukosefu wa maji wao wenyewe na mifugo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla kazi za kuwapatia maji wananchi hazifanywi kwa makini na hivyo ni wajibu wa mamlaka husika kuona la kufanya kurekebisha hali hii inayosikitisha na inayokatisha tamaa wananchi.

**MHE. VUAI ABDALLAH KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nakupongeza wewe kwa kusimamia Bunge kwa mashirikiano mazuri na Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wenzako. Pia nimpongeze Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii ya Maji, kwa kazi zao nzuri na kuleta Muswada wa Sheria hii. Naomba Wabunge wenzangu, tuipitishie Muswada huu ili tufaidike kwa faida yetu wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tunahitaji elimu na kupata wataalamu au kuwatumia wataalamu kwani maji tunahitaji kwa njia zote na pia tuyahifadhi na tuyatumie vizuri na vyanzo vyote kuvienzi ili kupata uhai na kutumia kwa miundombinu mingine; tufaidike na sheria hii tuwe na uzalendo na kujali nchi yetu kwa faida za wananchi na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. BENEDICT N. OLE-NANGORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Wizara na Waziri, kwa kuandaa Muswada huu mzuri na muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya III (10 – 12) ya Muswada huu, ibainishe kuwa rasilimali za maji ndani ya ardhi ya vijiji itamilikiwa na wanavijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni zitakazotungwa zibainishe usimamizi na ukarabati wa miradi ya maji. Pia Kanuni ziweke bayana taratibu za usimamizi na ukaguzi wa fedha za mifuko ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Kuunda Bodi za Maji katika ngazi ya Wilaya, Kata na Vijiji ikasimiwe kwa Baraza la Madiwani. Mapendekezo ya majina ya wanabodi yatolewe na Mkurugenzi Mtendaji na kuidhinishwa na Baraza la Madiwani.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba niipongeze Wizara ya Maji, Waziri wa Maji, Naibu wake, pamoja na Wataalamu wote kwa ujumla wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami pia nichangie machache tu katika Muswada huu muhimu. Naomba nikazie suala la ufungaji mita majumbani. Ni kweli

kabisa kuwa mita za maji husaidia sana kuwa na matumizi mazuri ya maji, hiyo nakubaliana nayo; lakini kwa nini mita au niseme watumiaji wa maji yanayosomwa na mita huwa gharama ni kubwa kupita kiasi? Je, inawezekana wakati mwingine mita huwa ni mbovu au ndio inavyokuwa pindi mteja anapofungiwa mita? Tatizo hili ni kweli na asilimia kubwa ya watumiaji wa mita wanalalamika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ijaribu kufuatilia, lakini pia ningependa kuelewa au nisaidiwe; utaratibu wa utoaji wa mita ukoje, kwani inaonesha kuwa mita hizo hufungwa kwa baadhi ya wateja wala siyo wote? Je, ni sababu zipi zinazofanya wateja wengine kufungiwa na wengine kuachwa bila kufungiwa mita? Lengo la Serikali ni kufungwa wateja baadhi tu au kila mtumiaji wa maji endapo ana bomba nyumbani kwake anapaswa kufungiwa mita?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyotangulia kusema wenzangu, ni kweli kwamba, lipo agizo la ulipaji wa fidia katika maeneo ambayo yanaonesha kuwa na chanzo cha maji na bahati mbaya kwa Serikali, eneo lile linakutwa ni mali ya mwananchi kwa muda mrefu, hivyo ni eneo lake halali. Naomba Serikali ipitie upya sheria ya fidia kwa mtumiaji wa eneo ili aweze kupata haki yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo la ulipaji wa maji endapo maji hayatoki ipasavyo au hayatoki kabisa, kwani kama kawaida ulipwaji wa bili ya maji unakuwa uko pale pale hata kama hukupata maji, maadam tu bomba lipo. Sababu zipi zinapelekea mteja kulipia maji hata kama hayatoki? Naomba maelezo ili wananchi waweze kuelewa vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. ARCHT. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali kabisa, nashukuru kwa kuletwa kwa Miswada yote miwili, kwani ilihitajika sana kwa muda mrefu na kuzingatia umuhimu wa maji kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ukurasa wa sita, kwenye *interpretation ya cluster* ninashauri kisipewe uzito mkubwa kisheria, kwani kuna uwezekano wa kudidimiza umiliki, uendeshaji na matengenezo ya baadhi ya Mamlaka ya Maji katika miji midogo. Ninashauri kila Mamlaka ipewe uwezo wa kujitegemea.

Katika kifungu cha 8(1)(a) ni vizuri Mamlaka ziwe na Wataalamu wake, kama watahitaji msaada wa *councils* lakini wawe huru kuepuka migongano na ukiritimba.

Kifungu cha 8(1)(c) katika maeneo tofauti zipo Bodi za Wadhamini zinazosimamia miradi ya maji. Mfano, katika Wilaya ya Hai na Siha zipo Bodi tano ambazo zimeandikishwa kisheria, kulingana na jiografia, vyanzo vya maji ambavyo vina *autonomous entities*. Ninashauri zitambuliwe na ziachwe ziendeleo kusimamia huduma katika maeneo yao na zimekuwa zinafanya kazi vizuri sana na pia Serikali itoe misaada ya kitaalamu pale itakapohitajika.

Katika kifungu cha 40(c) katika Wilaya zetu *By-laws* zimekuwa zikiandaliwa vizuri na mapema na kutumwa TAMISEMI, lakini wakati mwingine kumekuwepo na ucheleweshaji wa kuzipitisha mfano *by-laws* kutoka Wilayani Hai ambazo bado hazijapitishwa; ninaomba wahusika watusaidie.

Katika sehemu ya kumi na nne, adhabu zilizoainishwa hazitoshi kutokana na uharibifu utakaokuwa umefanyika. Mfano ni mtu aliyejiunganishia maji kinyemela kwa muda mrefu na wakati mwingine katika shughuli kubwa za kibiashara; mfano, viwanda au hoteli lakini adhabu anayopewa ni faini ya kulipa shilingi elfu hamsini tu na si zaidi ya milioni tano, wakati amekuwa akiyatumia maji hayo kwa muda mrefu.

Kuna umuhimu wa kutoa elimu kwa jamii kabla na wakati wa miradi mipya ya maji ili kuwatayarisha wananchi, kwa mfano *social workers* wanahitajika.

Ninasisitiza kila mtumia maji ayalipie kufuatana na matumizi yake ili miradi yetu iwe endelevu.

Ninaunga mkono hoja zote. Ahsante sana.

**MHE. DKT. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Mbozi hususan wale wa Jimbo la Mbozi Magharibi, naomba nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole kwa familia na Wananchi wa Wilaya ya Biharamulo, kwa kufiwa na aliyekuwa Mbunge wao, Mheshimiwa Phares Kabuye.

Baada ya hayo, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wale wote walioshiriki katika kuandaa Miswada ya Sheria hizi mbili. Naamini kwa dhati kuwa, Miswada hii imeletwa kwa wakati muafaka, kwani sheria zote mbili za awali zimepitwa na wakati. Nikianza na Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji unaolenga kuhakikisha ulinzi, matumizi, maendeleo, hifadhi, usimamizi na udhibiti wa rasilimali za maji kwa ajili ya mahitaji ya msingi ya binadamu kwa sasa na siku zijazo. Napenda kusema Muswada huu umechelewa sana. Kama Mheshimiwa Waziri alivyoelezea, mahitaji ya maji yanazidi kuongezeka jinsi miaka inavyopita, kutokana na ongezeko la idadi ya watu wakati kiasi cha maji kinapungua kutokana na mabadiliko ya hali ya nchi, kutokana na sababu mbalimbali ukiwepo uharibifu wa mazingira. Kutokana na hali hii, inatabiriwa na wataalamu wa mazingira kuwa ifikapo mwaka 2030, kutatokea vita kubwa ya kugombea maji sehemu mbalimbali za dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mbozi Magharibi lina nusu ya eneo kwenye bonde dogo la Maji la Rukwa na nusu nyingine kwenye eneo la miinuko inayopitisha maji (*watershed*) kwenye bonde hilo. Kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira uliosababishwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za binadamu kwenye vyanzo vya maji na kandokando ya mikondo ya maji, eneo hili kwa miaka ya hivi karibuni limekuwa

likitokea. Aidha, kutokana na uharibifu huo kumekuwepo na matukio ya mafuriko yasiyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, nadiriki kusema kuwa, kutungwa kwa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji, kutasaidia sana kuokoa vyanzo vya maji vilivyobaki na hata kurejesha vyanzo vingine vilivyopotea na hata uhifadhi wa mazingira. Katika sehemu ya II ya Muswada huu, kifungu cha 7 kinatoa fursa kwa kila mkazi wa Tanzania Bara, kulinda na kuhifadhi rasilimali za maji na kutoa taarifa kwa Mamlaka husika, panapotokea vitendo vinavyoweza kuathiri kwa kiwango kikubwa, uwingi na ubora wa rasilimali za maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda hata kabla ya Muswada huu kupitishwa, niliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, pale Vwawa (Makao Makuu ya Wilaya ya Mbozi) na Mbozi Mission, kuna vyanzo vikuu vya Mto Nkana ambao hutiririsha maji yake Bonde la Rukwa. Kwa makusudi kabisa, pale Vwawa chanzo hiki kimejengwa nyumba, vyoo vya shimo, kituo cha mafuta ya petroli na kana kwamba hiyo haitoshi, panapandwa minazi na migomba na hivyo kusababisha upungufu mkubwa wa mtiririko wa maji na kusababisha mto huo kukauka kuanzia mwezi Agosti. Kwenye chanzo cha mto huu pale Mbozi Mission, kumepandwa mahindi na majimbi, ambayo hurutubishwa kwa mbolea za chumvichumvi. Hali hii inapaswa kutupiiwa macho mara hseria hii itakapoanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sehemu ya IV inayohusu usimamizi wa rasilimali za maji, kifungu cha 18(7) kinakinzana na kifungu cha 18(1), kuhusiana na mamlaka na majukumu ya maafisa wenye mamlaka ya kuingia kwenye maeneo kwa nia ya kukagua matumizi ya maji au umwagaji wa maji. Wakati kifungu cha 18(1) kimempa mamlaka ya kuingia eneo lolote bila taarifa, kifungu cha 18(7) kinamwondolea mamlaka hayo. Vifungu hivi vingiangaliwa na kuwekwa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa pongezi kwa kuwekwa kwa kifungu cha 34 kuhusu upigaji marufuku uendeshaji wa shughuli za kibinadamu, kwa umbali unaozidi mita 60 kutoka chanzo cha maji kama hatua madhubuti ya kuhakikisha ulinzi na uhifadhi wa rasilimali za maji. Naamini kifungu hiki kitahakikisha shughuli za uharibifu wa vyanzo vya maji pale Vwawa, Mbozi Mission na Tunduma, zinadhibitiwa.

Kifungu hiki cha Sheria kikitumiwa ipasavyo, mbali ya kurejesha mazingira ya zamani Jimboni Mbozi Magharibi, kinaweza kurejesha hali ya mbubujiko wa maji iliyokuwepo zamani katika Jiji la Mbeya, ambalo sasa hivi linashuhudia mawingu ya vumbi mithili ya pepo za Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sehemu ya VII ya Muswada, kifungu cha 64(4)(b), kinatoa kiwango cha adhabu kwa makosa ya umwagaji maji au utupaji maji machafu kwenye maji. Kiwango cha faini na kifungu ni kidogo, ikilinganishwa na madhara yanayoweza kusababishwa na vitendo hivyo, kama vile milipuko ya magonjwa kama kipindupindu na homa ya matumbo, magonjwa ya saratani na kadhalika.



Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sehemu ya X ya Muswada, kuhusiana na usalama wa mabwawa na udhibiti wa mafuriko; naunga mkono moja kwa moja kifungu cha 87 kinachopiga marufuku ujenzi unaoweza kuzuia maji kutiririka kwenye mkondo wake bila kibali. Ujenzi wa aina hii ndiyo chanzo kikubwa cha upungufu wa maji katika meneo mengi ikiwa ni pamoja na pale Vwawa Mbozi kwenye chemchemi ya Mto Nkana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira, naomba nizungumzie machache yafuatayo:-

Sehemu ya II, kifungu cha 4(1), kinaelezea lengo kubwa la Sheria hii kuwa ni kuwezesha na kuhakikisha haki ya kila Mtanzania kupata huduma za maji endelevu kwa ufanisi na ubora na kuhakikisha usafi wa mazingira kwa kufuata Kanuni za Msingi na kutaja Kanuni hizo.

Kwa hakika utekelezaji wa Kanuni hizo utaleta ufanisi mkubwa katika upatikanaji wa huduma za maji. Upatikanaji wa vivutio kwa watoa huduma na upatikanaji wa huduma za maji wa uhakika na kwa bei nafuu ni kati ya mambo muhimu yanayoweza kuwa na maana kubwa katika uanzishaji wa Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sehemu ya XIV ya Muswada kuhusu makosa ya adhabu, kifungu cha 47(2) kinaelezea adhabu ya faini kuanzia shilingi 50,000 hadi shilingi 5,000,000 na kifungu cha kati ya miaka mitatu hadi mitano. Wigo huu wa adhabu ni mkubwa mno. Napendekeza faini iwe kati ya shilingi 3,000,000 na 5,000,000 na kifungu kiwe kati ya miaka mitatu hadi mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 52(1), kuhusu kosa la kutiririsha udongo, vitu au vimiminika, kwenye mfumo wa maji, adhabu zilizoainishwa hazina kiwango cha chini na hivyo kumpa Hakimu uhuru wa kutoa adhabu kwa mhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba niishukuru Wizara ya Maji na Umwagiliaji, kwa kufanikisha kwa kiasi kikubwa katika kipindi kifupi, ujenzi wa visima vya maji, usambazaji wa maji katika Jimbo la Mbozi Magharibi na upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi mpya wa Mradi wa Umwagiliaji wa Naming'ongo, ambao ulikuwa umeharibiwa na mafuriko mwishoni mwa mwezi Desemba, 2006 kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uharibifu mkubwa wa mazingira kwenye *watershed* ya Mto Nkana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono Miswada yote miwili na kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu, waiunge mkono kwa kuipitisha kwa kauli moja.

**MHE. DKT. CHARLES O. MLINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji Wakuu, kwa kuwasilisha Miswada ya Maji.

Pamoja na sheria tarajiwa ya huduma za maji na usafi wa mazingira, nashauri Wizara iweke mpango wa muda mrefu wa kuboresha usafi wa mazingira. Hii ni kwa

sababu mpaka sasa huduma za usafi wa mazingira upande wa maji machafu mijijni hazitoshi na zilizopo ni duni. Ikumbukwe, miji yetu inaendelea kukua sambamba na mahitaji ya usafi wa mazingira ili kuepuka kuwepo kwa magonjwa yaletwayo na uchafu wa mazingira.

Katika mpango huu wa usafi wa mazingira, miundombinu bora ya kusambaza maji safi inahitajika sana ili maji hayo yasiwe chanzo cha uchafuzi wa mazingira. Miundombinu bora pia inahitajika kwa ajili ya kukusanya maji machafu na kuyaondoa katika mazingira ya makazi ya watu.

Nasema hivyo kwa sababu leo hii mitaa mingi mijini haina mifereji ya maji machafu. Hata uunganishwaji wa mtandao wa maji safi, unafanyika kienyeji kwa maeneo mengi mijini.

Nawatakia kila la kheri, ahsante sana kwa kukamilisha mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria kwa Miji ya Shinyanga na Kahama. Sasa Shinyanga tumepona.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni nyenzo muhimu sana kwa maisha ya wanadamu, wanyama na mimea, lakini isipotumiwa ipasavyo inaweza kuleta majanga. Hivyo, naipongeza Wizara chini ya Waziri, Naibu Waziri na Watalaamu wote, kwa kuleta Muswada huu Bungeni ili kuwe na sheria ya matumizi endelevu na mazuri kwa wadau wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamekuwa na vikundi mbalimbali vinavyojishughulisha na kutoa huduma ya maji pale huduma ya Serikali inapolegalega au inapokuwa haipo. Hata hivyo, pamoja na ukweli kuwa imepunguza kero kwa kiasi kikubwa, lakini kuna usalama wa maji hayo, kwani hakuna chombo kinachojishughulisha na kazi hiyo.

Dar es Salaam ni moja kati ya maeneo yenye wachimbaji wengi wa visima binafsi, ingawa Muswada hauhusiani na Jiji la Dar es Salaam na maeneo yanayohudumiwa na DAWASA. Hii ni changamoto kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada unazungumzia juu ya kumwaga maji taka na utaratibu wa kumwaga maji taka. Mazoea ya matumizi ya maji ni kuwa maji taka hayajawekewa mpango wa pamoja wa kuyadhibiti. Ni wale wachache tu ndiyo wamo katika mpango wa pamoja wa kuyakusanya na kuyaelekeza mahali maalumu. Maji mengi huzagaa mitaani, hivyo kusababisha magonjwa hatari kama kuhara na kupindipindu. Aidha, watumiaji wakubwa, kwa mfano, wenye hoteli, huyaingiza maji machafu baharini au kwenye mito kwa ujanja ujanja; hivyo Sheria hii mpya lazima iwabane ili maji yawe *treated* kabla ya kuingizwa baharini au katika mito.

Lazima pia mtandao wa maji machafu utayarishwe kwa watu wote na kwa miji yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabonde yetu yamekuwa katika umaskini, pamoja na kuwa na rasilimali muhimu, kwa sababu hiyo hayaendelezwi. Mindombinu yao bado ni

duni na bodi zinazotawala mabonde hayo zimo katika hali ngumu kifedha. Tunategemea Sheria mpya itabadilisha sura ya sasa na kuleta ufanisi.

**MHE. EPHRAIM N. MADEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji kwa kazi nzuri.

Sheria itahusu Tanzania Bara na siyo Zanzibar, kwa sababu maji siyo suala la Muungano. Nitafarijika kuelezwa kama Serikali ya Zanzibar nayo inachukua hatua muhimu kama hii, kwani rasilimali maji ni muhimu kwetu sisi sote Watanzania bila kujali tunatoka upande gani wa Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu watu binafsi watakaomba na kupewa *water use permits* pia wapewe masharti yatakayowawezesha wananchi wanaoishi jirani na watu wenye vibali hivyo kuwa na uhuru wa kutumia (kwa gharama itakayodhibitiwa na EWURA), maji yanayotokana na vyanzo hivyo *for domestic purposes*. Pendekezo hili halihusu vyanzo vilivyo ndani ya miji (*urban areas*).

Sheria itamke kinagaubaga ya kwamba, pale ambapo mtu binafsi anaomba *water permits*, mahitaji ya maji ya umma lazima yapewe kipaumbele. Ni muhimu hili liwekwe kwenye Sheria yenyewe na siyo kwenye Kanuni (*regulations*) ili nguvu yake isipotee.

**MHE. MWERA C. NYANGURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Waziri, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na Naibu Waziri, Mheshimiwa Eng. Christopher Chiza, kwa Miswada yote kwa pamoja. Ni kweli kwamba, maji ni uhai na wakati wote yawe safi kwa ajili ya afya ya mlaji. Miradi ambayo ipo katika maeneo yetu bado ni michache katika vijiji, hasa katika Jimbo la Tarime. Kama unavyofahamu, Tarime Mjini ina tatizo kubwa la maji na kwa sasa hivi tank kwa ajili ya kuleta maji limeshajengwa. Naishukuru Serikali kwa kujenga tank, tatizo ambalo lipo sasa ni fidia kwa ajili ya kupitisha mabomba ya jumla ya shilingi milioni 30. Naomba Wizara itoe hizo pesa ili Wananchi wa Tarime wapate huduma ya maji ili kupunguza tatizo sugu la maji, ambalo hupelekea maambukizi ya kipindupindu ambacho huwa hakiishi kwa sababu ya maji machafu ya mito.

Naiomba Serikali shilingi milioni 30 ili zisaidie wananchi ama sivyo tank lililojengwa kwa thamani ya zaidi ya shilingi 265 milioni litapasuka na Serikali itakuwa imepata hasara. Hasara itakuwa kubwa sana na kodi za wananchi zitakuwa zinapotea bure. Ombi rasmi kwa ajili ya fidia kwa wananchi lipo Wizarani.

Lingine Mheshimiwa Waziri ni uchafuzi wa maji maeneo ya Nyamongo. Eneo la Mgodhi wa Madini wa Barrick, maji machafu huwa yanaelekea Mto Mara na kwenye mito jirani. Maji hayo ninavyofahamu ni ya sumu na huwa hayatibiwi. Wananchi wengi watakufa pamoja na wanyama kama ng'ombe, mbuzi na kondoo.

Kama Sheria itatekelezwa na kusimamiwa vizuri ni Muswada mzuri. Naomba yote yazingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, hatua ya Muswada kuingia kwenye Kamati ya Bunge Zima itatuchukua muda mrefu, kwa sababu Miswada ipo miwili. Sasa nilikuwa nafanya mawasiliano na Mheshimiwa Waziri, kuona ni namna gani watatumia muda wao kuweza kuhitimisha hoja yao. Maelezo niliyoyapata ni kwamba, nitampa nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri kwa dakika 25, halafu Mheshimiwa Waziri kwa dakika 50 na baada ya hapo tutaingia kwenye hatua ya Kamati ya Bunge Zima na kuipitisha Muswada mmoja baada ya mwingine. Itabidi tuamue kwa hatua tofauti kila mmoja kwa umuhimu wake.

Naomba sasa nimwite Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa dakika zake 25. Mheshimiwa Naibu Waziri karibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ada na mimi naomba kwa kifupi tu niungane na wenzangu waliotangulia, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo la Buyungu, basi nitoe rambirambi kwa wenzetu waliotutangulia mbele ya haki hususan Mheshimiwa Kabuzi Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Phares Kabuye na jana pia tulipata habari za Mama Sapi. Sasa mimi niseme tu; Bwana alitoa na Bwana ametwaa, Jina lake libarikiwe.

Naomba pia nimshukuru kwa dhati kabisa, Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwa umahiri mkubwa aliouonesha katika kutoa maelekezo na mwongozo wa kusumamia maandalizi haya ya Sheria hizi mbili na ukizingatia kwamba, imebidi zidadiliwe kwa utaratibu huu wa Hati ya Dharura. Mimi namshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru Kamati ya Kilimo, Ardhi na Mifugo kwa jinsi walivyofanya kazi bila kuchoka usiku na mchana hadi kufanikisha hatua hii tuliyoifikia.

Naomba pia nimshukuru Waziri Kivuli wa Maji na Umwagiliaji, dada yangu Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya; japokuwa tulisikia kwamba taa ikiwaka kivuli kinafutika, lakini naona bado yupo pale. Kwa hiyo, namshukuru sana kwa maoni yake ambayo aliyatoa jana na tumeyazingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kwa kifupi tu kwamba, hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi sana, wengine kama ulivyosema mwenyewe hawakuweza kupata nafasi ya kuchangia. Kwa hiyo, nataka niseme na niahidi kwamba, wale ambao hatutaweza kuwataja mmoja mmoja, basi nina hakika kwamba, tutaweza kuwapa majibu ya kina kwa maandishi. Baadaye kidogo, Mheshimiwa Waziri atapata nafasi ya kuwatambua wale wote waliochangia kwa maandishi na waliozungumza hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme na niwakumbushe machache tu kwamba, Sheria inayotumika sasa ni Sheria ya Miundombinu ya Maji na mimi hapa

ninazungumzia Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira (*The Water Supply and Sanitation Act, 2009*). Sheria hii kama alivyosema Mheshimiwa Waziri jana ni kweli ni ya tangu mwaka 1949. Wabunge wengi wamehoja kwamba imechelewa sana, lakini mimi nasema kwamba, pamoja na kuchelewa sasa inabidi lazima tutekeleze na tuweke Sheria mpya ili angalau tuendeleo kuboresha utendaji wa kazi kwa ajili ya manufaa ya vizazi vijavyo.

Jana Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatoa maelezo alitaja sababu nyingi; kabla sijakwenda kwenye kujibu hoja za Wabunge, naomba niwakumbushe sababu tano ninazofikiri kwamba ni muhimu sana na zimejitokeza sana katika majibu au katika hoja ambazo Wabunge wametoa. Siyo kwamba, zile alizozitoa nyingine hazifai lakini nimejaribu tu kuzi-*group* hizi na ninataka niwakumbushe.

Kwanza, tumesema tumeleta Sheria mpya ili kutoa fursa za jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi yetu yote ya maji kama ilivyoelezwa jana; na kutoa pia majukumu kwa ngazi zote bila kuondoa umuhimu wa Wizara yenye dhamana ya maji, ikiwa ni pamoja na Mamlaka ya Uteuzi katika ngazi husika. Naomba hili nisilisemie sana, kwa sababu Mheshimiwa Waziri atapata nafasi ya kulizungumza kwa kirefu kwa kuwa linagusa ngazi mbalimbali; yaani ngazi za Kitaifa, Mikoa na hususan katika sehemu ya Halmashauri zetu. Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Waziri atalieleza kwa kina na ninaomba niliache hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kuna jambo ambalo linaendelea kujitokeza ni miradi mikubwa ya maji ambayo nayo pia tumeitaja jana sipendi kuirudia. Nitoe tu mifano miwili; mradi kama wa Chalinze ni mkubwa; Kahama, Shinyanga ambao Mheshimiwa Rais ataufungua muda si mrefu nao ni mkubwa, unatoka mkoa mmoja unaingia mkoa mwingine, unatoka Wilaya moja unaingia Wilaya nyingine. Kwa hiyo, tunaamini kwamba, inabidi iendeleo kusimamiwa kitaifa. Kwa hiyo, sheria hii imelitazama hilo.

Ninaomba tutambue kwamba, baada ya sheria hii kama alivyosema jana Mheshimiwa Waziri, sheria ile iliyokuwa ikitumika (Sheria ya Miundombinu ya Maji ya Mwaka 1949), hiyo sasa itakuwa ndiyo imefika mwisho wake.

Naomba pia niwakumbushe kwa sababu Wabunge wengi wamechangia, katika Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Pwani, huduma hizo zinaendelea kusimamiwa na Sheria ya Mamlaka ya Maji na Uondoaji wa Maji Taka (*Dar es Salaam Water Supply and Sewage Authority Act No. 20 of 2001*).

Basi nilitaka niwakumbushe hayo matano kwa sababu mengi yamejirudiarudia katika hoja za Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba mimi nijikite katika mambo yafuatayo:-

Waheshimiwa Wabunge, wengi walipenda sana kujua mambo yanayofuata; yapo mambo ya kisheria ambayo yamejitokeza katika michango yao, yaani mambo ambayo yanaonesha Sheria hii itatusaidia nini ikiingia hapo; wengine wamesema mbona hii

italeta mchanganyiko na mambo mengi. Nitakuwa na kipengele kinachojibu hao waliohoji mambo yanayohusu sheria, lakini pia nitaingia katika mifumo ya taasisi ambazo ndiyo zinaunda na kuendesha sheria za maji. Naomba pia hizi nazo sitazisemea sana lakini nimependa tu nizigusie, kwa sababu kama nilivyosema, Mheshimiwa Waziri atazitungumzia katika sheria hiyo inayofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi, wametaka kujua kama chombo hiki cha EWURA kinatusaidiaje kinapoweka bei hizi; mbona wakati mwingine bei zinakuwa kubwa na kadhalika. Nitazungumzia kidogo kuhusu kazi za EWURA, zinatusaidiaje na zitasaidiaje hizi Mamlaka za Maji ambazo nyingi au zote zipo katika sehemu mbalimbali ambazo zinapishana kiuchumi.

Kwa mfano, Mamlaka iliyopo Dar es Salaam haiwezi kabisa kuwa sawa na Mamlaka iliyopo Kibondo, kwa hiyo, hiki chombo cha EWURA kina utaratibu wake wa kufanya kazi.

Naomba pia nizingumzie juu ya kuundwa kwa vyombo vya jumuiya za wananchi. Suala hili nalo limetuletea matatizo mahali pengi, Mheshimiwa Job Ndugai alizungumza sana kuhusu Kongwa na mimi nimepita kote huko, nimeona matatizo yanayojitokeza kutokana na vyombo hivi vilivyopo katika ngazi hiyo.

Sasa kwa kifupi tu nitazungumzia kuhusu makosa na adhabu na mambo mengine ya kijumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa dakika zangu ni 25 tu, naomba sasa niende katika hoja zile ambazo zimefanana fanana na kisheria. Waziri Kivuli wa Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, yeye alihoji kwamba, Waziri ana madaraka makubwa ya kutamka vyombo vya Mamlaka za Maji; hii ndiyo ilikuwa hoja yake kubwa. Ningependa kumjibu kwamba, rasilimali maji kama ilivyo rasilimali ardhi; hizi ni rasilimali ambazo sijui nitumie neno gani, lakini ni *public* na madaraka yake makubwa yapo chini ya Rais. Kwa hiyo, jinsi tunavyosimamia Sheria au matumizi ya ardhi, basi tungependa tuendeleo kusimamia rasilimali hii ya maji hivyo hivyo, maana hizi ni rasilimali ambazo huwezi kuziachia zikawa zinaogelea tu.

Sisemi kwamba, tusitoe Mamlaka kwa ngazi nyingine kama tunavyoeleza, lakini ni lazima kuwe na Mamlaka ambayo ni ya Kitaifa zaidi, inayosimamia rasilimali hizi ili kutoa mwanya kwa mtu anayetaka kulalamika au anayetaka kupata maelezo zaidi au maamuzi ya kitaifa. Ndiyo lengo kubwa hilo la kusema lazima katika ngazi ya Wizara na kama unavyojua, Waziri ndiyo anayemshauri Rais, lazima kuwe na madaraka kwa Waziri katika kusimamia vyombo hivi tunavyoviunda.

Mheshimiwa Ruhwanya pia alisema kuomba ushauri kwa Mamlaka nyingine wakati wa kuanzisha vyombo vya maji ni kama nadharia tu na Wajumbe wa Bodi za Mamlaka wawajibike kwa Baraza la Madiwani. Mimi ningependa kusema kwamba, hii si nadharia, suala linapokuwa limewekwa katika sheria za nchi na limetamkwa, Waziri hawezi kabisa akajifanyia vitu vyake kinadharia tu, hii ilikuwa ni kupitisha Sheria,

hapana. Tumeweka makusudi kabisa kwamba, Waziri atapata ushauri kutoka kwenye Mamlaka nyingine katika maeneo fulani, kwa sababu yeye yuko Dar es Salaam; sasa ni vizuri Waziri akapata ushauri wa Mamlaka nyingine ambazo zinasimamia jambo hili kule waliko. Kwa hiyo, lengo hilo siyo kwamba labda ni kupaka kilemba cha ukoka tu, hapana; Waziri sharti awasiliane na Mamlaka nyingine ili kuweza kutimiza azma ya ushauri au maamuzi anayotaka kuyafanya.

Naomba nimhakikishie kwamba, Waziri atashirikiana na kuwasiliana na Mamlaka nyingine na haitakuwa nadharia.

Nataka nimhakikishie pia kwamba, Bodi za Mamlaka hasa katika ngazi za chini, ambayo ndiyo hasa *concern* ya Mheshimiwa Ruhwanya; kubwa kabisa ni kwamba ukiisoma vizuri Sheria hii, utakuta watu hawa watasimamiwa na Mamlaka zilizopo pale chini na Baraza la Madiwani katika kila ngazi litaweza kupata *report*, litaelewa nani kateuliwa na mabaraza haya yatakuwa yanapata taarifa za utendaji kazi wa Mamlaka hizi. Kwa hiyo, bado ile *recognition* ya ngazi ile ipo katika ngazi hiyo ya chini.

Katika mfumo wa kitaasisi wa kuunda Mamlaka za Maji na Usafi wa Mazingira, Mheshimiwa Waziri Kivuli pia alisema zisiwe wanunuzi wa vifaa vya maji kwa watumiaji wa maji ila ziache kila kitu kiende katika soko huria. Mimi nina wasiwasi kidogo, hatuna kipingamizi na soko huria; tunataka litumike kama alivyosema jana ndugu yangu Mheshimiwa Kabwe Zitto kwamba, sasa haya mambo yanataka kuachiwa kuingia katika soko, jambo ambalo linaweza kuwa hatari. Si kwamba, tunataka kuingia moja kwa moja katika soko na kuachia mambo yaogele, hapa tunachotaka ni kwamba, sisi kama chombo, yaani Wizara ya Maji kama chombo ambacho kinadhibiti ubora, basi ihakikishe kwamba huduma ile tunayoitoa kwa wananchi wetu, inatolewa kwa ubora unaotakiwa. Kwa hiyo, kwa sababu hiyo hatuwezi kuwaachia tu watu wakaenda dukani wakanunua vitu halafu wakafunga. Nitakupa mfano; baadhi ya maeneo kwa utaratibu huu wa kufuata soko huria, baadhi ya vyombo ambavyo vimenunuliwa ni vile ambavyo ni *sub-standard* lakini wananchi wengine mradi wamepata kitu hiki au kifaa hiki kwa bei rahisi, basi wanaona wafunge lakini baada ya muda mfupi chombo hicho kimeharibika.

Tunachotaka hapa ni kuhakikisha chombo chetu cha Serikali kinatoa udhibiti, ubora na ushauri kwa wanunuzi wa vifaaa hivi, maana sisi ndiyo *regulatory authority*; maana yetu ni hiyo tu, kuingiza suala hilo la kudhibiti na kuhakikisha ubora, ndiyo maana huko mbele katika vifungu tumesema tunaingiza hata *code of practice* kwa wataalamuu wetu; lengo ni hilo hilo kwamba tusitoe huduma ambazo ni *sub-standard* kwa watu wetu.

Mheshimiwa Ruhwanya alitaka kujua kutatokea nini kwa vyombo vilivyoundwa kabla ya sheria? Vyombo hivi vilivyoundwa kabla ya Sheria, ukisoma vizuri kifungu namba 9(7) bado vitaendelea kutambuliwa, yaani siyo kwamba sasa tunavifuta; vyenyewe vitaendelea kuwepo isipokuwa kwa Sheria hii, ukiisoma vizuri utakuta kwamba, vinawajibika moja kwa moja chini ya Halmashauri husika. Haiwezekani ikatokea tena mambo yale ya zamani kwamba, chombo fulani kimeundwa na hususan katika vyombo vile vya ngazi ya chini kabisa kiliundwa kama *community water organisation*, kwa hiyo kinawajibika chini ya Kabidhi Wasii Mkuu. Ukitaka kuwauliza

au watoe taarifa kuwawajibisha kwa makosa, wanasema hapana sisi tuko chini ya Kabidhi Wasii Mkuu, hatuwezi kuwajibishwa na chombo hiki. Sasa mahali pengi tumegundua kwamba, Mamlaka husika na hasa katika Halmashauri zinapata matatizo haya. Kwa hiyo, hivi vyombo vilivyopo hatuwezi kusema sasa vimefutwa kwa sababu bado vinaendelea kutoa huduma, lakini vitalazimika kutii sheria hii.

Mheshimiwa Omar Kwaangw', yeye alisema Bodi za Maji ni nyingi kutokana na uwingi wa Mamlaka za Maji zilizoko wilayani. Kwanza, nilitaka tu niseme kwamba, sheria yetu imelitambua hilo na kwa kulitambua hilo, tumeongeza kipengele; ukiisoma vizuri sheria yetu hasa kifungu kile cha 9, utakuta kwamba pale ambapo tunaona kibiashara kuna haja ya kuunganisha baadhi ya Mamlaka fulani ndogo iungane na nyingine, basi utakuta sheria imetoa nafasi kwamba, Mamlaka hizi zitaunganishwa. Kwa mfano, Mamlaka ndogo kuunganishwa na Mamlaka ya Mji Mkubwa uliopo katika eneo hilo. Sasa zikiunganishwa pale, utakuta hata utendaji kidogo utakuwa tofauti katika kutoa huduma ile. Lengo ni kwamba, Mamlaka zile ndogondogo nazo zitakuwa zimepata nafasi kubwa kibiashara, kuweza kuendeshwa chini ya mgongo wa zile Mamlaka kubwa.

Kwa hiyo, pamoja na kwamba, Bodi za Maji sijui alikuwa anamaanisha Bodi zipi, lakini nafikiri alikuwa anamaanisha Bodi hizi za Mamlaka za Maji. Sasa na mimi nimelizungumza kimamlaka zenyewe za maji. Lengo kwa kweli ni hilo kwamba, tunapenda ziwepo, kwa sababu vyombo hivi lazima viwepo. Kwa kuwa kila chombo kinalingana na sehemu inayohudumiwa, sasa itakuwa si rahisi tuchukue kila chombo tukiondoe katika Mamlaka yake na ku-*cluster*. Tunaweza ku-*cluster* tu pale ambapo tunaona kwamba, hapa tukifanya hivi tutaweza kupata ufanisi na utendaji kibiashara.

Mheshimiwa Benson Mpesya alilalamikia sana suala la kulipishwa huduma ya maji ambayo mteja hakuipata au kukatiwa maji wakati hadaiwi na alitaka kujua Mamlaka inachukua hatua gani.

Kifungu namba 34 cha Sheria ya EWURA na Kanuni zake, inaruhusu mteja yeyote ambaye baada ya kuwasilisha malalamiko yake kwa mtoa huduma na kutopata majibu ya kuridhisha, awasilishe malalamiko yake moja kwa moja EWURA. EWURA inayo Mamlaka kamili ya kuangalia malalamiko hayo na inaweza ikatoa Mamlaka ikawa ni pamoja na kutoa Mamlaka au maagizo ya kurudishiwa fedha zilizolipwa na mteja kama ikidhihirika kwamba, kweli mteja huyo malalamiko yake ni ya kweli.

Kwa hiyo, naomba wakati tukisoma hizi Sheria, tuangalie Sheria ya EWURA nayo inasema nini. Sheria ya EWURA ndiyo chombo ambacho tumekiweka kwa ajili ya kusimama katikati pale na kuweza kutetea pande zote mbili kwa watoa huduma na wale wanaopata huduma hiyo.

Wabunge wengi wamependa kuzungumzia Kanuni, lakini kipekee Mheshimiwa Benson Mpesya, alitaka tutengeneze Kanuni za kutambua wajane na wazee katika kupata huduma ya maji.



Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili tumelizingatia japokuwa katika Sheria huwezi kukuta tumesema wajane, katika sheria utakuta tumesema Sheria imezingatia watu wa namna hiyo, katika kifungu kile cha 22 na tunawaita *economically disadvantaged persons*. Naomba nieleweke vizuri maana si Wanawake wote ni *economically disadvantaged*, naomba akina mama wasije wakasema hapana Mheshimiwa Naibu Waziri amesema Wanawake wote ni *economically disadvantaged*. Sheria yetu inatambua kwamba, wapo watu ambao kwa sababu fulani fulani za kiuchumi hawawezi kushiriki kikamilifu katika kupata maji na hawawezi kupata huduma zile kulingana na uwezo wao wa Kisheria. Kwa hiyo, Sheria hii imetambua hilo na ukisoma kifungu cha 22 utatambua hivyo.

Mheshimiwa Architect Fuya Kimbita alisema, *cluster* isipewe uzito mkubwa kwa kuwa itadidimiza umiliki, uendeshaji na matengenezo ya Mamlaka ndogo. Ningependa kumtaarifu kwamba, sehemu ya 9(b) katika Sheria yetu inasema, *cluster* itafanyika baada ya makubaliano na Waziri wa Serikali za Mitaa na Mamlaka endelevu kibiashara na itapunguza gharama za uendeshaji kama nilivyosema hapo awali.

Kwa hiyo, hapa *cluster* lengo lake kubwa ni kupunguza gharama za uendeshaji ili kuongeza ufanisi kibiashara.

Mheshimiwa Fuya Kimbita alitaka mamlaka ziwe na wataalamu wake siyo *Council*. Majukumu ya Halmashauri yameainishwa vizuri katika kifungu cha nane cha sheria na zitasimamiwa na Miji ya Wilaya na Miji Midogo. Ni vyema basi, watu hawa ndiyo wakahusika kuajiri wataalamuu na utaona kwamba, ukimwajiri mtu unaweza ukamwajibisha kuliko huyu anayeajiriwa huku halafu akikosea inakuwa ni rahisi kujificha nyuma ya mgongo wa mtu mwingine. Hayo tumeyaeleza vizuri sana katika kifungu cha 8 na cha 9.

Mheshimiwa Lucy Owenya yeye alitaka mifumo ya maji taka isijengwe karibu na mifumo ya maji safi. Hili limezingatiwa, lakini nataka niseme kwamba, katika mifumo hii yapo maeneo ambayo ni lazima yaende pamoja, kitachozingatiwa hapa ni ubora na miundombinu iliyowekwa. Kwa mfano, kama miundombinu inayopita huko katika bomba, basi bomba lile lazima liwe imara na litakuwa na rangi tofauti na bomba lingine la maji.

Kwa hiyo, katika maeneo ambayo ni lazima tufanye hivyo, hatutakwepa isipokuwa tutaongeza ufanisi na ubora wa kazi ile. Maana hata ardhi nayo kama mlivyosema wenyewe jana, si rahisi sana kupata maeneo kila miundombinu upite mahali pake. Kazi kubwa tutakayofanya ni kudhibiti ubora wa kazi inayofanyika na ndiyo maana tumeingiza suala hili la *code of practice* chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Paul Kimiti na Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy wote walizungumzia kuhusu bei, walitaka Serikali iweke utaratibu wa bei nafuu kwa maeneo yenye kipato kidogo. Haya nimeyazungumza, nafikiri yamefanana fanana na wale *economically disadvantaged groups*. Nataka niseme kwamba, sheria yetu hii inaainisha watu wasiokuwa na uwezo na hili nimelieleza kwa kifupi hapo mwanzo.

Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy amesema bei za maji zipangwe kwa kuzingatia hali halisi ya wateja; hili nalo nimeli-*cover* katika hayo ya mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya chombo cha udhibiti, yaani EWURA nimeyataja, lakini naomba nirudie kusema hivi; EWURA inaratibu utendaji wa Mamlaka za Maji kuhakikisha kuwa unaimarika kulingana na mpango wake wa kibiashara, yaani *Business Plan* ya EWURA, vikiwemo viashiria kama upotevu wa maji wakati wa kupitisha bei za maji na kadhalika.

Kwa hiyo, EWURA itaendelea kutenda kazi zake kulingana na *Business Plan*. Itakuwa rahisi bei ya viashiria ikiwa chini katika *Business Plan* zao, maana kwa kufanya hivyo watashindwa kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuundwa kwa vyombo vya Jumuiya za Wananchi, naomba hili nisilirudie kwa sababu nina hakika hata Mheshimiwa Waziri katika nafasi yake ataliainisha, kwa sababu linagusa sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi kabisa, mengine yanajieleza vizuri katika Sheria hiyo. Naomba nishukuru kwa nafasi hii na ninaiunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kutumia muda wako vizuri kabisa. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Waziri mtoa hoja ili aweze kuendelea kuhitimisha hoja yake, karibu sana Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo mkunjufu kabisa, nianze kwa kutoa shukrani zangu na za familia ya Mwandosya kwa rambirambi zilizotoka kwa Waheshimiwa Wabunge wengi, baada ya sisi kupatwa na msiba wa kufiwa na mama yetu mpendwa, usiku wa kuamkia tarehe 17 Aprili, 2009. Nawashukuru sana.

Shukrani nyingi zinakwenda kwa Wananchi wa Rungwe, waliojitokeza kwa wingi sana katika maziko hayo. Wananchi walitoka sehemu mbalimbali za Mbeya pamoja na viongozi wa dini, ninamshukuru Askofu wa KKKT, Askofu wa Morovian Jimbo la Kusini na Wachungaji kumi walioongoza misa ya maziko.

Vilevile ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Viongozi mbalimbali waliotutumia salamu za rambirambi. Nashukuru sana. Nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ilikuwa ya kina kabisa. Unaweza ukaandika kitabu kwa hizi siku mbili tu za michango ya Waheshimiwa Wabunge. Labda nitakapostaafu nitatumia haya niliyoyapata katika kuandika kitabu kitakachohusu udhibiti wa maji, matumizi ya maji na utunzaji wa rasilimali za maji. Lakini kama kuna mwanafunzi au mwananchi mwingine atanitangulia nitashukuru, kwa sababu haya

mambo ni mazito na ni muhimu kwa vizazi vinavyokuja. Michango ilikuwa muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmoja wa Waheshimiwa Wabunge alieleza kwamba, maji yapo pale pale lakini watu tunaongezeka. Huyo alikuwa ni Mheshimiwa Kidawa Salehe, maana yake mzunguko wa kihadolojia upo pale pale. Kwa hiyo, maji kuwa adimu inatokana na matumizi, vilevile na teknolojia na wingi wa watu. Matumizi yanaongezeka, watu wanaongezeka. Vyanzo vinapungua kutokana na hali ya hewa au mabadiliko ya tabia nchi, pamoja na uchafuzi wa mazingira. Tatizo lingine linalotukabili ni kwamba, palipo na maji watu hawapo na palipo na watu maji hakuna, lakini katika sehemu kama Kigoma pana watu hakuna maji; ni changamoto kubwa na hiyo ndiyo tutakayoikabili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nasoma ripoti moja hivi juzi kwamba, ili uweze kuzalisha kilo moja ya ngano unahitaji lita 1,000 za maji na ili uweze kupata kilo moja ya nyama ya ng'ombe unahitaji lita 15,000 za maji. Kwa hiyo, kila kitu ni maji, maji ni uhai. Kwa hiyo, jinsi tunavyoongeza kula nyama, ndivyo mahitaji yetu ya maji yanaongezeka na ndivyo kutakuwa na upungufu mkubwa wa maji. Sisemi kwamba tupunguze kula nyama wala ndafu. Ninataka tu kuonesha umuhimu wa maji katika uhai wa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia walikuwa ni wengi, nawashukuru kwa dhati kabisa. Naomba kama ilivyo ada, nitumie nje ya muda ulionipangia ili niweze kuwatambua. Wachangiaji walikuwa 91; waliochangia kwa kusema hapa Bungeni ni 20 na waliochangia kwa maandishi ni 71.

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kuongea ni Mheshimiwa Charles Keenja, ambaye alichangia kwa niaba ya Kamati ya Kilimo, Maji na Mifugo; Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Msemaji wa Kambi ya Upinzani (Waziri Kivuli), atulie kivulini kwa muda mrefu sana atuache sisi katika jua tuendelea na kazi, lakini namshukuru kwa mchango wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Kidawa Saleh, Mheshimiwa Kabwe Zitto, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa Zaynab Vulu, Mheshimiwa Kaika Telele, Mheshimiwa Zabein Mhita, Mheshimiwa Paul Lwanji na Mheshimiwa Engineer Christopher Chiza, Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Hawa ndiyo waliochangia kwa kusema hapa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia wa maandishi ni wengi nao ni pamoja na Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya,

Mheshimiwa Wilson Masilingi, Mheshimiwa Capt. John Komba, Mheshimiwa Fuya Kimbita, Mheshimiwa Beatrice Shellukindo, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Benson Mpesya, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Omar Kwaangw', Mheshimiwa Mwinchoum Msomi, Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Mwantumu Mahiza, Mheshimiwa Vuai Khamis, Mheshimiwa Stella Manyanya, Mheshimiwa Jackson Makwetta na Mheshimiwa Dkt. Samson Mpanda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Charles Nyanguru Mwera, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Juma Killimbah, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu, Mheshimiwa Jacob Shibiliti, Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Margreth Mkanga, Mheshimiwa Suleiman Omar Kumchanya, Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mheshimiwa Dkt. Maua Daftari, Mheshimiwa Felister Bura, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Dkt. Charles Mlingwa, Mheshimiwa Benedict Ole-Nangoro, Mheshimiwa Juma Said Omar, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga, Mheshimiwa Mwajuma Hassan Khamis, Mheshimiwa Dkt. Luka Siyame, Mheshimiwa Dkt. Guido Sigonda, Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu na Mheshimiwa Godfrey Zambi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, ninawashukuru kwa dhati kabisa wale ambao kwa njia moja au nyingine, kwa bahati mbaya nimewasahau. Nadhani kadiri ninavyoendelea kuchangia, majina yatakuja na nitawatambua ipasavyo; wataniwia radhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na masuala ya jumla katika mgawanyiko wetu wa kazi na sana sana nitajikita kwenye suala zima la usimamizi wa rasilimali maji na sheria inayohusika ambayo tunaipendekeza. Kwa kuanzia, nitajumuisha au nitazungumzia yale masuala ya kijumla, ambayo yamejitokeza hapa kwa kutoa ufafanuzi pale inapobidi zaidi ya ule ufafanuzi alioutoa kwa umahiri sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala zima la mgawanyo wa madaraka. Ukiisoma hii Miswada miwili na ukijaribu kuangalia chimbuko lake, Sera ya Maji ya Mwaka 2002, utaona kwamba ni utekelezaji wa dhana iliyojikita katika sera hiyo ya kurudisha madaraka inapobidi yawe, karibu na wananchi. Hili lipo bayana katika Miswada yote miwili na nitaeleza kwa maana hiyo; madaraka ya Waziri sasa yamepungua na hili halitupi shida sisi kwa sababu litaongeza ufanisi.

Nitoe mifano, kwa maana ya ule Muswada unaohusu Sheria ya Rasilimali, madaraka mengi ya Waziri ameyakasimu sasa kwa Mkurugenzi kiutendaji. Vilevile madaraka mengi ya Waziri sasa yanatekelezwa katika ngazi ya mabonde. Mambo mengi

ambayo Waziri alikuwa anayafanya sasa, sheria inasema yanafanywa moja kwa moja na Bonde; kwa maana ya kurudisha madaraka kule inakobidi yawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili ni kwamba, sasa mabonde yana uwakilishi mkubwa zaidi. Mabonde si sawasawa na Wilaya au Mikoa, mabonde yanachukua mipaka ya kihadolojia. Kwa hiyo, kwa maana ya hii sheria ya rasilimali, Halmashauri moja inaweza kuwa katika mabonde mawili, lakini bonde moja kwa mfano, Bonde la Rufiji lina Halmashauri au Wilaya 18. Kwa hiyo, hapo unapokuwa na Bodi huwezi kuwa na uwakilishi ambao unasema kila Halmashauri iwemo katika Bodi ya Bonde. Tunachosema sasa angalau katika ngazi ya Bonde, kuwe na uwakilishi ambao umewekwa kisheria kwa makundi ya watu, kwa sababu haiwezekani hata kidogo kuwa na wawakilishi toka kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, katika ngazi ya bonde dogo, basi madaraka ya kuteua Wenyeviti na Watendaji sasa yamekasimiwa kisheria kwa Bonde lenyewe. Kwa hiyo, Mwenyekiti hachaguliwi tena na Waziri anachaguliwa na Bonde lenyewe. Kwa hiyo, hii imepunguza kabisa madaraka ya Waziri, kwa maana ya shughuli za kila siku. Isipokuwa sheria inamtaka kama ilivyoorodhesha madaraka yake katika sheria, kusimamia zaidi sera, masuala ya sheria, kuleta Bungeni mabadiliko ya sheria na usimamizi wa kijumla. Kwa hiyo, wale ambao wakiisoma hii sheria wanafikiria kwamba, labda imemwongezea madaraka Waziri mwenye dhamana ya maji, hapana. Kwa kweli imepunguzia, lakini imempunguzia si kwa sababu sera inasema hivyo; imempunguzia kwa sababu ndivyo inabidi iwe kwamba, masuala ya maamuzi yafanyike katika ngazi za chini. Kwa hiyo, hili naomba lieleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi kwa maana ya ile sheria inayosimamia Maji na Usafi wa Mazingira, naomba mnisikilize jinsi madaraka ya Waziri yalivyopungua. Sheria hii tofauti na sheria nyingine, mtaona kila mahali inasema chochote atakachofanya Waziri, kinachohusu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, hawezi kufanya mwenyewe atashauriana na Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa; hii ni bayana kabisa popote pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hata katika uteuzi wa Bodi zilizo chini yake, inabidi apate ushauri kutoka Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kufuatana ama katika ngazi ya Mkoa au katika ngazi nyingine yoyote ile. Hiyo ni sheria, kwa hiyo hawezi kukurupuka kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini atazingatia sheria ambayo sasa inambana kwamba, wenye madaraka nao wana usemi katika sheria hii, hilo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, sheria hii inampunguzia Waziri madaraka ya kuchagua Bodi. Tunapendekeza hapa na ninaomba wale mlio na sheria muangalie kifungu cha 11(2)(b); kwanza kilikuwa kinasema, Waziri atakasimu madaraka yake ya kuteua bodi katika ngazi ya Wilaya na katika ngazi ya Miji ambayo ndiyo hasa ngazi ya Serikali za Mitaa.

Kipengele hicho sasa tumekiboresha zaidi katika jedwali la marekebisho kwamba, tumekifuta hicho na katika jedwali la marekebisho katika *schedule* ya kwanza

tunasema, uteuzi wa Bodi zote katika ngazi ya Halmashauri, utafanywa na Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa siyo Waziri wa Maji. Kwa maana hiyo, kwa mpigo sheria hii inamwondolea madaraka au inampunguzia madaraka Waziri wa Maji kuteua hizo Bodi. kutoka kuteua Bodi zaidi ya 120 kubakia na Bodi 19 za Makao Makuu ya Mikoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapo sijui waliokuwa wanafikiria kwamba, Waziri ameongezewa madaraka! Hapana, hajaongezewa isipokuwa amepeleka madaraka kule yanapotakiwa yawe. Tunasisitiza kwamba, bado sheria hii inambana Waziri kusimamia kwa ujumla sekta, lakini haimwondolei madaraka yake ya usimamizi wa kijumla kwa maana ya kusaidia katika masuala ya rasilimali watu, katika kupeleka rasilimali za fedha na katika viwango na kudhibiti kupitia EWURA.

Kwa hiyo, haya ndio maelezo na nitashangaa kama hii itakuwa ni hoja; si hoja tena kwa sababu hiyo ndiyo dhana ya kuleta Miswada hii kurudisha madaraka kwenye Halmashauri zenyewe na ndiyo msingi mkubwa wa sera hii.

Nadhani nimefafanua nilivyoweza kuhusu suala la mgawanyo wa madaraka. Kwa hiyo, mtakaposoma kila mahali tunasema Waziri pale alipo na madaraka, lazima ashauriane na Serikali za Mitaa. Tumeweka bayana sasa majukumu ya Sekretarieti za Mikoa ambayo hayakuwemo. Madaraka ambayo yangekuwa ya Waziri sasa yatafanywa na Halmashauri zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliona niliseme hili ili kuondoa hiyo dhana ambayo imejengeka na inaweza ikajengeka kwamba, Waziri ana madaraka makubwa, lakini anatajwa katika maeneo mengi kwa maana ya Wizara, siyo Waziri kwa maana ya utekelezaji wa majukumu yake. Hamuoni hapa Katibu Mkuu, lakini yeye ndiyo hasa Mtendaji Mkuu. Nilitaka kusema hili ili lieleweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye hoja nyingine za kijumla. Mheshimiwa Charles Keenja, Mheshimiwa Maige, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Kassim Mwandoro, Mheshimiwa Martha Mlata, Mheshimiwa Lucy Owenya na wengine wamesema, tutengeneze kanuni mapema na tutoe kipaumbele katika Sekta ya Maji kwa kuitengea fedha za kutosha kama Serikali. Mimi nawashukuru, hiki ni kilio cha kila Mbunge kwamba tatizo ni kubwa, kilio ni kikubwa, ni kero namba moja, lakini rasilimali kila mwaka zinapungua tutawafikishiaje wananchi maji safi, salama na ya uhakika katika mazingira ya namna hiyo?

Kwa hiyo, naamini kilio hicho Serikali imekichukua na tukumbuke Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka jana katika hotuba yake Bungeni akichangia katika shughuli zake za kawaida, alitoa kauli ya Serikali kwamba, maji yatapewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2009/2010. Sasa naamini Mheshimiwa Waziri Mkuu, hawezi kuzungumza hilo halafu watu wengine wakatenda vinginevyo. Kwa hiyo, nadhani mtatubana hapa hapa ilikuwa vipi? Nawashukuru sana kwa kutukumbusha hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wataalamu limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Tumeleta Muswada kwa Hati ya Dharura, wengi wenu mmesema na nawashukuru kwamba tumechelewa. Sasa kama tumechelewa tusiende pole pole kwa mwendo wa kinyonga. Tumesema Sera ya mwaka 2002 na utekelezaji wake kisheria ni 2009; kasi gani hiyo? Tunarudi tena tunasema mmekuja haraka mno, hapana. Hatukuja haraka na inajidhihirisha kwa michango iliyotolewa, hakuna uharaka wowote. Michango yote katika kipindi cha muda mfupi, inaonyesha umuhimu wa Miswada hii. Kwa hiyo, hakuna suala la uharaka hapa, tulichelewa kwa hiyo tumekuja kwa haraka. *We must run while they walk.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kidhana tu ukisema maji ni uhai, maana yake maji ni dharura. Sasa na mambo unayotaka kuyafanya lazima uyafanye kwa dharura, lakini kwa umakini. Kwa hiyo, ndiyo maana tumekuja kwa dharura. (*Makofi*)

La tatu, kuna mzunguko wa bajeti. Hii sheria tungeipitisha kwa mfano mwezi Novemba, maana yake utekelezaji wake na utekelezaji wa sheria unahitaji bajeti au unasimamia bajeti, kwa hiyo, ungekuja mwaka 2010/2011; tungekuwa tumepoteza mwaka mzima. Ndugu yangu Kabwe anasema kuna shinikizo. Kunaweza kuwa na ushauri sasa kama ni ushauri mzuri kwa nini ukatae? Tunaupokea ushauri, lakini ni jambo ambalo sisi wenyewe ilibidi tulifanye na tumelifanya. Kwa hiyo, niliona niseme hilo kuhusu udharura wa Muswada. Kwa yale yaliyotendeka katika siku mbili hizi, udharura haujajionesha hata kidogo. Michango mizuri sana, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nafikiri inadhihirisha ile *Peter's Principle* ambayo anasema kazi huongezeka kujaza muda uliopo (*work expands to fill the time available*). Muda ukiwepo kila kitu kinafanyika, lakini kazi inafanyika katika muda mfupi. Kwa hiyo, hakuna udharura wowote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la wataalamu ni muhimu sana, kwa sababu sera hii bila wataalamu, bila rasilimali watu, haiwezekani. Tuna mkakati wa kuendeleza wataalamu katika Sekta ya Maji na Umwagiliaji; tumeanza kuutekeleza chini ya Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Maji. Kwa hiyo, tunakipanua Chuo cha Maji, tunaboresha miundombinu, tunaongeza taaluma. Tunapeleka wanafunzi wetu nje ya nchi; tumeingia mkataba tunaishukuru Serikali ya India, tutapeleka wanafunzi wengi tu kwenda kusoma fani ya Uhandisi wa Maji India.

Tunalichukua hili suala lililozungumzwa na Mheshimiwa Kidawa Saleh, Mheshimiwa Bernadeta Mushashu na wengine wengi, kwa umuhimu unaotakiwa na hawa wote ndiyo tutakaowapeleka Wilayani. Kwa wale waliopo kilio ni kwamba, Wilaya nyingi hazina wataalamu. Tutaendelea kuwapeleka. Tunapopeleka sehemu nyingine kama tulivyopeleka Kondo wa wanakaa miezi sita wanarudi mjini. Hilo sasa ni tatizo la kitaifa tutaendelea kuliangalia. Labda tukiwa na wengi wakikosa kazi katika Miji Mikuu, watarudi katika Miji ya Wilaya. Kwa hiyo, labda tuwe na hiyo falsafa ya kusomesha watu wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mpangilio wa yaliyobaki nitakwenda sehemu kwa sehemu ili kusaidia twende pamoja katika kufafanua masuala ya kisheria kama tutakavyopitia kwenye kamati. Naanza na sehemu ya kwanza; jina la sheria, tarehe ya kuanza kutumika na tafsiri ya maneno. Hapa Mheshimiwa Ezekiel Maige, aliulizia maana ya *beneficial use* na tuiweke wazi. Tumeitolea tafsiri, *beneficial use* maana yake hasa ni kwamba, hati inakuwa imetumika kwa muda wote na kulingana na masharti yaliyo kwenye haki. Hati hii inakuwa imetumika vizuri, kwa hiyo, imekuwa na *beneficial use*. Katika sehemu ya pili, misingi na malengo ya sheria; Mheshimiwa Beatrice Shellukindo amesema, upangaji wa viwango vya ada ya matumizi ya maji uangaliwe upya. Napenda kusema kwamba, hili limezingatiwa katika kifungu cha 96(1) kinachohusu mamlaka ya bodi kutoza ada.

Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, amezungumzia kuhusu miradi kufanyiwa tathmini ya kimkakati ya athari, hasa jera na mipango. Aliulizia pia kwa nini miradi mikubwa nayo inafanyiwa tathmini ya athari kwa mazingira. Tumechukua haya maneno moja kwa moja kutoka kwenye Sheria ya Mazingira.

Kifungu cha 101(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 kinasema, pamoja na mengine kwamba, miradi mikubwa ya maji, miradi ya madini na miradi ya utafiti wa mafuta, inapaswa kufanyiwa mikakati ya athari za mazingira na Wizara zinazohusika. Kwa hiyo, hili namshukuru Mheshimiwa Profesa Raphael Mwalyosi, kutupatia nafasi ya kutoa ufafanuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kwamba neno *reserve* libadilishwe kuwa *conservation* katika kifungu namba 66(2)(b); sasa siyo *environmental reserve* ila kosomeke *reserve* na kifungu hiki tumekitolea ufafanuzi katika maana ya tafsiri ya maneno. Kwa hiyo, nadhani hilo limeeleweka kwa sababu linahusu uhai, linahusu hayo mazingira na linahusu matumizi mengine ambayo kinafanya. Watu wa bonde wanaweza kusema hatuwezi kutoa maji zaidi ya kiwango hiki kwa mtumiaji wa aina yoyote katika bonde au katika mkondo huo. Kwa hiyo, ndio maana ya *reserve* siyo *environmental conservation* tu, hapana matumizi ya bayoanuai na mambo mengine.

Sehemu ya tatu ni kuhusu umiliki wa rasilimali za maji, madaraka na majukumu ya Waziri na haki ya matumizi ya maji. Kuhusu madaraka ya Waziri nimelifafanua. Mheshimiwa Profesa Mwalyosi alizungumzia kwamba, kifungu cha 12(2) kizungumzie ulazima wa kufanya tathmini ya athari kwa mazingira, kwa miundombinu ya kuvuna maji. Tunakubaliana naye kwani miradi yote inatakiwa kisheria bila hata kuingiza humu kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, ifanyiwe tathmini ya athari za mazingira.

Sehemu ya nne, kuhusu mfumo wa kitaasisi, pamoja na mambo mengine, Mheshimiwa Charles Keenja kwa niaba ya Kamati alizungumza kwamba, sheria itumike; alisisitiza kutatua migogoro ya huduma za maji.

Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, alizungumzia kuhusu Bodi ya Maji ya Taifa kuwa chanzo cha ukiritimba. Labda nijibu kuhusu migogoro. Tunakubaliana na



ushauri wa Kamati na tutaitumia Sheria hii na ndivyo ilivyoandikwa kwamba, isaidie katika kutatua migogoro; kwa sasa itafanya hivyo kwa ufanisi zaidi kutoka ngazi za chini mpaka ngazi ya rufaa; kwa hiyo, itasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bodi ya Taifa niseme tu, haiwezi kuwa chanzo cha ukiritimba. Tumelifikiria sana hili suala. Hatutaki kuanzisha chombo kipya ni Bodi tu inayokutana mara tatu au nne kwa mwaka, kumshauri Waziri; haina Sekretarieti yake, Sekretarieti ni Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji. Kwa hiyo, Wizara yenyewe inakuwa ni Sekretarieti. Kwa hiyo, tunaoanisha umuhimu wa Waziri kupata ushauri lakini kutumia chombo hicho kwa kazi za siku hadi siku. Kwa hiyo, hakuna lolote la kuleta ukiritimba mwingine. Hii ni Bodi ya Ushauri tu.

Tukumbuke kwamba, tuna mabonde tisa, inatekeleza majukumu yake mengi, Bodi inatimiza wajibu wake; ina migogoro nadhani humo kuna masuala ya kuhamisha maji. Kuna ulazima kuwa na chombo kimoja kitakachomshauri Waziri. Zipo Bodi tisa; sasa Bodi zote hizo kila moja iende kumshauri Waziri. Si rahisi; inabidi kiwepo chombo kimoja ambacho kinaweza kumshauri Waziri kwa masuala ya rasilimali za maji Kitaifa na masuala ya Kimataifa.

Kwa hiyo, naomba kusisitiza kwamba, hakiwezi kuwa chanzo cha ukiritimba mwingine. Ndiyo maana tukaweka kwamba, Mkurugenzi wa Rasilimali Maji naye ni Mjumbe wa Bodi hiyo, vile vile ndiye Katibu wa Bodi na kwa shughuli za kawaida ndiye anayesimamia masuala yote ya Bodi.

Mheshimiwa Beatrice Shellukindo alizungumzia kwamba, Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji awe Mjumbe wa Bodi ya Maji ya Taifa. Hilo limezingatiwa vile vile kama nilivyosema katika jedwali la marekebisho. Wilaya ziwe chini ya bonde moja bila kujali mipaka ya mabonde ya maji; hili haliwezekani, kwa sababu wakati tunazungumzia maji, tunazungumza mfumo wa kihaidolojia, ndio maana Bonde la Rufiji lina Wilaya 18 na inawezekana hapa hapa Dodoma kuna Wilaya nyingine ambazo ziko kwenye bonde la kati na sehemu moja ya Wilaya katika Bonde la Rufiji; ndivyo ilivyo. Vinginevyo ukisema tugawe mabonde kisiasa; kiutendaji; ki-Wilaya; na Kimkoa haiwezekani kabisa katika masuala ya maji. Utekelezaji wake hautowezezekana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la ofisi za maji ni pamoja na kufanya utafiti na uchunguzi maji juu ya ardhi. Tunasema hilo ndilo jukumu lake, lakini vile vile tunasema taasisi nyingine za kiutafiti ziwe Vyuo Vikuu au sekta binafsi, wanaweza wakafanya kazi hiyo ilimradi wanaratibiwa na ofisi za maji katika mabonde na wanapata ruhusa kutoka mabonde. Kwa sababu kazi hizo zote zitasaidia katika shughuli za mabonde.

Sehemu ya tano kuhusu mipango ya pamoja ya rasilimali za maji. Mheshimiwa Keenja kwa niaba ya Kamati anasema, Serikali iwe na mipango endelevu ya upatikanaji wa maji kwa matumizi ya sasa na baadaye; ndio dhana nzima ya kuwa na mipango ya usimamizi na matumizi ya rasilimali za maji katika mabonde ambayo imejengeka katika sheria hii. Itahusisha wadau wote katika bonde na kuleta ile dhana kwamba, bonde si la

Wizara ya Maji au taasisi inayosimamia maji, bali bonde ni rasilimali ya Kitaifa na lisimamiwe kule ambako lipo.

Mheshimiwa Dkt. Samson Mpanda na Mheshimiwa Kidawa Saleh, walizungumzia kuhusu ubora wa kuwa na ramani za haidolojia. Hili ni suala ambalo tutalizingatia na lazima tuwe na ramani mpya ambazo tunaweza vile vile tukazihusisha mara kwa mara.

Mheshimiwa Bernadeta Mushashu na Mheshimiwa Salim Khamis walizungumzia kuhusu *Water Resources Data Base*. Wizara yangu imeanzisha *Data Base* ya Mito na vyanzo vyote vya maji nchini na sheria inataka Mkurugenzi wa Rasilimali za Maji na chombo hiki cha Kitaifa cha Bodi ya Maji, kuandaa ripoti za hali ya maji kila mwaka, ambapo lazima msukumo wake utatokana na ile *data base* ya *water resources*. Kwa hiyo, hilo ni suala ambalo litazingatiwa.

Mheshimiwa Profesa Mwalyosi amezungumza kwamba, huu mpango wa uwiano wa rasilimali za maji Kitaifa na katika mabonde ni mkubwa mno; kiutekelezaji itakuwa kazi ngumu. Tufanye nini sasa, ndio changamoto kwetu tutaifanya tutaona tutakapokwama lakini hatutaanguka. Kwa hiyo, niliomba niseme hilo; mmetupa changamoto na sisi tutaitekeleza. Niseme kidogo kuhusu Ziwa Natron, sitazungumzia masuala ya tathmini ya athari kwa mazingira, nitazungumzia majukumu yetu. Ziwa Natron liko katika bonde la kati. Ziwa Natron lenyewe ni rasilimali ya maji. Kwa hiyo, pamoja na mambo mengine yote, matumizi ya maji ya Ziwa Natron lazima yapate kibali cha Wizara yenye dhamana ya maji. Serikali ni moja, tutakwenda pamoja na kushirikiana. Kwa upande wetu sisi tunafanya mpango wa pamoja wa rasilimali za maji katika bonde la kati. Hiyo ni kazi muhimu, kabla hata hatujatoa, ujue kwamba maji tunayoyahitaji yako wapi, yanatosha, na kwa muda gani. Hatuwezi kutoa kibali chochote kile au kuruhusu mtu mwingine yeyote atoe kibali cha matumizi ya maji bila hiyo tathmini.

Kwa hiyo, hili lazima tulifanye na tutalifanya kwa muda wa miaka miwili kuanzia mwezi Januari, 2010 kwa bonde zima. Kwa sababu yote hayo yana uwiano, tushirikiane na Kenya, kwa sababu maji yanaingia Tanzania wakiamua kuyasimamisha basi Ziwa Natron halipo. Sehemu kubwa ya Bonde la Ziwa Natron lenyewe maji yanatoka Kenya. Hii ni rasilimali shirikishi, huwezi ukachukua maamuzi peke yako katika dhana nzima ya maji shirikishi. Matokeo ya mpango ndiyo yatakayotusaidia sisi na wengine watakaofanya tathmini ya athari kwa mazingira. Sasa lazima wajue maji ya kutosha yapo chini ya ardhi, yanakuwa *recharged* namna gani na yanawezekana kwa muda gani. Kwa upande wetu. Ndio kazi yetu. Nadhani nimeweza kujibu na kwa upande wetu sisi hatupo tayari mpaka mwaka 2012.

Sehemu ya sita ni utunzaji wa vyanzo vya maji. Wengi wamelizungumzia hili suala tunawashukuru. Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, amezungumzia sehemu hiyo ya utunzaji wa vyanzo vya maji kuhusu matumizi ya maji ardhini. Ameuliza; tunazungumzia *ground water controlled areas* je, sehemu nyingine? Nimkumbushe kwamba, sheria hii tunazungumza kuhusu *ground controlled areas* na maeneo mengine.

Kwa hiyo, hiyo tumeichukua katika sheria; umbali wa kutoka katika kisima hadi kisima hili ni suala la kitaalamu, unaweza wewe kama Waziri ukasema mita 20 unakuta mita 20 hamna kitu au kuna mwamba au nini, kwa hiyo haiwezekani kabisa. Hili ni suala la kitaalamu na hatuwezi kulifanya la kisheria.

Kuhusu fidia kwa waathirika wa uchafuzi wa maji, niseme na fidia kwa ujumla. Kwa kweli sisi tumezingatia maslahi ya watu wanaoweza kuathirika kwa uchafuzi wa maji kupitia vifungu namba 41(4) na kifungu 105, ambavyo vinazungumzia hatua za kisheria za kushughulikia fidia kwa waathirika wa uchafuzi wa maji. Tunaongozwa na sheria mama; Sheria ya Mazingira, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Nchini na Sheria Na. 20 ya Mwaka 2004. Hili suala ni la Kitaifa.

Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Capt. Komba, Mheshimiwa Maige, Mheshimiwa Diallo, Mheshimiwa Bafadhili, Mheshimiwa Samson Mpanda; ooh wengi sana ni zaidi ya 20 wamezungumzia kuhusu suala la ardhi oevu. Tunalisimamia kwa pamoja na Wizara ambayo ina dhamana ya suala zima la ardhi oevu kutokana na madaraka yaliyokasimiwa na Mheshimiwa Rais ni Wizara yenye dhamana ya Maliasili. Kutokana na asili ya chimbuko la maeneo oevu, kupitia Mkataba wa RAMSAR ambao asili yake ilikuwa ni maji yaliyo katika ardhi oevu na viumbe hasa ndege. Hili ndio ilikuwa chimbuko la ardhi oevu kuwa maliasili. Limeendelea hivyo; Serikali ni moja na tunafanya kazi pamoja.

Tupo katika Kamati mbalimbali za masuala ya ardhi oevu yanayosimamiwa na maliasili na utalii. Makatibu Wakuu wako katika *Steering Committee*, ambayo inasimamia ardhi oevu na ni Makatibu Wakuu wa Wizara nyingi tu; Wizara ya Miundombinu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Ardhi, Wizara ya Maji, Wizara ya Nishati na wao wenyewe Maliasili. Suala la maeneo ya ardhi oevu ni muhimu sana. Ardhi oevu ni chanzo cha maji; ni chujio ya maji; ni akiba ya maji; lakini vile vile ni muhimu kwa viumbe na bioanuwai. Kwa hiyo, tunashukuru kwamba, mmelileta hapa na mmetupa nafasi ya kulifafanua.

Mheshimiwa Profesa Mwalyosi na wengine, wamezungumzia kuhusu utekelezaji wa mita 60. Sisi tumelileta hapa, baada ya kuipitia Sheria ya Mazingira ambayo inazungumzia kuhusu mita 60 kutoka chanzo cha maji. Tunasema tu kwamba, Waziri mwenye dhamana ya maji akiona mita 60 hazitoshi kuhusu uchafuzi wa chanzo cha maji, basi anaweza akaenda zaidi ya mita 60, ndio tunalosema. Kwa hiyo, lote hili ni katika usimamizi wa mazingira na vyanzo vya maji. Kuhusu kifungu namba 35(2), ambacho kinazungumzia kutokufuta au tunapopunguza maji katika hati ya matumizi ya maji. Tunapunguza kwa pamoja katika eneo linalohusika. Nadhani ni sawa tu ili kuwe na uwiano katika punguzo kwa hati zote badala ya punguzo kwa mtu mmoja. Hii ni kuleta haki katika utekelezaji wa sheria.

Sehemu ya saba inazungumzia kuhusu mchakato wa kupata hati ya haki ya matumizi ya maji. Mgawanyo wa maji uzingatie hali halisi, tumeshauriwa tutafanya hivyo kupitia mipango ya maji ya mabonde. Mipaka ya mabonde ifafanuliwe; imo katika ramani kama nilivyosema, bonde moja linaweza kuwa na Wilaya 20, 15 na zaidi, lakini

ramani zipo; tutakapopata nafasi ya kuwa na ramani nzuri za mabonde, tutazisambaza kwa Waheshimiwa Wabunge katika Bunge lijalo.

Mheshimiwa Dkt. Willibrod Slaa na Mheshimiwa Maige, wamezungumzia kuhusu kupitia upya hati za haki ya kutumia maji na ndivyo sheria inavyotutaka, tumepata madaraka hayo. Kama nilivyosema katika maelezo ya utangulizi jana kwamba, kuna baadhi ya hati za haki ya kutumia maji zilitolewa kwa muda wote, *in perpetuity*, haiwezekani. Nyingine zilitolewa pamoja na hati ya kumiliki ardhi; hili ndio lina migogoro mingi sana na ndio tunataka kulipatia ufumbuji katika sheria hii. Hati ya haki ya watu kutumia maji karibu na vyanzo vya maji, ndio dhana nzima tunayojaribu kusema hapa kuhusu matumizi ya maji ya kijadi na vile vile afisa anapotoa haki au hati, lazima mchakato mzima upitie kwenye vijiji vile waridhike kwamba, nao wana maji ya kutosha kwa ajili ya matumizi yao kabla hawajawapa watu wengine. Kama kulikuwa na hitalafu ya utekelezaji huko nyuma, basi itakuwa imerekebishwa na sheria hii.

Nizungumzie kuhusu suala muhimu na nitoe ufafanuzi Kitaifa, kwa sababu kila sehemu nilipopita wanasema kwa nini Wilaya moja inapata maji yanayotoka Wilaya nyingine sisi wenyewe tusipate. Kimsingi haki ya matumizi ya maji inaweza ikatolewa kutoka chanzo chochote nchini, kwenda sehemu yoyote nchini, pale inapobidi kwa sababu rasilimali ya maji ni rasilimali ya Kitaifa ambayo haina mwenyewe. Utakuta kwa mfano, Wilaya ya Kyela na Mji wa Kyela unapata maji yake kutoka Rungwe Mashariki; huo ni mfano tu. Kwa hiyo, iko mifano mingi tu ambayo tungependa tufafanue kwamba ni dhana ile ya kwamba maji ni Taifa, maji sio ya Wilaya wala sio ya Mkoa. Naomba hili lieleweke. Tunachozingatia katika hati za matumizi ya maji ni kwamba zina masharti, zitakuwa na masharti kwa maana sharti moja ni kutochafua maji katika matumizi, kurejesha maji mtoni ili yabaki kwa ajili ya mazingira na matumizi mengine kutochukua maji zaidi ya kibali kinavyoruhusu na muda vile vile wa matumizi. Kibali chochote kile kitakuwa na masharti mengi, naomba hili lifahamike.

Mheshimiwa Profesa Mwalyosi amezungumzia pia kuhusu matumizi ya maji chini ya ardhi, yafanyike tu pale inapokuwa lazima. Hili litajitokeza katika mpango mzima wa uendelezaji wa rasilimali za maji katika mabonde na Kitaifa. Hili likijitokeza ukiwepo umuhimu tutafanya hivyo, lakini hatuwezi tukazuia maji chini ya ardhi kama maji juu ya ardhi katika eneo fulani hayapo na kama chanzo ni hicho hicho kama vile Dar es Salaam; sasa tumekwama na tunajua tunapata maji chini ya ardhi sehemu za Kimbiji, kwa hiyo tutayatumia. Tunaambiwa kwamba ni maji mengi sana lakini tutadhihirisha hivyo. Wataalamuu wanafikiri maji yaliyo maeneo ya Kimbiji ni zaidi ya nusu ya maji yaliyo katika Ziwa Victoria, lakini hatuwezi kuyaona maji chini, kwa hiyo tunaendelea na utafiti, lakini yapo sasa yameanza kutoka katika visima ambavyo vilichimbwa wakati wa kutafuta mafuta. Unapochimba au kutafuta mafuta au madini unapata maji. Tufanye nini kwa rasilimali ya maji; nalo limezingatiwa katika sheria hii.

Sehemu ya nane ni jumuiya za watumiaji maji; niseme tu kwamba, tumeombwa tuviimarisha na tunaviimarisha kama vinajulikana kisheria. Ndiyo maana ya sheria hii kuvileta vyote pamoja katika mfumo ambao unaweza ukatumia rasilimali za Taifa kuweza kuvisaidia vikundi kama vinakidhi taratibu fulani. Vinakuwa na Katiba zao,

vinasajiliwa na kuwa na uongozi wao ili viweze kupata misaada kupitia ofisi za mabonde kwa maana ya usafiri, mafunzo na mambo mengine. Kwa hiyo, hilo ni suala lingine tutalizingatia.

Kuhusu maji shirikishi, sehemu ya 12; niseme tu kwamba, mfumo mzima huu tumeuweka kwa sababu kuna masuala ya ndani ya nchi, kupitia mabonde kuna masuala ya Kitaifa. Kwa hiyo, kuna wajibu wa Wizara na kuna wajibu wa mabonde. Kwa mtiririko huo, Wizara itasimamia suala zima la maji shirikishi ya Kimataifa kupitia rasilimali za maji lakini mabonde katika ngazi za bonde pale walipo. Kwa mfano, Bonde la Ruvuma litashughulikia pamoja na majirani zao Mozambique, wakiongozwa na masuala ya Kitaifa kati ya Tanzania na Msumbiji kupitia Wizara ya Mambo ya Nje na mikataba mbalimbali Ushirikiano kati ya Tanzania na Mozambique. Tuna maeneo kama Ziwa Tanganyika, ambako tuna mamlaka ya Ziwa Tanganyika. Tuna Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, ambayo ni Kamisheni ya Afrika Mashariki. Vile vile sasa hivi karibu tutaleta Bungeni ombi la kuridhia Mkataba wa Kuingia katika Kamisheni ya Bonde la Zambezi, ambayo sehemu kubwa maji yake yanatoka Bonde la Ziwa Nyasa la Tanzania. Kama nilivyosema, tuna uhusiano na Mozambique, ambao tumeanzisha Kamisheni ya Pamoja kuhusu Bonde la Ruvuma. Kwa hiyo, hili tutalizingatia kwa maana hiyo.

Sehemu ya 13 inahusu makosa na adhabu, uharibifu na uchafuzi wa vyanzo vya maji; adhabu ni ndogo kwa Kampuni au Kiwanda. Suala hili limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi wametutahadharisha kuhusu suala hili; Mheshimiwa Mwakyembe, Mheshimiwa Meryce Emmanuel, Mheshimiwa Khadija Al-Qassmy, Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mheshimiwa Mpesya, Mheshimiwa Margaret Mkanga, Mheshimiwa Sakaya na Mheshimiwa Kwaangw'. Niseme tu kwamba, ukiangalia misingi ya sheria, tumeitoa ile misingi moja kwa moja kutokana na Azimio la Rio kuhusu maendeleo endelevu ya ulimwengu, pamoja na utunzaji wa mazingira. Moja ya misingi ni kwamba, mchafuzi hulipia gharama za kurekebisha uchafuzi huo na mchafuzi hulipa gharama za uharibifu wa mazingira na uchafuzi wa maji. Kwa hiyo, *polluter pays principles* ni dhana muhimu sana.

Hizi adhabu haziruhusu kurekebisha au kurudisha hali iliyokuwa nzuri kabla hawajachafua; ni gharama tofauti ambazo wachafuzi watalipa tu. Msingi mkubwa wa adhabu katika suala zima la uchafuzi wa mazingira na uchafuzi wa maji. Kwa hiyo, ukifanya marekebisha au *re-restoration* ili kurejesha hali kama ilivyokuwa kabla ya uchafuzi; ni msingi muhimu sana katika kuliangalia hili suala la adhabu.

Mambo ya msingi ambayo ni ya jumla, *miscellaneous provisions*; suala la fidia limejitokeza na niseme tu kwa maana ya fidia za ardhi na vitu vilivyo juu ya ardhi; suala zima hili linazingatiwa na sheria za ardhi na suala zima la uchafuzi wa mazingira linasimamiwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Kwa hiyo, suala zima la uchafuzi limezingatiwa katika sheria za nchi na vile vile katika sheria hizi ambazo tunazileta Bungeni ili Bunge liweze kuridhia na kuzipitisha hatimaye ziwe sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dada yangu Mheshimiwa Mwanne Mchemba, aniwie radhi, yeye amechangia kwa maandishi na kama ilivyo kawaida yake, mambo mengi yamehusu Tabora; tutayazingatia katika majibu yetu ambayo tutayaandaa, hatuwezi kujibu kila hoja, kwa hiyo, tumezungumza yale ya kijumla; na hata mpangilio jinsi nilivyoweke wa kujibu hizi hoja umekwenda kufuatana na vifungu au kufuatana na sehemu za Muswada ili itusaidie katika majadiliano yanayofuata ya kupitisha kifungu kwa kifungu. Yale masuala ya Mbunge mmoja, labda Rungwe Mashariki nina mradi wangu wa umwagiliaji; hili tutalijibu kwa maandishi na tutasambaza majibu hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti nirudie kusema tena kwamba, kila ninapokuwa Bungeni hapa kuwasikiliza Waheshimiwa Wabunge hasa katika mijadala mbalimbali, mimi ninakuwa shuleni; nasema elimu haina mwisho kila wakati nimefaidika. Nashukuru sana kwa yote mliyoyasema. Nashukuru sana kwa kuunga mkono, hata Mheshimiwa Zitto, mimi nilivyomsoma hakupinga; alilalamika tu kwamba, sheria zimekuja kwa haraka na ninaamini ataunga mkono kifungu kwa kifungu ili tuwe na sheria bora, tuweze kuwapatia maji Wananchi wa Kigoma haraka na kwa dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Naomba niseme tena, **maji ni uhai na usafi wa mazingira ni utu.** Hayo ndiyo kaulimbiu yetu. Kwa hayo niliyoyasema, nawashukuru tena ahsante sana na naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mwongozo wa Mwenyekiti. Kanuni ya 86 ya Kanuni zetu za Bunge, Toleo Mwaka 2007, inazungumzia suala la kurejesha Muswada kwenye Kamati wakati bado upo katika kusomwa kwa mara ya pili na kabla haijaenda kwenye Kamati ya Bunge Zima. Jana wakati nachangia, kuna masuala ya msingi (*fundamentals*), kabisa kuhusiana na *role* ya *state* na *market* katika suala zima la maji, ambapo Mheshimiwa Waziri alipokuwa anaeleza hapa hakuweza kufafanua; na kwa sababu ya kutokuwa na majibu na kutokufahamu hayo majibu, inakuwa ni vigumu sana kuweza kujua kama twende katika hatua ya tatu au tuurudishe kwenye Kamati Muswada huu wa *Water Supply and Sanitation*.

Ninachokizungumzia hapa ni kifungu cha 19, ambacho kinazungumzia suala la ugavi wa maji kwenye soko, kwa maana ya *service providers*. Kifungu cha 35 ambacho pia kinapeleka maji hata kwenye vijiji, zile *Community Association* za maji zinaweza kuwa *provided* na soko kwa maana ya *market* na zinapewa nguvu na kifungu namba 15(1)(2) kuhusiana na masuala hayo hayo. Siku za hivi karibuni tu hata miaka mitano haijapita, tumekuwa na tatizo kubwa sana hapa nchini kuhusiana na suala la ubinafsishaji wa maji na mfano mzuri ni suala la *City Water* na baadae DAWASCO sasa hivi kuna matatizo makubwa sana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kabla hatujakwenda kwenye hatua ya tatu ambayo ni ya Kamati ya Bunge Zima; na kwa sababu suala hili ni *fundamental*, linahusu uhai wa

mwananchi; je, tunafanya maji kuwa *commodity* ambapo soko ndilo litakalo-*provide* na *state* inajitoa katika suala hili?

Kwa hiyo, kwa mwongozo wako, nilikuwa napenda Mheshimiwa Waziri aweze kuutoa huo ufafanuzi, kuhusiana na vifungu hivyo vya 19 na 35 kama vinavyopewa nguvu na kifungu cha 15, ambacho sasa kinapeleka suala la maji kwenye soko na kinaondoa *role* ya *state* katika kuwapa watu maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninapokea mwongozo wa Mheshimiwa Kabwe Zitto, lakini tunasema kwamba, tunaingia katika hatua ya Muswada kusomwa mara ya pili, kwa maana ya kufanya maamuzi katika Kamati. Nikirejea Kanuni ya 84, kifungu alichokizungumza, inatakiwa pia aendelee mbele aangalie Kanuni namba 86(11), ambayo inakusudia kutoa maelekezo ya Wabunge kufanya marekebisho ya maeneo ambayo wanapenda yafanyiwe marekebisho. Kwamba, kama hoja hiyo ya msingi ya mchango wake wa mawazo ilitakiwa kwa Kanuni namba 86(11), angeiweka katika jedwali la marekebisho ili iweze kumfikia Katibu na kuona namna gani itahusishwa katika ajenda ya kufanya maamuzi leo.

Utaratibu wote wa kuingia kwenye hatua hiyo, unatupeleka Kanuni namba 88(2), inayoweka masharti hayo hayo ya kuzingatia wakati wa Kamati ya Bunge Zima katika kufanya marekebisho. Niseme tu kwamba, Mheshimiwa Zitto, unayo hoja na hoja yako ya msingi ni kumwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kupata ufafanuzi wa kina katika hayo ambayo umeyasema.

Waheshimiwa Wabunge; ni kweli kabisa kwa muda ambao Mheshimiwa Waziri ameupata, asingeweza kuyasema mambo yote; lakini tutakapofika kwenye vifungu, atapata nafasi ya kutoa hayo maelezo ya ufafanuzi. Katika hatua hiyo basi, Mheshimiwa Zitto Kabwe utapata nafasi ya kuwahoji Waheshimiwa Wabunge; wanafikiri nini katika uzito wa hoja ambayo utakuwa umeileta na majibu ya Mheshimiwa Waziri.

## **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

### **Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2009 (*The Water Resources Management Bill, 2009*)**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Kamati ya Bunge Zima; kama nilivyotoa maelezo yangu hapo awali, Miswada hii sasa tutaipitisha mmoja baada ya mwingine kwa hatua zote. Sasa tutaanza na Muswada wa kwanza ambao ni *The Water Resources Management Act, 2009* na ninaomba Katibu aanze kutuongoza.

Ibara ya 1

Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge)*

*Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3

Ibara ya 4

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 5

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 6

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 7

Ibara ya 8

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 9

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11

Ibara ya 12

Ibara ya 13

Ibara ya 14

Ibara ya 15

Ibara ya 16

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 17



*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 19

Ibara ya 20

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 21

**MHE. PROFESA RAPHAEL B. MWALYOSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichangia kwa kuzungumza, lakini vilevile nilichangia kwa maandishi; nilidhani pengine naweza kuzungumzia hapa kwamba, kuna Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji, ambalo lina majukumu yanayofanana na *Rufiji Basin Water Board*. Ninataka maelezo au ufafanuzi kuhusu Sheria hii; inaungana mkono au kupishana vipi na Sheria inayounda Mamlaka ya Uendelezaji wa Bonde la Mto Rufiji, kwa sababu yote mawili yanahusu maji ingawa Mamlaka ya Uendelezaji wa Mto Rufiji yanahusiana vilevile na masuala mengine si maji peke yake lakini maji ni kati ya *resource* ambayo inashughulikia?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba, tulipata mchango wa Mheshimiwa Mwalyosi, kuhusu suala zima la mwingiliano au uhusiano kati ya RUBADA na hizi Bodi za Maji na hasa kwa RUBADA maana yake ni Bonde la Mto Rufiji. Niseme tu kwamba, kama yeye alivyokiri, RUBADA ina upeo mkubwa kwa sababu ni kuhusu maendeleo ya Bonde la Rufiji, ambayo ni kubwa zaidi kuliko maji. Maji ni kiini cha maendeleo na kwa maana ya maji, tunamwona RUBADA ndiyo mtumiaji mkubwa, ambaye atakuwa chanzo cha kuyatumia maji kwa ajili ya maendeleo ya Bonde la Rufiji.

Kwa hiyo, yeye ni mdau mkubwa ambaye hatuwezi kufanya kazi bila kumshirikisha. Kwa maana ya Sheria ya Maji ya Nchi, Sheria ni moja ambayo ni hii tunayoipitisha; lakini pale palipo na mgongano tutajaribu kuurekebisha. Nikiri kwamba, RUBADA ni chombo muhimu sana, lakini ni kikubwa zaidi ya masuala ambayo tunayazungumzia hapa. Iwapo kuna maeneo ambayo RUBADA inayafanya, basi itakuwa inafanya kwa kushirikiana na Bodi na itakuwa kwa faida ya RUBADA yenyewe na kwa faida ya BODI. Kwa hiyo, hakuna moja inayofuta nyingine. Ingekuwa maendeleo yamefumka na ni makubwa ambayo yote ni kwa sababu ya RUBADA, basi tungemtegemea RUBADA ndiyo awe mtumiaji mkubwa wa maji katika Bonde. Kwa

maana ya kinchi, huwezi kuwa na Sheria ya Maji ya RUBADA halafu Sheria ya Maji ya Nchi. Ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23

Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 25

Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

Ibara ya 28

Ibara ya 29

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

Ibara ya 32

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 33

Ibara ya 34

Ibara ya 35

Ibara ya 36

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 37

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 38

Ibara ya 39

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 40

Ibara ya 41

Ibara ya 42

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 43

Ibara ya 44

Ibara ya 45

Ibara ya 46

Ibara ya 47

Ibara ya 48

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 49

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 50

Ibara ya 51

Ibara ya 52

Ibara ya 53

Ibara ya 54

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge*

*Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 55

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 56

Ibara ya 57

Ibara ya 58

Ibara ya 59

Ibara ya 60

Ibara ya 61

Ibara ya 62

Ibara ya 63

Ibara ya 64

Ibara ya 65

Ibara ya 66

Ibara ya 67

Ibara ya 68

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 69

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 70

Ibara ya 71

Ibara ya 72

Ibara ya 73

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 74

Ibara ya 75

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 76

Ibara ya 77

Ibara ya 78

Ibara ya 79  
Ibara ya 80

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 81  
Ibara ya 82  
Ibara ya 83

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 84  
Ibara ya 85

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 86

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na marekebisho hayo, lakini nilikuwa nashindwa kuelewa pengine ningepata ufafanuzi kwa sababu yanatoa baadhi ya ufafanuzi. Sasa nimeona kuna *interpretation* kwenye *clause three* na *clause 86* inahusu *interpretation* pia; kwa nini *interpretation* isingeweza kurudi kule nyuma kwenye *clause three* kwa sababu ndani ya Muswada kuna *clause* ambayo inatoa tena ufafanuzi wa maeneo badala ya kuwa kwenye *clause* inayohusika? Pengine ningepata ufafanuzi wa kisheria.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni suala la uandishi wa Sheria na limetumika katika Sheria nyingi. Unaweza ukampoteza mtu kwa sababu Sheria ni kubwa kwa kila tafsiri kuweka mwanzo. Anapofika mahali katika sehemu anataka kuitumia, basi inabidi arudi tena mwanzo na akifika katika sehemu ya kumi kwa mfano, kwa sababu ametoka mbali, inabidi aweke yale ambayo ni mahususi kwa sehemu ile alipo; inakuwa rahisi sana kufuatilia Muswada au Sheria ile. Nakushukuru ahsante sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 87  
Ibara ya 88  
Ibara ya 89  
Ibara ya 90  
Ibara ya 91  
Ibara ya 92

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 93  
Ibara ya 94

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 95  
Ibara ya 96  
Ibara ya 97  
Ibara ya 98  
Ibara ya 99  
Ibara ya 100  
Ibara ya 101  
Ibara ya 102  
Ibara ya 103  
Ibara ya 104  
Ibara ya 105

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 106  
Ibara ya 107

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 108  
Ibara ya 109  
Ibara ya 110  
Ibara ya 111  
Ibara ya 112  
Ibara ya 113  
Ibara ya 114

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia ukurasa wa 65, kifungu kidogo cha tano kinasema: *“The Minister may dissolve the*

*National Water Board.*” Lakini pia ukienda ukurasa wa 66, kuna kifungu kidogo cha nne kinasema: “*The Minister may dissolve the National Water Board.*” Sasa nataka kupata ufafanuzi kama linaweza likabaki hivyo hivyo kwamba, Waziri anaweza akavunja Bodi lakini hakuna sababu zozote ambazo zimetolewa kwamba kwa nini anaweza akaivunja Bodi. Ukienda kwenye kifungu cha nne, ukurasa wa 65 anasema, Waziri anaweza akamwondoa Mwanachama kwenye Bodi, baada ya kufanya makosa; kwa mfano, kutohudhuria kwenye vikao kadhaa au baada ya kutangaza kwamba amefilisika; hizo ni sababu ambazo Waziri anaweza kumwondoa mtu kwenye Bodi, lakini sababu kubwa za kuvunja Bodi hazitolewi. Sasa ninataka kujua; zitakuwa kwenye Kanuni au kwa nini hazikutolewa hizo sababu kwenye Sheria hii?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Zambi, kama kawaida anasoma sana Miswada hii. Kwanza, niseme tu kwamba, hili suala ni la kiutendaji zaidi, lakini lina nguvu ya kisheria kwamba, Waziri kama ana mamlaka ya kuteua basi anaweza kuwa na mamlaka ya kuvunja. Kwa hiyo, anasema “*may*”, ni lugha laini kwamba anaweza kwa sababu yeye ndiye aliyeteua. Kama Bodi imefanya mambo kwa pamoja na ikapingana na malengo iliyowekewa na Waziri akaona kwa maslahi ya taifa, basi anakuwa na mamlaka hayo ya kuvunja Bodi.

Mheshimiwa Mbunge aamini kwamba, Mawaziri bomu ni wachache sana. Hakuna Waziri ambaye wanaweza akakurupuka. Mfumo mzima wa Wizara ambao una mshauri kisheria mpaka Mwanasheria Mkuu, halafu Waziri avunje tu Bodi, aseme leo ameamka avunje Bodi, hapana. Hatuendi namna hiyo. Kama alivyopewa madaraka ya kisheria, inabidi afuate sheria na taratibu ili aweze kuvunja Bodi.

Kwa hiyo, naomba alichukulie hilo kama lilivyo ila wale walioteuliwa katika Bodi wajue kwamba, wana dhamana kubwa ya kutekeleza majukumu waliyonayo na kwamba, wakienda kinyume kwa pamoja, wanaweza wakaondoka wote kwa pamoja.

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali la 2  
Jedwali la 3  
Jedwali la 4

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya Bunge  
Zima pamoja na mabadiliko yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2009  
(*The Water Resources Management Bill, 2009*)**

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima, imeupitisha Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji wa Mwaka 2009 (*The Water Resources Management Act, 2009*), kifungu kwa kifungu na imeukubali pamoja marekebisho yaliyofanyika. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada huo sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa  
Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hatua za kuupitisha Muswada huo zimeshafikia mwisho, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri na timu yake ya Wataalamu. Ninaomba nichukue nafasi hii, niipongeze Serikali kwa ujumla, tunategemea sana kwa niaba ya Wananchi wote wa Tanzania na kama Mheshimiwa Waziri ulivyosema, maji ni uhai; basi ninaamini Muswada huu utakuwa kwa maslahi ya Wananchi wa Tanzania na baada ya hatua ya Mheshimiwa Rais, utaweza kufanyiwa kazi kiasi cha kutosha.

Waheshimiwa Wabunge, kwa muda tuliobakiwa nao ambao ni dakika chache, hauwezi kututosha kuendelea na upitishwaji wa Muswada unaofuata, basi ninafikiri nisitishie shughuli hizi ili tuweze kukutana jioni ili tumalizie kupitisha Muswada ambao umebakia na mara baada ya kuupitisha tutaingia katika hatua inayofuata ya kuendelea na ajenda za leo mchana.

Sasa nasitisha shughuli hizi mpaka saa kumi na moja jioni.

*(Saa 6.48 mchana Bunge lilifungwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mheshimiwa Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

## **KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa  
Mazingira wa Mwaka 2009**  
*(The Water Supply and Sanitation Bill, 2009)*



**MWENYEKITI:** Kabla sijamwita Katibu, niwakumbushe tu kwa sababu Miswada hii ni miwili, Muswada ambao tunaushughulikia jioni ya leo ni ule wa Sheria Mpya ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2009. Niwataarifu pia kwamba, hapa Mezani sina *schedule of amendment* yoyote kutoka upande wa Waheshimiwa Wabunge, lakini ipo ya Serikali.

Ibara ya 1  
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3  
Ibara ya 4  
Ibara ya 5  
Ibara ya 6  
Ibara ya 7  
Ibara ya 8  
Ibara ya 9

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 10

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 11  
Ibara ya 12

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 13  
Ibara ya 14

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 15

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 16  
Ibara ya 17  
Ibara ya 18  
Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20  
Ibara ya 21

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 22

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 23  
Ibara ya 24

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 25  
Ibara ya 26

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27  
Ibara ya 28  
Ibara ya 29

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 32

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 33

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 34

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 35

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ibara hii ya 35 inaenda pamoja na ibara ya 19 na zinajengewa msingi na ibara ya 15, ambayo inahusiana na suala la *private sector* kuwa *involved* kwenye ugavi wa maji (*supply of water services*). Kama nilivyoeleza hapo awali kwamba, Muswada huu unajaribu kutekeleza Sera ya Maji ya Mwaka 2002; Sera ambayo inataka huduma za maji kwa maana ya *water supply and sanitation*, ziweze kuendeshwa na *sector* binafsi (*private sector*). Kama nilivyosema hapo mwanzo kwamba, mimi siamini kama tumefikia wakati kama nchi kuweza ku-*privatize water services* na kuicha tu kwenye mikono ya watu binafsi, kwa sababu tayari tumeshaona matatizo mbalimbali.

Zipo nchi mbalimbali ambazo zimeingia kwenye matatizo, kwa sababu ya ku-*privatize water services*. Tuliona miaka ya mwanzo ya 2000, nchini Afrika Kusini, ambapo miji ambayo ili-*privatize water services* ilileta matatizo makubwa sana; Puertorico Private Sector, Vivend Company ya France, ilisababisha wananchi wapate maji ambayo ni *contaminated* kwa sababu siyo *public sector*. Nami siamini kabisa kwamba, tumefikia wakati sasa wa kuweza ku-*privatize supply* ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kutokana na hilo, nilikuwa Ofisini kwa Mshauri wa Sheria wa Bunge ili kuweza kuhakikisha kwamba, kifungu hicho cha 35, kifungu cha 19 na kifungu cha 15(1) na (2) ambavyo ndivyo vinabeba kifungu hicho, viweze kuongezewa... Sasa hivi nimempatia Waziri *schedule of amendment* kwamba, katika kile kifungu cha 15(1), baada tu ya maneno yale, naomba nisome: “A *water authority, shall as a licensee, be responsible for the efficient...*”

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, unasoma fungu lipi?

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Kifungu cha 15.

**MWENYEKITI:** Huko nilishavuka zamani!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 35 na kifungu cha 19, haviwezi kufanya kazi kwenye hii sheria bila kifungu cha 15. Kwa hiyo, nilikuwa naomba hilo lieleweke. Hata kwenye tafsiri, imeoneshwa wazi kabisa kifungu cha 15, kifungu cha 19...

**MWENYEKITI:** Nimeshasimama; Mheshimiwa Zitto, nikisimama wewe unakaa chini.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sikukuona.

**MWENYEKITI:** Hapa nilipo, nimesimama! Kifungu kilichopo ni cha 35, kwa hiyo, naomba ujielekeze hapo. Niseme tu kwamba, sijapokea *schedule of amendment* toka kwa Mbunge yeyote. Kwa kadiri ambavyo Mwenyekiti hana mabadiliko hayo; hayo mabadiliko hayapo. Kifungu hiki cha 35 kinahusu *appointment of service providers*. *Service provider* ni mwendeshaji si mmiliki. Haizungumzii habari ya ubinafsishaji. Sasa nilitaka tu nikupe mwongozo kidogo ili nikupe nafasi ujielekeze vizuri; unataka Mheshimiwa Waziri afafanue nini? Endelea Mheshimiwa Zitto. (*Kicheko/Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *City Water* ilikuwa ni *service provider* na ndiyo *point* ninayoizungumza. Inawezekana kabisa kwamba, tukataka tushindane kwa *technicality* hapa, lakini ukweli ni kwamba, tutawaingiza wananchi kwenye matatizo makubwa sana. Kifungu cha 35 kinazungumzia kuwa na *private operator* katika ngazi ya *community*, kijijini; na wala hapa hatuzungumzii Dar es Salaam, Arusha au Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 35 hakifanyi kazi bila kifungu cha 15. Naomba nikusomee, kinaanza na suala zima la *water authority* kuweza...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, nakuomba sana twende kwa taratibu zilizopo. Hatua hii ya Kamati ya Bunge Zima, tunakwenda kifungu kwa kifungu. Nikishauliza Bunge Zima mkaniidhinishia kwamba mnaafiki, tunavuka. Kwa hiyo, naomba ujielekeze kwenye 35, kama kuna tatizo kwenye 35 ulieleze ili Serikali iweze kutoa ufafanuzi. Usinirudishe kule ambako tumeshavuka. (*Makofi*)

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi; kwa nini Serikali inataka ku-*privatize water services*?

**MWENYEKITI:** Hilo swali; Mheshimiwa Waziri! (*Kicheko*)

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza kwa makini sana Mheshimiwa Zitto. Nimejaribu kumuelewa, lakini

nadhani tunasoma Miswada miwili tofauti; wa kwake na wa kwangu. Huu Muswada ambao naomba kwa heshima kubwa Bunge lako Tukufu liupitisha, unahusu ushiriki mkubwa na mkubwa zaidi wa Serikali katika Sekta ya Maji. Unahusu Wizara yenye dhamana ya maji kuhusika katika kila ngazi katika sumamizi wa Sekta ya Maji. Unahusu kuitaka Serikali iweze kuvisaidia vyombo mbalimbali kifedha na vinginevyo katika kuendeleza Sekta ya Maji.

Unahusu vile vile kuviruhusu vyombo huru wala siyo sekta binafsi, kama inavyoeleweka au kampuni toka nje; vyombo vya wananchi kupanga mipango yao jinsi wanavyotaka ilimradi viwe kwa mujibu wa sheria hii; na vile vile kupitisha maamuzi yote yanayohusu mtoa huduma ambaye wangependa kumtumia kupitia maamuzi ya Serikali kupitia Vikao vya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu msingi wake mkubwa ni hatimaye kumpatia Mwananchi wa Tanzania maji safi, salama na ya uhakika katika umbali wa mita 400 kutoka makazi yake na hilo ndilo jukumu ambalo Serikali ya Chama cha Mapinduzi inalibeba, si vinginevyo. Kwa hiyo, nadhani tunasoma Miswada miwili tofauti. Suala la ubinafsishaji hapa siyo msingi wa Muswada huu. Niseme tu kwamba, haiwezekani Serikali kujiondoa katika suala zima la kutoa huduma ya maji, kwa sababu maji ni msingi na tunasema humu katika Muswada kwamba maji ni haki ya binadamu. Sera inasema hivyo na sisi tunasema hivyo na Muswada huu umejengeka katika msingi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada ninaousoma ndio ambao Wabunge wamepewa; *The Water Supply and Sanitation Act*. Pamoja na kupata *assurance* zote za Serikali kuhusiana na suala hilo, lakini bado nilikuwa naomba Waziri apate fursa tena ya kulihakikishia Taifa ya kwamba, suala zima la uendelezaji wa miundombinu ya maji, maana yake sheria hii yote hamna hata *provision* moja inayosema kwamba, itakuwa ni *sole responsibility of the state* kuendeleza *infrastructure* ya maji. Matokeo yake kuna *insistence* kubwa na ndio maana nilisema pale mwanzo wakati nachangia kwamba, kuna uwezekano mkubwa sana kwamba, sheria hii imekuja na mashinikizo. Wewe ukasema kwamba ni ushauri. Mheshimiwa Waziri, naamini kabisa ni mashinikizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zitto, nimesimama hapa mara mbili sasa ni ya tatu, kukutaka urudi kwenye kifungu. Kifungu hiki kinaongelea habari ya watoa huduma; msingi wa maneno yako ni masuala ya ubinafsishaji ambayo hayako katika kifungu hiki. Sasa unapanua wigo, unaenda; nipo kwenye kifungu cha 35, kama una neno hapo sema, kama huna niwahoji Wabunge twende fungu lingine au kama una maneno katika fungu lolote linalofuata. Naomba nikurudishe tena kwenye kifungu cha 35 cha watoa huduma na siyo ubinafsishaji.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, watoa huduma ni watu binafsi na haina maana nyingine yoyote; lakini kama Serikali ya CCM ipo tayari ku-*privatize* maji, mnaweza mkaendelea.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, tunasoma Miswada miwili tofauti, lakini si mbaya kuendelea kuelimishana kwa sababu kama Mheshimiwa Kabwe nilivyosahau nikamwita ndugu, naye ameniita Profesa, sasa nataka kuwa Profesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtoa huduma katika kijiji au popote pale anaweza kuwa Serikali, anaweza kuwa mtu kama mtu, inaweza kuwa ni jamii, kikundi cha kijamii, inaweza kuwa asasi isiyo ya kiserikali. Kwa hakika sehemu kubwa ya utoaji maji nchi hii, haitolewi na Serikali hata kidogo. Kwa hiyo, nadhani tunasoma Miswada miwili tofauti.

Namwomba sana Mheshimiwa Kabwe arudi tena kwenye misingi ya Muswada huu; msingi mkubwa ni Serikali kuamua na kuji-*comit* kupitia Sera na sasa kuipa nguvu ya kisheria kwamba, tunataka kufika huko ambako tutampatia Mwananchi wa Tanzania maji safi, salama na ya uhakika. (*Makofi*)

Ibara ya 36

Ibara ya 37

Ibara ya 38

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 39

Ibara ya 40

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 41

Ibara ya 42

Ibara ya 43

Ibara ya 44

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 45

Ibara ya 46

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 47

Ibara ya 48

Ibara ya 49

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)

Ibara ya 50

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumzie uhalisia hasa wa kifungu hiki cha 50 ili baadae Mheshimiwa Waziri aweze kunipa ufafanuzi. Wananchi wengi mijini na vijijini wanapoomba kuunga maji, baadhi yao huwa ni kwa matumizi binafsi (*personal consumption*), lakini kuna suala la ujirani mwema; pengine katika eneo lile kuna wananchi hawana uwezo wa kuunga maji, kwa hiyo, wangehitaji msaada wa yule ambaye ameunga maji; na kwa bahati nzuri mwananchi yule anakubali, anatoa *extension* kutoka katika nyumba yake ili kuwapatia maji wale wananchi ambao hawana, lakini hawapatii bure ni kwa malipo labda ndoo moja shilingi 100/200.

Sasa ukiangalia kifungu hiki ni kwamba, ile *initial purpose* haipo kwa sababu ilikuwa *for personal use*, lakini sasa hivi amewapa wananchi wengine kwa ujirani mwema tu na siyo bure. Kwa hiyo, hapa naona huyu ni mkosaji kwa sababu anafanya jambo ambalo hakutakiwa afanye. Vile vile katika sehemu ya tatu ya kifungu hiki cha 50 kuna suala la *penalty* (adhabu), ambalo linasema *penalty* itatokana na *the value of water improperly used*, yaani yale maji ambayo amewapa majirani mimi ninafikiri ni *improperly used*. Sasa swali, atawezaje kujua *value* ya maji yale kwa sababu hakuna mita maalumu kwa ajili ya wale; yeye ametoa kwa ajili ya ujirani mwema tu, lakini hakuna mita *special* ambayo inasoma matumizi ya wale majirani ambao anawauzia, anafanya biashara? Kwa hiyo, ningependa kupata maelezo ya ufafanuzi katika hali kama hii, sheria hii inasemaje? Ahsante.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu jirani mwema ambaye anauza maji siyo mwema labda angetoa bure, halafu yeye alipie kwa kampuni ambayo inatoa huduma. Kwa hiyo, huu ni wizi mtupu wa maji! (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Ibara ya 51

(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)

Ibaraya 52

**MHE. DKT. LUKA J. SIYAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi, kifungu hiki cha 52 kinahusu yule mtu ambaye atatenda kosa la kutiririsha

udongo, vitu ama vimiminika kwenye mfumo wa maji. Tukiangalia ile adhabu ni shilingi zisizozidi milioni moja ama kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili.

Hapa ndiyo pale ambapo tunakuta hawa watu wanatenda kosa ambalo linaweza kuleta milipuko ya magonjwa kama kipindupindu, homa za matumbo ama kuhara damu na hata kumwagia sumu kwenye huo mfumo wa maji.

Kwanza, adhabu yenyewe, kiwango cha chini hakijatajwa na pia adhabu zenyewe nafikiri kwa kosa lenyewe ni ndogo mno. Hivyo basi, kwa lile suala nililosema la kwanza, inampa nafasi hakimumu kumwachia huyu mtuhumiwa, kwa sababu hakuna kiwango cha chini cha adhabu.

Pili, nafikiri ingekuwa vyema tukarekebisha adhabu hizi zikawa kali zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Siyame, mbona hukuleta mabadiliko?

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukashtakiwa kwa sheria hii, lakini vile vile ukabanwa na sheria nyingine. Kwa hiyo, usiangalie hiki kipengele tu ukafikiri ndicho kitambana huyu mtu, kwa sababu kuna sheria mbalimbali za uharibifu. Kwanza, lile kosa tu la kuingiza vitu vingine katika maji, inakuwa ni kosa moja, kosa lingine inawezekana ni kuharibu miundombinu ya maji.

Makosa chungu nzima; kosa la kuharibu mazingira, kosa kuhusiana na afya. Kwa hiyo, hapa sidhani kama mtu wa namna hii atatoka kwa shilingi milioni moja tu.

Mahakimu ni kama sisi tuliopo hapa; ni watu wenye busara tu na wanasoma. Mtu akiharibu miundombinu au aingize vitu ambavyo vinaweza vikaleta madhara kwa binadamu, halafu aambiwe umefanya kitu kizuri; shangwe, sherehe, ondoka mahakamani, uko huru! Huyo sidhani kama ni hakimumu ambaye ni Mtanzania.

Kwa hiyo, naomba akubaliane na sisi kwamba, hii kwa sasa inatosha, nadhani mbele ya safari tutajua nini la kufanya, lakini kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote viwili ni adhabu kali sana.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 53

Ibara ya 54

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 55



*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 56  
Ibara ya 57

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 58

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Ibara ya 59  
Ibara ya 60  
Ibara ya 61  
Ibara ya 62

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1  
Jedwali la 2

*(Majedwali yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima pamoja na mabadiliko yake)*

Jedwali la 3

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya  
Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa  
Mazingira wa Mwaka 2009  
(The Water Supply and Sanitation Bill, 2009)**

*(Kulisomwa Mara ya Tatu)*

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijatoa taarifa, nilipokuwa nawashukuru watu mbalimbali kufuatana na msiba ambao ulinipata, nilimsahau mtu mmoja muhimu sana, ambaye alisafiri kutoka Ibwera, Bukoba

Vijijini kuja Kijiji cha Lufilyo, Rungwe Mashariki, kwa ajili ya kilio hicho, naye si mwingine bali ni Ndugu Hamim Mahamudu, namshukuru sana.

Vile vile nawashukuru sana Wananchi wa Rungwe Mashariki, kwa ushirikiano mkubwa na kama kawaida naahidi kuwatumikia kwa nguvu na juhudi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kutoa taarifa kwamba, Kamati ya Bunge Zima imeupitia Muswada wa Sheria ya Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira ya Mwaka 2009 (*The Water Supply and Sanitation Act, 2009*), kifungu kwa kifungu na imeukubali pamoja na marekebisho yaliyofanyika. Hivyo basi, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada huo sasa ukubaliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maji ni uhai, usafi wa mazingira ni utu, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*  
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa  
Mara ya Tatu na Kupitishwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Muswada wetu umepita katika hatua zetu zote, kwa hiyo, unasubiri hatua inayofuata ya kupata kibali cha Rais ili uwe umekamilika kuwa sheria. Nawatakia Wizara ya Maji na Umwagiliaji na wadau wote wa maji kila la kheri katika kutekeleza Muswada huu wa sheria.

Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaendelea na suala lingine, nilikanganyikiwa kidogo maana yake ndiyo nilipata *schedule of amendment* ya Mheshimiwa Kabwe Zitto wakati Muswada ukiwa umeshapita hatua zake zote na yeye alikuwa analalamikia fungu Na. 15 wakati anaingia hapa Bungeni kumbe tulikwishavuka kwenye Fungu hilo. Kwa hiyo, niwatake Waheshimiwa Wabunge siku nyingine kama kuna mambo kama haya muwe mnawahi kidogo ili inapofikia kifungu husika, basi unajikuta unazungumzia jambo husika badala ya kusibiri kifungu kingine ambacho kidogo kiko mbali.

## **HOJA ZA KAMATI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, naomba nimwite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa John Momose Cheyo.

**MHE. JOHN M. CHEYO - MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Kabla ya yote na mimi nachukua nafasi hii kumtakia ndugu yangu Profesa Mwandosya pole kwa kufiwa na Mama yake,

kwa umri tulio nao hali ndiyo hizo. Kwa hiyo, tunaomba Mwenyezi Mungu aweke roho ya Mama mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu Na. 114 (15) cha Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2007 naomba kuwasilisha Taarifa ya kazi za Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kipindi kilichoanzia Aprili, 2008 mpaka Aprili, 2009. Katika kipindi hicho Kamati ilijadili Hesabu za Serikali za Mwaka wa bajeti wa 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati hii kwa ushirikiano wao na kwa kazi nzuri waliyoifanya Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yaliyoainishwa hapo juu. Michango hiyo imesaidia kuboresha na kujenga dhana ya kuwepo nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za Serikali kulingana na Sheria, taratibu na Kanuni zilizopo. Kwa heshima kubwa, naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa John Momose Cheyo - Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid - Makamau Mwenyekiti, Mheshimiwa Mohammed Rished Abdallah, Mheshimiwa Aloyce Bent Kimaro, Mheshimiwa Issa Kassim Issa, Mheshimiwa Hasnain Gulamabbas Dewji, Mheshimiwa Ruth Blasio Msafiri, Mheshimiwa Dr. Chrisant Majiyatanga Mzindakaya, Mheshimiwa Ponsiano Damian Nyami, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Severina Silvanus Mwijage, Mheshimiwa Rosemary Kirigini, Mheshimiwa Ali Haji Ali, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya na Mheshimiwa Manju Salim Msambya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake nzuri aliyotoa tarehe 31 Desemba, 2008. Katika hotuba hiyo Mheshimiwa Rais pamoja na mambo mengine alisisitiza kuwa ili kuondoa ubadhirifu wa fedha za umma, kuwepo na ukaguzi wa thamani ya kazi (*value for money audit*) badala ya kuishia kukagua nyaraka ambazo mara nyingi kinachoonekana kwenye nyaraka hizo hakifanani na thamani ya kazi iliyofanywa kwa fedha hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hotuba yake nzuri aliyotoa tarehe 31 Januari, 2009 iliyoainisha mikakati ya Serikali ya kubana matumizi kwa kupunguza ununuzi wa magari ya kifahari pamoja na semina, warsha na makongamono yasiyo ya lazima ili kupata fedha kwa ajili ya kununulia matrekta yatakayosaidia kuboresha uzalishaji katika kilimo. Kama nilivyoieleza kwenye taarifa ya Kamati mwaka uliopita, Kamati nyingi za Hesabu za Mabunge ulimwenguni sasa zinashughulika na kazi pana zaidi ya kuangalia taarifa na vitabu vya mahesabu (*financial statements*) mezani. Kazi muhimu inayolikabili Bunge ni kuhakikisha kwamba fedha zilizotolewa na Bunge zimeleta matokeo yaliyotarajiwa "*Value for money*". Suala hili linawezekana tu kama Kamati zinawezeshwa kusafiri na kuangalia miradi inayotekelezwa na Serikali. Hata Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pia imepanua shughuli zake ambapo sasa inajikita katika ukaguzi wa thamani ya kazi iliyofanyika, ukaguzi wa mazingira na miradi inayotekelezwa na fedha za wafadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi muhimu inayoongoza utendaji wa kazi za Kamati; naomba kurejea sehemu ya taarifa ya Kamati hii kwa mwaka 2008 kwa kutaja misingi muhimu inayoongoza Kamati wakati wa utendaji wa kazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msingi wa Kwanza ni kwamba tunafuata Katiba ya Tanzania Ibara ya 63, nanukuu; “*Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya majukumu makuu ya Serikali ni kukusanya kodi na fedha kutoka vyanzo mbalimbali vya walipa Kodi na kutumia fedha hizo kama vile Bunge lako Tukufu lilivyoidhinisha. Kazi yetu kama Bunge ni kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kutumia Kamati mbalimbali. Kazi ya Kamati ya Hesabu za Serikali ni kukagua Hesabu za Serikali (*financial audit*) na utekelezaji wa malengo ya bajeti (*performance Audit*) na kuishauri Serikali katika matumizi bora na endelevu ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tunashauri Bunge lako Tukufu lijielekeze kwenye Sura ya Saba ya Katiba Ibara ya 133 mpaka 144 (Masharti kuhusu Fedha za Jamhuri ya Muungano) na kwa msisitizo mambo yafuatayo yaangaliwe kwa makini:-

(a) Fedha za Serikali haziwezi kutumika bila Sheria iliyotungwa na Bunge (Ibara ya 136).

(b) Hakuna Kodi ya aina yoyote itakayotozwa isipokuwa kwa mujibu wa Sheria iliyotungwa na Bunge (Ibara ya 138).

(c) Majukumu ya Mdhambi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (Ibara ya 143) ambayo ni pamoja na kuhakikisha kwamba fedha zitatoka kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali kwa matumizi yaliyoidhinishwa na Bunge na angalau mara moja kwa Mwaka kukagua mahesabu yote ya Serikali na kupeleka taarifa ya Ukaguzi kwa Rais.

Aidha, Rais anawajibika kuwaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofuata baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile kikao kilipoanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Katiba katika eneo hili umepewa nguvu ya kisheria katika Sheria ya fedha (*Public Finance Act No.6*) kama ilivyorekebisha Mwaka 2004. Sheria inasisitiza kwamba Mdhambi na Mkaguzi Mkuu anafanya kazi yake ya Ukaguzi kwa niaba ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nanukuu kifungu 31(1) : *“The Controller and Auditor General shall on behalf of the National Assembly examine, inquire into and audit the accounts submitted to him under section 25 of this Act and perform any other functions which he is authorized to perform by or under this Act.”*

Mheshimwa Mwenyekiti, Sheria ya Ukaguzi wa Umma (*The Public Audit Act, 2008*) pia inatoa madaraka kwa Kamati za Bunge na hatimaye kwa Bunge zima kushughulikia masuala ya fedha za Serikali. Nanukuu: *“39 (1) The Public Accounts Committee, Local Authority Accounts Committee, Parastatal Organisations Committee and any other Parliamentary Sectoral Committee as the case may be, shall discuss the reports of the Controller and Auditor General after they have been tabled in the National Assembly.” (2) Upon the completion of hearing the Parliamentary Oversight Committees shall prepare and submit to the National Assembly reports which may include comments and recommendations”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni zilizotengenezwa na Waziri wa Fedha chini ya Sheria ya Fedha (*Public Finance Act, No.6 of 2001*) Sehemu ya Pili zimeeleza uwajibikaji wa Maafisa Wahasibu kwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), nanukuu:-

*“Every Accounting Officer shall be personally and pecuniarily responsible and accountable for the collection and receipt of all revenue or for all disbursements of expenditure in his vote, and shall be answerable to the Public Accounts Committee (PAC).”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu ya Kamati ya Hesabu za Serikali yameainishwa katika Kanuni za Bunge (2007) Nyongeza ya Nane (8) Kifungu cha 10 kama ifuatavyo:-

(a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hiyo yenye lengo la kuondoa matatizo hayo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali; na

(c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali kuhusu matumizi ya fedha za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hii, kila Afisa Mhasibu anawajibika kufika mbele ya Kamati ya Bunge na kutetea utekelezaji wa bajeti ya fungu lake na anaweza kuadhibiwa kwa mujibu wa sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ina sehemu tano, yaani sehemu ya kwanza - utangulizi, sehemu ya pili -masuala ya ujumla, sehemu ya tatu - matokeo ya ukaguzi,

sehemu ya nne - maoni na mapendekezo ya Kamati, sehemu ya tano - ziara za Kamati na mapendekezo yake na sehemu ya sita ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili ni masuala ya jumla, Mzunguko wa Uwajibikaji (*accountability loop*). Kamati inasisitiza kuwa Serikali inapashwa kuwajibika kwa Bunge kwa fedha zote inazopewa na Bunge. Aidha, Katiba inamtaka Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua na kutoa taarifa kwa Bunge kupitia Ofisi ya Rais. Taarifa ya Ukaguzi ndiyo msingi wa kazi za Kamati na pia ni kigezo cha kutathmini uwajibikaji wa Serikali katika mapato na matumizi ya fedha na rasilimali za Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukamilisha mzunguko huo, Taarifa ya CAG huletwa mbele ya Bunge na baadaye kwenye Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ambayo hufanya uchambuzi kwa kuwahoji Maafisa Masuhuli na kuleta mapendekezo yake mbele ya Bunge lako Tukufu. Ni wajibu wa Serikali kuyachukuwa mapendekezo hayo kwa ajili ya kuyafanyia kazi na kutoa majibu kupitia Ofisi ya CAG kwa ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya Serikali kujibu mapendekezo ya Kamati na CAG ndiyo inakamilisha mzunguko wa uwajibikaji. Kamati inasikitika kutoa taarifa kwamba tangu Mwaka uliopita Serikali iko kimya na haijajibu mapendekezo ya Kamati ya mwaka 2008. Ukimya huu wa Serikali unadhoofisha kazi ya Bunge ya kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake ya kibajeti kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inasisitiza kuwa mzunguko huu wa uwajibikaji ni muhimu na wote inabidi tuufuate ili kuonyesha kwamba wote tunajali na tunawajibika kwa fedha na rasilimali za Taifa. Hivyo Serikali ianzishe utaratibu wa kujibu mapendekezo ya Kamati katika mfumo wa “*treasury notes*” ndani ya muda maalumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) Kamati inatoa pongezi kwa Serikali na Bunge lako Tukufu kwa kupitisha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 inayotoa uhuru kwa ofisi ya CAG na hivyo kuifanya itekeleze majukumu yake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya CAG inaikagua Serikali kwa niaba ya Bunge kama ilivyoielezwa katika Sheria ya fedha (*Public Finance Act No.6*). Sheria inasisitiza kwamba Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anafanya kazi yake ya Ukaguzi kwa niaba ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatumia nafasi hii kumpongeza Mthibiti na Mkaguzi Kuu wa Hesabu za Serikali na watumishi wote wa Ofisi yake kwa kazi nzuri wanazofanya kwa niaba ya Bunge pamoja na mazingira magumu ya kifedha yanayoikabili Ofisi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kifungu cha 41 cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma (*Public Audit Act, 2008*) kinamtaka kila Afisa Masuhuli kuandaa taarifa ya

Mpangokazi (*Action Plan*) wa namna ya kuondoa upungufu uliojitokeza wakati wa ukaguzi katika Wizara na Idara husika.

Nanukuu: “41(1) *The accounting officers shall respond to the Controller and Auditor- General’s annual audit reports and prepare action plan of the intended remedial actions for submission to the Paymaster General. (2) On receipt of the responses and action plans, the Paymaster General shall submit to the:-*

(a) *Minister who shall lay it before the National Assembly in the next session;*

(b) *Controller and Auditor- General a copy of the consolidated responses and action plan; and*

(c) *The Controller and Auditor-General shall include an implementation of the action plan in the next annual report.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii bado hajatekelezeka na hata katika taarifa iliyowasilishwa na CAG hakuna majibu ya Wizara ya fedha na mipangokazi ya kutatua mapungufu yaliyoelezwa na CAG. Jambo hili ni la kisheria na Kamati inatumia nafasi hii kusisitiza Katibu Mkuu wa Wizara ya fedha (*Paymaster General*) atimize wajibu wake kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Aprili, 2008 mpaka Aprili, 2009 Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ilifanya kazi zifuatazo:-

(1) Kujadili Hesabu za Serikali Kuu zilizokaguliwa za mwaka 2006/2007; Kamati ilijadili Hesabu za Serikali zilizokaguliwa zilizoishia tarehe 30 Juni, 2007 ambapo mafungu 36 kati ya 70 yalijadiliwa sawa na asilimia 51 ya mafungu yote;

(2) Kufanya ziara ya kukagua thamani ya kazi zilizofanywa kwa fedha za Serikali kwa mwaka 2006/2007; katika mwaka 2008 Kamati ilifanya ziara ya kukagua thamani ya kazi katika maeneo yafuatayo:-

(i) Barabara ya Dar es Salaam-Kibiti-Lindi-Mingoyo ;

(ii) Mradi wa gesi iliyoko Mnazi Bay, Mtwara ;

(iii) Mradi wa bomba la maji ya Ziwa Victoria– Shinyanga– Kahama;

(iv) Bwawa la maji la Manchira, Mugumu;

(v) Vitega uchumi vilivyo katika mbuga ya Serengeti; na

(vi) Mradi wa kutengeneza boti za Jeshi Kigamboni, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho Kamati pia ilipata Semina mbalimbali ambazo zilizokusudia kujenga uwezo kwa Wajumbe. Semina hizi ziliendeshwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Mradi wa *Deepening Democracy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia ilijadili Azimio la Bunge kuhusu Azma ya Kufuta Madeni na Upotevu wa Vifaa vya Serikali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2007 na maoni yake yaliwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu katika Mkutano wa 12 wa Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ukaguzi yamebaini dosari zilizosababisha kujitokeza Hoja za Ukaguzi katika mafungu mbalimbali yaliyojadiliwa na Kamati, kwa muhtasari, hoja nyingi za ukaguzi zilihusisha kuwepo kwa dosari zifuatazo:-

(1) Masurufu yasiyorejeshwa; hadi kufikia Juni 30, 2007 jumla ya masurufu ya Sh.3,138,942,669/= yalikuwa bado hayajarejeshwa kinyume na sheria na kanuni za Fedha ikiongozwa na Ofisi ya Waziri Mkuu (Idara ya Mpira Chapa Mkuu wa Serikali) iliyokuwa na masurufu ya Sh.1,310,093,343/=. Kiambatisho (A) Kamati haikujadili Hesabu Fungu hili kwa hiyo, haijui hali yake ilivyo kwa sasa.

(2) Tofauti ya malimbikizo ya maduhuli yaliyoonyeshwa katika hesabu; kwa mwaka 2006/2007 kulikuwa na tofauti ya hesabu za malimbikizo ya maduhuli kati ya hesabu za Taifa (*National Consolidated Final Accounts*) na hesabu za ukaguzi (*Audited Accounts*). Malimbikizo ya maduhuli kwenye hesabu za Taifa yalikuwa Sh.6,081,130,117/ na hesabu za Ukaguzi ni Sh.14,424,611,011/=. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi pekee ilikuwa na malimbikizo ya Sh.11,940,719,660/= Kamati ilikutana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi 17 Oktoba, 2009 na maduhuli yaliyobaki na Sh. 7,186,341,440/= ambazo zinaombewa kibali Hazina ili zifutwe.

Aidha, maduhuli haya yanatokana na malimbikizo ya ada za wanafunzi ambazo hazijalipwa. Kamati iliagiza juhudi zifanywe ili kuondoa malimbikizo hayo. Kiambatisho (B) Kanuni ya 83 ya Sheria ya Fedha Na.6 ya 2001 kama ilivyorekebisha mwaka 2004 inamtaka Afisa Mhasibu kukusanya maduhuli yote katika siku 30 baada ya mwisho wa mwaka wa fedha unaohusika. Licha ya Maafisa Wahasibu kukumbushwa na CAG katika taarifa zilizopita baadhi ya wahusika wameshindwa kufuata sheria ya fedha. Inaonekana juhudi za kukusanya mapato ya Serikali ni ndogo na jambo hili linasababisha upungufu mkubwa katika bajeti ya Wizara husika. Kamati inasisitiza Maafisa Wahasibu wafuate Sheria ya Fedha.

(3) Mwaka wa Fedha wa 2006/2007 kulikuwa na malipo yenye shaka (*Questionable payments*) ya Sh. 82,820,848,330/= yakiongozwa na Wizara ya Fedha na Uchumi iliyokuwa na malipo yenye shaka ya Sh. 80,572,857,053/=. Kamati ilikutana na Wizara ya Fedha na Uchumi tarehe 15 Oktoba, 2008 na kubaini kwamba Wizara imeonyesha nyaraka zinazohusika na



kwa sasa hoja hiyo imeshafungwa Kiambatisho (C) CAG alitoa taarifa kwamba kutokuwepo kwa nyaraka za matumizi kulileta shaka kwamba matumizi hayakuwa halali.

(4) Malipo kwa ajili ya matumizi ya mwaka uliopita (*Deferred Payments*) jumla ya malipo yanayofikia Sh. 904,567,135/= yalilipwa Mwaka wa Fedha 2006/2007 baada ya mwaka wa fedha husika kupita na iliongozwa na Wizara ya Usalama wa Raia iliyolipa Sh. 801,431,484/=.

Katika kikao cha Kamati kilichofanyika tarehe 01 Februari, 2009 Kamati iliambiwa kuwa mawasiliano na Hazina yalikuwa yanaendelea ili kupata kibali cha kuhalalisha maliop hayo. CAG ametoa taarifa kwamba malipo haya yalizuiwa makusudi ili Wizara isionekane imetumia fedha zaidi ya zile zilizoruhusiwa na Bunge. Kamati ilisisitiza sheria ya fedha ifuatwe. (*Avoidance of excess spending*).

(5) Malipo yasiyo na Hati za Malipo (*Unvouched Expenditures*) ni yasiyokuwa na ushahidi wa maandishi kuthibitisha uhalali wa matumizi yake. Jumla ya Sh.1,288,040,677/= zilitumiwa bila kuwa na kumbukumbu ikiongozwa na Wizara ya Ulinzi (Ngome) iliyolipa Sh. 614,980,930/=. Kamati haikujadili Hesabu za Fungu hili kwa hiyo, haijui hali yake ilivyo kwa sasa. Aidha, mwaka 2005/2006 Wizara iliyoongoza kwa tatizo hili ilikuwa Wizara ya Afya iliyotumia Sh. 771,322,380/= bila nyaraka na mwaka 2006/2007 tatizo hili lilidhibitiwa. Kamati inasisitiza juhudi za kuzuia hoja na sio umahiri wa kujibu hoja.

(6) Katika mwaka 2006/2007 kulikuwa na malipo yenye hati pungufu yenye jumla ya Sh. 9,489,465,695/= ikiongozwa na Jeshi la Kujenga Taifa lililokuwa na malipo yenye hati pungufu ya Sh. 3,045,290,483/=. Kamati ilipokutana na Afisa Mhasibu wa Fungu hili tarehe 16 Aprili, 2009 hoja hii ilikuwa imeshajibiwa kwa hiyo, imeshafungwa. Kamati iliona pamoja na tatizo hili kuendelea udhibiti umeongezeka kwani mwaka 2005/2006 upungufu huu ulikuwa na thamani ya Sh. 36,665,182,261.

(7) Ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Wizara ya Usalama wa Raia umeonesha kuwa kumbukumbu za Wizara hiyo zilionesha madeni yasiyolipwa na bidhaa na huduma mbalimbali yalifikia Sh. 18,525,429,295 katika mwaka wa fedha 2006/2007. Ni dhahiri kuwa madeni haya yana athari kubwa kwa matumizi ya Wizara kwa bajeti iliyofuata. Katika kikao cha tarehe 01 Februari, 2009 Kamati ilielezwa kuwa madeni haya bado hayajalipwa. Kamati iliagiza Wizara iwasiliane na Hazina ili kuhakikisha kuwa madeni haya yanalipwa. Aidha, juhudi zifanywe kuhakikisha kuwa madeni haya yanadhibitiwa.

(8) Fedha zilizocheputuliwa na Wizara ya Nishati na Madini Fungu 58 – Sh. 208,662,656/=; Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2006/2007 pia imeonyesha kuwa hesabu za Fungu 58 zilionyesha matumizi yasiyosadikiwa kufanywa na Ofisi ya TANSORT nchini Uingereza ya Sh. 1,405,961,585/=. Hata hivyo ilibainika kuwa Sh. 1,613,624,242/= zililipwa kwa ofisi ya TANSORT Uingereza. Tofauti ya Viwango hivyo ya Sh. 206,662,656/= ilitumika

kugharamia shughuli nyingine za Wizara. Hakukuwa na kibali toka Hazina cha kuidhinisha matumizi ya juu ya kiwango kilichoidhinishwa.

(9) Mrahaba usiokusanywa kutoka kwenye almasi, jumla ya Dola za Kimarekani 1,086,577.11 zilikuwa ni mrahaba usiochukuliwa toka kampuni ya *Williamson Diamond Limited* katika mwaka wa fedha 2007/2008. Kampuni hiyo ililipa Dola za Marekani 370,716 na kuacha bakaa ya mrahaba Dola za marekani 715,861.49 ambazo ni sawa na fedha za Tanzania Sh. 841,137,251/= zinazotakiwa kulipwa kwa Serikali mara moja.

(10) Wadai na Miadi isiyolipwa Sh. 9,146,364,218; Katika mwaka wa fedha 2006/2007. Idara moja na Sekretarieti moja ziliripoti wadai na miadi isiyolipwa yenye jumla ya Sh. 9,146,364,218/= kinyume na mfumo wa bajeti ya fedha taslimu na udhibiti wa bajeti chini ya *IFMS*, kama ilivyooneshwa hapa chini:-

<b>Fungu</b>	<b>Wizara/ Idara inayojitegemea/ Mkoa</b>	<b>Kiasi Sh.</b>
29	Idara ya Magereza	9,132,581,369
74	RAS-Kigoma	13,782,849
	<b>Jumla Shilingi</b>	<b>9,146,364,218</b>

(11) Mwaka 2006/2007 bidhaa zenye thamani ya Sh. 4,635,051,714/= hazikuingizwa kwenye leja ikiongozwa na *RAS* Tanga Sh.134,772,216/=. Kamati ilipokutana na Afisa Mhasibu wa Fungu hili tarehe 20 Januari, 2009 iliambiwa kuwa vifaa hivi vimeshaingizwa vitabuni na hivyo hoja hii imefungwa. Vifaa/huduma vilivyolipiwa ambavyo havikupokelewa; aidha, bidhaa na huduma zenye thamani ya jumla ya Sh. 10,490,648,384/= hazikujulikana kama zimetolewa au kufanyika pamoja na ukweli kwamba zilikuwa zimelipiwa ikiongozwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Sh. 8,103,130,448/=. Katika kikao chake cha tarehe 15 Januari, 2009 hoja ilikuwa imeshajibiwa na hoja imefungwa.

Bidhaa na huduma zenye thamani ya Sh. 645,092,064/= zilinunuliwa ikiongozwa na Ofisi ya Waziri Mkuu *TAMISEMI* Sh. 178,450,630/= bila kuwa na Zabuni za Ushindani. Katika kikao cha *PAC* tarehe 9 Aprili, 2009 Kamati ilitibitishiwa kwamba manunuzi yalifanywa kupitia manunuzi ya zabuni za Wizara na vifaa vimeingizwa kwenye vitabu na kuhakikiwa na hoja imefungwa. Kamati ilisisitiza kuzuia hoja na kufuata sheria ya manunuzi.

(11) Udhaifu katika uingiaji na usimamizi wa mikataba kwa mwaka 2006/2007 udhaifu wa mikataba katika maeneo machache yaliyokaguliwa ulikuwa na jumla ya Sh.12,444,277,577/= ikiongozwa na Wizara ya Mambo ya Ndani kiasi cha Sh. 9,624,295,729/=. Mpaka Kamati ilipokutana na Afisa Masuhuli tarehe 16 Oktoba, 2009

ilibaki Sh. 5,386,302,000/=. Kamati ilielezwa kuna jitihada zinafanyika kurekebisha kasoro hizi.

Ni matumaini ya Kamati kuwa mpaka kufikia leo, kasoro hizi zitakuwa zimerekebishwa kwa kiasi kikubwa. Malipo yaliyofanywa kabla ya vifaa na huduma kupokelewa; Mwaka 2006/2007 jumla ya malipo yenye thamani ya Sh. 178,539,995/= yalifanywa kabla ya bidhaa/huduma kupokelewa ikiongozwa na Ofisi ya Bunge kiasi cha Sh.119,741,801/=. Hata hivyo, katika kikao cha Kamati tarehe 7 Aprili, 2009 wakaguzi waliambia Kamati kuwa hoja hiyo imeshafungwa.

(12) Katika mwaka 2006/2007 kulikuwa na malipo yenye kasoro mbalimbali jumla ya kiasi cha Sh. 1,232,832,255/= ikiongozwa na Jeshi la Kujenga Taifa Sh.417,245,087/=. Katika kikao cha Kamati kilichofanyika tarehe 16 Aprili, 2009 kasoro zilizobaki zilikuwa ni Sh. 73,862,000/= tu. Kamati iliagiza juhudi ziendele kufanyika ili kufuta kasoro zilizobaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonyesha kuwa Maafisa Wahasibu wanao uwezo wa kutunza na kufuata sheria za fedha kwani walio wengi wameweza kujibu hoja zote na kuzifunga. Kamati inasisitiza umuhimu wa kuzuia hoja badala ya kujibu hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya Nne ni Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Mapendekezo ya jumla ni kwamba baada ya kuchambua udhaifu uliopo katika kudhibiti matumizi mabaya ya Serikali Kamati inatoa maoni na mapendekezo kama ifuatavyo:-

(1) Kamati inasistiza kusudio la Serikali la kurudisha *TANSORT* nchini kutoka London, Uingereza katika mwaka wa fedha wa 2009/2010. Kamati inapendekeza jambo hili litekelezwe haraka ili kudhibiti mapato yatokanayo na almasi.

(2) Ili kuboresha utendaji na kurudisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria za Fedha na Sheria za Ununuzi kama miongozo ya kufanyia kazi, Wizara na Idara za Serikali zinazopata Hati Chafu, Maafisa Wahasibu husika wachukuliwe hatua zaidi ya kupewa tozo ikiwemo kushushwa Cheo kwa vile adhabu ya tozo haiwezi kufidia fedha zilizopotea.

(3) Serikali ifanye juhudi kupunguza matumizi ya kawaida (*Recurrent Expenditure*) katika bajeti ya nchi badala yake iongeze bajeti ya maendeleo ili kuimarisha utekelezaji wa miradi na kupunguza utegemezi kutoka kwa wafadhili. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007 Serikali ilitenga kiasi cha Sh. 1,099,977,174,403/= kwa ajili matumizi ya kawaida kwa Mikoa na kiasi cha Sh. 66,266,763,875/= tu ikiwa ni kwa ajili ya maendeleo kwa Mikoa hiyo ambayo ni 6% tu ya matumizi ya kawaida.

Katika nchi nyingine ambazo zinapata misaada fedha ya wafadhili na mikopo kutoka nchi za nje hazichanganywi katika bajeti ya nchi. Fedha zote kutoka nje

zinapelekwa kwenye miradi chini ya kamisheni ya mipango na maendeleo na zinaangaliwa kama miradi inayojitegemea.

Utaratibu huu utafanya bajeti ya maendeleo itekelezeka zaidi. Vitabu vinaonyesha kwamba fedha itokanayo na fedha za ndani inatekelezeka kwa zaidi ya asilimia 90 na ya maendeleo inatekelezeka kwa kiasi cha chini ya asilimia 54. Kwa mfano, katika bajeti Wizara ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2006/2007 fedha zilizotarajiwa kutoka nje ya nchi ilikuwa Sh. 119,430,658,460/=. Hata hivyo, fedha iliyotolewa ilikuwa Sh.10,760,085/= ambayo ni takribani 9% tu Wakati fedha za ndani zilizotarajiwa zilikuwa Sh. 165,129,190,452/= na zilizotolewa zilikuwa Sh.164,832,405,900/= ambayo ni 99.8%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwaka 2007/2008 fedha zilizotarajiwa kutoka nje zilikuwa ni Sh. 244,234,325,600/=. Kiasi kilichotolewa kilikuwa ni sh 23,636,100,000/= sawa na asilimia 9.7 wakati fedha kutoka ndani zilizoidhinishwa kwa matumizi ya maendeleo zilikuwa Sh. 233,984,530,000/= na fedha zilizotolewa kwa matumizi hayo ni Sh. 213,955,010,000/= sawa na asilimia 91.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu wa fedha kiasi cha fedha za maendeleo zilizoahidiwa kutoka nje ni Sh. 237,026,480,900/= wakati kiasi kilichotolewa mpaka kufikia tarehe 31 Machi, ni Sh. 1,644,659,024/= ikiwa ni 0.7%. Kwa upande wa fedha za ndani kwa miradi ya maendeleo, kiasi cha Sh. 356,150,302,000/= kiliidhinishwa na mpaka kufikia tarehe 31 Machi, 2009, kiasi cha Sh. 350,472,943,561/= kilikuwa kimekwishatolewa ikiwa ni asilimia 98.4 na kiasi cha Sh. 165,879,289.10 kilikwishatumika. Athari za hali hii zaidi katika Wizara hii ni miradi kutokukamilika kwa wakati na kuongezeka kwa gharama za uendeshaji (*overrun costs*) na madeni makubwa kutokana na hati (*certificates*) kuwa zimekwishaiva.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, makubaliano (*memorandum of understanding*) baina ya Serikali na wafadhili yajulikane na Bunge na wadau wote yakiwemo masharti yanayotolewa na wafadhili kwa Serikali katika makubaliano hayo. Misaada na mikopo ni sehemu ya bajeti ya Serikali; ni wajibu wa Bunge kuiidhinisha na kujua matumizi yake pamoja na masharti ya upatikanaji wake. Fedha ambayo inayotoka nje kuingia kwenye bajeti iwe ni mikataba isiyobadilika kwa kipindi chote cha mwaka unaohusika.

(4) Bunge na Kamati za Ukaguzi wachukue hatua kuhakikisha kuwa Maafisa Masuhuli wanatekeleza mapendekezo yanayotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwani pamoja na juhudi ya Mdhibiti na Mkaguzi kupitia Bunge lako Tukufu kutoa mapendekezo ya kusaidia Wizara na Idara za Serikali kuondoa hoja za ukaguzi kwa mwaka 2005/2006 bado hoja za Sh. 64,504,129,099/= zilikuwa hazijajibiwa. Kamati inakumbusha kuwa Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 (*The Public Audit Act, 2008*) inawataka Maafisa Masuhuli kutoa majibu ya mapendekezo

ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu, (*Treasury note*) hii haifanyiki.

(5) Mikataba ya aina zote ambayo inatekelezwa na fedha za Serikali isimamiwe kwa umakini kuanzia katika hatua za mwanzo hadi ukamilikaji wake ikiwa ni pamoja na ulazima wa kuzingatia matakwa kifungu 24 cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 kama ilivyorekebisha mwaka 2004. Nanukuu kifungu hicho: “ 24. *Where for the purposes of any development project which has been approved by the National Assembly by resolution or otherwise a contract for the supply of goods or services is entered into on behalf of the United Republic which provides that any payment (other than a payment charged on the Consolidated Fund by virtue of the provision of this or any other Article) is to be made on or after the first day of the making of such contract, give notice thereof to the National Assembly and every such notice shall specify:-*

*the names of the contracting parties:-*

*the nature of the goods or services to be supplied;*

*the total amount payable by the United Republic in respect of such goods or services and the date or dates on which payment is to be made; and*

*the development project to which such contract is referable.”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara na Idara za Serikali hazitekelezi kifungu hiki katika shughuli za mikataba ya ukandarasi. Kutozingatiwa kwa kifungu hiki cha Sheria kwa kiasi kikubwa kunavutia hasara na vitendo vya rushwa. Kamati inasisitiza kuwa Maafisa Masuhuli wote watekeleze majukumu yao kwa kuzingatia matakwa ya Sheria.

(6) Maafisa Masuhuli wapange matumizi kwa kuzingatia fedha walizonazo kwa mwaka wa bajeti husika kwa mujibu wa Kanuni ya 85 (3) ya Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake. Nanukuu kanuni hiyo: “*The expenditure properly chargeable to the account of a given year must, as far as possible, be met within that year, and must not be deferred for the purpose of avoiding an excess on the amount provided in the Estimates*”, mipango (*commitments*) yote ya Wizara na Idara za Serikali ipangwe kwa kuzingatia bajeti ya mwaka husika kwani kutofanya hivyo kunaifanya Serikali kuelemeza na madeni pamoja na riba inayotokana na madeni hayo na hivyo kusababisha hasara isiyo ya lazima.

(7) Serikali ipitie upya mfumo wa kubakiza fedha katika maeneo ya makusanyo (*Retention Schemes*). Serikali kupitia Hazina inatakiwa kuweka taratibu madhubuti za kudhibiti mfumo wa ubakizaji maduhuli katika vyanzo hivyo ili kuweza kuhakikisha mifumo iliyopo haikiuki Katiba ya nchi Ibara ya 135(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 (ilivyorekebisha mwaka 2003) inavyotaka. Nanukuu Ibara hiyo: “*Fedha zote zitakazotokana kwa njia mbalimbali kwa ajili ya matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, isipokuwa fedha za aina iliyotajwa katika*

*ibara ndogo ya (2) ya ibara hii, zitawekwa katika mfuko mmoja maalum ambao utaitwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kifungu 11 cha Sheria ya Fedha za Umma 2001, kinataka maduhuli yote ya umma yanayokusanywa yaingizwe katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hivyo kuruhusu ubakizaji wa maduhuli katika taasisi zilizoyakusanya ni kukiuka Katiba ya nchi na sheria za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali irekebishe vifungu vya Sheria vinavyokinzana. Kanuni ya 53 ya Kanuni za Fedha za 2001 inataka hesabu za Serikali kutayarishwa katika misingi ya fedha taslimu (*Cash Basis*) ili kiasi kinachotumika katika kila jambo kiweze kulinganishwa na kile kinachoidhinishwa na Bunge. Kwa upande mwingine, kifungu cha 25 cha Sheria ya Fedha za Umma Na. 6 ya 2001 (iliyorekebishwa mwaka 2004) inamtaka Mhasibu Mkuu wa Serikali na Maafisa Masuhuli wote kuandaa pamoja na taarifa nyingine, taarifa ya maduhuli yasiyokusanywa na matumizi yasiyolipwa na taarifa ya mali na madeni ambazo zinaonekana kuwa nje ya mfumo wa Uhasibu wa fedha taslimu (*Cash basis*). Matakwa ya kisheria katika vifungu hivi yanaonekana kukinzana na hivyo kuwa na uwezekano wa kuwachanganya Maafisa Masuhuli na Umma kwa jumla. Kamati inamshauri Waziri wa Fedha achambue vifungu vyote vya Sheria vinavyokinzana na kuandaa mapendekezo kwa Bunge kwa ajili ya marekebisho hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha usimamizi wa deni la Taifa, Serikali inatakiwa kuhakikisha kuwa wakati wote taarifa zote zinazotolewa kuhusu deni hilo ni sahihi.

Aidha, kuwe na mtandao wa kuwezesha pande zote zinazohusika na deni la Taifa yaani Benki Kuu, Hazina na Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kuwa na taarifa ya mwenendo wa deni la Taifa, hivyo utaratibu wa usimamizi wa deni la Taifa uboreshwe kwa kuanzisha vitengo mahsusi katika maeneo yaliyotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maafisa masuhuli wasishinikizwe na wanasiasa katika kupanga matumizi ya fedha bali watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa taratibu za fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya fedha za dharura yawekwe wazi na yasiachwe mikononi mwa Waziri wa Fedha peke yake kwani hali hii inatoa mianya ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007 pekee, kiasi cha Sh. 382, 582,641,807/= matumizi yake yaliidhinishwa na Waziri wa Fedha bila kupata kibali cha Bunge. Kiasi hiki ni kikubwa mno kuamuliwa na mtu mmoja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie utaratibu wa kudhibiti watumishi wanaotoroka vituo vyao vya kazi kuendelea kupokea mishahara kupitia Benki kwani kwa sasa mishahara yote watumishi wa Umma inapitia Benki na hivyo kuweza kuchukuliwa wakati wowote kupitia *ATM* bila kulazimika kutia saini mahali popote. Fedha zinazorudishwa Hazina baada ya mwaka wa fedha kwisha zijulikane na Bunge na wadau

mbalimbali na matumizi yake yajulikane, pia zionyeshwe kama kianzio cha bajeti ya mwaka unaofuata. Kwa mwaka 2006/2007 Wizara, Mikoa na Idara za Serikali zilibakiza kiasi cha Sh. 3,111,620,099/= ambazo hazikuonyeshwa kwenye bajeti ya mwaka uliofuata na Bunge hili halijapewa taarifa yoyote kuhusu fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zote zinazotolewa kama ahadi ya viongozi wa nchi kwa miradi mbalimbali nchini wakati wa ziara katika Mikoa mbalimbali ikiwemo shilingi bilioni moja zinazotolewa kwa kila Mkoa (maarufu kama fedha za JK) kwa ajili wa wajasiriamali wadogo wadogo zionekane katika vitabu vya fedha vya Maafisa Masuuli ambako fedha hizo hupokelewa pamoja na zinakotoka fedha hizo. Fedha hizi ni nyingi, zisipofuatiliwa zinaweza kutumika kinyume na ilivyokusudiwa. Kamati imegundua kuwa hakuna afisa masuuli (*accounting officer*) anayewajibika kwa fedha hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza mapato ya Serikali nchi yetu imekuwa ikitegemea misaada kutoka kwa wafadhili katika bajeti yake kwa miaka mingi sasa.

Hata hivyo, kwa mwelekeo wa kuyumba uchumi duniani hivi sasa kuna uwezekano mkubwa kuwa wafadhili wetu watapunguza au kuondoa kabisa misaada yao kwetu na hivyo kutuathiri kibajeti kwa kiasi kikubwa. Kwa hali hii, Kamati inasisitiza kuibua vyanzo vya ndani vya mapato (*domestic sources of revenue*) kama njia ya kugharamia bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kuanza kujitegemea katika matumizi ya kila siku ya kuendesha Serikali (*Recurrent Budgets*) bado kuna haja ya kujipanga upya ili kujiondoa katika utegemezi ambao unaweza kuisababishia nchi yetu matatizo makubwa. Kwa mantiki hiyo, Kamati imeamua kuweka mapendekezo ya kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ni tajiri sana tukijipanga vizuri tunaweza kujitegemea kibajeti kwa asilimia mia. Kamati inashauri Serikali ijipange vizuri katika maeneo mbalimbali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mapato ya Tanzania iendeele kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa kupanua wigo wa kodi. Vyanzo ambavyo bado kuangaliwa vizuri ni sekta za Madini, Misitu, Utalii na Uvuvi. Mamlaka ya Mapato Tanzania ibuni mkakati maalumu ya kukusanya mapato katika sekta hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inashauriwa kuimarisha makusanyo ya maduhuli yatokanayo na vyanzo vya ndani ili kupunguza utegemezi wa Wafadhili katika kugharamia bajeti. Ni imani ya Kamati kuwa kama Serikali itaweza kudhibiti uvujaji wa maduhuli pamoja na kudhibiti matumizi inaweza kugharamia kwa ujumla matumizi yake bila kutegemea ufadhili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itumie kikamilifu faida za kijiografia (*geographical advantages*) zilizopo katika nchi yetu. Kijiografia nchi yetu ina bandari ambazo zinategemewa na nchi sita (Rwanda, Uganda, Burundi, DRC, Zambia na

Malawi) ikiwa ni pamoja na bandari zilizoko katika ziwa Viktoria, Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa. Tukiimarisha bandari zetu, tukiboresha reli zetu, tukiondoa urasimu katika utendaji wa kazi zetu bandari hizi zinatoshwa kuifanya nchi yetu ijitegemee kibajeti. Aidha, mbali na bahari ya Hindi, *Ziwa Viktoria*, Ziwa Nyasa, Ziwa Tanganyika Tanzania ina mito mingi mikubwa maeneo yote haya yamejaa samaki ambao tunaweza kuwatumia kupata fedha za kutosha. Tukijipanga vizuri katika uvuvi wa kisasa na kulinda mapato yanayotokana na samaki nchi yetu inaweza kujitegemea kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni kuna meli ya wavuvi haramu iliyokamatwa ikiwa na samaki wenye uzito wa jumla ya zaidi ya tani 200 waliovuliwa ndani ya mpaka wetu. Yawezekani kuna meli nyingi zinazofanya hivyo kila siku na rasilimali hiyo inatajirisha nchi nyingine wakati Watanzania wakiendelea kuwa maskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina madini ya kila aina, karibu katika kila Wilaya kuna madini ya aina moja au nyingine. Madini haya ambayo kwa sasa mengine yanachimbwa kiholela na mengi yananufaisha mataifa ya nje; yakitumiwa vizuri kwa kuwa na mipango na sera nzuri pia yanatosha kuiwezesha nchi yetu kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina visima vya Gesi ya asili ambayo ni nyingi sana katika maeneo ya Songosongo na Mnazi *Bay* na maeneo mengine ambako utafiti unaendelea. Gesi hii inafaa kwa kuzalishia umeme, kuendeshea mitambo, magari, matumizi ya nyumbani na kadhalika. Tukiitumia gesi hii kwa umakini inatosha kuinua uchumi wetu na kuondoa utegemezi wa bajeti kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina vivutio vya utalii vingi sana, vivutio hivi ni pamoja na mbuga za wanyama, milima, tamaduni na historia. Zipo nchi duniani zenye vivutio vichache sana lakini uchumi wao unategemea utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina ardhi kubwa sana ina mito mingi na mabonde mengi yanayofaa kwa kilimo cha kutegemea mvua na kilimo cha umwagiliaji ikiwemo bonde la Mto Rufiji, Mto Kilombero, Mto Ruaha, Mto Malagarasi, Mto Pangani, Mto Mara na mingine mingi. Nchi ya Misri ni jangwa, lakini kwa kuwa na mto mmoja tu, *Mto Nile*, nchi hiyo inazalisha na kuuza ziada ya chakula nje ya nchi. Hapa pia tukijipanga vizuri kilimo kinaweza kuifanya nchi yetu ijitegemee kibajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wataalam wa ndani watumike iapasavyo. Vyuho Kikuu vya Dar es Salaam na Sokoine vimekuwa vikizalisha Wahandisi wa kila aina na wataalamu wa fani mbalimbali za kilimo kwa zaidi ya miaka ishirini iliyopita. Kwa sasa tunavyo Vyuho Vikuu na Vyuho Vikuu Vishiriki zaidi ya 25 vinavyozalisha wataalamu wa kila aina. Tukiwatumia wataalamu hawa na kuwawezesha wataiondoa nchi yetu katika dimbwi la umaskini tulionao sasa.

Hatua ya Serikali kuthamini zaidi wataalam wa nje sio tu kunaathiri uchumi wa nchi, bali kunaashiria kuwa Serikali inaamini kuwa elimu itolewayo nchini iko chini ya kiwango.



Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati katika majadiliano yake na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi imebaini kwamba kuna fedha nyingi za Serikali zinazotumika kwa ajili ya matibabu ya nje na pia kwa upande wa wataalamu Serikali haijawekeza vya kutosha (*investment in human resources development*) hususan kwa Madaktari na Wauguzi, ingawa Kamati imebaini kuwa kuna upendeleo wa mikopo kwa Madaktari. Kwa maoni ya Kamati, upendeleo huu hautoshi na wataalamu hawa wangepewa ruzuku badala ya mikopo ili kuhamasisha vijana wengi zaidi kujiunga na taaluma hii na hatimaye kupunguza kiasi cha pesa kinachotumika kupeleka wagonjwa nje ya nchi kwa matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwe na hisa katika kila mradi hapa nchini hasa katika madini, gesi, mahoteli na mabenki. Serikali ya Malawi, kwa mfano, inamiliki hisa katika mahoteli yote ya kitalii pamoja na vitega uchumi vingine vikubwa. Kamati inaishauri Serikali iangalie upya mtazamo wa Serikali kujitoa katika kuendesha shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihimiza uzalishaji, hivyo uchumi wa nchi utakua kwa kasi kutokana na wananchi kuhimizwa kuzalisha mali na siyo kufanya biashara za bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi kama ilivyo sasa ambapo maduka na *supermarkets* nchini zimejaa bidhaa za nje. Aidha, msisitizo uwekwe kwa wazalishaji wadogo wadogo na siyo wafanyabiashara wadogo wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inashauriwa kuimarisha udhibiti katika ukusanyaji wa maduhuli yanayotokana na stika za Viza katika Balozi zetu. Kumekuwa na utaratibu wa watu binafsi katika nchi mbalimbali kukusanya mapato ya Viza kwa niaba ya Balozi zetu. Hata hivyo, hakuna udhibiti wa kutosha kuhakikisha kuwa mapato hayo yanaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa mfano, baadhi ya mawakala wa Balozi zetu wanachukua 60% ya mauzo ya Viza, wengine 30% na wengine wanachukua stika za viza moja kwa moja toka kwa watengenezaji bila kupitia hazina na hivyo kusababisha upotevu wa mapato ya Serikali. Huku ni kukosa umakini kwa watendaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha, ni vyema mauzo ya viza yakawa chini ya Wizara moja badala ya hali ya sasa ambapo Idara ya Uhamiaji (Wizara ya Mambo ya Ndani) na Balozi (Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa) zote zinatoa Viza na zinabakiza mapato hayo kwa matumizi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa vitambulisho vya uraia uharakishwe kwani vitambulisho hivi mbali na kusaidia kuimarisha usalama wa nchi vitasaidia kutambua walipakodi. Nchini Kenya, kwa mfano, kila raia ana kitambulisho na hivyo hurahishisha ukusanyaji wa mapato ya ndani ya kutosha kujitegemea kibajeti. Aidha, matumizi ya namba ya mlipakodi (*TIN*) kukusanya kodi yazingatiwe kwa makini zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubana matumizi ya fedha za Serikali; Kamati inarejea agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutoa maelekezo kwa watendaji wa Serikali kubana matumizi kwa kutofanya Semina zisizo za

lazima na kupunguza ununuzi wa magari ya kifahari. Matumaini ya Kamati ni kwamba huu ndio mwelekeo mpya unaolenga kufikia kujitegemea kwa bajeti ya maendeleo ambayo sasa hivi ni tegemezi sugu. Utegemezi wa nchi yetu kwa wafadhili katika kugharamia bajeti yetu umeonekana kuwa mwelekeo uliojikita katika uchumi wetu. Hata hivyo, jitihada za kupunguza utegemezi huo hazikuweza kuonekana wakati wa ukaguzi. Japokuwa makusanyo ya maduhuli yameonekana kuongezeka toka Shilingi trilioni 2.9 katika mwaka wa fedha 2004/2005 hadi shilingi trilioni 4.2 mwaka wa fedha 2006/2007 kwa mujibu wa taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Mchango wa ongezeko hilo kwa bajeti umekuwa mdogo sana. Baadhi ya sababu zinazoendeleza utegemezi wa bajeti ya Serikali ni hizi zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu imebainisha kuwa kuna matumizi mabaya ya fedha katika ununuzi wa samani za maofisa wanaostahili kutumia samani za Serikali. Mbali na ukweli kuwa samani nyingi zinanunuliwa nje ya nchi na hivyo kutumia fedha nyingi za kigeni na kukuza masoko ya nje, samani hizi ni hafifu na hazidumu na pia zinanunuliwa kutokana na matakwa ya mtumiaji na siyo kufuata viwango vilivyopangwa kwa ngazi za watumishi husika. Kamati inashauri Samani zote za Serikali zinunuliwe ndani ya nchi na watumishi wa Serikali wapewe aina ya samani wanazostahili na siyo wanazotaka wao. Ushauri huu ukizingatiwa utahamasisha viwanda vya samani nchini pamoja na kukuza ajira na matumizi mazuri ya rasilimali zetu za misitu.

Aidha, Jeshi la Magereza na Jeshi la Kujenga Taifa wana utaalum wa kutosha wa kutengeneza samani. Ni vyema Serikali ikaimarisha majeshi haya ili kuwawezesha kutengeneza samani za kutosha kwa matumizi ya Ofisi na nyumba za Serikali ikizingatiwa kuwa nchi ina mbao za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamana ya mikopo ni eneo lingine la matumizi makubwa ya Serikali, na mara nyingine bila tija. Kwa mfano, kwa mwaka 2006/2007 Serikali ilitoa dhamana ya jumla ya Sh. 202,547,947,047/= kwa mashirika tisa ikiwemo Shirika la *SUKITA* lililodhaminiwa kwa Sh.10,139,494,512/=. Kamati inaamini kuwa *SUKITA* haifanyi biashara tena, katika hali hii Serikali inajitokea katika hatari ya kuingia kwenye gharama kubwa ya madeni kutokana na udhamini wa aina hii na hivyo kuongeza mzigo usio wa lazima kwa walipa kodi. Serikali ifanye tathmini ya kutosha kabla ya kutoa dhamana ya mikopo kwa mashirika mbalimbali ili kupima uwezo wa mashirika hayo kukopesheka.

Misamaha ya kodi ni eneo lingine linaloikosha Serikali mapato na kuimarisha utegemezi. Kwa mwaka 2006/2007 Serikali ilikosa mapato ya jumla ya Sh. 791,407,467,938/= sawa na asilimia 30 ya mapato yaliyotarajiwa kutokana na misamaha ya kodi. Kamati inashauri misamaha ya kodi inayotolewa na Sheria mbalimbali iangaliwe upya ili kupunguza hasara kwenye mapato ya Serikali. Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) inafanya juhudi kukusanya kodi ambayo ndiyo chanzo kikubwa cha mapato ya Serikali. Hata hivyo, juhudi hizi zinarudishwa nyuma na misamaha ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutofuata sheria na kanuni za manunuzi ni udhaifu mwingine unaoleta matumizi makubwa ya Serikali kuu. Aidha, Mkaguzi na Mdhhibiti

Mkuu wa hesabu za Serikali ametoa taarifa kuwa ununuzi wa vifaa, huduma na kandarasi ukizingatia kiasi cha fedha kinachotumika katika matumizi ya Serikali na kufuatana na matokeo ya kutozingatiwa kwa sheria ya ununuzi ambao ukaguzi umebainisha, ni dhahiri kuwa Wizara na Idara za Serikali hazijafikia kiwango kizuri cha usimamizi wa ununuzi. Tafsiri ya kutokusimamia vizuri sheria ya ununuzi inaweka mazingira ya kuleta hasara, matumizi mabaya ya fedha, utendaji mbaya wa makandarasi na rushwa. Kamati inapendekeza kuwa sheria ya rushwa na mapendekezo ya CAG katika eneo hili yazingatiwe kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ziara zilizofanywa, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Serikali kujenga mradi mkubwa wa maji wa Ziwa Victoria– Shinyanga - Kahama. Mradi huu ni kielelezo kuwa tukidhamiria kujikwamua kutoka katika umaskini tunaweza, kwani mradi huu umetumia zaidi ya shilingi bilioni 270 ikiwa ni mapato ya ndani ya nchi. Juhudi ziendeele kufanyika ili kuhakikisha kuwa maji hayo yanainufaisha jamii ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iwasimamie vizuri wahandisi wakazi katika ujenzi wa barabara ili kuondoa mvutano kati ya Mkandarasi na Serikali, hali ambayo inaigharimu sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilifurahishwa na mradi wa Gesi ya *Mnazibay* na kwa Serikali kuwa na hisa katika mradi huu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa Serikali imepata hisa hizi kupitia *TPDC* bila kuwekeza fedha yeyote. Jambo hili linaipunguzia sauti Serikali katika mradi huu.

Aidha, Kamati inashauri Serikali ifanye juhudi kuhakikisha kuwa mradi huu unainufaisha nchi yetu kwani kuna hazina kubwa ya gesi katika eneo hilo. Serikali ielezee hali ya sasa ya mradi huu baada ya msukosuko wa uchumi duniani na vurugu la uongozi ndani ya kampuni ya *Artumas*. Kamati inasikitishwa na ucheleweshaji wa miradi ya mabwawa ya maji ya Bariadi na Manchira kwani mradi wa bwawa la Bariadi ulianza mwaka 1988 na Manchira ulianza mwaka 1977 lakini hadi Kamati ilipotembelea tarehe 2-4 June, 2008 miradi yote ilikuwa haijakamilika na kumbukumbu nyingine kupotea kabisa. Uanzishwaji wa miradi ya aina hii unaisababishia hasara Serikali. Hata hivyo, Serikali iliahidi kuwa Mradi wa Bwawa la Manchira ungekamilika Mwezi Oktoba, 2008. Katika kikao cha Kamati tarehe 21 Aprili, 2009 Kamati ilielezwa kuwa ujenzi wa bwawa hilo umeshakamilika kilichobaki ni miundombinu ya kusambaza maji hayo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iongeze juhudi ya kukusanya fedha zinazotokana na mbuga za wanyama kutokana pia na thamani ya ardhi inayotumika kwa uhifadhi. Asilimia 94% ya Wilaya ya Serengeti ni hifadhi ya wanyama na 6% tu ya Wilaya hiyo inatumiwa na wananchi. Iwapo eneo lote hilo limetengwa kwa ajili ya uhifadhi, basi mapato yake yafanane na ukubwa wa eneo hilo ambalo iwapo lingetumika

vinginevyo yamkini lingeleta tija kubwa zaidi. Aidha, Watanzania wapewe fursa zaidi katika kumiliki na kuendesha shughuli za kitalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ihakikishe kuwa wawekezaji katika nchi yetu hawaonyeshi ubaguzi wa aina yoyote kwa Watanzania, kwani katika ziara ya Kamati katika mbuga ya Serengeti kulikuwa na malalamiko ya kuwepo kwa ubaguzi katika ajira na maeneo mengine hususan katika Hoteli inayomilikiwa na mwekezaji wa *Grumeti*. Mapato yanayotokana na mbuga za wanyama, kwa mfano mapato ya hoteli za kitalii, yagawiwe kwa wadau mbalimbali ikiwemo Halmashauri zinazozunguka mbuga hizo kwa mujibu wa sheria na sio kwa matamko ya viongozi wa Serikali kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isimilikishe ardhi kwa wageni kinyume na sheria ya Ardhi ya mwaka 1998. Nanukuu; *“19 (2) a person or a group of persons whether formed into a corporate body under the Companies Ordinance or otherwise who is or are non-citizens, including a corporate body the majority of whose shareholders or owners are non-citizens may only obtain a right of occupancy or derivative right for purpose of investment prescribed under the Tanzania Investment Act, 1997”*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmiliki wa Hoteli ya Grumeti iliyoko katika Pori la Akiba la Grumeti siyo Mtanzania, lakini amemilikishwa ardhi kwa miaka 99. Kamati inaona kwamba sheria ya mgeni kutokumiliki ardhi inayang’anywa nguvu na sheria ya uwekezaji ya 1999 na iko haja ya kutazamwa upya sheria hizi ili kuondosha mgongano huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tafsiri ya Kampuni ya ndani (*local company*) na kampuni ya nje (*foreign company*) iangaliwe upya ili Kampuni ya ndani ijulikane, hivyo siyo kwa vile imesajiliwa ndani ya nchi, bali wamiliki wake wawe ni Watanzania au idadi kubwa ya wanahisa wake ni Watanzania na Kampuni ya nje maana yake iwe kwamba wamiliki au wanahisa wake wawe siyo Watanzania badala ya hali ya sasa ambapo tafsiri yake inahusu mahali iliposajiliwa bila kujali uraia wa wamiliki wa kampuni husika. Udhaifu huu wa sheria unatumiwa sana na wageni kuchukua maeneo makubwa ya ardhi ya migodi ya madini na mbuga za wanyama na wanatumia ardhi kama dhamana ya kukopa mtaji nchini na nje badala ya kuleta mtaji kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri juu ya baadhi ya mafungu, Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44) Kamati yangu ilikutana na afisa masuhuli wa Wizara ya Viwanda na Biashara tarehe 17 Machi, 2009 mjini Dar es Salaam.

Katika kikao hicho Kamati ilipitia na kujadili taarifa ya CAG kuhusu Wizara hii na baadaye kupata wasaa wa kujadiliana na Afisa Masuhuli kuhusu hoja za ukaguzi na mipango ya Wizara. Kilikuwa ni kikao kizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya hoja zilizojadiliwa ilikuwa ni suala la makusanyo ya Halmashauri na gharama za ufuatiliaji. Hoja hii ilikuwa ni agizo la Kamati kutaka kujua matokeo ya uchunguzi unaofanywa wa fedha zilizokusanywa na Halmashauri. Katika majibu yake, Afisa Masuhuli aliiambia Kamati kuwa wilaya

zilikwa zinashawishika kukusanya ada za leseni kutokana na ada hizo zilizokuwa zinatolewa na Wizara kuwa kubwa. Sababu hii imebadilika kutokana na mabadiliko katika ada za leseni mwaka 2004/2005 ambapo leseni za chini ya kiwango cha mauzo ya milioni 20 zinatozwa Sh. 20,000/= tu. Aidha, kufutwa kwa kwa sheria Na. 25 ya leseni ya mwaka 1972 na badala yake biashara kuandikishwa bila ada kwa zile zisizohitaji udhibiti kama mabenki, hospitali na kadhalika kutolewa na mamlaka husika. Hoja ya Wilaya kukusanya mapato bila kuzingatia utaratibu haitakuwepo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia maoni ya Mkaguzi, Kamati imekubali kuwa maelezo ya Wizara ni sawa. Uchambuzi wa kina umeonesha hakuna “*value for money*” kukagua Wilaya ukilinganisha na fedha zilizokusanywa na ambazo zimeshatumika kwa shughuli za maendeleo na nyingine kuingia *TRA* kwani baadhi ya malipo yalilipwa kupitia *TRA*. Kwa mfano, Arusha na Tanga walikusanya Sh. 2,800,000/= na Sh. 4,900,000/= sawia. Gharama za kwenda kukagua Arusha ni takribani Sh. 10,400,000/= na Tanga ni Sh. 10,250,000/= bado fedha hizo sio rahisi kuzipata. Kwa kuzingatia hili, Kamati ilitoa maelekezo kuwa makusanyo hayo yaachwe kwenye ngazi ya Wilaya, kama hatua za kushusha mamlaka ya maendeleo katika ngazi za chini (*Decentralisation by Devolution*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa maendeleo ya viwanda katika nchi yetu bado yako nyuma ikilinganishwa na nchi nyingi duniani, Kamati iliona umuhimu wa kujua mipango ya Wizara katika kuikwamua nchi katika eneo hili. Afisa masuuli alitoa maelezo mazuri kuhusu mipango yake ya kuinua sekta hii na Kamati inamtakia kila la kheri. Kama sehemu ya utekelezaji wa azma hii, Kamati ilielezwa kuwa mikakati madhubuti imeandaliwa kuendeleza Sekta ya Viwanda. Tayari Wizara iliandaa utaratibu wa kukusanya taarifa kuhusu maendeleo ya viwanda nchini na kufanya “*industrial survey*” katika Mikoa 21 ya Tanzania Bara ambao ilikamilika mwezi Aprili, 2007 kama hatua za awali.

Hivi sasa Serikali inayo mamlaka ya *EPZ* kusimamia uendelezaji wa *EPZ* kama mkakati wa kuvutia sekta binafsi. Kamati ilielezwa kuwa Mradi wa *SEZ* ambao pia sasa uko chini ya Wizara ya Viwanda na biashara uko tayari kwa matumizi na tayari wamejitokeza wawekezaji kadhaa katika mradi huu. Kamati inapongeza sana juhudi hizi. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kwa ujumla kuchukua juhudi za makusudi kuinua Sekta ya uzalishaji mdogo mdogo na wa kati. Hii itasaidia sana kuinua hali ya uchumi wa nchi kwa kuongeza uzalishaji na ajira na kukuza wazalishaji wa ndani ambao pia ni sehemu ya uwekezaji wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa katika taarifa ya ukaguzi kuwa Wizara inaendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera ya Viwanda vidogo na biashara ndogo. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara ilipanga kuanzisha programu ya kuendeleza viwanda vidogo vijijini kwa kuanzia na Mikoa sita ambayo ni Pwani, Tanga, Manyara, Mwanza, Iringa na Ruvuma kama mkakati mwingine wa kuendeleza sekta binafsi. Gharama ya programu ilitegemewa kuwa shilingi billioni 25 ambazo ni mkopo toka *IFAD*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na mtazamo hasi kuhusu bidhaa za ndani ya nchi ukilinganisha na zile za nje ya nchi. Kama ilivyozungumzwa awali, huu mtazamo kwa Serikali umekuwa chanzo kikubwa cha kuiongezea Serikali gharama zisizo za lazima. Mfano mzuri ni wa samani, ambapo tayari umezungumziwa kwenye aya za awali. Kamati inaona kuna umuhimu mkubwa wa kubadili fikra zetu (*mindset*) kuhusu bidhaa toka nje. Uwezo tunao wa kutengeneza bidhaa zenye ubora. Ni kubadili mtazamo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na tatizo sugu la uingizaji wa bidhaa zisizo na ubora wa kutosha katika nchi yetu. Hivi karibuni tumeshuhudia habari za kuharibiwa bidhaa nyingi toka nje kwa kutokidhi ubora ama kutofuata taratibu za ushindani. Kamati ilichukua fursa ya kukutana na Afisa masuhuli kuisisitiza umuhimu wa kuimarisha taasisi zetu zinazosimamia ubora na ushindani ili kuhakikisha kuwa tatizo la ubora na wizi wa haki za kibiashara unakoma ama kupungua kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, Kamati ilielekeza shirika la viwango nchini kubadili mtazamo katika kupima ubora wa bidhaa zinazolingia nchini. Kamati inatambua kuwa sio rahisi kwa kila bidhaa kupimwa ubora wake na badala yake, sampuli huchukuliwa kuwakilisha bidhaa zote za aina husika.

Kamati imesisitiza kuwa uchukuaji wa sampuli hizi uwe makini vya kutosha kupata uwakilishi sahihi wa bidhaa bila kutabirika. Pia Kamati, ilisisitiza kuwa, kipaumbele kisiwe ada zitolewazo kama gharama za kupatiwa cheti cha ubora, bali ubora halisi wa bidhaa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango nchini (*TBS*) ni shirika la umma lililo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko. Shirika hili lina mamlaka ya kisheria ya kukagua ubora wa bidhaa zote zinazozalishwa hapa nchini na zile zinazolingizwa nchini toka nchi za nje na hivyo kuhakikisha kuwa nchi yetu haigeuzwi jalala la bidhaa duni. Katika kutekeleza jukumu lake la kulinda soko la Tanzania lisiwe jalala, shirika limekuwa likihakiki ubora wa bidhaa zinazolingia kutoka nje ya nchi, yakiwemo magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Watanzania wengi na makampuni wamekuwa wakiingiza nchini magari yaliyotumika, ilibidi kiandaliwe viwango vya lazima vya kukagua magari ili kuhakikisha magari yaingiayo nchini ni mazima na salama. Viwango hivi vilianza kutumika rasmi mwaka 2002. Katika kutekeleza hili, *TBS* iliidhinisha makampuni kadhaa ili yafanye kazi ya ukaguzi wa magari hayo kabla ya kusafirishwa kuja nchini (*pre-shipment inspection*). Itakumbukwa kwamba utaratibu wa kukagua bidhaa kabla ya kusafirishwa uliwahi kutumika na kusitishwa baada ya kubainika kuwa, ilikuwa ni moja ya vyanzo vya kutumia fedha nyingi za kigeni, ambazo tunazihitaji sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku Kamati yangu ilipokutana na Afisa Masuhuli wa Wizara ya Viwanda na Biashara, hoja ya ukaguzi wa magari na mapato yatokanayo na ukaguzi huu iliwagusa sana Wajumbe. Suala kuu ambalo Wajumbe wa Kamati

wanajiuliza ni kwamba, kwa kuwa kuna magari mengi sana ambayo yanaingia toka Japan, Dubai, Hong Kong na kwingineko (wastani wa takriban magari elfu 80 kwa mwaka) na magari haya hulipiwa gharama za ukaguzi takribani dola za kimarekani 150 kwa kila gari, hii inamaanisha kuwa kwa ada za magari pekee kwa mwaka Tanzania hupoteza sio chini ya dola za Marekani 12,000,000 (sawa na shilingi za Kitanzania 15,600,000,000/=). Ni dhahiri kuwa ukaguzi wa magari ingekuwa ungefanyika nchini kingekuwa ni chanzo kizuri cha mapato. Tangu utaratibu huu ulipoanza, Tanzania imepoteza takribani dola za Marekani milioni 48 kwa wastani wa magari uliotajwa awali ambao ni sawa na shilingi za kitanzania billion 62.4 ambayo ni zaidi ya bajeti ya ujenzi wa barabara ya Mbwemkuru- Mingoyo ya shilingi bilioni 51.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kamati ni kutaka kujua nchi yetu inavyonufaika na ukaguzi wa aina hii. Taarifa ya *TBS* inaonyesha kuwa kwa kipindi cha mwaka 2002 hadi 2007 shirika limeweza kukusanya jumla ya dola za kimarekani 584,779.11 (Shilingi 672,341,550.28) ikiwa ni ada ambayo inatozwa kwa kila gari. Kamati inaona hiki ni kiasi kidogo sana ikilinganishwa na gharama ya bilioni 48 inayolipwa na Tanzania kupata mapato tajwa ya Sh. 672,341,550.28. Kamati inaamini kuwa kiasi kikubwa cha fedha za kigeni kinapotea na kunufaisha mawakala walipo nchi za nje na sio ajabu kuna rushwa na ufiisadi ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo tetesi kuwa waagizaji hulipia tu gharama za ukaguzi ili kupata cheti bila kupitia ukaguzi wenyewe. Tetesi hizi zina mantiki ukiangalia mazingira halisi ya nchi magari haya yanakotoka. Ukichukua Japan kama mfano, sio rahisi kwa kampuni iliyoteuliwa kufanya ukaguzi kusafiri kwenda kuiona hiyo gari kutokana na msongamano mkubwa wa magari. Ni rahisi zaidi kulipia tu ada inayotakiwa, yaani Dola za Marekani 150 ili kupata kiambatanisho cha kutoa mzungu bandarini. Katika majadiliano wakati wa Kikao, Ushahidi uliotolewa haukuweza kufuta ukweli kwamba *TBS Certificate* inatolewa kwa kununua tu na si kwa kukagua magari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama ya shilingi bilioni 48 iliyolipwa na Tanzania ilikuwa ni makusanyo tu ya wakala wa *TBS* ambayo ni sawa na kupeleka fedha za kigeni nje bila tija (*nugatory expatriation of foreign currency*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kama tulivyosema mwanzo, utaratibu wa kukagua kabla bidhaa haijaingia nchini, ulishajaribiwa kwa miaka mingi nchini Tanzania. Makampuni ambayo yamekuwa na historia ndefu ni kama vile *SGS* na *COTECNA*. Kwa sababu Tanzania ilikuwa inapoteza fedha nyingi sana za kigeni, takribani asilimia moja ya thamani (*F.O.B. Price*) ya bidhaa zote zinazoingizwa nchini, makampuni haya yalikuwa yanakagua ubora na bei na nyaraka zilizokuwa zinatolewa na makampuni haya (*clean certificates*) zilikuwa zinatumika kama mojawapo ya nyaraka za kutolea mzungu bandarini na kulipa malipo ya nje kwa njia ya *L/C (Letter of Credit)*. Utaratibu mbadala ambao Serikali iliweka ni ukaguzi wa bidhaa bandarini (*port of destination*) na ndio maana kuna kitengo cha *TSCAN* bandarini. Katika mazingira haya ambayo yanaingizia nchi yetu hasara kubwa ya fedha za kigeni, takribani bilioni 62.4 kwa magari tu tangu utaratibu huu ulipoanza, Kamati inashauri jambo hili la kukagua magari nje lisitishwe mara moja.

Magari yote yakaguliwe baada ya kutoka bandarini. Maana ya utaratibu huu ni kwamba, anayeleta gari atalipia ushuru wa gari yake kama itakavyoamuliwa na *TRA* na baada ya kutoa gari hilo bandarini, gari hilo lisipate usajili mpaka limekaguliwa na *TBS* na limefikia kiwango kilichowekwa. Utaratibu huu hautaleta msongamano wowote bandarini na pili utahakikisha kuwa kila gari linaloingia barabarani limekaguliwa na *TBS*. Kwa upande wa mapato, kwa *TBS* na Serikali, ada maalum inaweza kuwekwa kwa kila gari linalokaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama fedha zote tulizoacha Dubai, Japan, Hong Kong na kwingine zingekusanywa nchini kama gharama ya ukaguzi na zikaingia katika mfuko wa Serikali, Kamati hii isingekuwa na hoja. Kwa wakati huu ambapo nchi yetu inatafuta kila kona fedha za kigeni, inaombaomba kila nchi, ni aibu kuona kuna utaratibu wa kufuja fedha za kigeni kwa kiasi cha bilioni 62.4 kwa utaratibu wa ukaguzi usiokuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujadili ukaguzi wa bidhaa nyingine, Kamati ilielezwa na Mkurugenzi wa *TBS* kwamba kuna utaratibu sasa wa kukagua bidhaa zote zinazolingia nchini kabla hazijaingia Tanzania (*pre-shipment inspection*) na kuna makampuni yaliyoandaliwa katika nchi mbalimbali kutekeleza utaratibu huu. Tumeeleza awali kuwa Serikali ilishasitisha utaratibu wa *pre-shipment inspection* kwa sababu ulikuwa unapoteza fedha nyingi za kigeni. Gharama ya ukaguzi kama tulivyosema awali, ni asilimia moja ya bei (*FOB value*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *TBS* kurudisha utaratibu wa *pre-shipment* ni kurejea kwenye madhara ya kifedha tuliyokwisha yaepuka kwa kuondoa *pre-shipment inspection*. Ni dhahiri kuwa hii ni njia nyingine ya kutorosha fedha za kigeni kutoka nchini bila tija. Kama tulivyoeleza awali, Tanzania ilikuwa inalipa 1% kwa ajili ya *pre-shipment inspection*. Kwa mfano, kwa mwaka 2007, bidhaa zenye thamani ya dola za Marekani milioni 4,826.9 ziliingizwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, 1% ya gharama za ukaguzi kwa mwaka huo peke yake ingekuwa ni Dola za Marekani milioni 48.299 sawa na Sh. 65,203,650,000/= ambazo nchi yetu ingepoteza kwa ajili ya ukaguzi kufanyika nje ya nchi. Kwa eneo hili Kamati inashauri *TBS* ikague bidhaa zote zinazolingia nchini baada ya kulipiwa kodi na kutolewa bandarini.

Bidhaa zikishaondolewa bandarini, zipelekwe kwenye vituo maalum zikisindikizwa na *TBS*, Tume ya Ushindani wa Biashara na Polisi ambako zitafanyiwa ukaguzi wa ubora. Iwapo hazitakuwa na ubora zitateketezwa kwa gharama za mwagizaji na pia atashitakiwa kwa mujibu wa sheria. Bidhaa zikiwa na ubora, mwagizaji atapewa cheti cha ubora toka *TBS* ambacho atalipia. Iwapo bidhaa hafifu ama bandia zikikutwa madukani, muuzaji na *TBS* na Tume ya Ushindani watawajibishwa.



Mheshimiwa Mwenyekiti, faida za utaratibu huu kwanza ni kuzuia utoroshaji wa fedha za kigeni, takribani bilioni 65 kila mwaka. Pili, kuhakikisha kwamba kweli ukaguzi halisi (*thorough inspection*) unafanyika na tatu, kwa kuwa ukaguzi unafanyika baada ya bidhaa kuondoka bandarini, hapatakuwa na msongamano wa bidhaa bandarini kwa kusubiri ukaguzi. Kama tulivyosema kwenye magari, *TBS* ikikubaliwa kuendelea na utaratibu iliobuni, Tanzania itapoteza takriban shilingi bilioni 65 kila mwaka na *TBS* itakuwa kitengo cha utoroshaji wa fedha za kigeni badala ya kuwa kitengo cha viwango. Ni dhahiri kuwa haiwezekani kwa mazingira halisi kuwa wakaguzi watakagua ubora wa bidhaa za aina zote zinazoingia nchini kwani ni nyingi mno na zinatoka katika kila pembe ya Dunia. Kwa hiyo, utekelezaji wake utakuwa kama kwa magari ambapo waingizaji mali watanunua tu cheti cha *TBS* ili iwe nyaraka ya kutumika kuondosha bidhaa zao bandarini na kwa gharama ya shilingi bilioni 65 kila mwaka itatumika tu kuhalalisha bidhaa hafifu na kujenga mazingira ya rushwa na ufisadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu pia imeiagiza *Brella*, kupitia Wizara kuwa ihakikishe biashara zote zinazostahili kuandikishwa, zinafanya hivyo. Hii itaongeza makusanyo ya Serikali na pia mipango ya Wizara katika kuendeleza sekta mbalimbali za biashara na masoko nchini. Pia Kamati imeagiza kutanuliwa kwa shughuli za *SIDO* hadi vijijini ili kuinua uzalishaji mdogo mdogo maeneo yote yenye rasimali za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii inahusika na masoko pia, kuna umuhimu wa kufanyika kwa juhudi za makusudi kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje ili kuweza kupata masoko kwa wakulima na wazalishaji wetu na pia kuvutia wawekezaji wa kigeni nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ubora wa mafuta yanayoingia nchini, Kamati ilihakikishiwa na Shirika la Viwango nchini kuwa mafuta yote yanayoingia nchini ni safi na salama. Tatizo la uchanganyaji wa mafuta linafanyika ndani ya nchi.

Hata hivyo, mara kwa mara *TBS* imekuwa ikichukua sampuli kutoka kwenye vituo mbalimbali na kupima ubora wa mafuta hayo ili kubaini ubora wake. Katika zoezi hili, *TBS* hushirikiana na *EWURA* pindi inapopata shaka kuhusu ubora wa mafuta katika kituo cha mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulingana na taarifa ya *TBS* ambayo imetolewa kwa Kamati, zinaonesha kuwa katika uchunguzi uliofanywa na *TBS* mwezi Aprili, 2007 ambao ulihusisha jumla ya vituo vya mafuta 29 ambapo sampuli 31 zilichukuliwa na kupimwa, matokeo yalionesha kuwa sampuli 17 ambazo ni sawa na asilimia 54.8 inawezekana zilikuwa zimechanganya na mafuta ya taa. Hii inaonyesha kuwa tatizo hili bado lipo ingawa linaonekana linapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka *TBS* iendelee na ukaguzi wa kushitukiza na adhabu kali zichukuliwe si kwa kituo tu, bali kampuni nzima itakayobainika kuwa na tabia hii ya kutokuwa waaminifu na kuharibu magari ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) chini ya Fungu 50 mnamo tarehe 15 Aprili, 2009, Kamati ya Hesabu za Serikali ilikutana na Katibu Mkuu Hazina kama Afisa Masuhuli wa Mamlaka ya Mapato nchini (*TRA*). Kiujumla Kamati iliagiza kutekelezwa na kufungwa kwa hoja zote ambazo bado hazijafungwa zilizomo kwenye ripoti ya mkaguzi na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Fungu hili lilipata hati safi katika mwaka husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Kamati ilipopitia mahesabu ya mamlaka hii, mambo kadhaa yalijitokeza. Suala la misamaha ya kodi, suala la makusanyo yaliyozidi, malimbikizo ya madeni ya kodi za mafuta, uaminifu wa maofisa wa *TRA*, suala la udhibiti wa bidhaa bandia na mengine mengi.

Mheshimiwa Spika, misamaha ya kodi imekuwa ikilikosesha Taifa mapato kwa kiasi kikubwa sana. Pamoja na kuwa njia hii ni moja ya vivutio vya uwekezaji toka nje, Tanzania imekuwa kati ya nchi zenye misamaha mikubwa mno ikilinganishwa na uwezo na mahitaji ya nchi. Misamaha hii inafikia asilimia 30 ya makusanyo yote ya nchi kwa mwaka. Hiki ni kiasi kikubwa mno. Katika hili Kamati imetoa agizo kwa *TRA* kusimamia kwa karibu zaidi misamaha ya kodi na kutoa ushauri Serikalini juu ya upunguzaji wa misamaha ya kodi.

Lakini pamoja na jitihada hizi, Kamati inaona kuna umuhimu wa Bunge kama chombo cha kutunga sheria kuangalia uwezekano wa kusaidia kutatua tatizo hili kwani misamaha yote hutolewa kwa mujibu wa sheria, ambazo hupitia hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa maelezo ya *TRA* iliyoyatoa kwa Kamati, misamaha na nafuu za kodi hutolewa kwa mujibu wa sheria mbalimbali za kodi na sheria nyingine ya uwekezaji. Kwa mujibu wa kifungu cha 14 cha Sheria ya *TRA CAP 399 (R.E 2006)* Waziri wa Fedha ana uwezo pia kutoa misamaha ya kodi kwa maslahi ya Taifa, baada ya kupata ushauri wa Bodi ya *TRA*. Mamlaka katika kutimiza wajibu wake imekuwa ikisimamia utoaji wa misamaha ikiwa ni pamoja na kufanya kaguzi za mara kwa mara kwa walipa kodi waliopata misamaha hiyo. Katika kutekeleza wajibu wake wa kutoa ushauri juu ya masuala ya misamaha ya Kodi, mamlaka imekua ikitoa mapendekezo Serikalini juu ya uboreshaji wa Sera za kodi kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo mamlaka ya mapato imependekeza kwa Kamati kuwa ni maeneo ya misamaha yanayohitaji kuangaliwa upya ili kuyaboresha yanahusisha sheria ya ongezeko la thamani ya mwaka 1997, misamaha ya kodi ya ushuru wa forodha kwa wawekezaji na sheria ya kodi ya mapato 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni makusanyo ya mamlaka ya mapato. Pamoja na kazi nzuri ya mamlaka ya mapato kukusanya kodi vizuri, Kamati imeona kuna umuhimu wa mamlaka hii kuangalia upya jinsi malengo ya ukusanyaji yanavyowekwa. Kuliko kujiwekea viwango vinavyofikikika kiurahisi, hapana budi mamlaka kuhakikisha inavumbua vyanzo vingi iwezekanavyo vya kodi na kujiwekea viwango ambavyo vitaleta changamoto katika ukusanyaji. Hii itaondoa dhana ya kuvuka malengo ya ukusanyaji kila mwaka. Kamati pia iliagiza *TRA* kuboresha mifumo ya udhibiti wa ndani (*Internal*

*Control*) Hii itapunguza kwa kiwango kikubwa hoja za wakaguzi na itasaidia kuendeleza upatikanaji wa hati safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu pia iligundua kuwa kuna udanganyifu katika ulipaji wa kodi za mafuta kwa baadhi ya waingizaji wa mafuta hayo nchini. Katika hicho cha Kamati ilielezwa kwamba thamani ya hoja zote ya mwaka unaohusika zinazohusu udanganyifu wa malipo kwa Serikali zilikuwa na thamani ya Sh. 38,465,007,647.81 kati ya hizo fedha, hoja yenye thamani ya Sh. 35,574,859,055.02 ambayo ni sawa na asilimia 92.5 zilihusu kampuni moja tu *TIOT Limited*.

Kamati ilielezwa kuwa kampuni hii ni sugu kwa ukwepaji wa kodi za mafuta. Aidha, Kamati inaipongeza *TRA* kwa kuweza kukusanya shilingi bilioni 29.8 ya hoja zote na kubakiwa na bakaa ya shilingi bilioni 8.420 ambazo shilingi bilioni 5.66 zinaihusu kampuni ya *TIOT*. Kamati ilielezwa njia kuu inayotumika kuzuia *TRA* isipate mapato yake ni kampuni ya *TIOT* kukimbilia mahakamani. Kamati inapendekeza kwa Serikali kufanya uchunguzi wa kina kwa kutumia vyombo vyake vyote, Serikali kama vile TAKUKURU kubaini msingi wa ujeuri wa Kampuni hii unatoka wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeiagiza *TRA* kushirikiana kikamilifu na mamlaka za udhibiti hususan *EWURA* na *TBS* kuhakikisha mafuta yanayoingizwa nchini ni salama na yanalipiwa kodi kama inavyotakiwa. Pia, Kamati iliagiza *TRA* kuhakikisha inawachunguza wafanyakazi wake na kubaini wale wasio waaminifu na kuwachukulia hatua muafaka. Hata hivyo, Uongozi wa *TRA* uliihakikishia Kamati kuwa, utaratibu maalum wa kuwahamisha watumishi kwenye vituo mbalimbali vya forodha unatumika ili kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ilivyokuwa kwa Wizara ya Viwanda na Biashara, Kamati ilijadili suala la bidhaa bandia (*counterfeit*). Kwa kuwa *TRA* inahusika na ukusanyaji wa kodi katika maeneo yote ya kuingizia bidhaa, ni dhahiri ina mchango mkubwa katika kudhibiti bidhaa ambazo hazikidhi ubora ikishirikiana na *TBS*. Lengo lisiwe kukusanya mapato tu. Kwa zile bidhaa ambazo mamlaka itazitilia shaka, ni vyema mamlaka ikaripoti kwa mamlaka husika ili hatua zichukuliwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Miundombinu (Fungu 98) Kamati yangu ilipitia mahesabu ya Fungu 98, Wizara ya Maendeleo ya Miundombinu mnamo tarehe 16 Aprili, 2009 mjini Dar es Salaam. Fungu hili lilikuwa na hoja za ukaguzi takribani saba ambazo Wizara ilizijibu na hivyo hoja hizo kufungwa. Hata hivyo, kuna maeneo kadhaa ambayo Kamati imeona ni vyema kuyazungumza na kuyatolea maoni ili kuepuka kujirudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza ni uwasilishwaji wa taarifa za fedha kwa ajili ya Ukaguzi. Kifungu cha 25 (2) cha sheria ya fedha za Umma Na. 6 ya mwaka 2001 (iliyorekebishwa 2004) inamtaka Afisa Masuhuli kuandaa hesabu za mwaka na kuziwasilisha kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi ifikapo au kabla ya tarehe 30 Septemba kila mwaka.

Katika mwaka wa fedha 2006/2007 Wizara iliwasilisha hesabu zake tarehe 29 Septemba, 2007. Hata hivyo, mamlaka ya Mawasiliano nchini *TCRA*, ambayo ipo chini

ya Wizara ya Miundombinu zilikuwa bado hazijawasilisha. Hii ni kutokana na kuwepo kwa sheria ya *TCRA* (Sheria namba 12 ya *TCRA* ya mwaka 2003 kifungu 51 (2)) ambayo inatoa mwanya kwa *TCRA* kuteua Mkaguzi wake mwenyewe kukagua hesabu zake. Kwa kuwa hii ni mamlaka ya umma, Kamati imeona kuna umuhimu wa kuhuisha sheria hizi mbili ili kumruhusu Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kupitia hesabu za taasisi hii kama inavyohitajika kisheria (sheria ya fedha ya mwaka 2001 kifungu no 37 na sheria ya ukaguzi ya mwaka 2008 Na. 9(a)(i).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu pia imeguswa sana na suala la mafungu mengi kutoweza kufikia malengo yao kutokana na kutopata fedha, kama ilivyoainishwa kwenye bajeti husika. Tatizo hili lipo hasa katika fedha za maendeleo, hususan maeneo yanayotegemea fedha za wahisani. Katika Wizara ya Miundombinu kumekuwepo na tatizo hili kwa kiasi kikubwa. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 kiasi cha fedha za maendeleo kilichoidhinishwa toka kwa wahisani ni Sh. 119, 430,658,460/= na kiasi kilichotolewa mpaka kufikia June, 2007 ni Sh.10,760,685,085.56 sawa na asilimia tisa ya kiasi kilichoahidiwa. Huwezi ukajenga barabara kwa msingi huo. Kati ya kiasi kilichotolewa, Sh. 10,722,357,029.16 kilitumika na hivyo kubakisha bakaa ya Sh. 38,327,056.40

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha, mpaka kufikia tarehe 30 June 2008, kati ya Sh. 244,234,324,600/= zilizoidhinishwa kuingia kwenye akaunti ya maendeleo, Sh. 23,636,100,000/= tu zilikuwa zimetolewa. Kwa hali hii ni vigumu sana kujenga barabara. Hata kama ukijenga mwishoni unakuwa na certificate ambazo hazilipwi ambazo zinaongeza madeni.

Kwa kazi yetu hapa tunafikiri njia nzuri ni kuhakikisha fedha zaidi za ndani kuliko kuweka fedha za nje. Hii ni sawa na asilimia 9.7 ya fedha zote. Kwa mifano hii miwili, inaonekana kabisa kuwa miradi mingi ya maendeleo inakwama ama kuchelewa kukamilika kwa sababu ya utegemezi wa bajeti yetu, hasa kipindi hiki ambapo hata wahisani ambao twawategemea pia wanakopa. Hata hivyo, kuchelewa ama kutotolewa kwa fedha na Wahisani yawezekana kunasababishwa na mambo kadhaa kwa upande wetu kama nchi. Hapana budi basi Wizara ya Fedha kuweka bayana sababu hizo ili jitihada za pamoja zifanyike kuharakisha upatikanaji wa pesa hizi kwa wakati ili kuokoa miradi mingi ya maendeleo inayokwama.

Aidha, kama tulivyoeleza awali, bajeti ya miundombinu igawiwe fedha za ndani tu ili kuwa na uhakika wa miradi kumalizika kwa wakati, malipo kwa makandarasi kulipwa gharama kubaki karibu na makisio na kazuia riba ambayo inapelekea miradi mingi kuongeza gharama mara dufu na migogoro na makandarasi. Mfano wa mradi ambao gharama zake ziliongezeka kwa sababu ya mgogoro na mkandarasi na hivyo kuongezeka kwa gharama za mkataba ni ule wa ujenzi wa barabara ya Mbwemkuru-Lindi-Mingoyo, kama ilivyotajwa awali. Katika mradi huu, kulikuwa na ongezeko pamekuwa na (*over cost run*) la asilimia 46 sawa na Sh. 75,053,368,563.07 zaidi ya gharama za awali na kwa hiyo, mradi huo umekamilika kwa gharama ya shilingi bilioni 126 badala ya thamani ya mkataba iliyokuwa shilingi bilioni 51.477. Kwa hali hii hatuwezi kujenga barabara za kutosha. Karibu barabara zote zina *cost over run*. Kwa

hiyo, tunafikiri njia mojawapo ni kuhakikisha fedha inayopatikana ya ndani ipewe zaidi kwa upande wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa karibu miradi yote ya barabara haimaliziki bila ongezeko kubwa la gharama na hali hii inasababishwa na kutokuwa na uhakika wa fedha za maendeleo na matatizo ya makandarasi kutokidhi makubaliano ya mikataba kama ilivyokubaliwa awali wakati wa kusaini mikataba. Kamati inapendekeza Serikali izingatie utoaji wa fedha za ndani kulingana na mpango wa miradi ya mwaka wa bajeti husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mabadiliko ya hivi karibuni kuhusu mamlaka ya manunuzi ya Serikali, Wizara ya Miundombinu imebakia na jukumu la kununua mitambo ya Serikali. Hii ni kwa sababu ya utaalumu unaotakikana katika ununuzi wa aina hii. Katika kikao na Kamati, Afisa Masuhuli wa Wizara hii aliihakikishia Kamati kuwa, utaratibu unaotumika sasa wa kununua magari mengi kwa wakati mmoja na kutoka kiwanda ama mtengenezaji mmoja unasaidia sana kupunguza gharama za ununuzi wa magari haya.

Kamati imefarijika kusikia nia hii ya Serikali ya kupunguza gharama kwa utaratibu huu. Hata hivyo, Kamati bado inaona kuna umuhimu mkubwa wa Serikali kubadili aina ya magari inayonunua. Pamoja na sababu za msingi ambazo zinapelekea kununuliwa kwa magari ambayo yanatumia na Serikali kwa sasa, bado kuna umuhimu wa kupunguza idadi ya magari hayo ya gharama kubwa. Kwa maafisa wa ngazi za juu waliopo Dar es Salaam na Mikoani, bado wanaweza kutumia gari ambazo ni nzuri na za heshima, lakini zenye gharama nafuu, kama inavyofanyika katika nchi jirani na zilizoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tumeangalia ni Wizara ya Maji na Umwagiliaji (fungu 49). Kwa Wizara ya maji pia ni mambo ya bajeti. Wizara ya maji inategemea sana fedha kutoka nje. Jambo hili linafanyika kila mahali. Kamati yangu pia ilikutana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji mnamo tarehe 21 Aprili, 2009 hapa mjini Dodoma. Kwa ujumla Kamati ilifurahishwa sana na mtazamo wa Wizara kuhusu suala la maji na umwagiliaji. Kama ilivyo kwa Wizara nyingine nyingi za Serikali, Wizara hii ilikuwa na hoja za ukaguzi takribani 70, ambapo 69 kati ya hizo zilikuwa zimetolewa maelezo ya kutosha na kufungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja moja iliyobaki ilihusu “*Ghost employees*” ambapo maelezo yake yalitolewa mbele ya Kamati. Suala lililopo katika hoja hii ni kukosekana kwa umakini wa kusitisha malipo ya wastaafu na Marehemu kwa wakati. Orodha ya wale waliolipwa isipo stahili ilitolewa mbele ya Kamati na Kamati kuridhika kuwa uwezo wa watu hao kulipa deni hilo ni mdogo sana kwa kuwa ni watu waliokuwa na kipato cha wastani na sasa wanaishi kwa pensheni ndogo sana na wengine ni Marehemu sasa. Kamati ilipendekeza kuwa suala hili liombewe kibali ili deni hili lifutwe kwenye vitabu vya mahesabu kwa kuwa halilipiki kirahisi.

Hata hivyo, Kamati ilisisitiza kwa Wizara hii, kama ilivyofanya kwa Wizara nyingine nyingi, kuachana na dhana ya kusubiri kujibu hoja na badala yake kuzuia hoja

hizi ambazo imeonekana kabisa zipo ndani ya uwezo wa Maafisa Masuhuli kuhakikisha hazitokei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango mizuri ya Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Afisa Masuhuli alieleza jinsi Wizara yake inavyoshindwa kukamilisha mipango yake kutokana na kutotolewa kwa ukamilifu kwa fedha zilizotengwa kwa miradi mbalimbali, hasa zile zinazotoka kwa Wahisani. Kwa upande mwingine, mtiririko wa fedha za ndani kwa miradi ya maji unaonesha kuwa, mwaka hadi mwaka fedha hizo zimekuwa zikipungua, huku ikiacha kiasi kikubwa cha fedha za miradi ya maji kuwa ni kutoka kwa wafadhili. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2006/2007 kiasi cha Sh. 99,397,994,100/= fedha za ndani kilitolewa kwa miradi ya maji sawa na asilimia 58.9 ya fedha zote za maendeleo, wakati kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kiasi cha fedha za ndani kilichotengwa ni Sh. 70,770,035,000/= sawa na asilimia 31.1 na kwa mwaka huu wa fedha kiasi cha ndani kilichoidhinishwa ni Sh. 46,463,373,000/= sawa na asilimia 33.2. Hali ikiendelea hivi, hasa kipindi hiki ambapo wahisani nao wana matatizo ya kifedha, miradi hii itakwama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijulishwa kuwa Wizara ina mpango kabambe wa kutatua tatizo la maji katika jiji la Dar es Salaam kwa kutumia vyanzo vipya vya maji ambavyo vimegunduliwa hivi karibuni. Kamati inapongeza sana mpango huu. Hata hivyo, bado kuna wasiwasi jitihada hizi zikakwama kama mgawo wa fedha utakuwa katika mtiririko kama ilivyojionesha hapo juu. Afisa masuhuli aliihakikishia Kamati kuwa akipatiwa shilingi bilioni 70 kwa miradi ya maji, hatua kubwa itapigwa. Kamati inaisihi Serikali kuwekeza katika maji kwa kutoa kiasi cha fedha zisizopungua shilingi bilioni 70 kwa bajeti ya maendeleo ili kuwezesha Wizara hii kutimiza lengo la kutoa maji safi na salama kama vile malengo ya milenia yanavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa imeonekana miradi ya maji imekuwa na tatizo la fedha (*funding*) na kwa kuwa tunaamini kuwa maji ni uhai, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuruhusu miradi hii kukopa katika vyanzo vya ndani kama vile *NSSF*, *PPF*, *GEPF* na *PSPF* na Serikali kuwa mdhamini wa mikopo hii. Utaratibu huu wa kukopa hautakuwa mgeni kwa sababu yamefanyika hayo kwa nyumba za Polisi, majengo ya vyuo vikuu na majeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la umwagiliaji, Kamati yangu inaona kuna umuhimu mkubwa wa kubadilishwa kwa muundo uliopo sasa hasa katika suala la miundombinu ya umwagiliaji. Kwa kuwa kumekuwa na mabadiliko ya mara kwa mara ya muundo wa Wizara mbalimbali, na suala la umwagiliaji limekuwa likihamahama katika wizara mbalimbali, Kamati inapendekeza suala la kujenga miundombinu ya umwagiliaji na fedha zote za umwagiliaji kuwa chini ya Wizara ya maji na umwagiliaji. Hii itasaidia kuwa mipango endelevu ya umwagiliaji na kutumika vyema kwa vyanzo vya maji nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na mtindo katika Wizara hii kujenga mabwawa mengi makubwa na madogo bila kuweka miundombinu itakayowezesha maji hayo kutumika katika njia ya usafi na usalama. Kwa mfano, bwawa la Bariadi

limejengwa mwaka 1988 mpaka leo bwawa hilo halina miundombinu ya mabomba, chujio na kwa hiyo, maji yaliyomo hayawezi kutumika. Aidha, Kamati inajua kuna mifano mingi ya aina hii nchi nzima. Kamati inapendekeza kuwa miradi yote ya mabwawa iambatane na ujenzi wa miundombinu itakayoweza maji hayo kutumika kiusalama kwa watu na mifugo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali kuhusu utekelezaji wa shughuli zake kwa mwaka 2006 na 2007. Kwa mara nyingine, naomba kukupongeza wewe binafsi, pamoja na Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Spika, Mheshimiwa Anne S. Makinda, Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Job Y. Ndugai, uliopo leo na Mheshimiwa Zuber Ali Maulid kwa uongozi wenu wa pamoja. Nawatakia baraka za Mwenyezi Mungu katika kutekeleza kazi nzito na muhimu ya kuliongoza Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyoihusu Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya Taarifa hii na kunipa heshima ya kuiwasilisha mbele ya Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati katika kutekeleza kazi zake ilikuwa ikisaidiwa na Maafisa Waandamizi kutoka Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mdhbiti na Mbaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mhakiki Mkuu wa Mali za Serikali. Nawashukuru sana kwa mchango wao wa kitalaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Dr. Thomas D. Kashillilah kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, nawapongeza Makatibu wa Kamati hii Ndugu Angumbwike Lameck Ng'wavi na Ndugu Michael Lucas Chikokoto kwa kuratibu shughuli zote za Kamati hii kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nataka kuwashukuru sana kwamba leo tukisoma pia tumekuwa na mazungumzo na wafadhili zaidi wa sehemu mbalimbali ya nchi yetu ambao ni kutoka Sweden, Denmark na Norway. Naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii na kuijadili na hatimaye ipitishe mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. SVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Cheyo kwa uwasilishaji wako mzuri. Sasa Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe kuhusu utaratibu ni kwamba hoja zote za Kamati mbili zitawasilishwa kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, baadaye kidogo baada ya Mheshimiwa Cheyo ambaye amewasilisha hoja ya Kamati ya Hesabu za

Serikali baadaye kidogo nitamwita Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa kwa ajili ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

Lakini kabla sijamwita niwaambie kwamba hoja ya Mashirika ya Umma itawasilishwa kesho. Kwa hiyo, wanaotaka kuchangia kuhusu hoja ya Mashirika ya Umma nawaomba waleta karatasi zao kesho asubuhi. Halafu mpaka sasa katika orodha yangu karibu Wabunge wote ambao wameomba kuchangia hoja zote mbili ni CCM peke yao. Kwa hiyo, upande mwingine msije mkanilaumu. Niwataarifu kwamba, baada ya Mheshimiwa Dr. Slaa kuwasilisha hoja yake, tutaanza ule uchangiaji wa jumla na mchangiaji wetu wa kwanza humu ndani atakuwa Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir.

**MHE. DR. WILLIBROD PETER SLAA- MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC):** Mheshimiwa Spika awali ya yote napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa juu ya Taarifa ya Mdhiliti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iliyowasilishwa Bungeni mwezi Machi, 2008 kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Halmashauri za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 30 Juni, 2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa imeshagawiwa inawezekana sitasoma yote kwa ajili ya muda. Nikiruka basi mjue kwamba nimeruka, lakini iko kwenye vitabu vya Hansard ambavyo vimeshagawiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaanza kutekeleza Kanuni ya 114(15) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007, naomba nitumie nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu ambao uliwateua kwa mujibu wa Kanuni ya 113(3) ya Kanuni za Bunge Toleo la 2007, kwa ushirikiano wao na kwa kazi nzuri waliyoifanya ikiwa ni pamoja na kushiriki ipasavyo katika vikao vya Kamati, kufanya uchambuzi yakinifu wa hesabu, kukosoa pale jambo linapofanywa kinyume na matarajio ya Kamati, kujitolea kwao kusiko na kikomo na kutoa michango na maoni ya msingi katika kuhakikisha dhana ya kuwepo na nidhamu ya matumizi ya fedha na mali za Umma inajengwa na kuimarishwa upya kwa kuzingatia taratibu, Kanuni na Sheria zilizopo.

Aidha, niwashukuru kwa kujitolea kwao, kwani mara nyingi majukumu ya Kamati yaliwalazimu wajumbe kumaliza vikao usiku na wakati mwingine kufanya vikao siku za sikukuu. Hivyo, Kwa heshima naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Dr. Willibrod P. Slaa - Mwenyekiti ambaye ndiyo nimesimama hapa, Mheshimiwa Mgana I. Msindai - Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima O. Kimbau, Mheshimiwa Dr. Juma A. Ngasongwa, Mheshimiwa Dr. Zainab A. Gama, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Samueli M. Chitalilo, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Mwanne S. Mchemba, Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mheshimiwa Ernest G. Mabina, Mheshimiwa Eng. Laus O. Mhina, Mheshimiwa Dunstan D. Mkapa, Mheshimiwa Idd M. Azzan Mbunge, Mheshimiwa Bernadeta K. Mushashu,



Mheshimiwa Eng. Benito W. Malangalila, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Dr. Zabein M. Mhita na Mheshimiwa Ahmed A. Salum. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa pia kutoa shukurani zangu za dhiti kwa ushirikiano na mchango wa kitaalam uliokuwa ukitolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, Ndugu Ludovick Utouh na Maaafisa Waandamizi kutoka Ofisi yake, Maaafisa Waandamizi kutoka Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Hazina, Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Sekretarieti ya Ofisi ya Bunge. Kwa niaba ya Kamati yangu, niwapongeze sana kwa juhudi na kujitolea kwao kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Kamati yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati, majukumu ya Kamati hii yametajwa kwenye Nyongeza ya Nane, kifungu Na.12 chini ya Kanuni ya 115 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la 2007 na kwa mwaka wa taarifa hii, Kamati ilifanya kazi zake katika namna kuu tatu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilijadili na kuchunguza Hesabu za Halmashauri za mwaka wa Fedha wa 2006/2007 zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. Kazi hiyo imefanywa kwa Halmashauri 73 kati ya Halmashauri 124 zilizokuwepo mwaka 2006/2007 zilikaguliwa katika vikao vilivyofanyika vikao vilivyofanyika Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuzingatia yaliyojitokeza kwenye ukaguzi wa vitabu vya Halmashauri, Kamati ilifanya Ukaguzi wa thamani ya miradi ya maendeleo (*Value for Money Audit (VFM)/Performance Audit*), katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha (isipokuwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro), Manyara (isipokuwa katika Halmashauri za Wilaya za Kiteto na Simanjiro), Mkoa wa Mwanza (isipokuwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba), Mara, Kagera, Kigoma, Rukwa, Tabora, Tanga na Morogoro. Hivyo, Kamati imeona mengi kuhusu utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika Halmashauri za Mikoa niliyoitaja ambazo ni sawa na asilimia 41.2 ya Halmashauri zote 124 zilizokuwepo katika Mwaka wa Fedha wa 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kuhudhuria mafunzo na warsha katika nyakati tofauti kama ifuatavyo:-

(i) Mafunzo yaliyoandaliwa na TAMISEMI kuhusu Awamu Mpya ya Maboresho ya Serikali za Mitaa (*Local Government Reform*). Mafunzo haya yalifanyika kwa pamoja na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu programu ya uboreshaji wa mfumo wa Serikali za Mitaa, Dar es Salaam tarehe 26 - 27 Mei, 2008.

(ii) Mafunzo yaliyoandaliwa na *Deepening Democracy Program (UNDP)*, mpango wa Bunge. yalihusu Usimamizi na Ufuatiliaji wa matumizi sahihi ya Fedha za Umma, yaani *Expenditure Tracking*. Mafunzo haya yalifanyika kwa pamoja na Kamati ya Hesabu za Serikali (*PAC*), Dar es Salaam tarehe 08 Aprili, 2009; na

(iii) Warsha iliyoandaliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali akishirikiana na Benki ya Dunia kuhusu Changamoto zinazokabili Serikali za Mitaa katika Usimamizi wa Fedha za Umma. Warsha hiyo ilihusisha Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa, Wafadhili toka Nje ya Nchi, Wenyeviti na Watendaji wa baadhi ya Halmashauri, Wawakilishi toka Tamisemi, Hazina na Benki ya Dunia, na ilifanyika Dar es Salaam, Karimjee Hall tarehe 22 Januari, 2009.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani nyingi kwa Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Program ya Maboresho ya Serikali za Mitaa), Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Wafadhili toka nje ya Nchi na watoa mada wote kwa kuwawezesha wajumbe wa Kamati kupata mafunzo na kupanua uwezo wao katika kuuelewa vyema Mfumo wa Serikali za Mitaa na kuchambua Hesabu zilizokaguliwa za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa Zilizowasilishwa Mbele Ya Kamati, kila Halmashauri iliyofika mbele ya Kamati ilitakiwa kuwasilisha mambo yafuatayo:-

(a) Taarifa ya Wilaya (*District Profile*) yenye Maelezo ya shughuli zote zilizomo katika Halmashauri ya Wilaya;

(b) Taarifa ya Mapato na Matumizi halisi inayoonyesha pamoja na Makisio kwa muda wa miaka mitatu.(2005/2006,2006/2007 na 2007/2008);

(c) Taarifa na michanganuo ya kina ya Mapato na Matumizi ya Miradi yote inayopata Ruzuku ya Serikali, Wahisani, Halmashauri na Wananchi (kama Mfuko wa Barabara (*Road Fund*), Mfuko wa Maendeleo (*Development Fund*), Mfuko wa Afya wa Pamoja (*Basket Fund*), *MMEM*, *Irish Fund*, *DANIDA*, *TASAF*, *PADEP* n.k. pamoja na Taarifa ya Uchambuzi wa Matumizi ya Miradi yote iliyomo kwenye Halmashauri ikionyesha salio anzia, fedha iliyopokelewa, fedha iliyotumika na salio ishia kwa mwaka husika; haya mengine nadhani mnaweza kusoma yako kwenye kitabu.

(d) Majibu ya hoja za ukaguzi yaliyohakikiwa na Wakaguzi;

(e) Majibu ya hoja za Kamati ya *LAAC* yaliyowasilishwa kwa kila Halmashauri wakati wa vikao vya nyuma na kuhakikiwa na Wakaguzi;

(f) '*Certificate of Balance*', '*Bank Reconciliation*' na '*Bank Statement*' kwa kila Akaunti ya Halmashauri iliyoko Benki; na

(g) '*Bill of Quantities*' (*BOQ*) na Mikataba yenye saini ya Mwenyekiti wa Halmashauri kwa mwaka unaohusika na Ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uwasilishaji wa Taarifa hizi mbele ya Kamati na ushirikishwaji wa Wenyeviti wa Halmashauri katika vikao vya *LAAC*, umeisaidia Kamati

kubaini kuwa Taarifa zinazowasilishwa mbele ya Baraza la Madiwani (*Full Council*) la kila Halmashauri kwa lengo kufanyia uchambuzi wa kina na kutoa maamuzi, hazina michanganuo ya kina ya mapato na matumizi ya fedha za miradi, hivyo huliwia vigumu Baraza katika kuendeleza jitihada za kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za Umma.

Aidha, Kamati imebaini kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kuendelea kuwashirikisha Wenyeviti wa Halmashauri, lengo kubwa likiwa ni kuendelea kuwaelimisha juu ya shughuli za Kamati yetu na kuwapatia mbinu na uzoefu wa kutosha katika kusimamia vema utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo katika Halmashauri zetu. Mambo Yaliyobainika Katika Uchambuzi Wa Hesabu: mwelekeo wa utendaji kazi katika Halmashauri zetu unaridhisha, kwa maana watendaji kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakifanya kazi zao kwa mujibu wa taratibu, Kanuni na Sheria zilizowekwa, ingawa kwa baadhi ya Halmashauri hakuna ushirikiano mzuri wa kiutendaji baina ya Idara na idara kulingana na utaalum unaohitajika, na pia bado kuna wazembe wachache ambao wanaharibu sifa na mazuri yanayofanywa na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeona kuna mwelekeo mzuri katika ufungaji na uwasilishaji wa Hesabu za Halmashauri kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa maana Halmashauri zote 124 (100%) ziliwasilisha taarifa za mwaka za fedha ilipofika tarehe 30 Septemba, 2007 ambalo ni hitaji la kisheria. Hata hivyo Halmashauri 15 ziliondoa taarifa zao na kuwasilisha taarifa za fedha zilizorekebisha kati ya Novemba na Januari, 2008 (mwaka wa ukaguzi 2006/2007) na kuacha Halmashauri 109 zikizingatia uwasilishaji wa hesabu kwa mujibu wa Sheria. Hata hivyo na hili ni muhimu, idadi ya Halmashauri 15 zilizoondoa taarifa zao za fedha na kuwasilisha taarifa zilizorekebisha ziliongezeka kutoka 8 katika mwaka 2005/06 hadi 15 katika mwaka 2006/2007.

Kwa hiyo, Halmashauri 109 (88%) ndizo ziliwasilisha taarifa zao za fedha kwa mujibu wa Sheria na hivyo kumwezesha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kufanya ukaguzi kwa wakati na kuwasilisha Taarifa yake ya Ukaguzi mapema katika Bunge la mwezi Aprili, 2008. Kamati inapongeza jitihada na juhudi zilizowekwa ambazo zimefanywa na Halmashauri katika ufungaji wa hesabu na kuwasilisha vitabu hivyo kwa Wakaguzi kwa wakati uliowekwa kwa mujibu wa Sheria. Tunasema hayo ni mafanikio makubwa kwa Halmashauri zetu kwa sababu kwa miaka mingi wananchi hawakuweza kujua Halmashauri zao zinafanya nini na kwa kiwango gani katika kuleta maendeleo kwenye maeneo hayo. Kamati inaikemea tabia hii ya Halmashauri chache kuwasilisha Taarifa na hatimaye kuziondoa kwa lengo la kufanyia marekebisho nje ya muda uliowekwa na Sheria kwani siyo tu ni ukiukwaji wa sheria bali inaifanya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hesabu za mwaka 2006/2007 mapendekezo na maoni mbalimbali yametolewa na Kamati pamoja na Wakaguzi kuhusu masuala muhimu yaliyojitokeza katika ukaguzi uliofanyika miaka iliyopita yanayohusu usimamizi wa fedha za Halmashauri. Halmashauri nyingi zimeonyesha juhudi ya kutekeleza maoni ya Ukaguzi na ya Kamati. Hata hivyo, kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi

Mkuu wa Serikali, hadi kufikia Juni, 2007 Halmashauri 52 zilikuwa hazijatekeleza masuala yanayotokana na ukaguzi wa miaka ya nyuma yanayofikia kiasi cha Sh.4,643,565,831/=, Halmashauri ya Wilaya ya Musoma ndiyo ilikuwa na kiwango kikubwa zaidi cha Sh.463,074,416/= na Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, ndiyo iliyokuwa na kiwango cha chini zaidi cha Sh.820,000 kwa taarifa Waheshimiwa Wabunge huko nyuma ya taarifa yetu kuna vielelezo kwa kila eneo.

Kamati yangu imekuwa ikitoa ushauri na maagizo mbalimbali kwa Halmashauri ili ziweze kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza haraka katika kuboresha mfumo wa udhibiti wa ndani na usimamizi wa rasilimali za Halmashauri. Hulka ya kutoshughulikia maoni, mapendekezo na maagizo kutoka kwenye taarifa ya Ukaguzi au Kamati inaweza kusababisha kujirudia kwa dosari zilizojitokeza na kulisababishia Taifa hasara au upotevu wa mabilioni ya fedha, iwapo haitakemewa kwa ukali, kudhibitiwa au kuchukuliwa hatua kali za kisheria na kinidhamu. Aidha, Hali hii ni kiashiria cha kutokuwepo kwa umakini na uwajibikaji kwa Menejimenti za Halmashauri husika, hata hivyo, kwa upande mwingine hali hii husababishwa na vyombo vya dola, kama vile PCCB na Polisi ambapo upelelezi wa kesi za ubadhirifu na wizi huchukua muda mrefu mpaka kukamilika, pia Mahakama zimekuwa zikisababisha hali hii kutokana na ucheleweshaji unaosababisha kesi kuchukua miaka mingi mpaka kufikia hatua ya kutajwa bila kusikilizwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa fedha kwa ujumla unahusisha makusanyo na mapokezi ya fedha za Umma na pia usimamizi wa akaunti za benki za Halmashauri. Agizo Na. 68 la *Memorandum* ya Fedha za Serikali za Mitaa ya mwaka (1997) limeweka bayana kuwa Mweka Hazina wa Halmashauri ahakikishe kwamba ulinganifu wa kibenki na udhibiti kati ya daftari la fedha na hesabu za benki unafanyika kila mwezi. Kwa mwaka 2006/2007 Halmashauri 48 hazikuzingatia agizo hili, hivyo kuwepo kwa kiwango kikubwa cha mambo yasiyosuluhishwa katika ulinganifu wa kibenki, kama ifuatavyo:-

- (a) Jumla ya Sh.392, 220,923/= ziliingizwa kwenye daftari za fedha za Halmashauri lakini hazikuonekana katika taarifa za benki. Kwenye vielelezo huko nyuma inaonekana ni Halmashauri zipi zinahusika;
- (b) Hundi za jumla ya Sh.4,913,727,424/= zilitolewa kwa watu mbalimbali lakini hazikupelekwa benki mpaka mwisho wa mwaka wa fedha tarehe 30 Juni, 2007;
- (c) Jumla ya Sh.1,277,787,933/= hazikupelekwa benki na hakukuwa na jitihada za kuhakikisha zinapelekwa benki;
- (d) Jumla ya Sh.360,510,539/= zilionekana kama malipo katika taarifa za benki lakini hazikuonekana kama malipo katika daftari la fedha la Halmashauri; na
- (e) Jumla ya Sh.489,624,271/= zilikusanywa na benki kwa niaba ya Halmashauri bila kuonekana katika daftari la fedha la Halmashauri kama mapokezi. Hali hii sio tu

inaonyesha kutokuwepo kwa umakini na uwajibikaji wa kutosha kwa Wakurugenzi na Menejimenti za Halmashauri bali pia huonyesha kuwepo kwa mazingira ya ubadhirifu wa fedha ya umma. Katika kutafuta suluhisho la mapungufu haya na ikizingatiwa yalifanyika 2006/2007, Kamati yangu katika vikao vyake imeagiza kila Halmashauri kuhakikisha hoja zote za ukaguzi za miaka iliyopita zinajibiwa kikamilifu, na usuluhisho wa kibenki uwe unafanywa kila mwezi, na maagizo haya yatashughulikiwa kwa umakini zaidi na Kamati katika kaguzi zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika ukaguzi wa Hesabu za Halmashauri, ukaguzi umeonyesha kuwa Halmashauri 76 hazikukusanya jumla ya Sh.5,614,010,055 ambayo ni (ongezeko la asilimia 21.5 toka mwaka wa fedha 2005/2006) toka kwa wadaiwa (*Debtors*) hadi mwisho wa mwaka wa fedha, yaani 30 Juni, 2007 Kitendo hiki ni kinyume na maagizo Na.120 na 121 ya *Memorandum* ya Fedha ya Serikali za Mitaa 1997 yanayosema kwamba: “*ni jukumu la Mweka Hazina kufanya mipango ya kutosha ya fedha na hesabu ili kuhakikisha uwekaji kumbukumbu mzuri wa fedha zote za Halmashauri na ukusanyaji, utunzaji kwa usalama na uwekaji benki wa fedha hizi*” na “*Kadiri iwezekanavyo mapato yote yatakusanywa kulingana na huduma iliyotolewa au wakati wa kutoa huduma.*”

*Kama sehemu ya mchakato wa bajeti ya mwaka, Halmashauri itaweka kiwango cha chini cha mwisho ambacho kitawezesha malipo kamili kufanywa kabla na (kama ni lazima) viwango vya chini vya kuweka amana*”. Kushindwa kukusanya fedha toka kwa wadaiwa wa Halmashauri kunadhihirisha udhaifu mkubwa wa udhibiti wa ndani wa ukusanyaji wa madeni toka kwa wadaiwa na kutozingatiwa kwa maagizo ya Memorandum ya fedha ambayo kwa kiwango kikubwa husababisha Halmashauri kushindwa kutimiza majukumu yaliyowekwa ikiwemo kuchelewa kukamilika kwa miradi iliyopangwa kwa wakati. Hivyo ni muhimu kwa Mamlaka hizi za Serikali za Mitaa kuimarisha utaratibu wa kukusanya madai toka kwa Wadaiwa ili fedha hizo zilipwe kwa wakati na kutumika kwa kukamilisha shughuli zingine za maendeleo. Kamati yetu, kupitia taarifa za Fedha za Halmashauri imebaini deni kubwa la Wadai (*Creditors*) la jumla ya Sh. 6,402,099,278/= Hali hii inaweza kusababisha Halmashauri kupoteza uaminifu na kutokopesheka. Hadi kufikia 30 Juni, 2007 Halmashauri zilizokuwa na deni kubwa la Wadai ni Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji, jumla ya Sh.363,055,047/= ikifuatwa na Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro Sh. 355,924,490/= na ya tatu ilikuwa Halmashauri ya Wilaya ya Babati iliyokuwa ikidaiwa Sh.298,717,255. Halmashauri zinapochelewa kulipa madeni ya Wadai huleta athari mbaya zikiwemo:-

- (a) Hatari ya kuanzisha madaiano na wadai mahakamani;
- (b) Kupoteza hadhi na uaminifu wa mkopo;
- (c) Halmashauri kunyimwa huduma muhimu; na
- (d) Kuathiri bajeti.

Hivyo Kamati inapendekeza Bunge lako Tukufu, kuhimiza Mamlaka za Serikali za Mitaa kulipa madeni yao haraka mara yanapoiva ili kuweza kufungua milango mingine ya kukopa kwa maendeleo ya mamlaka hizo na au kuzifanya Halmashauri hizo zikopesheke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri zetu zina uwezo mdogo sana wa kujitegemea kifedha, yaani mapato yao ya ndani. Ulinganisho uliofanywa kati ya mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani vya Halmashauri, ruzuku za Serikali Kuu na fedha za Wahisani kwa mwaka 2006/2007 umeonyesha kuwa mapato kutoka vyanzo vya ndani vya Halmashauri yalikuwa Sh.77,310,930,607/= ikilinganishwa na Sh. 914,713,448,103/= zilikuwa ni fedha toka ruzuku ya Serikali Kuu na Wahisani Mapato toka vyanzo vya ndani yalikuwa ni asilimia 7.8 tu ya mapato yote ya Halmashauri.

Hali hii inaonyesha kwamba Mamlaka za Serikali za Mitaa katika uendeshaji wa shughuli zake zinategemea kwa kiasi kikubwa ruzuku toka Serikali Kuu na fedha za Wahisani. Halmashauri zetu sio tu kwamba haziwezi kujitegemea kwa sababu ya ukusanyaji mdogo wa mapato, bali hata mipango waliyonayo ya kuongeza mapato si mizuri na haina tija kwa Halmashauri. Taswira tunayoipata hapa ni kwamba Halmashauri nyingi zinapotengeneza makisio yao kuna vyanzo vingine havifikiriwi au juhudi za kukusanya mapato kutokea kwenye vyanzo vyake haziwekwi bayana. Mfano, kwa mwaka 2006/2007 Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ilikisia kukusanya Sh.930,000,000/= lakini ilikusanya Sh.1,177,159,803/= ambazo ni sawa na tofauti ya asilimia 26. Aidha, kutokana na mipango ya ukusanyaji mapato isiyo na tija, kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007 Halmashauri nyingi zilikusanya chini ya makisio waliyojiwekea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na *District Profiles* zinazowasilishwa kwenye Kamati yangu, imebainika kuwa kuna mapato mengi sana hayakusanywi na wala hayajawekewa mikakati madhubuti ya ukusanyaji. Hivyo, Kamati yangu imeziagiza Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa makini katika kufuatilia makusanyo ya makisio yake, lakini pia kuwa wabunifu katika kutafuta mbinu mbadala ambazo zitaongeza wigo wa vyanzo vya mapato vya ndani. Hatua hii ni ya muhimu sana katika kulitoa Taifa letu kwenye utegemezi mkubwa tulionao toka kwa Wahisani na vyanzo vingine vya nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa kuwa sehemu kubwa ya vyanzo vya mapato ya ndani vimechukuliwa na Serikali Kuu, Kamati yangu inashauri utumike utaratibu kama unaofanyika Japan, na au Nchi za Kinordic, ambapo Mamlaka ya Serikali Kuu, inakusanya mapato yote, na hatimaye kugawa kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa uwiano uliokubalika. Utaratibu huu utaondoa hali inayojitokeza sasa ya mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa tegemezi kwa Serikali Kuu, jambo ambalo ni hatari kwani mamlaka hizo kwa utaratibu uliopo sasa, zitapoteza uimara wake kama Serikali, jambo ambalo ni kinyume na dhana nzima ya kupeleka madaraka kwa Wananchi, yaani “*D by D*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa sehemu kubwa ya vyanzo vya mapato ya ndani vimechukuliwa na Serikali Kuu, Kamati yangu inashauri utumike utaratibu kama unaofanyika Japan, na au Nchi za Kinordic, ambapo Mamlaka ya Serikali Kuu, inakusanya mapato yote, na hatimaye kugawa kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa uwiano uliokubalika. Utaratibu huu utaondoa hali inayojitokeza sasa ya mamlaka za Serikali za Mitaa kuwa tegemezi kwa Serikali Kuu, jambo ambalo ni hatari kwani mamlaka hizo kwa utaratibu uliopo sasa, zitapoteza uimara wake kama Serikali, jambo ambalo ni kinyume na dhana nzima ya kupeleka madaraka kwa Wananchi, yaani “*D by D*”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hivi sasa Utendaji mzuri wa Mtumishi wa Serikali katika Halmashauri zetu unapimwa kwa kulinganisha maelezo ya matumizi ya fedha na hali halisi kwenye miradi husika, yaani “*Value for Money*”. Pamoja na jitihada hizo, bado baadhi ya Wakuu wa Idara ni wazito katika kuchukua hatua za kubadilika na kuwa waangalifu katika matumizi yao ya fedha walizokasimiwa. Aidha, Kamati imebaini kuwa baadhi ya Halmashauri ambazo Watendaji wamekaa muda mrefu bila kuhamishwa, wamejijengea tabia ya kutekeleza majukumu yao kwa mazoea na si kwa kufuata taratibu ama miiko maalum ya kazi zao “*Code of Ethics*”, au ubunifu wao umefikia kikomo katika maeneo hayo, au wamejenga mazingira ya kuhodhi madaraka kuzidi Viongozi wao kiasi cha kutokuwa na ushirikiano wa kutosha. Hivyo, Kamati imeona kuwa ni tatizo kubwa kwa Mtendaji kukaa kwenye kituo kimoja kwa muda mrefu na itaendelea kushauri kwamba kuna umuhimu mkubwa wa kupitia upya na kusimamia Kanuni za Ajira ili Watumishi wanaostahili wapewe madaraka na wasikae kwa muda mrefu kwenye kituo kimoja cha kazi kwa masilahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imebaini pia tatizo zima la Maafisa kukaimu nafasi zilizo wazi kwa muda mrefu bila kuthibitishwa katika nafasi hizo. Kamati inaitaka *TAMISEMI* kuchukua hatua ya haraka pale ambapo Wakuu wa Idara wamekaimu kwa muda mrefu na wanazo sifa stahiki, wathibitishwe mapema iwezekanavyo ili kuongeza uwajibikaji, tija na usimamizi katika utekelezaji wa majukumu yao. Iwapo hawajafikia vigezo basi wapatikane mara moja wenye sifa hizo kujaza nafasi zilizokaimishwa kwa muda mrefu. Kuna Wakuu wa Idara wamekaimu kwa muda mrefu kutokana na wahusika kuwa na kesi za muda mrefu mahakamani. Hali hii inaathiri sana utendaji katika Halmashauri, hivyo ni vema Serikali ikaangalia upya kanuni za ajira katika mazingira kama haya, ili utoaji huduma usiathirike bila sababu, mathalan, idara ya ujenzi kuongozwa na Fundi mchundo (*Technician*) kwa muda mrefu, ni jambo linaloathiri sana utendaji kazi katika Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu imekuwa ikichukua hatua kali kwa mujibu wa Kanuni za Fedha, ikiwa ni pamoja na kupiga tozo. Napenda ieleweke kwamba si nia ya makusudi ya Kamati kutoa tozo kwa Watendaji wa Halmashauri au kuirudisha Halmashauri ikaandae upya Hesabu zake, bali hulazimika kufanya hivyo pale inapogundua kuwa kuna walakini katika taarifa zinazowasilishwa mbele yake. Kama nilivyo sema awali Halmashauri zinatakiwa kuwasilisha taarifa mbalimbali nilizozitaja, endapo tunagundua kuwa Watendaji hawatolei maelezo ya kina taarifa zao walizoziwasilisha, maana yake ama hawasimamii ipasavyo kazi zao au kuna ubadhirifu

umefanyika. Katika hali kama hiyo Kamati haina budi kuchukua hatua kali na itaendelea kuchukua hatua kali kwa Watendaji ambao hawatowajibika ipasavyo katika kutekeleza majukumu yao.

Katika kutilia mkazo suala la uwajibikaji, Kamati ilitoa adhabu ya tozo kwa Watendaji wa Halmashauri za Wilaya za Kyela, Ludewa, Simanjiro, Monduli, Muheza, Mkuranga, Mbulu, Sumbawanga, Songea, Tunduru na Jiji la Tanga kwa kushindwa kutekeleza majukumu/maelekezo ipasavyo. Aidha, katika kuhakikisha Watendaji wanawajibika ipasavyo, Kamati ililazimika kuzirudisha baadhi ya Halmashauri kwenda kuandaa upya vitabu vyao kwa Hesabu za mwaka wa Fedha wa 2006/2007 na kisha kurudi mbele ya Kamati. Mfano Halmashauri za Wilaya za Kyela, Muheza, Mkuranga, Monduli, Same, Mbulu, Simanjiro, Tunduru, Dodoma (Bahi na Chamwino), Kilwa, Mikindani, Ludewa na Halmashauri zote za Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu ilijielekeza vilevile katika kusimamia utunishaji na ukuaji wa Mfuko wa Wanawake na Vijana ambapo kimsingi Kamati yangu katika vikao vyake vya nyuma ilikwisha agiza kwamba Halmashauri zote ambazo hazikutekeleza kikamilifu maelekezo na agizo lililotolewa na Serikali kwa Halmashauri zote nchini kutenga kutoka katika mapato yake asilimia 10% kwa mwaka 2000 na asilimia 5% kwa mwaka 2003, zitenge kwenye bajeti zake fedha wanazodaiwa katika kuchangia mfuko huo wa Mikopo na pindi zinapopatikana kuziweka kwenye Mfuko huo kwa lengo la kuwezesha vikundi vya Wanawake na Vijana kupata mikopo kwa ajili ya kujikomboa na umaskini. Aidha, Kamati imekuwa ikiagiza Halmashauri zinazoshindwa kumalizia kikamilifu michango yake kwenye Mfuko huo, kukiri au kuonyesha wazi wazi wakati wanapofunga Hesabu zao za Mwaka kuwa zinadaiwa.

Mheshimiwa mwenyekiti, Kwa mwaka wa fedha wa 2006/2007 ulipaji wa deni kwa Halmashauri ambazo hazikumalizia michango yake katika Mfuko huo ulikuwa wa kiwango cha chini sana. Hivyo, Kamati imeagiza Halmashauri zote zinazodaiwa kumaliza madeni yao ifikapo tarehe, 30 Decemba 2009. Aidha, Halmashauri zimeagizwa kuandaa utaratibu mzuri wa kusimamia ukusanyaji wa marejesho ya mikopo inayotolewa kwa Wanawake na Vijana ili Mfuko uwe endelevu ikiwa ni pamoja na kuingia kwenye mkataba na Serikali za Vijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia ilitoa maelekezo kuwa Halmashauri zote zitenge asilimia 20% kutoka kwenye ruzuku inayotolewa na Serikali kama fidia ya mapato, na fedha hizo zipelekwe kwenye Vijiji kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ya Vijiji hivyo. Fedha hizi ni zaidi ya fedha zinazopelekwa na Halmashauri kama matumizi ya kawaida ya Vijiji katika kufuatilia, kusimamia na kuchangia miradi hiyo kama Halmashauri. Kamati imegundua kuwa Halmashauri nyingi hutenga fedha pungufu kutoka kwenye fidia wanayopata na kuendelea kutumia fedha iliyobaki kwa shughuli nyingine, hivyo kusababisha deni kuwa kubwa sana kiasi cha kushindwa kulilipa. Kamati yangu imeziagiza Halmashauri zote kuweka mikakati ya kulipa madeni yatokanayo na maelekezo hayo ya Serikali na yawe yamelipwa yote ifikapo Decemba 31, 2009. Pamoja na mapungufu hayo kuonekana karibu katika kila Halmashauri, Kamati inaipongeza



Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto kwa juhudi zake za kupeleka fedha kamili (20%) katika Vijiji vyake vyote kwa miaka yote ya nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unaonyesha kuwa wananchi ni wepesi sana kuchangia kwenye miradi ya maendeleo inayobuniwa na wao wenyewe. Aidha, wananchi pia ni wepesi wa kulipa ushuru na michango mbalimbali kama wataelezwa na kupata Taarifa kamili michango yao hiyo imetumikaje. Hivyo, Kamati inapenda kuwapongeza wananchi wanaochangia miradi yao ya maendeleo nchi nzima na kuziagiza Halmashauri kuhakikisha zinawahamasisha wananchi katika uibuaji na uchangiaji wa miradi ya maendeleo na wakati huo huo kuweka utaratibu mzuri wa kuwarejeshea Taarifa kamili ya jinsi fedha zao zilivyotumika katika utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na utegemezi mkubwa uliopo wa Mamlaka hizi kwa Serikali na wepesi wa wananchi katika uibuaji na uchangiaji wa miradi ya maendeleo, ni vyema Serikali ikahakikisha kuwa fedha za miradi ya maendeleo zinatolewa mapema kama ilivyopangwa katika Bajeti ya mwaka husika ili zitumike kukamilisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati. Aidha, ni muhimu fedha hizo zikatolewa mapema na kwa wakati muafaka, kwa maana katika Halmashauri nyingi ambazo Kamati ilikagua Hesabu zake, imejidhihirisha kuwa kinachosababisha miradi mingi ya maendeleo kutokamilika ukiachilia uzembe uliopo katika usimamizi wa miradi, ni kuchelewa kwa fedha za utekelezaji wa miradi kutoka Serikali. Hivyo ni vizuri Serikali ikaweka mikakati mizuri ya kuondoa tatizo hili ambalo kwa kiasi kikubwa linachangia kurudisha nyuma maendeleo ya Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yatokanayo na Ziara za Ukaguzi wa Miradi. Wajumbe wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa walifanya ziara kwenye Halmashauri za Mikoa kumi na moja (11) katika vipindi tofauti. Kamati ilifanikiwa kuona Miradi ipatayo 307; ambapo mgawanyo wake ni kama ifuatavyo, Mkoa wa Tanga miradi 54, Mkoa wa Kagera miradi 40, Mkoa wa Kigoma miradi 28, Mkoa wa Mara miradi 31, Mkoa wa Rukwa miradi 20, Mkoa wa Mwanza miradi 32, Mkoa wa Morogoro miradi 43, Mkoa wa Kilimanjaro miradi 21, Mkoa wa Manyara miradi 13, Mkoa wa Mbeya (*H/W ya Kyela*) miradi tisa na Mkoa wa Arusha miradi 16. Utekelezaji wa Miradi hiyo umechangiwa kwa viwango tofauti na Serikali, Nguvu za Wananchi, Halmashauri, na Wahisani mbalimbali. Miradi hiyo imegawanyika katika makundi mbalimbali kama ifuatavyo:-

- (a) Miundo Mbinu - Barabara zilizo chini ya Halmashauri zinazotengenezwa kwa fedha za *Road Fund*, *TASAF* na kadhalika;
- (b) Elimu - Vyumba vya Madarasa na Nyumba za Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari zimetengenezwa kupitia fedha za *MMEM*, *MMES*, *TASAF*, Nguvu za Wananchi na Halmashauri zenyewe;
- (c) Afya - Ujenzi na Ukarabati wa Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali kwa Fedha toka *Basket Fund*, *TASAF* na kadhalika;

- (d) Kilimo - Miradi yote ambayo imegharamiwa kupitia Halmashauri za Wilaya kwa fedha za Wahisani, Halmashauri au Serikali Kuu kupitia *DADPS, Capital Development Grant na PADEP* ikiwemo ile ya Umwagiliaji;
- (e) Maji - Miradi ambayo imetekelezwa kwa kutumia fedha za Halmashauri, Serikali Kuu na Wahisani; na
- (f) Miradi mingine yoyote ambayo kwa namna moja au nyingine imetekelezwa na Halmashauri za Wilaya kwa fedha za Wahisani mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; Miradi ya sekta ya miundo mbinu. Kamati ilifanikiwa kutembelea miradi thelathini na tano (35) ya sekta ya miundombinu zikiwemo barabara na madaraja. Katika Mikoa ya Tanga na Kagera, Kamati iliridhishwa na miundo mbinu ya barabara jinsi zilivyotengenezwa kwa kulinganisha kiasi cha fedha kilichotolewa na kutumika, na kwa jinsi zinavyotunzwa. Kwa ujumla miumbombinu iliyotengenezwa katika Halmashauri zetu inakidhi viwango vinavyokubalika na kuonyesha thamani halisi ya matumizi yaliyoonyeshwa kwenye taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati kwa maana ya Value for money. Kamati iliridhishwa na viwango vya utengenezaji wa barabara na madaraja mengi, hata hivyo katika baadhi ya maeneo, miundombinu ya barabara inahitaji matengenezo makubwa kutokana na kuharibiwa na mvua kubwa zinazonyesha wakati na baada ya matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni miradi ya barabara ambayo Kamati haikuridhishwa na jinsi ilivyokuwa imejengwa:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kahororo – Mugeza katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba – Barabara haina *Calvert* za kutosha kuweza kuilinda ili idumu kwa muda mrefu lakini pia mifereji (*drainage system*) haifanyiwi usafi hivyo kusababisha maji kukwama kutokana na mrundikano wa uchafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya *NMC Fire-PPF* katika Halmashauri ya Manispaa ya Arusha – Ujenzi wa barabara hii umegharimu kiasi cha shilingi milioni 152 na una lengo la kupunguza msongamano wa magari mjini lakini barabara haina mitaro/mifereji ya kupitishia maji machafu (*drainage system*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kisawasawa–Mpanga, Ujenzi wa daraja katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero, Daraja ni madhubuti lakini halina kingo (*guide rails*) za pembeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kitisa Mamboleo – Kwemkunde (*km 4.1*) iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza – Barabara ilifanyiwa matengenezo ya kawaida yaliyogharimu kiasi cha shilingi milioni 5.8 kwa kusafisha barabara, kuchimba mifereji, kuchomelea bomba kwenye daraja na kupaka rangi kingo za nguzo za daraja,

lakini Kamati ilipotembelea daraja hilo haikukuta bomba zozote katika daraja hilo na hakukuwa na rangi katika kingo za daraja kwani ilikuwa imebanduka. Aidha barabara karibu na daraja ilikuwa imemeguka na ilishauriwa hatua za haraka zichukuliwe ili kuepusha barabara kukatika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mpirani/Chongoleani (*km 10*) iliyopo katika Halmashauri ya Jiji la Tanga – Ujenzi wa barabara hii uligharimu kiasi cha Shilingi milioni 54 ingawa kazi iliyofanyika ni ya kiwango cha chini. Barabara ni nyembamba sana, Kalvati zimeanza kubomoka, barabara haitunzwi wala majani hayafyekwi. Ni muhimu kwa Halmashauri kusimamia utunzaji wa barabara hii na ikiwezekana kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa barabara ili waweze kukubaliana na upanuzi wa barabara hiyo kwani ni nyembamba sana.

Mheshimiwa mwenyekiti, Barabara ya Stakishari – Mwandusi (*km 6.8*) iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga - Sehemu korofi katika Barabara hii zilitakiwa kufanyiwa matengenezo ikiwa ni pamoja na kujenga Kalvati lenye urefu wa mita 6 na kipenyo cha mm 600 pamoja na ujenzi wa kuta zake zenye mita za ujazo mbili kwa jumla ya shilingi milioni 10.6 kama ilivyooneshwa kwenye Kitabu cha Hesabu. Cha kusikitisha ni kwamba pamoja na fedha kuonekana zimetumika Halmashauri ilishindwa kuithibitishia Kamati uwepo wa Kalvati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi hii ya barabara imetengenezwa katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 ikiwa inagharimiwa kwa fedha za Halmashauri na *Road Fund*. Kwa ujumla barabara nyingi hazikuwa na Kalvati za kutosha kuweza kuzilinda ili zidumu kwa muda mrefu lakini pia baadhi hazikujengewa mifereji (*drainage system*) au kama imejengewa haifanyiwi usafi wa mara kwa mara hivyo kusababisha maji kukwama kutokana na mrundikano wa uchafu na baadhi ya Madaraja hayakuwa na kingo (*guide rails*). Hivyo Kamati imeagiza Halmashauri kuhakikisha zinatenga fedha kwenye bajeti za kila mwaka kwa ajili ya kuzifanyia barabara matengenezo ya mara kwa mara (*Routine Maintenance*) ili kuokoa barabara hizi zisiharibike na Wahandisi wawe makini katika utoaji wa '*Certificates*' kwani husababisha Wakandarasi kulipwa wakati kazi iliyofanyika haina ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Sekta ya Elimu. Kamati ilifanikiwa kutembelea miradi Sabini na Nane (78) ya Elimu. Miradi hiyo inahusu Shule za Msingi (Madarasa na Nyumba za Walimu) na Shule za Sekondari (Madarasa, Mabweni na Nyumba za Walimu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla kuna tatizo kubwa la kutofuata miongozo ya kitaifa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na hivyo kufanya miradi mingine kukosa fedha za kuikamilisha, au kutekelezwa chini ya viwango vilivyokusudiwa. Baada ya kutembelea miradi ya sekta ya Elimu, Kamati haikuridhishwa na ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu katika maeneo mengi hasa kwenye Shule za Msingi. Ujenzi wa madarasa katika Shule nyingi zilizojengwa chini ya usimamizi wa Halmashauri haukufuata miongozo na ramani sahihi zilizotolewa na Serikali ambapo Halmashauri nyingi katika ujenzi wa madarasa hazikuzingatia ramani iliyoko kwenye

Mpango wa *MMEM*, Madarasa mengi yamejengwa kwa kutumia ramani ya zamani ambayo kimsingi hatoi mwanga wa kutosha ndani na kuwa na madarasa madogo. Ujenzi wa madarasa mengi umekiuka taratibu za kihandisi kwa maana yameezekwa kwa mabati ya geji 30 badala ya geji 28 na baadhi ya madarasa yamejengwa kwa udongo bila ya kutumia Saruji hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni miradi ya ujenzi wa madarasa ambayo Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wake pamoja na kuwa fedha zimetolewa na kuonyeshwa kuwa zimetumika:-

Ujenzi wa madarasa mawili katika Shule ya Msingi Nengo iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo- Ujenzi wa madarasa haya haukufuata ramani iliyotolewa na mpango wa *MMEM* na bado hayajakamilika kwa maana hayajapauliwa, hayajawekwa plasta, hakuna milango wala nyavu za madirisha. Ujenzi wa madarasa mawili katika Shule ya Sekondari Makitutu iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe - Ujenzi wa madarasa hayo haukutumia ramani iliyotolewa na mpango wa *MMES* na kuta za madarasa zilikuwa na nyufa kubwa. Ujenzi wa madarasa 2 na Ofisi ndogo katika Shule ya Sekondari Zakia Meghji iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo - ujenzi haujakamilika hadi sasa ingawa Sh. 21.2m zilitengwa na kutumika kutoka *LGCDG* na Shilingi milioni 8.1 kutoka kwa wananchi, madarasa hayana “*ceiling bord*” na madirisha hayana voo. Taarifa ya matumizi ya fedha ya ujenzi huo haukuridhisha, hivyo Kamati ililazimika kuwasiliana na Ofisi ya *CAG* ili kukagua Hesabu za mradi huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa madarasa nane katika Shule ya Sekondari Kajunjumele iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela- Halmashauri ilipata jumla ya shilingi milioni 43 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa hayo nane na nyumba tatu za Walimu, lakini baadhi ya madarasa yalikuwa hayajakamilika na haikueleweka darasa 1 lilitumia kiasi gani cha fedha. Katika Ujenzi huu taratibu nyingi za kihandisi hazikufuatwa, nondo zilizotumika ni za milimita 12 badala ya milimita 16 kama ilivyoandikwa kwenye Kitabu cha Hesabu cha Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa madarasa katika Shule ya msingi Haysam iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati - Ujenzi wa shule hii ulianza tangu mwaka 2002 na mpaka kufikia mwaka 2007 jumla ya shilingi milioni 6.56 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matano na jengo la Ofisi. Kamati ilipotembelea shule hiyo, ilibaini kuwa Madarasa yote hayajakamilika ingawa wananchi wamechangia na Halmashauri imekuwa ikipeleka fedha tangu mwaka 2002, Madarasa hayana sakafu, shata na *frame* za milango na madirisha. Kwa ujumla, Halmashauri ya Wilaya ya Babati ina madarasa 135 katika shule za msingi ambayo hayajapauliwa kabisa kitu ambacho ni hatari kwa usalama wa Wanafunzi. Hata hivyo, katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 Halmashauri imeweka katika mpango wa kupauwa madarasa 18 tu kati ya 135 na kuihakikishia Kamati kuwa, kwa miaka ijayo, asilimia 40 ya fedha toka *LGCDG* ziendazo vijijini, zitatumika kumalizia madarasa ya shule za msingi kwenye vijiji husika. Kamati imeagiza

Halmashauri kuandaa mpango kazi (*Action plan*) wa kumalizia madarasa ya shule za msingi ili wanafunzi wasome katika mazingira yanayoridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la ujenzi wa madarasa kutokamilika limeonekana sana pia katika shule ya Sekondari ya Kiomoni na Shule ya Sekondari ya Masechu zilizopo katika Halmashauri ya Jiji la Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa madarasa, jengo la utawala, bwalo la chakula na nyumba ya Mwalimu katika Shule ya Sekondari Nanja iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Ujenzi wa shule hii ulianza mwaka 2006 kwa kushirikisha nguvu za wananchi kwa Serikali za vijiji husika. Katika ujenzi wa jengo la Utawala kiasi cha shilingi milioni 35.4 kilitengwa na *Tanzania Wildlife Conservation Fund (TWCF)* ikaahidi kuchangia shilingi milioni 20 ambazo mpaka Kamati inakagua zilikuwa hazijapelekwa kwenye shule ingawa zilipelekwa Halmashauri na kuwekwa kwenye akaunti ya Amana na baadaye kutumika kwa shughuli nyingine ambayo Kamati haikuweza kupatiwa ufafanuzi wa kuridhisha. Hivyo ujenzi wa shule hiyo bado haujakamilika kwa sababu ya matumizi mabaya ya fedha na usimamizi hafifu ambao ulisababisha Bwalo la chakula lililojengwa kuanguka. Aidha, Kamati ilibaini upotevu wa takriban shilingi milioni 94 kwenye akaunti hiyo ya Amana, suala ambalo Kamati inalifuatilia kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa darasa katika shule ya watoto wenye mahitaji maalum ya Uvinza iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma - Kamati ilitembelea shule hiyo na kukuta darasa hilo bado halijakamilika, kwani vifaa vimenunuliwa na Halmashauri lakini mchango wa wananchi haujapatikana. Pamoja na tatizo hilo shule haina *Patron* wala *Matron* kwa ajili ya kuwaangalia watoto hao wenye mahitaji maalum. Kamati imeagiza ujenzi huo ukamilike kwa Halmashauri kuwahamasisha wananchi kuchangia na vilevile Kamati inapenda kuwasihia wananchi wote wenye moyo wa kujitolea kuichangia shule hiyo ili watoto hao wenye mahitaji maalum wapatao 75 wapate elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa madarasa katika Shule ya Sekondari Sitalike iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda, ujenzi wa madarasa haujakamilika na bati 33 za darasa zimeezuliwa na upepo mkali, hivyo ukarabati wa hali ya juu bado unahitajika katika shule hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iligundua kuwa Nyumba nyingi za Walimu zilizotolewa taarifa katika vitabu kuwa zimekamilika na Walimu wakiwa wanaishi humo, hazikuwa zimekamilika na ramani hazikuzingatiwa. Nyumba nyingi zina jengo la kulala tu bila kuwa na choo, jiko, bafu na stoo kama michoro inavyoonyesha. Lakini pia Kamati iligundua kuwa katika mchoro unaotumika kujenga nyumba hizo za kuishi umepitwa na wakati kwa walimu ambao wana familia ya wavulana na wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni miradi ya ujenzi wa nyumba za Walimu na mabweni ya kulala wanafunzi ambayo Kamati haikuridhishwa na utekelezaji wake:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Nyumba tatu za Walimu katika Shule ya Sekondari ya Kajunjumele iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela – Kama nilivyosema awali kwa mwaka wa fedha 2006/2007, Shule hii ilitengewa shilingi milioni 43 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa nane na Nyumba tatu za Walimu. Kamati ilipotembelea shule hiyo Mwezi Juni, 2008 ilibaini kwamba nyumba hizo tatu za Walimu hazikujengwa kwa kisingizio cha kuwepo kwa mafuriko yaliyoziua hata kuanza ujenzi huo katika kipindi cha miaka yote miwili iliyopita. Aidha, kamati ilipohoji fedha zilizotengwa kwa shughuli hiyo zilitumikaje, ilijibiwa kuwa vifaa vimenunuliwa na viko dukani. Hakuna ushahidi uliotolewa kuwa kweli vifaa hivyo vimenunuliwa na kuhifadhiwa dukani kwa kipindi chote cha miaka miwili. Huu ni uvunjaji wa taratibu za manunuzi zilizowekwa kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa nyumba mbili za walimu, Shule ya msingi Migombani iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli. Kitabu cha Hesabu za Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2006/2007 kimeonyesha kuwa ujenzi wa nyumba hizo mbili za walimu uliharimu kiasi cha shilingi milioni 31. Kamati ilipotembelea Shule hiyo, Mwalimu Mkuu alieleza Kamati kuwa, ujenzi wa nyumba hizo umefanyika kwa msaada wa *TANAPA* ambayo ilitoa kiasi cha shilingi milioni 13.8. Hata hivyo, Watendaji wa Halmashauri walipinga maelezo ya Mwalimu huyo na kusema nyumba hizo zimejengwa kwa kutumia fedha za *MMEM* na nguvu za Wananchi. Kutokana na mapungufu mengi yaliyoonekana katika Hesabu zao, Kamati ililazimika kuirudisha mbele ya Kamati kwa mara ya pili *H/W* ya Monduli tarehe 9 Aprili, 2009 ambapo katika kikao hicho Taarifa ya Wakaguzi ilionyesha kukiri kwa Halmashauri hiyo, kuwa ujenzi wa nyumba hiyo ya mwalimu ulitekelezwa kwa kutumia fedha ya *TANAPA*. Hivyo, mpaka sasa Kamati inasubiri ripoti ya ukaguzi ya *NAO* ili iweze kujua Fedha za Serikali zilitumika kwenye shughuli gani kama hazikutumika katika ujenzi wa nyumba hiyo. Aidha, Kamati yangu itahakikisha inapata ufumbuzi na usahihi wa suala hili linaloashiria dalili za upotevu au ubadhirifu wa fedha za umma. Ujenzi wa Nyumba za Walimu katika Shule ya Msingi Mshikamano iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma – mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi milioni 19 na bado haujakamilika. Nyumba haina choo wala bafu, haina jiko, haijasakafiwa na thamani yake ni ndogo ukilinganisha na kiasi cha fedha kilichotumika. Kamati iliagiza Halmashauri kuhakikisha nyumba hiyo inakamilika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa nyumba tatu za Walimu katika Shule ya Msingi Igekemaja iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Magu – Kwa mwaka wa fedha 2006/2007 shule ilitengewa shilingi milioni 29 toka *TASAF* na shilingi milioni 4.5 toka nguvu za Wananchi. Lengo lilikuwa ni kujenga nyumba 1 ya Mwalimu na nyumba nyingine mbili zilizounganishwa kwa pamoja (*Two in One*). Mradi mpaka sasa haujakamilika na nyumba zina vyumba viwili badala ya vitatu. Mbao zilizotumika kwenye madirisha na milango sio imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa bweni la wasichana Shule ya Sekondari Engutoto iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, ujenzi wa jengo hilo ulianza mwaka 2006 kwa msaada wa Shirika la *PANSIASI TOURS* na limegharimu hadi sasa kiasi cha shilingi milioni 60. *Hostel* ina sehemu tatu na moja ndio inatumika hadi sasa.

Baada ya Kamati kutembelea jengo hilo ilibaini kuwa limejengwa chini ya kiwango na sakafu ina nyufa kubwa. Hivyo, Kamati inatilia mashaka usalama wa wanafunzi kwa maana siku yoyote bweni hilo litaporomoka kutokana na ukubwa wa nyufa zilizopo. Kamati iliagiza Halmashauri kufanya uthamini wa kina kuhusina na ujenzi wa jengo hilo kwa kushirikiana na ofisi ya Mkuu wa Mkoa kwa kupeleka Wataalam wa ujenzi, Wathamini Majengo na Wakaguzi wa ndani na Taarifa kupeleka Ofisi ya Ukaguzi kwa uhakiki. Kamati inafuatilia utekelezaji wa agizo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Bweni katika Shule ya Sekondari ya Kasanda iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo - Ujenzi wa bweni umekamilika isipokuwa hakuna vitanda, *ceiling board*, ngazi za kuingilia, jiko la kupikia na hakuna mwalimu wa kike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa bweni katika Shule ya Sekondari ya Kalangasa iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, ujenzi wa bweni umekamilika lakini halijaanza kutumika. Aidha, pamoja na kukamilika kwa bweni hilo Kamati haikuridhishwa na mbao zilizotumika katika shata za madirisha na milango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Aidha Kamati yangu ilibaini matatizo makubwa yanayozikabili shule hizo ni kama ifuatavyo:-

- Upungufu wa Walimu;
- Upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia;
- Upungufu wa matundu ya vyoo;
- Kucheleweshwa au kutolipwa kwa malipo/madai ya Walimu; na
- Upungufu wa Nyumba za Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kutokana na mapungufu yote tuliyoyaainisha, agizo la jumla kwa Wakurugenzi wote limekuwa kwamba Shule zitakazojengwa sasa zizingatie mchoro wa *MMEM* ambao ndio mchoro mpya uliotolewa na Wizara kwa madarasa yote na Nyumba za Walimu zinazojengwa sasa ziwe na vyumba vitatu vya kulala. Aidha, wananchi wahamasishwe kuchangia ujenzi wa Madarasa na Nyumba za Walimu kwani ndizo zitafanya Walimu wakae na kufundisha. Serikali nayo iwe na mpango madhubuti wa kupeleka kwa wakati fedha za *MMES* na *MMEM* ili kuzingatia ubora wa Shule kwa lengo la kutumika kwa miaka mingi ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya sekta ya afya. Kamati ilifanikiwa kutembelea miradi Arobaini na Saba (47) ya Afya. Miradi hiyo ilihusu ujenzi na ukarabati wa Zahanati, Vituo vya Afya, Ofisi na Wodi mbali mbali, Ujenzi wa Bohari la Madawa na jengo la *X-ray* katika Hospitali za Wilaya kwa kutumia Fedha kutoka *Basket Fund*, *TASAF*, *Capital Development Grant*, Nguvu za Wananchi na fedha toka vyanzo vya Halmashauri na fedha za Wahisani. Baadhi ya miradi imetekelezwa kwa kiwango

kinachokubalika na thamani yake imeonekana. Na mahali pengine ni mifano ya kuigwa na Halmashauri nyingine nchini. Sehemu ambazo zimekuwa ni Kivutio na mifano ya kuigwa ni:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa umeme wa Biogas katika Hospitali ya Wilaya ya Kasulu ulifanyika katika mwaka wa fedha 2006/2007 na kugharimu kiasi cha shilingi milioni 131 kutoka katika fedha za ruzuku ya maendeleo (CDG). Kamati iliridhika na kiwango cha utekelezaji wa mradi huo na ubunifu wa Halmashauri hiyo katika kutatua tatizo la umeme katika Hospitali ya Wilaya. Pamoja na jitihada zote hizo, umeme huo wa asili bado hautoshi hivyo Halmashauri imelazimika kuingia mkataba wa kununua Jenareta kwa Shilingi milioni 46 toka kwa Mkandarasi aitwaye *General Enterprises*. Aidha, Halmashauri imetenga jumla ya shilingi milioni 46 kwa ajili ya ununuzi wa jenereta hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa ujenzi wa jengo la *X-ray* katika kituo cha Afya Butimba kilichopo katika Halmashauri ya Jiji la Mwanza. Mradi huu umegharimu kiasi cha shilingi milioni 54 na umetekelezwa kwa kiwango kinachoridhisha isipokuwa bado mradi haujaanza kutumika ukisubiri kufunguliwa rasmi. Maoni ya Kamati ni kuwa Mradi huu ni mfano wa kuigwa kwa Halmashauri nyingine ambapo utasaidia sana kutoa huduma ya *X-ray* ambayo awali ilikuwa ikipatikana kwa shida sana. Aidha, Kamati ilishauri jengo hilo lifunguliwe haraka bila kusubiri ufunguzi rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Wodi ya watoto katika Hospitali ya Wilaya ya Mbulu umefanyika katika mwaka wa fedha 2006/2007 na kugharimu kiasi cha Tshs 65m/= kutoka katika fedha za ruzuku ya maendeleo (CDG). Kamati iliridhika na kiwango cha ujenzi wa wodi hiyo hasa kutokana na jinsi wodi ilivyojengwa kwa kufuata taratibu zote zinavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni baadhi ya miradi ya Afya iliyotekelezwa kwa kiwango cha chini na kwa kutofuata utaratibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Jengo la Upasuaji (*Theater room*) na *Surgical Ward* – Kituo cha Afya cha Karume katika Hospitali ya Wilaya ya Rombo - Ujenzi wa miradi ya *Theater* na *Surgical ward* ilipangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2005/2006 kwa gharama ya shilingi milioni 25 kwa kila mradi. Miradi hii haikuweza kutekelezwa katika kipindi hicho kutokana na kuchelewa kufika kwa fedha hizo. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Halmashauri ilitangaza Zabuni kwa miradi hiyo na mkandarasi hakuweza kupatikana kwa kuwa bei ya vifaa ilikuwa imepanda. Suala hili lilirudishwa kwenye vikao vya Halmashauri ili kulipatia uamuzi wa namna ya kulitekeleza. Maamuzi yaliyofikiwa katika mwaka wa fedha 2008/2009 ni kutumia “*Force Account*” kutekeleza mradi huo, kitu ambacho ni kinyume na taratibu za matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotembelea miradi hiyo ilibaini mambo yafuatayo:-



Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *Theater* upo katika hatua ya msingi na mradi wa *Surgical Ward* utekelezaji haujaanza na hata eneo halijulikani. Gharama za kutekeleza kila mradi zimepanda kutoka shilingi milioni 25 hadi shilingi milioni 45. Ujenzi wa msingi wa *Theater* haukuzingatia taratibu za kihandisi kwa kuweka mota ya udongo katika mawe badala ya saruji. Mchakato wa kutoa maamuzi umechukua muda mrefu takriban mwaka mmoja na nusu hivyo kusababisha gharama kupanda kutokana na kushuka thamani ya shilingi. Aidha, iligundulika kuwa ucheleweshaji wa mradi ulitokana na urasimu uliopo wa viongozi na tabia ya kutopenda kufuata taratibu za zabuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukarabati Hospitali ya wilaya Tarime iliyopo katika Kata ya Bomani – Kwa mwaka wa fedha 2006/2007 jumla ya Sh 200m zilitengwa kwa ajili ya Ujenzi wa chumba cha kuhifadhia maiti na ukarabati wa jengo la upasuaji, Wodi mbili, Chumba cha dawa (*Pharmacy*) na Masijala. Hata hivyo, chumba cha kutunzia maiti hakijaanza kutumika, sakafu kwenye jengo la upasuaji ina nyufa kubwa na kwa ujumla Hospitali ni chafu. Hivyo, thamani ya fedha zilizotumika haionekani katika ukarabati uliofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa jengo la upasuaji Kituo cha Afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda - Kamati ilitembelea jengo na kukuta limekamilika isipokuwa halijaanza kutumika. Kamati ilipokagua, ilibaini kuwa jengo lina nyufa kubwa sakafuni na ukutani na hakuna barabara ya uhakika kuingia kituoni hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Ofisi ya *DMO* katika Hospitali ya Wilaya ya Muheza – Mradi uligharimu jumla ya shilingi milioni 43.6 kutoka katika fedha za ruzuku ya maendeleo (*CDG*) katika mwaka wa fedha wa 2006/2007. Mradi umekamilika na jengo linatumika isipokuwa gharama na vipimo vilivyoonyeshwa kwenye kitabu zinaonekana kuongezwa (*inflated*) ukilinganisha na hali halisi. Kwa mfano, jengo lina mita za mraba 500 tu lakini *Ceiling Board* zilizoonyeshwa kwenye kitabu zina mita za mraba 1,300 jambo linaloonyesha dhahiri kuwa hakuna ukweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Zahanati ya Kinonko iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro - Ujenzi wa zahanati ulianza mwaka 2000 kwa nguvu za wananchi na Halmashauri ilichangia jumla ya shilingi milioni 16.8. Kamati ilipotembelea Zahanati hiyo, ilibaini kuwa ujenzi wa jengo hilo haujakamilika, ni wa kiwango cha chini, haukufuata ramani ya Wizara, hakukuwa na mpango kazi unaonyesha mkakati wa kukamilisha ujenzi huo, Mhandisi hakushirikishwa au hasimamii kikamilifu utekelezaji wa miradi ya ujenzi (*Poor Supervision*) na Halmashauri ilipeleka vifaa vya ujenzi bila kufanya tathmini ya kina ili kubaini ni aina na kwa idadi gani vifaa vinahitajika. Aidha, Kamati iliwasiliana na Wakaguzi ili kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha katika mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Hanang’ - Kamati ilitembelea Hospitali ya Wilaya ya Hanang’ na kukagua usafi wa wodi, vyoo na utoaji wa huduma hasa madawa. Katika ukaguzi huo Kamati ilibaini kuwa kuna tatizo la utawala katika Hospitali hiyo, hakuna *Laundry* na badala yake wanatumia sehemu ya kuogea katika Wodi ya watoto ambapo athari yake ni ongezeko la magonjwa ya kuambukiza, vitanda

vya wagonjwa havina mashuka, vyoo katika wodi havitumiki isipokuwa choo kimoja kilichopo katika wodi ya wazazi, hospitali haina maji japo Mji wa Katesh unao mradi mkubwa wa maji, wodi zilikuwa chafu na hakuna Stoo, hivyo vifaa na mashuka machafu yamerundikwa katika Ofisi ya Muuguzi Mkuu. Kamati iliagiza Halmashauri kuhakikisha hospitali inapewa upendeleo maalum wa kupatiwa maji na isiingizwe katika mgao wa maji, Usafi uzingatiwe, ijengwe *Reserve Tank* kubwa, *Laundry* ihamishwe mara moja kwenye wodi ya watoto na kuweka uzio kuzuia wizi na Mkaguzi wa ndani afanye uchunguzi wa madeni na upatikanaji wa madawa kutoka *MSD* na kupeleka kwa Wakaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Geita, ukarabati wa jengo la upasuaji katika Hospitali ya Wilaya ya Geita uligharimu kiasi cha shilingi milioni 13 umefanywa bila usimamizi wa kitalaam hali inayofanya majengo hayo kuonekana chakavu kutokana na kubomoka kwa kuta, sakafu na milango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukarabati wa kituo cha Afya Mafiga kilichopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Ukarabati wa kituo hicho ulianza mwaka 2006/2007 kwa Halmashauri kutenga kiasi cha shilingi milioni 8.5. Ukarabati umefanyika, viyoyozi viwili vimenunuliwa isipokuwa Kamati ilibaini kuwa kati ya nakshi 90 zilizoripotiwa kwenye kitabu ni nakshi 32 tu ndizo zilizowekwa, radio ya upepo haina matunzo ya kutosha na kuna uwezekano mkubwa wa kugharimu fedha za matengenezo pindi itakapoharibika. Aidha, Kamati ilipotembelea kituo haikukuta mgonjwa hata mmoja na kwa Mwezi Disemba, 2008 ni wagonjwa tisa tu walitibiwa. Kwa hali hii inaelekea kwamba kituo hicho kimetelekezwa na thamani yake haionekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa zahanati ya Longuo B iliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi – Ujenzi ulianza mwaka 2006 lakini bado haujakamilika na umeishatumia jumla ya Shilingi milioni 20. Kazi zilizofanyika hadi sasa ni sawa na 40% ya lengo. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, hakuna fedha iliyotengwa kwa ajili ya kazi hiyo, 2008/2009 Halmashauri imetenga shilingi milioni 15 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Zahanati hiyo. Kamati ilitilia mashaka kiasi hicho cha fedha kilichotengwa na kazi iliyobakia. Aidha, kutokana na udogo wa vyumba, Kamati ilihoji na kubaini ujenzi haukufuata ramani iliyotolewa na Wizara ya Afya na ilijidhihirisha kuwa Ujenzi wa Zahanati hiyo umetelekezwa kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa wodi ya Wazazi katika Hospitali ya Chato iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo, katika mwaka wa fedha 2006/2007 mradi uligharimu jumla ya shilingi milioni 24.9. Hata hivyo, kazi iliyofanyika hailingani na thamani ya fedha zilizotumika kwa maana design ya jengo ni mbaya, chipping iliyopigwa haina ubora, sakafu ina nyufa nyingi, shata za milango zimejengwa kwa mbaao laini na ceiling board imeanza kuoza kutokana na popo kuwa wengi katika paa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa zahanati ya Kibiboni iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga - Ujenzi wa Choo katika Zahanati hiyo ulianza katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 kwa Halmashauri kutumia jumla ya shilingi milioni 9.3. Kamati ilitembelea mradi huo na kubaini kuwa; Sakafu ina mita za mraba kubwa kuliko

za bati, kitu ambacho si sahihi, Dari au Ceiling ina mita za mraba kubwa kuliko za sakafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Handeni iliyomo katika Kitabu cha Hesabu sio sahihi – Vifaa vya jumla ya shilingi milioni 4.5 zilisemekana kutumika katika ujenzi, ambavyo ni bati 70, kofia za bati 20 na mifuko 100 ya saruji. Aidha, Kamati ilikuta bati zilizotumika ni nne tu na mifuko 100 ya saruji kuonekana ni mingi sana ukilinganisha na kazi iliyofanyika. Hata hivyo, baada ya Kamati kuhoji, ilibainika kuwa choo kimejengwa kwa nguvu za wananchi katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, kwa hiyo gharama zilizoingizwa katika Hesabu za 2006/2007 sio sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yafuatayo ni matatizo yanayoikumba Sekta ya Afya katika ngazi ya Halmashauri. Kwanza ni upungufu wa Watumishi. Upo upungufu mkubwa wa Watumishi hasa katika Zahanati na Vituo vya Afya. Suala hili Kamati imewaagiza Afisa Tawala za Mikoza kuhakikisha linafikishwa Wizarani ili lipatiwe ufumbuzi. Mfano Zahanati ya Ifukutwa iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda haina Muuguzi Mkuu hivyo Afisa Tabibu ndiye anayefanya kazi zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lipo tatizo la miradi kutokamilika kwa wakati na kwa ile inayokamilika kuna baadhi huchelewa kuanza kutumika jambo ambalo ni kinyume na utumiaji mzuri wa rasilimali za umma. Mfano wa miradi ya sekta ya Afya ambayo imekamilika lakini haijaanza kutumika ni jengo la upasuaji Kituo cha Afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpanda na Mradi wa ujenzi wa jengo la *X-ray* katika kituo cha Afya Butimba kilichopo katika Halmashauri Jiji la Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Lakini pia limekuwa likijitokeza suala la ukosefu wa madawa na vitendea kazi kutoka *MSD*. Waganga wote wa Wilaya wamethibitisha kukosa huduma muhimu kutoka *MSD* pale zipohitajika wakati fedha zipo na hawana uwezo wa kuzihamisha ili mahitaji muhimu yawezekupatikana kutoka kwa vyanzo vingine. Kamati imeona hili kuwa ni tatizo na kuna umuhimu wa kuwasilisha Bungeni na kutafutiwa ufumbuzi. Katika Taarifa ya mwaka 2008, Kamati ilipendekeza kuwa fedha zinazotolewa *MSD* zipunguzwe ili asilimia 30% ipelekwe moja kwa moja kwenye Halmashauri na zitumike kwa vigezo vitakavyowekwa ili kuondoa ukiritimba wa kutumia *MSD* peke yake. Pendekezo hili hadi leo halijafanyiwa kazi na Serikali. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali ichukue hatua za haraka na zenye manufaa katika jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya Sekta ya Kilimo na Ufugaji. Kamati ilifanikiwa kutembelea miradi ishirini na mbili (22) ya Kilimo na Ufugaji. Kamati imeridhika na Miradi ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Ufugaji Nyuki na Ujenzi wa kituo cha kukusanyia mazao ya Nyuki katika Kijiji cha Suwa, Kata ya Mazingara iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Handeni – Mradi ulianza mwaka 1999 na mpaka sasa kuna vikundi 27 vya wafugaji wa Nyuki. Mradi una mizinga ya asili 2,500 na mizinga ya kisasa 40 ambayo inatumika kufugia Nyuki wanaouma na wasiouma. Katika mwaka wa fedha 2006/2007 jumla ya Shilingi milioni tisa zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa jengo la

kukusanyia mazao ya Nyuki ambalo lilikuwa halijakamilika pindi Kamati ilipotembelea mradi. Aidha, wanavikundi bado hawajapata soko la uhakika la kuuzia asali, hivyo ni vyema jitihada za Serikali pamoja na Wanakijiji zikaongezwa katika kupata soko la uhakika la mazao ya Nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa umwagiliaji katika vijiji vya Mangisa, Diyomati na Harsha vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu – Mradi huo ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2005/2006 na kuendelea katika mwaka wa fedha 2006/7 ambapo Halmashauri ilitenga Tshs shilingi milioni 374.7 na kutumia shilingi milioni 370.1. Kamati ilibaini kuwa mradi unasaidia sana umwagiliaji wa mazao hasa mahindi, unyweshaji wa mifugo na matumizi ya nyumbani katika vijiji hivyo vitatu, hata hivyo kuna umuhimu wa haraka kupanda miti na kupiga marufuku ulimaji wa mashamba kuzunguka bwawa ambalo ni chanzo cha maji cha mradi huo. Kamati vilevile iliweza kuona ghala la kisasa la vitunguu ambalo bado halijakamilika na mashamba ya mahindi yanayomwagiliwa kwa kutumia mradi huu. Kamati iliridhishwa na kiwango cha utekelezaji wa mradi na kuagiza Halmashauri kuhakikisha mazingira yanayozunguka bwawa yanatunzwa na sheria ndogondogo zinasimamia utumiaji wa mradi huo kwa vijiji hivyo vitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yangu haikuridhika na utekelezaji wa miradi ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Matuli Irrigation Scheme* iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro. Ujenzi wa banio na matoleo ya maji kwa ajili ya umwagiliaji kwa kuvuna maji ya mvua katika kijiji cha Matuli ulianza kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2005/2006. Mradi unategemea kuwanufaisha wakulima wapatao 95 lakini bado haujakamilika na kwa mwaka 2006/2007 umegharimu jumla ya Sh. 31,000,000/= ukiwa umefikia kiwango cha 60%. Aidha, Kamati ilibaini mapungufu yafuatayo:-

- (i) Milango 4 ndio iliyowekwa kati ya 6 iliyosemekana kuwekwa;
- (ii) Mfereji umejengwa kwa urefu wa mita 7 tu badala ya kilomita 1.5 zilizoonyeshwa katika kitabu;
- (iii) Nguzo nne zilizotumia mifuko 200 ya Saruji hazikuonekana kabisa;
- (iv) Nondo zilizowekwa ni za 10mm na si za 12mm na 16mm kama zilivyo kwenye kitabu cha Taarifa ya Mapato na Matumizi kilichowasilishwa mbele ya Kamati;
- (v) Mradi umetelekezwa kwa muda mrefu; na
- (vi) Hakukuwa na maji pamoja na kwamba mradi ni wa umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa ujumla Kamati haikuridhishwa na usimamizi na utekelezaji wa mradi huu hivyo iliagiza mradi ukamilike na kutoa huduma iliyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ukarabati wa Lambo la Dirma lililopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' - Ukarabati wa lambo lililobomoka ulifanyika katika mwaka wa fedha 2005/2006 na kugharimu jumla ya kiasi cha shilingi milioni 28 ikiwa shilingi milioni mbili bado hazijalipwa kwa mkandarasi kama fedha ya *retention*. Aidha, Kamati ilipotembelea Lambo hilo na ilikuta limekauka kabisa, hali ambayo ilisikitisha na kukatisha tamaa kwa maana fedha nyingi zilitolewa kwa nia ya kuinua maisha ya wananchi lakini mradi haufikii malengo yaliyowekwa. Kamati iliagiza Halmashauri kusimamia na kuweka utaratibu mzuri wa utumiaji wa malambo ili yasiharibike au kukauka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Uzio katika Machinjio ya Nakatunguru yaliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe, katika mwaka wa fedha 2006/2007 jumla ya shilingi milioni 11.3 zilitengwa kwa ajili ya ujenzi wa uzio kwenye machinjio hayo lakini Kamati ndogo ilipokwenda kukagua haikukuta uzio huo na haijulikani fedha hiyo imetumikaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Umwagiliaji wa Qanded uliopo katika Wilaya ya Karatu. Mradi huu uliibuliwa na Wananchi katika Mkutano Mkuu wa kijiji 2005, ukaandaliwa andiko na kufadhiliwa na Halmashauri kupitia *PADEP* kwa shilingi milioni 35 na kupata fedha mwaka 2006/2007. Mradi ulilenga kuwanufaisha vijana 240. Lakini Serikali ya kijiji bila kufuata utaratibu, ukakodisha eneo hilo kwa mkulima tajiri. Kamati yangu ilimwagiza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya (*DED*) ahakikishe mradi huo umerejeshwa kwa walengwa, na wahusika waliokiuka taratibu wachukuliwe hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Miradi ya sekta ya maji. Kamati ilifanikiwa kutembelea miradi ishirini na moja (21) ya Visima na Matanki ya Kuvunia Maji katika Halmashauri mbalimbali. Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa Miradi ya Maji ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Vituo 5 vya Maji uliyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Arusha. Kamati iliweza kutembelea kituo kimoja cha Sanawari ambacho ni kati ya vituo vitano vilivyotekelezwa kwa fedha za *TASAF* kiasi cha shilingi milioni 23 katika Kata ya Sanawari na kuridhika na utekelezaji na uendeshaji wa kituo hicho. Mradi unawasaidia sana wananchi wa Kata hiyo kupata maji safi kwa utaratibu waliojiwekea wenyewe wa kuchangia gharama ili kuendeleza mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa umwagiliaji wa Butiama uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Musoma- Mradi ulitekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2006/2007 kwa msaada toka *JICA* na kugharimu jumla ya shilingi milioni 43.5. Fedha hizo zilitumika katika ukarabati wa jengo na ununuzi wa transformer ya umeme wa kuendeshea mitambo. Aidha, kutokana na hitaji la Halmashauri la kuongezewa pump moja ya maji, *JICA* wameahidi katika mwaka huu wa fedha kutoa fedha ya kununulia pump ya kusukuma maji yenye uwezo wa kumwagilia hekali 350 za mashamba. Aidha, Kamati ilishauri Halmashauri kuongeza usimamizi wa mradi huo kwani ni msaada mkubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika baadhi ya maeneo, miradi ya maji inashindwa kukidhi mahitaji ya wananchi kutokana na utekelezaji na usimamizi mbaya:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika Halmashauri ya Wilaya ya Geita, miradi wa maji inashindwa kukidhi mahitaji ya wananchi kutokana na uchafuzi na uharibifu uliopo wa vyanzo vya maji, ambapo katika Halmashauri hii vyanzo vingi vya maji vimechafuliwa kutokana na shughuli za uchimbaji wa madini hasa yenye *mercury* unaoendelea katika maeneo hayo ya machimbo. Hivyo, ni vema Serikali ikaandaa utaratibu mzuri wa kuwasaidia wananchi wa Wilaya ya Geita ili wapate mradi mkubwa wa maji utakaowaondolea adha ya maji na hatari ya kuathiri afya zao kwa kutumia maji yasio salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa maji wa Maganjwa uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati – Utekelezaji wa mradi huu ulianza mwaka 2006/2007 na kugharimu kiasi cha shilingi milioni 33.7. Mradi wa maji una vituo sita na unahudumia wananchi wapatao 1,920 kwa kutumia Tanki lenye ujazo wa lita 90,000. Kutokana na usimamizi mbaya wa mradi, kwa sasa unatoa maji kidogo sana ambayo hayakidhi mahitaji ya jamii iliyopo. Hata hivyo, wananchi hawaonyeshi nia ya kuuendeleza mradi kwani hawataki kuchangia gharama za uendeshaji na kutaka huduma ya maji itolewe bure.

Aidha, kutokana na *feasibility study* ya chanzo cha maji iliyofanywa awali kutokuwa nzuri ambayo ilipelekea kutumia mlima Shamna kama chanzo cha maji cha mradi, Halmashauri imebidi itenge shilingi milioni 50 kwa ajili ya kujenga mradi wa maji kwa kutumia vyanzo vya chini ili kuweza kuokoa wananchi katika tatizo kubwa la maji linaloikabiri wilaya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika Halmashauri za Wilaya za Kilindi, Handeni na sehemu nyingi za Tanzania, miradi mingi ya maji iliyofadhiliwa na Benki ya Dunia (*World Bank*) utekelezaji wake umesimama na haitoi huduma kwa sababu Halmashauri hizo bado hazijakamilisha hatua mbalimbali ambazo zingeshawishi Benki ya Dunia kuendelea kutoa fedha za kukamilisha miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla matatizo yote hayo tuliyoyatolea mfano ni kutokana na tatizo kubwa la kutofuata miongozo ya kitaifa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na hivyo kufanya miradi mingine kukosa fedha za utekelezaji, au kutekelezwa chini ya viwango vilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sambamba na tatizo hilo, pia utekelezaji wa miradi mingi hasa ile ya ujenzi katika ngazi ya Kata, haufuati ushauri wa kitaalam unaotakiwa kutolewa na Idara husika. Katika baadhi ya majengo, wahandisi hawajawahi kuonekana wala kutoa ushauri toka majengo hayo yaanze kujengwa mpaka yamepauliwa. Hali hii imechangia kwa kiasi kikubwa miradi kutokamilika katika muda uliokusudiwa ama kukamilika ikiwa katika kiwango cha chini. Kila sehemu yenye matatizo hayo Kamati

ilikemea tabia hiyo na kushauri wahusika watekeleze wajibu wao mara moja lasivyo watahesabika kushindwa kuyamudu majukumu yao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri zetu hakuna utamaduni endelevu wa kuyafanyia ukarabati wa mara kwa mara majengo ya Serikali ili yazidi kuwa imara. Hii imejidhihirisha katika majengo mbalimbali ya vituo vyetu vya afya, nyumba za walimu, masoko na madarasa ambapo majengo hayo kama si kwamba yanavuja, basi yana nyufa kubwa, yamepasuka na kutoboka sakafu au yameparuliwa rangi na kuonekana machakavu. Katika hili Kamati kila ilipopita iliwaagiza Wakuu wa Idara zenye miradi yenye kuhusika na uchakavu huo kutumia *OC* zao kuhakikisha wanafanya routine maintenance kwa miradi iliyochini yao bila kusubiri Kamati iwakague ama kuwatolea karipio au maagizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kupongeza sana Watanzania wote kwa kukubali kwao kutoa michango pale inapohitajika kwa nguvu zao zote. Hata hivyo Nguvu na michango ya wananchi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo havithaminishwi kupata uhalali wake kifedha hivyo kutowatia moyo kabisa wananchi kujiingiza katika utekelezaji wa baadhi ya miradi katika baadhi ya maeneo. Lakini pia kutothaminishwa kwa nguvu hizo kunaweza kuhusishwa na ubadhirifu kwa fedha zinazotolewa na Serikali au kwamba zinatumiwa lakini kwa kiasi kidogo sana huku mzungu mkubwa wa utekelezaji ukiachwa kwa wananchi kujitolea. Kutokuwepo kwa mchanganuo wa nguvu za Wananchi ni hatari kwani kuna hatari ya kujua kama kweli ni wananchi walitoa mchango wao au ni fedha za Serikali ndizo zilizotumiwa katika ujenzi wa mradi husika. Lakini pia katika Halmashauri zetu bado hakuna uwazi wa kutosha katika kuwaonyesha wananchi na wadau wengine wa maendeleo kiasi cha mapato na matumizi katika kila mradi na katika baadhi ya zabuni. Jambo hili huwavunja moyo wananchi na wadau wengine wa maendeleo hasa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya Halmashauri za Majiji, Miji, Manispaa na Wilaya 124, ni Halmashauri 24 tu zilipata Hati yenye shaka na Halmashauri 100 zilizosalia zilipata Hati Safi/inayoridhisha kwa Hesabu za mwaka wa fedha wa 2006/2007. Hata hivyo Kamati inategemea kufikia mwaka wa fedha wa 2008/2009 kutakuwa na Halmashauri chache sana zitakazopata Hati yenye mashaka kutokana na jitihada za kuzibana halmashauri hizo kwa njia ya kuzikagua vitabuni na zaidi kuzikagua moja kwa moja katika miradi inayotekelezwa (*value for money audit*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupata *Hati inayoridhisha*, haimaanishi kuwa Halmashauri inafanya vizuri ukilinganisha na hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Baada ya Halmashauri nyingi kupata Hati safi ndipo umuhimu wa kutembelea miradi (*Site Visitation*) unapojitokeza. Kama nilivyoainisha hapo awali, baadhi ya Halmashauri zenye hati inayoridhisha zimetumia fedha vibaya na kuandaa Hesabu ambazo hazilingani na hali halisi ya utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Halmashauri inapewa sababu zilizoifanya ipate hati chafu hivyo ni imani ya Kamati kwamba Halmashauri zote zilizotajwa kwenye

Taarifa ya Mwaka 2006/2007 ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwa zilipata hati chafu zitakuwa zimejirekebisha ipasavyo; na zile zilizopata Hati Safi zitaendelea kudumisha umakini huo katika matumizi na utayarishaji wa Taarifa za matumizi ya fedha za umma. Ili kuziba kabisa mianya ya ubadhirifu, Kamati yangu inashauri Halmashauri kuacha utaratibu wa kuwasilisha nyaraka muhimu kwa Wakaguzi mara baada ya Ukaguzi kumalizika ili zifanyiwe uthibitisho.

Utaratibu huu unatoa mwanya kwa maafisa husika kutafuta nyaraka, mathalan *Delivery, Cash sale*, na kadhalika, kuhalalisha matumizi yaliyofanyika vibaya. Hakuna sababu za msingi za Afisa mhasibu mwenye cheti kutokuwa na nyaraka zote zilizokamilika kabla ya malipo, na hizo nyaraka kuhifadhiwa katika Batch kwa ajili ya ukaguzi mara wanapofika wakaguzi. Agizo hili, linalenga kufuta kabisa matatizo yanayotokana na maeneo kama ya *Unvouched, improperly vouched, purchase on proforma invoice, not in ledger* na kadhalika.

Ni mategemeo ya Kamati yangu kuwa jitihada hizi za Kamati zitaungwa mkono na waheshimiwa wabunge wote hasa wakati wanakaa katika Kamati za Fedha katika Halmashauri zao na viongozi wote wenye majukumu ya kusimamia matumizi ya Fedha za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na yaliyoyaeleza hapo awali, Kamati inatoa ushauri kuwa mfumo wa Kamati kufanya kazi zake sasa ujikite katika kutembelea miradi ya maendeleo husika kama tulivyofanya katika kipindi cha mwaka tunaotolea Taarifa, ili Kamati ipate fursa kubwa ya kujiridhisha na yale yaliyoandikwa kwenye vitabu vya Hesabu vya Halmashauri, na vile vile kuyaona kwenye hali halisi. Ni imani ya Kamati kuwa ushauri huu utapokelewa na Bunge lako Tukufu Mheshimiwa Mwenyekiti, na Kamati kuwezesha kutekeleza jukumu lake na TAMISEMI kuendelea kushirikiana na Kamati hilo kwa ufanisi ili kuhakisha kuwa fedha zote zinazotolewa kwa miradi ya maendeleo inatumika ilivyokusudiwa. Tija ya zoezi hili ni kubwa kuliko kupitia vitabu tu wakati hali halisi ni tofauti kwenye maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapato Kutokana na Vyanzo vya Halmashauri, hali halisi katika vyanzo vya Halmashauri kidogo inasikitisha kwa sababu mapato ya Halmashauri ni kidogo sana, kwa ujumla wake mtasoma pale asilimia ya Halmashauri zetu ukilinganisha na ruzuku inayotoka Serikali kuu, average yake ni asilimia 7.5 yu kwa namba hiyo Serikali Kuu itakuwa vigumu vilevile kuondoa utegemezi wa hisani kwa sababu tutakuwa tunategemea sehemu kubwa kutoka Serikali kuu. Wakati wa uchambuzi wa Hesabu za Halmashauri, Kamati ilichunguza kwa undani mwenendo wa mapato ya Halmashauri ili kuona na kushauri ni kwa namna gani Halmashauri zinaweza kuongeza mapato yao na hivyo kuwa na uwezo wa kutekeleza malengo yaliyowekwa na wananchi wa Halmashauri hizo.

Kamati imefanya hivyo kwa imani kuwa Halmashauri yenye mapato ya kutosha ndiyo inayoweza kuwahudumia wananchi kwa kuchangia kwenye miradi inayoibuliwa na wananchi wenyewe. Kamati ilibaini kuwa malengo ya makusanyo ya mwaka yanapachikwa tu, hayafanyiwi uchambuzi wa kina kwa kuzingatia takwimu sahihi. Isitoshe, Serikali kuu imekuwa ikipeleka fedha nyingi sana kwenye Halmashauri kwa



ajili ya usimamizi na uendeshaji mzuri wa Halmashauri hizo, lakini sehemu kubwa ya fedha hizo zinatoka kwa Wahisani.

Utegemezi huu utaisha tu, iwapo kila Halmashauri zitasimamia vizuri ukusanyaji wa mapato katika vyanzo vyake vya ndani, na kubuni vyanzo mbalimbali ambavyo sasa mapato yake hayakusanywi.

Aidha, msingi wa kazi hii umeishajengwa kwani Halmashauri zimeandaa *District Profile*, ingawa kuandaa ni jambo moja na kutekeleza yaliyomo ndani ya *District Profile* ni jambo lingine. Katika kuhakikisha Halmashauri zinafanikiwa katika hili, Kamati imeagiza Halmashauri zote kuandaa Mpango Mkakati wa muda mfupi na muda mrefu ambapo katika mpango mkakati wa muda mrefu, Halmashauri zizingatie kuweka jitihada za kuhakikisha ifikapo 2025, uwezo wa kujitegemea uwe asilimia 50. Naomba tusiwe na hisia kwamba itashindikana, au hatuwezi kufikia kiwango hicho, nasema “inawezekana” na itawezekana tu, iwapo tutakuwa tayari kuwa kitu kimoja katika kuhakikisha hili linawezekana kama taifa moja. Ni muhimu kuanzia sasa wananchi na Watendaji katika Halmashauri zetu kuwa makini katika kuondoa mianya yote ya ubadhirifu na udokozi ili tuweza kukamilisha ndoto yetu ya muda mrefu ya kujitegemea kama taifa katika kuendesha shughuli za Serikali yetu kwa manufaa ya Taifa letu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Mapendekezo ya Kamati, Wakaguzi wa Nje Waanzie Katika Ngazi ya Wilaya tumependekeza hivi kwa sababu wakaguzi kwa sasa wako kwenye ngazi ya mkoa na inakuwa ni vigumu kwa wao kufanya ukaguzi katika ngazi ya wilaya. Lakini tatizo la pili ni kwamba fedha nyingi sana sasa hivi zinapelekwa kule chini na miradi inatekelezwa kwenye vijiji na vitongoji wakaguzi wanafika kwenye wilaya tu kwa sasa. Kwa hiyo unavyokuwa na mkaguzi kwenye ngazi ya wilaya sasa atatelemka chini kule ambapo fedha zipo. Na suala hili mkaguzi katika taarifa ya mwaka huu amieleza vizuri amesema kwamba wenzetu wamefanya delegation lakini wakafanya total obligation ni kopi hii kutoka kwenye sentensi ya CAG ya jana. Pamoja na ushauri au mapendekezo tuliyotoa kwenye mambo ya jumla, Kamati inapenda kuongeza mapendekezo yafuatayo ambayo inaamini yataboresha utendaji kazi kwa Halmashauri zetu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Wakaguzi wa nje wako katika kila Mkoa, na katika mkoa kwa wastani zipo karibu Halmashauri tano, Kamati imebaini kuwa kazi ya ukaguzi imekuwa kubwa sana kwao kwa sababu wako wachache. Hali hii kwa kiasi kikubwa inapunguza ufanisi wa Kazi ya Ofisi ya Ukaguzi. Hivyo, Kamati inashauri uwekwe utaratibu wa kuiwezesha Ofisi ya Ukaguzi kuwa na Wakaguzi wa nje katika ngazi ya Wilaya. Hii itasaidia kwa kiasi kikubwa, kwani Mkaguzi huyo atakuwa na jukumu la kukagua kwa umakini Hesabu za Halmashauri moja tu. Jambo hili ni la muhimu sana kutokana na fedha nyingi sana kupelekwa katika ngazi ya Wilaya na miradi mingi kutekelezwa katika ngazi ya Vijiji na Mitaa. Aidha, kama utaratibu huu utakubalika, ni vyema Wakaguzi hao wakawezeshwa na kupewa nyenzo zinazohitajika katika kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuimarisha Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, nadhani ka kuwa imeandikwa vizuri Mheshimiwa Waziri ataliangalia pendekezo hili kwa kweli bila kuimarisha kitengo cha ukaguzi wa ndani fedha nyingi sana tunazopeleka kwenye Halmashauri zitakuwa zinapotea hivi hivi na lengo hili maana yake nini, kwa kweli pendekezo hapa ni kwamba wakaguzi wa ndani wasiwe chini ya mkurugenzi, utaratibu ufanyike au wawe chini CAG ya ACG yaani Mhasibu Mkuu wa Serikali na watoe taarifa zao kule au watengenezewe line yao tofauti. Wakaguzi wa ndani katika kila Halmashauri pia inatakiwa waongezwe.

Kamati imeridhika na ajira za Wakaguzi wa Ndani, maana kila Halmashauri sasa ina Mkaguzi wa ndani. Lakini tumegundua kuwa bado Wakaguzi hawa hawafanyi kazi zao kwa kiwango kinachotakiwa. Chini ya Programu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa, Halmashauri hizi sasa zinapata fedha nyingi zinazoelekezwa kwenye miradi. Kamati imekuwa na wasiwasi kama kweli Mkaguzi wa Ndani anawezeshwa na anapata uhuru wa kutosha kufanya kazi yake kwa uadilifu na kwa kuzingatia Kanuni na Sheria zinazomuongoza. Mfano mzuri ni Wakaguzi wa Elimu ambao wako chini ya Mkurugenzi kwa masuala ya kiutawala tu, lakini uwajibikaji wao uko moja kwa moja kwa Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Marekebisho kadhaa yanaweza kufanyika katika mfumo wao wa kazi kulingana na malengo ya kazi yao. Kamati imebaini bado hilo ni tatizo kubwa, hivyo inashauri yafuatayo:-

(i) Wakaguzi wa Ndani wapewe vifaa bora vya kutendea kazi, ikiwa ni pamoja na usafiri na marupurupu mengine yatakayowafanya wasiwe ombaomba kwa Mkurugenzi;

(ii) Wakaguzi wa Ndani waongezwe katika kila Halmashauri kwani mmoja hatoshi kulingana na wingi wa kazi zilizopo na muda mdogo unaopatikana; na

(iii) Ukaguzi wa Ndani kiwe ni kitengo kinachojitegemea (kisiwe chini ya Mkurugenzi wa Halmashauri) na kisimamiwe na Wizara ya Fedha moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuimarisha Ukusanyaji Mapato, Halmashauri zinashindwa kufikia malengo ya ukusanyaji mapato kutokana na uzembe wa kufuatilia na kudhibiti wakusanyaji. Msingi wa tatizo hili ni kuwa Halmashauri kadhaa hazijafanya utafiti wa kina wa “Resource Base” yao, na hivyo hawana namna ya kufanya malinganisho wanapokutana na mawakala wasio waaminifu. Isitoshe, baadhi ya Halmashauri zilizoweka Wakala wa kukusanya, zinashindwa kufuatilia Mawakala wao, matokeo yake wanaridhika na mapato madogo yanayopatikana. Lakini pia kwa Halmashauri ambazo zinatimia Watendaji wake kukusanya mapato zinazembea kuwalipa Watendaji hao mishahara yao. Matokeo yake ni kwamba mapato mengi yanabaki ama kwa Wakala au Watendaji. Kwa mujibu wa sheria, Halmashauri zinatakiwa kuwatumia Watendaji wa Kata na Vijiji katika kusimamia shughuli zote za mapato kuanzia kwenye Vijiji, Kata na mwisho kuwasilishwa kwenye Halmashauri. Watumishi hawa ni muhimu kwa mafaniko ya Halmashauri, hivyo ni muhimu wakashiriki katika Mabaraza ya Madiwani kwa lengo la kutoa maoni katika mchakato mzima wa kupanga malengo ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuwaendeleza Watumishi Kielimu, kwa kweli ni suala tulilogundua kwamba linahitajika sana fedha nyingi tumezipoleka kwenye ngazi ya vijiji na vitongoji lakini watendaji wetu hasa ma-*VEO* na ma-*WEO* hatujawajengea uwezo wa kutosha kusimamia mamilioni ya hela ambazo zinaenda. Kijiji kwa ghafla kinapata milioni 40 milioni 100 kwa kweli ni vigumu sana wasimamie hizo hela kama hatutawajengea uwezo. Katika mahojiano ambayo kamati imekuwa ikiyaendesha katika Halmashauri zetu nyingi imebainika kuwa suala la kuwaendeleza watumishi kielimu ikiwa ni pamoja na maafisa watendaji wa vijiji (*VEOs*) na kata (*WEOs*) ni la muhimu sana na ni vizuri likapewa kipaumbele. Kamati inashauri Waajiri katika Serikali za Mitaa, kwa kuzingatia Kanuni za Utumishi wa Umma, wasikwepe wajibu huu muhimu na wa kimsingi kwa watumishi wao.

Fedha nyingi za Serikali zinazopelekwa vijijini zitaendelea kupotea iwapo watendaji, na hata Madiwani wetu hawatapewa elimu ya kutosha kutunza na kusimamia fedha hizi. Aidha, kutokana na utaratibu wa Serikali kupeleka fedha ya kutosha katika Chuo cha Serikali za Mitaa cha Hombolo, ni vyema kikatumika kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa Watendaji wa Halmashauri na Madiwani badala ya kila Halmashauri kuendesha mafunzo kwa utaratibu wao kwani lengo ni kupata mafunzo yaliyo bora na sawa kwa wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kurudisha Nidhamu ya Matumizi ya Fedha Za Umma, Kutokana na kushuka kwa uadilifu na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa majukumu ya Serikali za Mitaa kwa kuzingatia Sheria za Fedha na Sheria za Ununuzi kama miongozo ya kufanyia kazi, Kamati inashauri adhabu inayotolewa sasa ya Tozo kwa Maasifa Masuhuli wanaoshindwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo haitoshi, ni vyema wakachukuliwa hatua kubwa zaidi ikiwemo kushushwa cheo, kushitakiwa au kufukuzwa kabisa kazi kwa maana adhabu ya Tozo haifidii fedha zinazoendelea kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuongeza Mapato Kutokana Na Vyanzo Vya Halmashauri. Kama nilivyosema awali, Halmashauri zetu zina uwezo mdogo sana wa kujitegemea kifedha, na hali ilivyo sasa makusanyo katika vyanzo vingi vya mapato yamechukuliwa na Serikali kuu. Hivyo, Kamati imeshauri uangaliwe uwezekano wa kutumia utaratibu ambao wenzetu wa Japan na Nchi za Nordic wanaoutumia katika kukusanya mapato na kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, Wakati taratibu hizo zinajadiliwa kwa kina, ni vyema Mamlaka za Serikali za Mitaa zikazingatia yafuatayo:

- (a) Kuandaa mpango mkakati wa kuongeza mapato;
- (b) Kuongeza ubunifu katika kuibua miradi itakayowaongezea mapato;
- (c) Kutengeneza sheria ndogo zinazolenga kuongeza vyanzo vya mapato;

(d) Wizara inayohusika na Sheria ndogo, iondoe urasimu ulioko ambao unachelewesha sana zoezi la kuthibitisha Sheria hizo, hali inayozinyima zaidi mamlaka ya Serikali za Mitaa uwezo wa kukusanya mapato;

(e) Kuondoa kabisa upotevu wa fedha wa aina yoyote;

(f) Kushirikisha Serikali za Vijiji katika ukusanyaji wa mapato; na

(g) Kutoa elimu kwa wakusanyaji mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Halmashauri kufanya tathmini ya utimilifu wa malengo waliyojiwekea kwa muda mrefu, Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zimekuwa zikitekeleza taratibu, vigezo, viwango na sheria zilizowekwa na Serikali ikiwa ni pamoja na kufunga Hesabu zao vizuri na kuziwasilisha kwa Ukaguzi, kuhakikisha sera na miongozo iliyowekwa na Serikali inafuatwa. Kwa kifupi mamlaka hizi zimekuwa zikitumia miongozo ya Serikali kama vigezo vya ufanisi wa utekelezaji wa majukumu yao. Si nia ya Kamati kutilia mashaka utaratibu huo ambao ni mzuri, lakini ni vyema mamlaka hizo zikaendelea kujitathmini kwa kutumia miongozo ya Serikali kama viwango endapo miongozo au sera hizo zinajumuisha kwa asilimia 100 matatizo yanayozikabili jamii zetu. Kwa kuwa miongozo hiyo hajumuishi matatizo ya jamii zetu kwa asilimia 100 ni vyema mamlaka zetu zikajitathmini kwa kuangalia na kuzingatia mipango ya jamii zetu inayotoa suluhisho la matatizo yanayozikabili. Kwa kusema hivyo namaanisha kwamba ni vyema mamlaka zetu zikajitathmini kwa kutumia vigezo toka sura zote mbili, ambazo zitazingatia utimilifu wa malengo na miongozo ya Serikali na utimilifu wa malengo yaliyowekwa na jamii husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa shughuli uzingatie bajeti ya mwaka husika. Menejimenti za Mamlaka za Serikali za Mitaa zipange matumizi kwa kuzingatia fedha walizonazo kwa mwaka wa Bajeti kwa mujibu wa Kanuni ya 85(3) ya Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001 pamoja na marekebisho yake ambayo inamtaka Afisa Masuhuli kupanga matumizi kwa kuzingatia Bajeti ya mwaka husika wa fedha. Utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya mamlaka za Serikali za Mitaa lazima uzingatie bajeti ya mwaka wa fedha husika kwani kutokufanya hivyo kunaisababishia Serikali kurudia zoezi la kupeleka fedha kwa ajili ya shughuli ambayo awali ilitengewa fedha na pia mamlaka za Serikali za mitaa kushindwa kutimiza majukumu yake ikiwemo kuchelewesha ukamilifu wa miradi iliyopangwa.

Aidha, linaloshabihiana na hili ni suala la mamlaka hizi kubadili malengo ya matumizi ya fedha yaani *“reallocation of funds”* bila kupima athari itakayotokea katika utekelezaji wa miradi mingine ya maendeleo na wakati mwingine hufanya hivyo bila kupitisha maombi katika vikao vyao vya kisheria ambavyo ni *“Finance Committee”* na *“Full Council”* na au kupata kibali cha Wizara husika. Kwa kufanya hivyo kwanza Halmashauri zinavunja sheria na kutengeneza mazingira ya ubadhirifu wa fedha za umma. Hivyo Kamati inaagiza utekelezaji wa mipango ya maendeleo lazima uzingatie

bajeti ya mwaka husika na utaratibu wa kubadili malengo ya matumizi ya fedha ufuata sheria na kanuni zilizopo. Huu ni utaratibu wa kisheria na hivyo si hisani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuongeza ufanisi katika ufungaji wa vitabu, Kutokana na uchambuzi wa Vitabu vya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2006/2007 imedhihirika kuwa hakuna uratibu wa kina (*coordination*) katika utayarishaji wa Taarifa za Miradi zinazowasilishwa mbele ya Kamati na pia inaonyesha hazijadiliwi na kuhakikiwa katika vikao vya Kamati ya Wataalam (*District Management Team- DMT*), Kamati ya Fedha na Mipango na Baraza la Madiwani.

Taarifa nyingi zimeonekana kuwa na dosari kama:-

- (i) Kutotumika kwa vipimo vinavyokubalika kitaalam;
- (ii) Taarifa ya matumizi ya miradi kutokuwa na michanganuo ya kina na takwimu zinazoaminika;
- (iii) Thamani ya vitu kuwekwa katika kadirio la juu yaani “inflated” ili kupata ulinganifu wa Hesabu;
- (iv) Kutothaminisha michango ya Wananchi katika Taarifa za miradi ya Maendeleo; na
- (v) Madiwani katika Kamati yao ya Fedha ambayo ndiyo mamlaka ya awali ya udhibiti kutokupata Mchanganuo wa kina unaowaruhusu kusimamia kikamilifu matumizi ya fedha za umma.

Hali hii husababishwa na ushirikiano duni uliopo kati ya Wakuu wa Idara wakati wa maandalizi ya Taarifa za miradi mbalimbali. Aidha, ni vema ikaeleweka kuwa ufungaji wa vitabu unahitaji kuhusisha Wataalam wa mahesabu na Wakuu wa Idara ili iwe rahisi kwa Halmashauri kuondoa dosari zote zinazojitokeza kwenye ufungaji wa Vitabu. Kamati yangu imetoa maelekezo kwa Halmashauri zote nchini kuwa, utaratibu wa Mchanganuo unaotumika kutoa Taarifa kwa Kamati ya LAAC utumike pia katika Taarifa zote za kila mwezi kwa Kamati ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa miradi uzingatie ubora na miongozo iliyowekwa na serikali, Miradi mingi ya maendeleo hususan miradi ya ujenzi inayotekelezwa katika ngazi za Vijiji na Kata haifuati miongozo na ramani zilizotolewa na Serikali Kuu. Kamati baada ya kufanya ukaguzi wa thamani ya miradi imesikitishwa kwa maana baadhi ya majengo yanayojengwa kwenye Halmashauri zetu hayana ubora kabisa na hayatoweza kustahimili muda mrefu kabla hayajabomoka, mfano; Jengo la Bweni la Wasichana katika Shule ya Sekondari ya Engutoto iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, lina nyufa kubwa katika kuta zote, Zahanati ya Kinonko katika Halmashauri ya wilaya ya Morogoro- ujenzi haukufuata ramani ya Afya, Jengo la Ofisi ya Kata ya Bigwa katika Manispaa ya Morogoro- nyufa zimetapakaa katika kuta na Madarasa ya Shule za sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto (Kata ya Makanya)- Madarasa yamejengwa kwa udongo toka chini hadi juu bila ya kutumia Saruji

kabisa. Katika Halmashauri za mikoa iliyo katika Kanda ya Ziwa (Mwanza, Kagera na Mara), majengo mengi yanaathiriwa kwa kiasi kikubwa na popo wanaokaa katika dari na hivyo kusababisha majengo hayo kuwa hatarishi au kutotumika kabisa. Kutokana na hali hiyo, Kamati imekuwa ikishauri Halmashauri kutumia mabati yanayopitisha mwanga ili kupunguza tatizo hilo.

Aidha, ni vyema Serikali ikatoa muongozo utakaoweza ujenzi wa majengo yote nchini ukazingatia mazingira ya eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa majengo ya Shule, baadhi ya Halmashauri hazifuati miongozo ya Serikali ya kuezeka kwa kutumia mabati ya geji 28 na kuhakikisha katika kila mfuko wa Saruji unatoa matofali yasiozidi 28 - 30, bali Halmashauri zimekuwa zikiezeka majengo ya Shule kwa bati za geji 30 na kufyatua matofali zaidi ya 35 kwa mfuko mmoja wa Saruji.

Huu ni utumiaji mbaya wa fedha za Umma na Michango ya Wananchi. Aidha, baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa hazitoi ushauri wa kitaalam (*Back Stopping*) kwa Kamati za Ujenzi za Vijiji, hivyo husababisha miradi ya Ujenzi kutekelezwa chini ya kiwango pamoja na kuwa wahandisi ndio wanaotoa "*Certificates*" kabla ya malipo mbalimbali yanayohusiana na majengo hayo. Ni muhimu Mamlaka za Serikali za mitaa zikatambua kuwa majengo haya yanajengwa kwa mategemeo kwamba yatadumu kwa muda mrefu, hivyo ni bora utekelezaji wake ukazingatia ubora na miongozo ya Serikali. Aidha, ni vema utaratibu ulioanzishwa wa kufanya "*Value for Money Audit*" na NAO pamoja na Kamati ya LAAC ukatiliwa mkazo zaidi ili kuondoa hasara hii kubwa tunayoingia kama Taifa, kutokana na majengo na miradi isiyo na ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Uchapishaji wa Taarifa za Ukaguzi za Halmashauri izingatiwe, Uchapishaji wa Taarifa ya Ukaguzi katika Magazeti kwa kuzingatia sheria zilizowekwa bado ni tatizo kwa baadhi ya Halmashauri.

Aidha, Halmashauri nyingi huchapisha Taarifa zao za Ukaguzi kabla ya kuzipitisha kwanza kwenye Kamati ya Fedha na Mipango na baadaye kwenye Baraza la Madiwani. Kitendo hiki ni ukiukwaji wa Maagizo ya *Memorandum* ya Fedha za Serikali za Mitaa hivyo haina budi kikemewe vikali. Hata hivyo, Halmashauri nyingi zilizopata Hati ya Mashaka (*Qualified Opinion*) zimechapisha taarifa zao bila ibara inayoonyesha "*Matters leading to qualified Opinion*" suala ambalo ni kosa la kuidanganya jamii isijue mapungufu katika utendaji wa Halmashauri hizo. Hivyo, ni muhimu taratibu na sheria zote zikafuatwa kabla ya kuchapisha taarifa za ukaguzi na dhana ya ukweli na uwazi katika shughuli za Serikali idumishwe katika suala hili.

Watendaji wa halmashauri wasikae katika kituo kimoja kwa muda mrefu, Watendaji wa Halmashauri wasikae katika kituo kimoja kwa muda mrefu kwani hujijengea tabia ya kutekeleza majukumu yao kwa mazoea na si kwa kufuata taratibu ama miiko maalum ya kazi zao "*Code of Ethics*" na kusababisha kutokuwa wabunifu au kusahau utendaji bora katika utekelezaji wa majukumu yao. Kwa mfano, Idadi kubwa ya Wakuu wa Idara katika Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga wameanzia kazi hapo na

hadi leo ni zaidi ya miaka 15 hawajahamishwa. Watumishi wanaohamishwa ni wajibu wao kisheria kuripoti kwenye vituo vyao vipya na kusiwe na ushawishi wa mtu yoyote kwa kutumia wadhifa wake Serikalini kuwakingia kifua kwenda au kubaki sehemu wanazozitaka wao. Ifuatayo ni mifano dhahiri inayotoa taswira kamili ya suala hili:

(i) Daktari aliyehamishwa toka Mbeya kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma hajaripoti mpaka leo na Idara hiyo inaendeshwa na Afisa Afya kwa sasa; na

(ii) Daktari aliyetakiwa kwenda Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga mpaka leo yupo Hospitali ya Amana katika Jiji la Dar es Salaam.

Halmashauri ziweke mikakati ya kushughulikia kesi zake, kesi nyingi zinazozikabili Halmashauri zetu hutumia fedha nyingi za uendeshaji na huchukua muda mrefu mpaka hukumu kutolewa. Cha kusikitisha zaidi mara nyingi Halmashauri zetu hushindwa kesi hizo, hivyo kupoteza fedha nyingi katika uendeshaji wa kesi na zile wanazozidai kama kesi iliyofunguliwa ni ya madai. Wakati umefika wa kuweka mikakati madhubuti ya kushinda kesi hizi ili Halmashauri zisiendeleo kupoteza fedha kutokana na kushindwa kesi. Aidha, imedhihirika kwamba Halmashauri hushindwa kesi nyingi kwa sababu ya kutokuwa na Wanasheria au uzembe wa watumishi kwa:-

- (i) Kushindwa kuhudhuria mahakamani pindi kesi inapoendeshwa;
- (ii) Kutopeleka nyaraka muhimu kama ushahidi katika kesi hizo; na
- (iii) Mikataba mingi kutozingatia maslahi ya Halmashauri.

Hivyo, Kamati inashauri Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha zinaweka mikakati madhubuti itakayozingatia, kwanza, kudhibiti dosari za kiutendaji zinazopelekea kufunguliwa kwa kesi dhidi ya Halmashauri au mtendaji wa Halmashauri na pili, kushinda kesi hizo. Kamati imeweza kukagua Hesabu za Halmashauri zote na kufanikiwa kutembelea miradi ya maendeleo katika Halmashauri za mikoa kumi na moja (11) kwa mafanikio makubwa. Katika kuhakikisha shughuli hizi zinafanywa kwa ufanisi, Halmashauri zote zilijadiliwa na miradi yake kukaguliwa bila kujali kuwa zimepata Hati inayoridhisha au yenye mashaka, na kuthibitika kwamba kupata *Hati inayoridhisha*, hakumaanishi kwamba hakuna madhambi yanayotendeka. Aidha, utaratibu huu umesaidia sana kwa maana Kamati imeweza kukagua Hesabu na kuthibitisha usahihi wake kwa kuhakiki utekelezaji wa miradi ya maendeleo, "Value for Money". Kwa kuwa utaratibu huu unahitaji mahojiano marefu na kukagua miradi ya maendeleo bila kuwa na uharaka wa kuangalia mradi mwingine, Kamati inapendekeza kwanza, ipate muda wa kutosha kupitia maandishi yanayotolewa na Watendaji na pili, uangaliwe uwezekano wa kuiwezesha Kamati kifedha ili iweze kuendelea na utaratibu wa kufanya ukaguzi wa thamani ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, "Performance Audit", utaratibu ambao kama utaendelea kutumika, utaongeza uwajibikaji kwa kiasi kikubwa katika Halmashauri zetu na kurudisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete pamoja na Serikali ya Jamhuri ya

Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu wa kuondoa ubadhirifu wa fedha za Umma na kusisitiza kuwa ukaguzi wa thamani ya kazi yaani “*Value for Money Audit*” utiwiwe mkazo na si kuishia kwenye ukaguzi wa nyaraka yaani “*Financial Audit*” kama ilivyokuwa awali. Napenda kuunga mkono juhudi hizi kwa kusema kwamba hii ni hatua moja ya muhimu sana katika kujenga Taifa lenye misingi ya uzalendo, uadilifu na uwajibikaji kwa maendeleo ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha napenda kutoa shukrani nyingi kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati kwa Mheshimiwa Mizengo Pinda - Waziri Mkuu na Mheshimiwa Celina Kombani, – Waziri wa Nchi, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Katibu Mkuu, TAMISEMI, Bibi Maimuna Tarishi, kwa jinsi wanavyoathamini sana shughuli zinazofanywa na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Baada ya Ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika mwezi Januari 2009, Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa aliomba kukutana na Kamati ili aweze kujua ni masuala gani ya msingi ambayo Kamati imeyaona kwenye ziara hiyo ambayo yanahitaji mwongozo ama usimamizi wa Wizara. Kamati iliridhia bila pingamizi ombi la Waziri na kukutana naye Tarehe 17 Aprili, 2009, ambapo majadiliano ya msingi na yenye mtazamo wa kuleta maendeleo katika Halmashauri zetu yalifanyika kwa mafanikio makubwa.

Aidha, Mheshimiwa Waziri Kombani mara kwa mara amekuwa akishauriana na Kamati yangu kuhusu changamoto mbalimbali zinazokabili uendeshaji wa Halmashauri zetu. Hivyo, kutokana na jitihada za Mheshimiwa Waziri katika kutoa ushirikiano na kuchukua hatua mbalimbali za msingi kufuatia ushauri unaotolewa na Kamati yangu, naomba nichukue nafasi hii kumshukuru kwa namna ya pekee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru tena Wajumbe wa Kamati hii kwa kujitolea bila kuchoka katika kufanya kazi ya kuchunguza Hesabu, kuhoji masuala mbalimbali ya msingi na kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali katika Halmashauri zote 124 zilizokuwepo katika mwaka wa fedha wa 2006/2007. Aidha, niseme kwamba ni jambo la kushukuru sana kuwa na Wajumbe wenye ushirikiano, moyo wa kujitolea na uadilifu kama waliouonyesha wajumbe wa Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nitumie nafasi hii kuwashukuru, Wenyeviti wa Halmashauri waliokubali kuongozana na Watendaji kuja mbele ya Kamati. Kama ilivyo kwetu Wabunge, nao wanalo jukumu kubwa la kuhakikisha Halmashauri zao zinawajibika kikamilifu kwa wananchi wake kwa mujibu wa Sheria na Kanuni. Kamati inawashauri waige mazuri kutoka katika Kamati yetu na kuyatumia wakati wa vikao vyao katika halmashauri zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Katibu wa Bunge – Dr. Thomas D. Kashililah kwa kuhakikisha Kamati inatekeleza majukumu yake kikamilifu bila vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali – Ndg. Ludovick S.L. Utouh na Watendaji wake, kwa umahiri wao wa kutoa maelezo kwenye Kamati ambayo kwa kiasi kikubwa ndiyo yaliyoongoza majadiliano wakati wa vikao vya Kamati. Lakini pia ninawashukuru Watendaji toka Hazina Bibi



Batuli Kilo na Ndugu Mzikila, na TAMISEMI, Ndugu. Juma Madaha (*ambaye ameteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Tunduru*), ambao walishirikiana ipasavyo na Kamati katika kutoa ufafanuzi na mchango wa kitaalam katika masuala mbalimbali.

Aidha, niwapongeze sana kwa juhudi na kujitolea kwao kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa shughuli za Kamati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, niwashukuru na kuwapongeza Ndugu John N. Joel pamoja na Ndugu Mathew N. Kileo – Makatibu wa Kamati yetu kwa ushirikiano wao na kwa kazi nzuri ya kuandaa, kuratibu na kuihudumia Kamati hasa katika kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya namna ya kuendesha shughuli za Kamati yetu kwa kufuata misingi ya Kanuni zilizowekwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Slaa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mawasilisho yako. Waheshimiwa Wabunge, waombaji ambao wangependa kuchangia hoja hizi mbili za Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa jumla yao ni 20 na kwa muda ambao umebakia hadi shughuli za Bunge hili kwisha na bado tunashughuli za Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma itakuwa tabu sana kwa Bunge hili kupata nafasi kuweza kuchangia hesabu hizi.

Kwa hiyo, ushauri wangu kwa hesabu za mashirika ya umma kesho hebu ripoti ziwe fupi zijikite kwenye mambo gani wanataka kuliambia Bunge, badala ya kutuchukua ile saa nzima ile kwamba tuna saa nzima, tujitahidi iwe hivyo wale wa kesho ili kutoa muda kwa Waheshimiwa Wabunge. Kwa hiyo, kama nilivyoahidi mwanzoni, Mheshimiwa Mudhihir Mudhihir atakuwa wa kwanza kuchangia na Mbunge wa mwisho kuchangia kwa jioni ya leo ni Mheshimiwa Msindai.

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo umeamua vizuri. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Wajumbe wote wa Kamati ya LAAC pamoja na Kamati ya PAC kwa uwasilishaji mzuri ambao wameufanya, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa pongezi za dhati Mkaguzi Mkuu wa Serikali CAG kwa kazi nzuri ambayo ameifanya, nayo imeturahisishia sana kujua Serikali ikoje kwa maana ya Serikali Kuu na kujua Halmashauri zetu zikoje kwa maana ya Halmashauri ambazo ni Serikali zetu za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, nachukue fursa na nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais ameanzisha mpango mzuri nami ningependekeza tuongeze ili uwe na ufanisi mzuri sana. Mwaka juzi na mwaka jana ameiita Serikali yake yote kwa maana ya Watendaji wa Serikali, Serikali Kuu, Mawaziri, Makatibu Wakuu na hata Watendaji wa Halmashauri wakakaa katika kujadili *report* hii ya CAG.

Hilo jambo ni zuri sana kwa sababu napenda kumnukuu Rais mwenyewe alisititiza katika hotuba zake na kuonya kwamba katika maeneo mengi ya Serikali kuna uvujaji mkubwa sana wa fedha na hasa akazingatia Wizarani na pamoja na katika Halmashauri zetu za Wilaya. Kwa maneno yake mwenyewe alisema kuna mchwa ambaye kwa msemo wa sasa hivi ni jambo la ufisadi.

Sasa hatua ambayo aliichukua ya kuwaweka watendaji wote hawa wa Serikali mimi napendekeza Bunge lako hili kwa hatua tunayojadili *report* hizi tatu kwa maana ya *report* ya Mashirika ya Umma, Serikali yenyewe na Halmashauri na *report* ya CAG.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza hatua hii tuweze kuishusha hata Halmashauri zetu ziweze kujadili katika maeneo husika kwa sababu pesa nyingine zimeshuka katika Halmashauri zetu lakini tukiishia tu kujadili sisi kwa upande wa Wabunge peke yake bila Halmashauri zetu kwa maana ya Kamati ya Fedha kwa maana hata ya Madiwani wote kwa ujumla tutakuwa tunafanya kazi ambayo haina manufaa.

Kwa hiyo, napendekeza Kamati hii ya Fedha pamoja na Kamati ya Madiwani wote yaani *Full Council* waweze kuiga mfano mzuri ambao Rais wetu ameanzisha kwenye Serikali lakini vilevile waweze kujadili katika halmashauri zao zote ili kuweza kuelewa ni kitu gani ambacho CAG amekigundua, kitu gani ambacho Kamati ya LAAC ya Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa na wenzake wamegundua katika Halmashauri zao. Hawawezi kujadili katika upana wa nchi nzima, lakini wajaadili katika eneo lao la Halmashauri ambalo linawahusu katika *report* ambazo zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa napendekeza hili lingeweza kusaidia sana kuona kwamba mchwa huu ambao uko katika Halmashauri zetu kwa maana ya kupambana nao vizuri basi ni vizuri vilevile Kamati hizi zote tatu zikawasilishwa katika maeneo ya Halmashauri zetu za Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile si Halmashauri peke yake, haya mambo yote yanatakiwa yawe wazi, ipelekwe kwenye Halmashauri ya Wilaya lakini vilevile kwa sababu Serikali imeanzisha Kamati ya Ushauri ya Wilaya ambayo inaongozwa na Mkuu wa Wilaya na yenyewe ijadili kuona upungufu gani upo na kuona mikakagi gani ya kufanya ili kurahisisha uwezeshaji wa kuhakikisha kwamba hayatokei tena na ngazi ya Mkoa ambao kuna Kamati ya RCC ile ya Mkuu wa Mkoa na yenyewe iweze kujadili namna gani na kitu gani kitafanyika. Huo ndiyo ushauri wangu wa kwanza

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, fedha nyingi sana zimepelekwa kule kwenye Halmashauri zetu nyingi sana na pesa hizo ukiangalia *report* ya CAG na ukiangalia maelezo ambayo wametoa wenzetu wanakamati taarifa nyingi za Halmashauri

zina dosari kwa hiyo, mimi napenda vilevile pamoja na kuimarisha ukaguzi huo wa CAG, lakini vilevile na Kamati hizi ziongezewe nguvu na meno kwa maana ya Kamati ya LAAC, PAC pamoja na Kamati ya Mashirika ya Umma. Ukiangalia *report* ambayo inatoka kwa mshauri wa Serikali CAG sana anakwenda anapeleka shauri hili kwa TAKUKURU peke yake, lakini kwa sababu Waheshimiwa Wabunge wenzetu wako hapa na wanapata fursa ya kutembelea katika maeneo mbalimbali na kuona uozo na ubadhilifu unaofanyika, mimi ningeshukuru sana Kamati hizi zingeweza kuongezewa nguvu na kuongezewa fedha ili ziweze kutoka mara kwa mara na zifanye kazi kwa muda mrefu zaidi kufikia maeneo ambayo pengine hayawezi kufikika kwa haraka. Hata hivyo, Kamati za Halmashauri na zenyewe ziongezewe nguvu za fedha ili ziweze kutembelea maeneo mbalimbali katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu kwa haraka sana ningependa kuishauri Serikali muda ule ambao tulikuwa tunakusanya kodi, zile kodi zilikuwa zinafanya kazi ya maendeleo katika maeneo mbalimbali. Pamoja na nia nzuri ya Serikali iliyoichukua ya kuondoa kero iliyokuwepo ilifanya mpango wa kuweka 20% ya fedha za kodi za fidia zirudi kwenye Serikali za Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia *report* ya CAG na ukisikiliza *report* za wenzetu wa LAAC pamoja na PAC wanadhahirisha kabisa kwamba karibu robo tatu ya Halmashauri zetu hazijarudisha fedha kwenye vijiji. Huu ni uonevu, wizi na ni kitu kibaya kwenye miradi ya maendeleo ya vijiji vyetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni baya, hizi pesa zimeshaletwa kwenye Serikali, zimeshaletwa mpaka kwenye ngazi ya Halmashauri, kwa nini Mkurugenzi na Halmashauri yake wanaachiwa bila kuzirudisha kwenye Serikali za Vijiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote ambao hawajarudisha fedha hizi wanatakiwa wachukuliwe hatua kali na za haraka sana mara moja. Naomba Serikali ilichukue hili. Naomba vilevile na Kamati zetu zote pamoja na CAG na wenyewe wahakikishe hatu kali na haraka zinachukuliwa kwa watu wote ambao wanafanya pesa ya Serikali ya vijiji ambazo zingeshiriki katika kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo yao ziweze kurudi katika vijiji vyote vinavyohusika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo lingine la nne ambalo ningependa kulitoa mbele ya Bunge lako Tukufu baada ya kuona taarifa hizi nyingi zina dosari. Ningependa kitengo kile cha Mkaguzi wa Ndani, yaani *Internal Auditor* kiweze kuimarishwa. Kwanza Halmashauri nyingi ukisoma *report* hasa ya CAG ambayo tuliipata muda mrefu jana tumeisoma Halmashauri nyingi watumishi ni wachache sana ukisoma *report* ile watumishi hawa wako chini ya Mkurugenzi, wako chini ya DT, haitakuwa na ufanisi mzuri kama watumishi hawa watabaki kuwa chini ya DT au kuwa chini ya Mkurugenzi. Nilikuwa napendekeza kwa sababu ya unyeti wa watumishi hawa wa kitengo hiki cha Mkaguzi wa ndani kinafanana sana na kitengo alichonacho CAG, kwa nini isiwepo mtiririko wa moja kwa moja watumishi wa Wakaguzi wa Ndani wakawa chini ya CAG? Watatusaidia zaidi kuliko kuwa chini ya Mkurugenzi na kuwa chini ya DT, kwanza

akimfuatilia sana *DT* au *DED* anaweza akamnyima usafiri, posho za kwenda kuangalia miradi mbalimbali ambayo inagharimikiwa na Serikali.

Kwa hiyo, napenda kitengo hiki muhimu ambacho ni cha maana sana ambacho ni jicho hata la Halmashauri yetu ambacho ni jicho hata la Kamati ya Fedha kingekuwa chini ya *CAG* na kama haiwezekani, basi kiwe moja kwa moja chini ya Hazina, kitakuwa na uwezo mzuri zaidi kwa sababu kitakuwa huru. Mkurugenzi yeyote ambaye atachelewesha kukiwezesha kwa nyenzo kukiwezesha kitengo hiki, basi na yeye aangaliwe kwa jicho la ukonekana kama yeye ni mchwa na kitu kinafichwa lazima ujue kina matatizo ambayo Mkurugenzi huyo au *DT* huyo lazima achukuliwe hatua kali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo langu la sita na la mwisho ni juu ya kitengo cha manunuzi, Kitengo hiki cha manunuzi hakina watumishi wengi vilevile na wengi bado hawafanyi manunuzi kutokana na utaalumu ambao unatakiwa ufuatwe, hawafuati miongozo waliyonayo, hawatangazi kwa uzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nadhani hawa nao vilevile waweze kuimarisha ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Ni kweli tunashusha madaraka mengi sana kwenye Halmashauri zetu kama ambavyo tunashusha pesa nyingi sana kwenye Halmashauri zetu na kama vile ambavyo tunashusha miradi mingi sana kwenye Halmashauri zetu, lakini bila kuimarisha vitengo hivi, basi hizo fedha na miradi yote itaweza kupotea kwa sababu Waswahili walisema: “Mali bila daftari hupotea bila bila habari.” Kwa hiyo, katika ujumla wake sasa napenda kutoa mapendekezo hayo sita ambayo nadhani yataweza kutuimarishia katika miaka ijayo ili kuona Halmashauri zetu ili kuona fedha za Serikali zimefanya kazi iliyokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kupata *report* hizi tatu zote ambazo kweli zinatuashiria na kutuelekeza mahali pazuri pa kwenda ambazo wenzetu Wabunge ambao wako kwenye Kamati ya *LAAC* na Wabunge ambao wako kwenye Kamati ya *PAC*, mimi nina hakika kuwa kazi nzuri ambayo anaifanya *CAG* kwa niaba ya Serikali na Bunge. Ninatoa mapendekezo kwamba watu hawa kwa kweli kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa jinsi ambayo wanajituma, amesema hapa mtoja hoja wa pili - Mwenyekiti wa Kamati ya *LAAC* kwamba kazi walikuwa wanafanya mpaka usiku, walikuwa wanafanya kazi ngumu, walikuwa wanasafiri maeneo makubwa, kwa kweli lazima tufike mahali ambapo tunawapongeza na jambo ambalo linatakiwa kupongezwa, basi waangaliwe maeneo wanakokwenda wapewe urahisi wa kufika na nyenzo za kuwafikisha katika maeneo kama ambavyo wamekusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu umekwenda sana na kwa hiyo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucas L. Selelii nakushukuru sana kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, muda wetu uliobakia ni mdogo sana kwa hiyo, baada ya wachangiaji hao niliobahatika kuwapata ambao ni watatu, muda

hauruhusu kwa mchangiaji mwingine yeyote. Sasa nina matangazo mawili, la kwanza ni la Waheshimiwa Wabunge wa *TWPG*, yaani Wabunge akina Mama.

Kesho kuanzia saa 2.00 mpaka saa 11.00 jioni nyuma ya Ukumbi wa Pius Msekwa kutakuwa na shughuli ile maalum ambayo mmejipangia wenyewe.

Kwa hiyo, mnaombwa kutoa ushirikiano, kesho nyuma ya Ukumbi ule na kila mmoja ajaribu kufika pale kati ya saa 2.00 na saa 11.00 jioni. Tangazo hili limeletwa na Mheshimiwa Eliatta M. Switi ambaye ni Katibu wenu.

Pili, naomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge wote mliopo katika Ukumbi huu na wale wote ambao mko hapa Dodoma kwamba mara baada ya kikao hiki mkusanyike kwenye Ukumbi wa Pius Msekwa, kwa ajili ya Kikao cha mwendelezo wa *Briefing* ile ya Jumanne, tarehe 21 Aprili, 2009.

Katika kikao hicho agenda mbili muhimu zitazungumziwa. Moja, tutapewa taarifa kuhusu maandalizi ya uchaguzi wa TAMISEMI utakaokuja baadaye mwaka huu na agenda ya pili ni hali ya chakula. Baada ya hapo Wabunge wa CCM wataendelea na kikao chao cha kawaida hapo hapo katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Baada ya matangazo hayo, ninapenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa *Order Paper* yetu shughuli zilizopangwa zote zimakamilika na muda wetu kama nilivyoeleza mwanzo umekwisha. Kwa hiyo, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi. Ahsanteni. (*Makofi*)

(*Saa 1.40 usiku Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano,  
Tarehe 29 Aprili, 2009 Saa 3.00 Asubuhi*)